

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 20 Mei, 2019**

*(Bunge Lilianza saa Tatu Asubuhi)*

#### DUA

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa 15, leo kikao cha 31.  
Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

#### TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nasikitika kuwatangazia kifo cha mwanasiasa mkongwe na kiongozi aliyepata kuhudumia kwa muda mrefu hasa kule kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Marehemu Ally Juma Shamhuna.

Waheshimiwa Wabunge, katika uhai wake, marehemu Ally Juma Shamhuma amepata kushika nyadhifa mbalimbali zikiwemo hizi zifuatazo; amepata kuwa Mkurugenzi wa Mifugo, amewahi kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, amewahi kuwa Katibu Mkuu, *Export Processing Zone* Zanzibar, amewahi kuwa Waziri wa Mipango, amekuwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi, aliwahi kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo na wakati huo huo akiwa ni

Naibu Waziri Kiongozi, katika uhai wake amekuwa Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati na alipata kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Aidha, Marehemu Mheshimiwa Shamhuna kwa muda mrefu alikuwa ni mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi kutokea Zanzibar na baadhi yenu humu Wabunge mtamkumbuka marehemu Mheshimiwa Shamhuna kama Mbunge wa Bunge la Katiba na alikuwa Mjumbe wa Kamati namba 8 kwenye Bunge la Katiba, Kamati ambayo nilikuwa Mwenyekiti wake.

Kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge, tunatoa pole kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Tunatoa pole kwa Wazanzibari wote na Watanzania wote kwa ujumla kufuatia kifo hicho na tunamuomba Mwenyezi Mungu aihifadhi roho yake mahali pema peponi, amina.

Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvubi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Ulega.

Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali. Swali la kwanza linaelekezwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, litaulizwa na Mheshimiwa

Tauhida Cassian Galoss. Mheshimiwa Tauhida uliza swali lako tafadhali, kwa niaba yake.

Na. 252

**Mgogoro Kati ya Kituo cha Polisi Bububu na Soko**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA (K.n.y. MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS)** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua mgogoro wa muda mrefu kati ya kituo cha polisi Bububu na soko dogo la wananchi lililopo karibu na kituo hicho?

(b) Je, kiutaratibu umbali kati ya kituo cha polisi na makazi ya wananchi ni hatua ngapi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa *Engineer Hamad Masauni* tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Galoss, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, si kweli kuwa kuna mgogoro wa kiwanja kati ya wananchi na Jeshi la Polisi katika eneo la kituo cha polisi Bububu. Ndiyo sababu wakazi wa eneo hilo ikiwemo wafanyabiashara wa soko hilo dogo hupata huduma za kiusalama katika kituo cha Bububu bila shaka yejote. Aidha, kiwanja kilipojengwa kituo cha polisi Bububu na majengo mengine ya kituo yanamiliikiwa kihalali na Jeshi la Polisi ingawa kuna kibanda cha kuuza samaki karibu na kituo hicho cha polisi kinachoitwa soko dogo la wananchi. Kibanda hicho kipo kati ya kituo cha Polisi Bububu na majengo mengine ya kituo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli upo utaratibu wa kuwepo kwa umbali kati vituo vya polisi, kambi za makazi ya askari ya wananchi. Hii ni kutokana na sababu za kiusalama kwa miundo mbinu ya Jeshi la Polisi. Aidha, kutokana na changamoto za makazi na ujenzi holela mijini. Uvamizi wa maeneo sehemu mbalimbali na kuongezeka kwa shughuli mbalimbali za kibinadamu zisizo rasmi imesababisha maeneo mengi ya vituo vya polisi kuingiliwa na kusogeleana na makazi ya wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma nimekuona. Swalii la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi hii, nashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa majibu yako mazuri lakini nitakuwa na suala moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muingiliano umekuwa mkubwa na watu wamekuwa wengi, kwanini hiki kituo kisitafutiwe sehemu nyngine, kikajengwa huko, kikawa na nafasi kubwa kikaelekea kama kituo kweli cha polisi kuliko pale kilivyokaa, hakijapendeza wala haifai. Huku kituo, huku soko, nafikiri Serikali ifikirie kukihamisha kikapate nafasi kubwa zaidi na majengo ya kisasa yaliyokuwa bora zaidi. Ahsante.

**SPIKA:** Swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani, tunaomba majibu Mheshimiwa *Engineer Hamad Masauni* tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hoja ya kuhamisha kituo hiki kwa sababu ya ufinyu wa nafasi kiusahihi ni kwamba eneo la kituo lile ni kubwa mno, labda Mheshimiwa Mbunge tukipata nafasi tukatembelee ili nimuoneshe. Ni juzi tu hapa kuna eneo ambalo liliwahi hata kupewa mwekezaji na kutokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kwamba maeneo ya vyombo vya usalama yabakie kwa matumizi ya vyombo hivi tulitoa maelekezo na kuhakikisha kwamba tumemhamisha yule mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, lakini utakumbuka pia hata eneo ambalo liko pembeni ya kituo cha polisi ambacho kimetumika kama soko kama alivyozungumza kwenye swalii msingi ni eneo pia la polisi ukiachia mbali eneo la nyuma ambalo ni kubwa. Kwa hiyo, kimsingi kuhamisha kituo hiki kwa sababu ya ufinyu wa eneo nadhani haitakuwa sahihi kwa sababu kuna eneo la kutosha. Cha msingi ni kuendelea kutoa wito kwa wananchi kutumia nafasi yao yoyote ya kuvamia maeneo ya polisi kuacha maeneo ya polisi yaendelee kutumika kwa ajili ya shughuli za kiusalama.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Paulina Gekul, uliza swalii lako tafadhali.

**MHE. PAULINA P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri kwanza nikushukuru kwa kutupatia zile 150,000,000 ambazo zimetusaidia kujenga majengo ya polisi katika eneo la Bagara Ziwani na nyumba zinakamilika.

Mheshimiwa Spika, sasa eneo hilo halijawahi kufidiwa, wananchi hawajawahi kufidiwa tangu 2004, polisi wanajenga majengo yao, wananchi hawajalipwa fidia tangu 2004. Nini kauli ya Serikali juu ya wananchi hawa ambao wametoa eneo kwa polisi lakini hawajapatiwa fidia mpaka leo?

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa *Engineer* Masauni tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa tunachukua pongezi kama Serikali kutokana na kazi ambayo inaendelea nchi nzima maeneo mbalimbali ya ujenzi wa nyumba za askari polisi.

Mheshimiwa Spika, la pili nimpongeze yeye binafsi kwa kufuatilia kwa karibu hii kadhia ya wananchi wake kutolipwa fidia. Hata hivyo, naomba nimhakikishie kwamba jambo hilo nimelichukua na tutalifanyia kazi na baadaye tutarudi kwake kuweza kumpatia majibu ya hatua ambazo zimefikiwa na

changamoto gani kama zipo na nini mikakati ya Serikali katika kukabiliana na changamoto hizo ili hatimaye wananchi hawa waweweze kupata fidia stahiki.

**SPIKA:** Bado tupo Wizara hiyo hiyo Waheshimiwa Wabunge, swali lifuatalo litaulizwa na Mheshimiwa Rehema Juma Migilla. Mheshimiwa Rehema.

Na. 253

### **Polisi Kukamata Bodaboda na Kutoa Baadhi ya Vifaa**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Pamoja na jitihada za vijana wengi kujajiri wenyewe kwa kuendesha bodaboda wamekuwa wakisumbuliwa na polisi kwa pikipiki zao kukamatwa mara kwa mara:-

Je, kwa nini pikipiki zao zinapokamatwa na wanapoenda kuzichukua hukuta baadhi ya vifaa kama betri hazipo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, kwanini pikipiki zikikamatwa betri zinaibiwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usalama Barabarani sura ya 168 iliyorejewa mwaka 2002 inampa mamlaka Askari Polisi kusimamisha chombo chochote barabarani na kukikagua kubaini kama kina makosa na hatimaye kukizuia na kukamatwa. Chombo cha moto kinapokamatwa hutunzwa kituoni kwa mujibu wa mwongozo wa Jeshi la Polisi Namba 229.

Mheshimiwa Spika, inapotokea kielelezo kimeharibiwa uchunguzi hufanyika na hatua kuchukuliwa kwa waliohusika na upotevu huo.

**SPIKA:** Umeridhika?

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naona majibu haya yamejibiwa kisiasa kuliko uhalisia wenyewe ulioko huko kwa waendesha bodaboda.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio hai kabisa bodaboda hawa wamejiajiri wenyewe na wanafanya kazi katika mazingira magumu na wamekuwa wakisumbuliwa sana na polisi *especially* hawa *PT. Wanawakamata* na wakishawakamata hata uchunguzi wa kina haufanyiki na *sometimes* wanawabambikizia makosa. Wanapotaka zile hela pikipiki zao zinapelekwa polisi. Zikifika polisi, pindi wanapotaka kuzichukua wanakuta baadhi ya vitu kama betri, mafuta na hata wakati mwagine wanakuta hadi gamba zimebadilishwa na tunaelewa kabisa polisi ni mahali ambapo pana usalama wa kutosha na hakuna mtu ambae anaweza akaenda kubadilisha kitu chochote pasipo kukamatwa.

Mheshimiwa Spika, sasa je, Mheshimiwa Waziri, unataka kutuambia wanaohusika na hili zoezi la kuchomoa vitu au vielelezo ni Polisi au akina nani na tunajua kabisa pale ni mahali salama?

Mheshimiwa Spika, swali la pili nataka kufahamu pia pamekuwa na mrundikano mkubwa sana wa pikipiki katika vituo vya polisi na ukizingatia chanzo cha kukamatwa kwa hizi pikipiki na mrundikano huo ni hawa hawa polisi wanazikamata na kuwataka hao watu walipe...

**SPIKA:** Sasa swali.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** ... swali langu; Je, Serikali ina mpango gani kuwarudishia hawa watu pikipiki zao ambapo kwa kuendelea kukaa pale znaidi kuharibika?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoa ya Mheshimiwa Rehema, Mheshimiwa Mbunge ambaye kwa muda mfupi tangu alipoingia Bungeni ni Mbunge machachari na nimekuwa nikimpa ushirikiano kwa masuala ya Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni nilikuwa najiuliza kwanini watu wanaoagiza magari bandarini vitu vinachomolewa au watu kwenye viwanda vya ndege kunakuwa na *pilferage* lakini baadaye nikaja kushangaa hata kwenye vituo vya polisi vitu vichomolewe nikaona ni jambo ambalo linashangaza sana.

Mheshimiwa Spika, nilichofanya, kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwenye ilani hii ya CCM Ibara ya Nne, CCM imeamua kwamba katika changamoto zile nne za Ibara ya 4 za kupunguza umaskini, za kutatua tatizo la ajira tena tukataja bayana vijana, nataka nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba bodaboda ambazo nimetoa maelekezo ili wapambane na umaskini na tatizo la ajira ni bodaboda za makundi manne tu zitakazochukuliwa kupelekwa kituo cha polisi na hata kwenye bajeti hapa nilisema. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kundi la kwanza, ni bodaboda ambayo imehusika kwenye uhalifu, kwa sababu bodaboda zinatumika kufanya uhalifu. Hiyo ikikamatwa itapelekwa kituoni. Kundi la pili ni bodaboda ambayo inahusika na kesi na kesi yenyewe, moja ni kama bodaboda hiyo imehusika kwenye ajali ya barabarani ama bodaboda iliyoibiwa sasa katika *recovery*kawa imekamatwa, ni kielelezo. Kundi la tatu na la mwisho ni bodaboda ambayo haina mwenyewe sisi (*found and unclaimed property*) sasa polisi kwa sababu

wanalinda mali za raia wataichukua ikae kituo cha polisi, ikipata mwenyewe ichukuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, boda boda zingine zozote ambazo hazipo kwenye kundi hilo, sijui huyu hana *helmet*, huyu hana *side mirror*, huyu amepakia mshkaki, hakuna bodaboda itakayokamatwa kupelekwa kwenye kituo cha polisi. Nimewapata utaratibu wa kuwapa siku saba kama ni faini watalipa na nimeelekeza bodaboda ambazo ziko kwenye makundi matatu ztakazopelekwa kituo cha polisi na zenyewe wataandikiwa hati inayoonesa vitu ambavyo viko kwenye bodaboda ile ili atakapokuja huyu mtu a-cross check na hati aliopewa ili yule aliyechukua kama kuna upotetu aweze kushughulikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi bodaboda nchi nzima wanakula raha mstarehe, wanajinifasi. Kama Tabora suala hilo bado linaendelea, Mheshimiwa Rehema nikuhakikishie itakapofika jioni kama Tabora pale kuna pikipiki ambayo haiko kwenye makundi hayo, ama zao ama zangu. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Swali hilo limejibiwa vizuri sana, hakuna nyongeza. Tunaendelea na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, uliza swali lako tafadhalii.

Na. 254

### **Hitaji la Ofisi na Nyumba za Polisi Kilolo**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Tangu Wilaya ya Kilolo ipate hadhi ya kuwa wilaya mwaka 2002 Serikali haijaweza kujenga ofisi za polisi na nyumba za kuishi yalipo Makao Makuu ya Wilaya:-

Je, ni lini Serikali itajenga ofisi na nyumba hizo za polisi Wilaya ya Kilolo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Eng. Hamad Yusuf Masauni, majibu tafadhali ya swali namba 254.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabatti, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Iringa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi lina jumla ya wilaya 168 za kipolisi na zile za Kiserikali, kati ya hizo 127 zina majengo kwa ajili Ofisi na vituo vya polisi na wilaya 41 zilizobaki hazina majengo kwa ajili ya ofisi na vituo vya polisi wilaya ikiwemo Wilaya ya Kilolo. Hii in atokana na ufinyu wa bajeti ya maendeleo kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Jeshi la Polisi limejikita kukamilisha miradi iliyokwisha anzishwa huko nyuma, pindi miradi hiyo itakapokuwa imekamilika na hali ya kibajeti itakapokuwa imeimarika Jeshi la Polisi litajikita katika ujenzi wa vituo vya polisi vya wilaya pamoja na nyumba za askari katika wilaya ambzo hazina majengo hayo ikiwemo Wilaya ya Kilolo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta, swali la nyongeza nimekuona tafadhali.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali ya nyongeza na nishukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umbali yalipo mahabusu, Ofisi ya *OCD*, karibu kilometra 70 mpaka yalipo Makao Makuu ya Kilolo, hivi Serikali inatumia gharama kubwa sana kusafirisha mahabusu, kumsafirisha *OCD* na askari kwenda yalipo Makao Makuu. Je, Serikali huwa inaangalia tathmini ya gharama inazozitumia kwa kuchelewesha kujenga hizi Ofisi za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa nyumba za polisi zilizopo wilaya ya Mufindi, zilizopo *FFU* Kihesa na *Central line* polisi Iringa MJINI ni nyumba ambazo kwakweli ni chakavu mno, vyo haviingiliki, askari wetu wamekuwa wakiishi familia 5 chumba kimoja na kuna adha nyingi sana ambazo wanazipata hata watoto na kinamama ambao wanaishi katika zile nyumba.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri anipe siku, tarehe na mwezi ambao tutakwenda kukagua nyumba zote za Mkoa wa Iringa na kubwa ambazo wamekuwa wakizipata askari wetu walioko katika Mkoa Iringa, ili mwenyewe ajionee na aone jinsi gani ambavyo pamoja na ufinyu wa bajeti yeye mwenyewe ataona kwamba iko haja sasa haya majengo ya Askari au nyumba za askari ziweze kukarabatiwa?

**SPIKA:** Ahsante sana, majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa *Engineer Hamad Yussuf Masauni*, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Rita Kabati, kwa jinsi ambavyo amekuwa akitetea sana Jeshi letu la Polisi katika Mkoa wa Iringi, lakini siyo kwamba amekuwa akitetea kwa maneno, ni mlongoni mwa Wabunge ambao wameshiriki kikamilifu katika kuhakikisha kwamba wanapunguza changamoto za Askari wetu kwa yeye mwenyewe kujitolea kujenga kituo cha polisi kilichopo eneo la Semsema.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya pongezi hizi, Mheshimiwa Rita Kabati na jitihada kubwa ambazo tunaziona anazozifanya katika kupigania polisi, nimhakikishie kwamba tutaambatana mimi na yeye kwa ruhusu ya Mheshimiwa Spika, ili twende tukashirikiane kwa pamoja kubabiliana na changamoto ambazo amezizungumza. Hata hivyo, nataka nimhakikishie kwamba tayari Serikali imeshaanza jitihada. Kwa mfano hivi tunavyozungumza kuna ujenzi wa nyumba sita unaendelea kwenye Makao Makuu ya *FFU* pale Iringa ni

kuonyesha kuguswa na upungufu na uchakavu wa nyumba za Askari katika Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tayari kuna eneo ambalo tumelibaini kwa ajili ya ujenzi wa kituo kwa baadaye kwenye wilaya yake, tukitambua kwamba kuna umuhimu wa Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya kuwa katika Makao Makuu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani nimeshamjibu maswali yake mawili ya nyongeza kwa pamoj.

**SPIKA:** Ahsante, sana, ahsante sana, Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo swali linahusu Kilolo, nimekuona tafadhali, uliza swali lako.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa hii nafasi. Kwa kuwa swali limekuwa likijirudia kila mara na majibu ambayo yanatofautiana, sasa niombe, tu kwa kuwa umbali huo ni mrefu na gari hakuna, Serikali itakuwa tayari sasa kutoa gari na kuongeza mafuta kwa ajili ya kwenda Kilolo na kurudi?

**SPIKA:** Majibu mafupi ya swali hilo fupi, kupeleka gari pale na kuongeza bajeti kidogo ya kuendesha gari hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tutakuwa tayari kupeleka gari Kilolo pale ambapo fedha zitakapopatikana.

**SPIKA:** Ahsante, maswali mawili ya mwisho yatakuwa ya Mheshimiwa Shekilindi na Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Shekilindi kwanza!

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, kituo cha Polisi katika Wilaya ya Lushoto ni cha tangia Mkoloni, lakini

nashukuru Serikali imetutengea fedha tumejenga kituo cha Polisi lakini kituo kile mpaka sasa hivi takribani miaka mitano sasa kiko kwenye mtambao wa panya. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kumalizia kituo kile.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali, kituo hicho kisichoisha, lini mtapeleka fedha huku, karibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shekilindi, Mbunge wa Lushoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lugha ambayo ameitumia kidogo imenipa utata kuielewa...

**SPIKA:** Iko kwenye leta.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Ameseama mtanda wa panya...

**SPIKA:** Iko kwenye lenta, pale, wanaita mtambaa panya.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, sawa sawa, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo amependekeza, tutakweda mimi na ye ye kuangalia nini cha kufanya ili sasa tuvuke hapo mtandaa panya kuelekea kwenye kukimaliza kitu hicho.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Mnyika, swali la mwisho.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, katika majibu yake ya msingi Mheshimiwa Naibu Waziri aliesema kwamba kwa upande wa wilaya mpya, Serikali inatafuta fedha ili iongeze bajeti kwa ajiliya ujenzi. Sasa Wilaya yetu ya Ubungo ni Wilaya mpya na Serikali kuititia Serikali, nguvu za wananchi na Mfuko wa Jimbo, tumejega kituo cha polisi cha wilaya pale Gogoni.

Mheshimiwa Spika, sasa kituo kile cha polisi ni kituo kikubwa, lakini huduma zinakuwa finyu kwa sababu Askari wanatoka maeneo ya mbalimbali sana. Sasa je, Serikali iko tayari, katika kutafuta fedha za ujenzi, itafute vilevile fedha za kujenga nyumba za Askari katika Jimbo la Kibamba karibu na Kituo cha Polisi cha Gogoni?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Kibamba, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimi Eng. Hamad Yusuf Massauni, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naye nimpongeze kwa jitihada zake kama alivyozungumza, kwamba kupitia Mfuko wake wa Jimbo na nguvu za wananchi wameweza kujenga hicho kituo. Nikijibu swali lake ni kwamba, tutakuwa tayari, pale ambapo fedha zikipatikana basi tutashirikiana naye katika kumaliza ujenzi wa nyumba iki kituo hicho kiweze kutumika masaa yote.

**SPIKA:** Ahsante, tuhamie Wizara ya Maji, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga.

Na. 255

**Kukarabati Miundombinu ya maji katika Kata za Jimbo la Igunga**

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU** aliuliza:-

Mwaka 2018 ulikuwa msimu wa mvua nydingi sana zilizosababisha kubomoka kwa mabwawa ya maji kwenye Kata za Kinungu, Nguvumoja, Mwamashimba, Nanga, Bukoko na Mbutu na kuwaacha wananchi wa vijiji zaidi ya 24 bila maji; maeneo haya ni mbuga na hayana maji chini ya ardhi hivyo wananchi hutegemea mabwawa hayo tu. Aidha, Halmashauri ya Igunga haina uwezo wa kifedha kuyakarabati mabwawa hayo mara moja:-

Je, ni kwa nini Serikali isileté mradi mkubwa wa kukarabati miundombinu ya maji katika kata hizo kuwaondolea wananchi hao tabu ya maji?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, tafadhalil!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Jimbo la Igunga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwaka 2018 kulikuwa na mvua nyingi zilizonyesha na kuharibu miundombinu ya malambo katika Kata za Kinungu, Nguvumoja, Mwamashimba, Nanga, Bukoko na Mbutu na kuwaacha wananchi wa vijiji zaidi ya 24 bila ya huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari inaendelea na ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka bomba kuu la KASHWASA kupeleka katika Miji ya Tabora, Igunga, Nzega na Wilaya ya Uyui, ambao unatekelezwa kwa ghamama za dola za Marekani milioni 268.35, fedha ambazo mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India. Katika mradi huo visto vijiji mbalimbali vya Kata Nanga na Mbutu zitapata huduma ya maji kupitia mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kukarabati miundombinu iliyoharibiwa na mvua hizi kwa Kata za Kinungu, Nguvumoja, Mwambashimba na Bukoko kwa kadri fedha zinavyopatikana ili kuhakikisha wananchi hawa wanapata huduma ya maji kama ilivyokuwa awali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dalaly swali la nyongeza, tafadhalil.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana Serikali kwa kutuletea maji kutoka Ziwa

Victoria na kuhakikisha kwamba Kata tano za Nanga, Bukoko, Mwamashiga, Igunga, Mbutu na Itundulu zitapata maji, lakini nipayende kuiuliza Serikali, ni lini sasa Serikali itafikisha maji ya Ziwa Victoria kwenye kata zingine zilizobaki?

Swali la pili, shida ya maji kwenye kata ambazo mabwawa au miundombinu yake iliharibika ni kubwa sana na wananchi wanateseka. Naomna kufahamu, Serikali *in-commitment* gani juu ya kukarabati miundombinu hii kwa sababu majibu ya Naibu Waziri yanaonekana ni ya jumla. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante, majibu ya maswali hayo ya wananchi wa Igunga, Mheshimiwa Naibu Waziri maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, tafadhal!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana, lakini kikubwa sisi kama Serikali kutoekana na changamoto hii ya maji, tumeona haja ya kutumia zaidi ya bilioni 600 katika kuhakikisha tutatatuoa tatizo la maji katika Wilaya ya Igunga, Nzega pamoja na Tabora. Lakini ametaka mkakati ni lini tunakwenda kukamilisha? Mradi ule unatakiwa ukamilike mwaka 2020, Mheshimiwa Waziri ametoa agizo pindi itakapofika mwezi huu wa tisa mradi uwe umekamilika na wananchi waweze kupata huduma ya maji na sisi tutalismamia hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu swali lake la pili, kuhusu suala la fedha za ukarabati. Katika Bunge lako Tukufu, tarehe sita mwezi huu, tuliiidhinishiwa zaidi ya bilioni 610 katika kuhakikisha tunatekeleza miradi ya maji, lakini katika Jimbo la Igunga tumetenga zaidi ya bilioni moja. Nimuombe sana na watalamu wetu wa Igunga waone haja sasa hizi fedha ziwe kipaumbele katika kuhakikisha zinatumika katika kukarabati miundombinu hiyo na wananchi waweze kupata huduma muhimu ya maji.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza, wakandarasi wengi wanaofanya shughuli za miradi ya maji kwenye Wilaya ya Tanganyika, Mradi wa Kamjela, Kabungu, Ifukutwa na Mhese, asilimia kubwa hawajalipwa fedha zao. Je, ni lini Serikali itawalipa fedha hizo kwa ajili ya kukamilisha hiyo miradi.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, nikubaliane naye kwanza, ni kweli tulikuwa na madeni takribani zaidi ya bilioni 88, lakini kama unavyotambua, utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha, umepata fedha hizo zaidi ya bilioni 88 katika kuhakikisha tunawalipa wakandarasi, na hata hivyo pia tumepata bilioni 12.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie hata wewe katika Jimbo lako la Kongwa wakandarasi wako sasa tumekwishawalipa. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge baada ya saa saba tukutane ili tuweze ku-*crosscheck* ile taarifa na ye ye katika wakandarsi wake katika kuhakikisha tunawalipa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, tuendelee na swali linalofuata Waheshimiwa Wabunge, bado tuko Wizara hii hii ya Maji, litaulizwa na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, Mheshimiwa Kitandula tafadhali.

Na. 256

### **Mradi wa Maji Toka Mto Zigi**

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA** aliuliza:-

Je, ni lini mradi wa maji kutoka chanzo cha Mto Zigi kwenda Mkinga na Horohoro utaanza?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la siku nyingi, lililojirudiarudia sana, karibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Jimbo la Mkinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza maandalizi ya mpango wa utekelezaji wa mradi wa kutoa maji Mto Zigi kwenye mji wa Kasera ambaao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga, pamoja na Mji wa mpakani wa Horohoro. Kwa sasa taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasa zabuni zinaendelea. Matarajio ni Mtaalam Mshauri atakayepatikana atakamilisha kazi hilo mwezi Septemba, 2019. Ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza baada ya kukamilika kwa usanifu.

Mheshimiwa Spika, wakati tunasubiri usanifu wa mradi wa kutoa maji Mto Zigi kukamilika, Serikali imeandaa mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji kwa mpango wa muda mfupi katika Mji wa Horohoro kwa gharama ya kiasi cha shilingi milioni 595. Kazi zitakazotekelawa ni ulazaji wa bomba, ujenzi wa mtambo mdogo wa kusafisha na kutibu maji, ukarabati wa tanki la maji na ujenzi wa vituo vitano vya kuchotea maji. Mradi huo unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2019 na kukamilika baada ya miezi sita.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dunstan Kitandula nimekuona, uliza swali la nyongeza.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, na kama ulivyosema, ni kweli kwamba swali hili ni la muda mrefu. Kwa kuwa wananchi wa Mkinga wanazo taarifa kwamba mtaalam huyu

amekwishapatikana tangu mwezi Novemba, na ilikuwa waingie mikataba lakini yakawa yanafanyika majadiliano yallyokuwa na lengo la kupunguza scope ya kazi kwa vijiji vile 37, jambo ambalo limeleta tataruki. Je, Waziri yuko tayari kutuhakikishia kwamba hayo majadiliano hayatapunguza wigo ambao utawahakikishia wananchi wa Mkinga vijiji vile 37 vyote vipate maji? (*Makofii*)

Swali la pili, kwa kuwa mradi wa Horohoro umepigisha kelele sana kwa muda mrefu na sasa unakwenda kutimia, kutekelezwa, na mwezi wa sita sio mbali. Je, Waziri yupo tayari mwezi wa sita utakapofika atoe ahadi kwamba ataandamana na mimi kwenda kuweka msingi wa kuanza ujenzi wa mradi ule kwa wakati?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhalii!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kiukweli nitumia nafasi hii, dhati ya moyo wangu kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, amekuwa mfuatiliaji mkubwa sana si kuchangia tu Bungeni lakini hata ofisini amekuwa akija mara kwa mara kuhusu suala zima la mradi huo.

Mheshimiwa Spika, sisi kama viongozi wa Wizara tulikwishesema kwamba hatutakuwa kikwazo kwenye utekelezaji wa miradi ya maji. Wakati mwagine tunatumia muda mrefu sana kwa kuwatumia wakandarasi wetu, sisi kama viongozi tumejadiliana tumeona haja sasa kazi zile zifanywe na wataalam wetu wa ndani ili kuhakikisha kwamba hii kazi inafanyika kwa haraka na wananchi wake waweze kupata maji safi na salama katika kuhakikisha kwamba tunamtua mama ndoo kichwani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Nyanhwale, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, nimekuona.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa

wakandarasi wa Wilaya ya Nyang'wale wamekuwa wakiuchezza ule mradi na kuchukua muda mrefu na fedha ya Serikali kupotena na juzi Mheshimiwa Naibu Waziri umefanya ziara ukajjonea mwenyewe. Je, Serikali inawachukulia hatua gani ya haraka hao wakandarasi.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Jumaa Hamidu Aweso, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, nipende kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ambayo nimejionea mimi kwa macho nilipoenda hapo Nyang'wale, lakini kikubwa tulikuwa tunatabua kabisa na Waheshimiwa Wabunge wamelalamika sana, hususan utekelezaji wa miradi ya maji vijiji, imekuwa na changamoto kubwa sana na ndiyo maana sisi kama Wizara ya Maji tukaleta Muswada wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na Wakala wa Maji Vijiji.

Mheshimiwa Spika, tunalishukuru Bunge lako Tukufu kwamba limetupitishia haraka na Mheshimiwa Rais ameshatusainia ule Muswada na sasa ni Sheria. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Viongozi wa Wizara ya Maji, hakutokuwa na Mkandarasi ambaye atashindana na sisi, sisi tumejipanga vizuri, mkandarasi yeoyote mbabaishaji ama awe mtalaam, kwa maana ya Mhandisi wa Maji, tutamchukulia hatua haraka iwezekanavyo katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma hii muhimu ya maji.

**SPIKA:** Ahsante sana, nilikuona Mheshimiwa Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Swali lililoulizwa namba 256 linafanana kabisa na changamoto iliyopo Wilaya ya Ngara katika mradi wa Muhweza, ni mionganoni mwa vijiji 10, lakini mradi huu umechukua muda mrefu sana bila kukamilika. Je, ni lini mradi huu utakamilika ili kuwatua ndoo kina mama?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, dada yangu Mheshimiwa Oliver amekuwa mpambanaji mahili katika kuhalikisha kuwapigania wananchi wa Kagera ili waweze kupata huduma hii muhimu ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini, kutokana na swali lake nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge, nimelipokea na nilifuatilie kwa haraka na tuweze kuongeza nguzu zetu ili mradi huo uweze kukamilika na wananchi waweze kupata huduma hii muhimu.

**SPIKA:** Ahsante, bado tuko Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Ndassa, tafadhali uliza swali lako, Mbunge wa Sumve.

Na. 257

#### **Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria hadi Malampaka**

**MHE. RICHARD M. NDASSA** aliuliza:-

Mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Miji ya Sumve, Malya hadi Malampaka ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ambao usanifu wake umeshakamilika.

Je, ni lini mradi huo utatekelezwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, bado tupo kwenye Wizara yako, tafadhali!

#### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Jimbo la Sumve kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Miji ya Sumve, Malya na Malampaka ni ahadi ya Mheshimiwa Rais katika Awamu ya Nhe. Tayari Wizara ya Maji kuitia mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza ilinza mchakato wa kufanya upimaji ili kujua ni eneo gani lipo karibu kutoka Ziwa Victoria, ili iwe rahisi kufikisha maji kwenye miji hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina ili kuanza na maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa maji katika miji hiyo baada ya gharama halisi kufahamika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndassa, uliza swali lako tafadhalii.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, swali hili limekuwa likijirudiarudia kama ulivyo sema, lakini nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, na najua Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali sikivu, najua itatekeleza hili kwa sababu ni ahadi yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali langu, kwa sababu wakati wa kuhitimisha bajeti ya Wizara ya Maji, ilituomba sisi Waheshimiwa Wabunge kwa sababu miradi hii mikubwa inachukua muda mrefu, ikatuomba tulete orodha ya pampu au visima vilivyoharibika ambavyo havitoi maji na mimi kama Mbunge wa Jimbo la Sumve nimeshafanya hivyo, nimekuletea Mheshimiwa Waziri. Lini sasa miradi hii midogomidogo ya maji itakamilika na kutekelezwa? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, la Senator Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, nipende kwa dhati ya moyo kumpongeza Mheshimiwa mkongwe mahili katika kuhakikisha kwamba anapigania wananchi wake katika Jimbo la Sumve. Lakini pia amekuwa funzo kwa hasa hususan kwa sisi viongozi vijana tumekuwa tukijifunza mambo mengi sana katika

ujengaji wake wa hoja na hata katika suala zima la ufuatiliaji wa mambo mbalimbali yanayohusiana na maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, nataka nimuhakikishie Mhehsimiwa Mbunge, Mheshimiwa Waziri alishatoa agizo kwa maana ya Waheshimiwa Wabunge waliohitaji vizima ama ukarabati walete orodha ile kwa haraka, mionganii mwa Wabunge walioleta haraka ni Mheshimiwa Ndassa, nataka nikuhakikishie kwa uharaka ulioufanya na sisi kama viongozi wa Wizara tutalifanya kwa jithhada kwa haraka ili tuweze kumchimbia visima katika kupunguza shida ya maji katika Jimbo lake, ahsante.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Amina Makilagi tafadhali uliza swali lako.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali yetu ya chama cha Mapinduzi kujenga mradi mkubwa wa maji na kufikia kiwango cha asilimia 90 wananchi wanapata maji. Pamoja na mipango iliyopo ya kupeleka maji Mji wa Mgumu, Mji wa Rarya na Mji wa Tarime na Mganga Kiabakari Butiama, Mkoa wa Mara bado unazungukwa na ziwa lakini changamoto ya maji ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua Serikali imejipangaje kuhakikisha Mkao wa Mara katika Vijiji vyote vya Mkao wetu ambavyo vinazungukwa na ziwa za Victoria vinapelekewa maji, safi na salama? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, maji Mkao wa Mara tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimimiwa Spika, nipende kumpongeza Mheshimiwa Mbunge mama yangu mama Kilagi kwa kazi kubwa anayoifanya kuwapigania wakinamama wa Mara si mara

moja na wala si mara mbili na amewekuwa mfuatiliaji mkubwa sana hususani katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara kwa kutambua changamoto hii ya maji tumetenga fedha au tulizopewa na Mheshimiwa takribani dola milioni 500 katika kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la maji zaidi ya Miji 28 na tumesha saini mkataba. Nataka nimuhakikishie katika Miji ya Mgumu pamoja na Tarime ile kazi inaenda kufanyanyika kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine tunaenda kusaini sasa wa mkaba wa kupeleka maji Mganga Kiabakari Butiana katika kuhakikisha tuna tatu tatizo hili la maji. Kazi hizi tutazifanya kwa haraka pia bajeti yako umetuidhinishia wizara yetu ya Maji zaidi ya bilioni 610 katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji. Nataka nimuhakikishie sisi kama viongozi kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge tutafanya kila linalowezekana katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji katika Mkoa wa Mara. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante kwa sababu ya muda Waheshimiwa tuendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, swali linauliza na Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani, tafadhali Mbunge wa Tunduru Kaskazini uliza swali lako.

Na.258

### **Ikama ya Wataalam wa Ardhi Tunduru**

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI** aliuliza:-

(a) Je Ikama ya Wataalam wa Ardhi Katika Halmashauri za Wilaya ni ipi na ni lini Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru itafikia kiwango hicho?

(b) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kurudisha eneo la Hekari takribani 2,000 za Shamba Pori la Nambarapi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ili nayo

irejeshe ardhi kwa Wananchi wa Vijiji husika kikiwemo Kijiji cha Nambarapi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi, Mheshimiwa Angelina Sylvester Mabula tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer Ramo Makani Mbunge* wa Tunduru Kaskazini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimimiwa Spika, kwa mujibu wa viwango vyatia utendaji ya mwaka 2015, ikama ya Wataalam wa ardhi katika Halmashauri za Wilaya Maafisa Ardhi watatu, wanatakiwa Wapima Ardhi watatu, Maafisa Mipangomiji watatu, Wathamini watatu na Mafundi Sanifu Upimaji pamoja na Maafisa Ardhi Wasaidizi wanne. Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kwa sasa ina watumishi wanne katika Sekta ambao ni Maafisa Mipangomiji wawili, Mpima Ardhi mmoja na Afisa Ardhi Msaidizi mmoja. Serikali inaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya watumishi wa Sekta ya Ardhi ili kufikia kiwango kinachohitajika na hivyo kuongeza ufanisi. Aidha, Wizara itawapanga upya watumishi wa Sekta ya Ardhi ili kuwa na uwiano wenye tija.

Mheshimimiwa Spika, sehemu ya (b) ya swali lake shamba hili linatambuliwa kama "Shamba Namba 69 Nambarapi" na lina ukubwa wa hekta 774 ambazo ni sawa sawa na (ekari 1,913). Mwaka 2003 kulianza kujitokeza migogoro wa kugombea ardhi ya shamba hili hali iliyosababisha kufunguliwa kwa Shauri namba 03 la mwaka 2016 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Tunduru. Shauri hili lilikuwa kati ya *TAMCU Ltd* dhidi ya wananchi wanne (Hassan Mussa Ismaili, Ismail Mussa Ismail, Sophia Mussa Ismail na Said M. Ndeleko. Katika Shauri hili Chama cha Ushirika Wilaya ya Tunduru kilipata ushindi. Pamoja na ushindi wa *TAMCU Ltd*, wananchi wa kijiji cha Nambarapi waliomba

ardhi katika shamba hilo kwa TAMCU ambapo ekari 1,000 zilimegwa na Mrajisi wa Vyama vyatia Ushirika na kugawa kwa wananchi. Hivyo, sehemu ya shamba iliyobaki ni mali ya chama cha Ushirika Wilaya ya Tunduru yaani (*TAMCU Ltd*).

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer Ramo Makani* ameridhika, tunaendelea Mheshimiwa Injinia.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimimiwa Spika, nakushukuru, napongeza pia kwa majibu mazuri ya Serikali, hata hivyo nina maswali ya nyongeza mawili, swali la kwanza kuhusiana na kipengele (a) cha swali langu ili wataalam waweze kufanya kazi zao vizuri na watoe matokeo yanayostaili wanapaswa kutosha kwa idadi, pia wanapaswa kutosha kwa umahili wao yaani vile *competence* ya utaalam aliyonayo, pia wawe na maadili ya kitaaluma. Bila shaka ni ukweli kwamba wakiwa wachache hawawezi kukamilisha matakwa hayo.

Je, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru inaupungufu wa wataalam wa Sekta ya Ardhi, kwa zaidi ya asilimia 81 na kwa kuwa Serikali ina mpango wa muda mrefu wa kuendelea kutumia bajeti ya kila mwaka. Je katika mpango wa muda mfupi ambao ni wa kuwapanga upya watumishi katika nchi nzima Serikali iko tayari kuweka upendeleo maalum kwa halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kwa sababu ya changamoto zilizopo hivi sasa?

Mheshimimiwa Spika, swali la pili katika kipengele (b) cha swali langu naona hapa kuna haja ya kupambanua iko shida ya kupata ukweli na uhakika, familia ya watu wanne inayotanjwa inamiki sehemu ndogo sana ya hili eneo ni kama eka 40 tu katika zile eka 1,913, eneo kubwa zima linalalamikiwa na halmashauri ya Kijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata kesi inayotajwa siyo kesi ambayo inahusika mahali hapa sasa mimi nafikiri wakati tunaendelea kusubiri kupata uhakika juu ya umiliki wa eneo hili na hapa nitatoa ushauri kwa ufupi. Kwa nini tusiendane na maagizo ya Serikali maagizo ya Chama cha Mapinduzi

kupitia ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo kwa kujibu wa Ibara ya 37 inasema Serikali inatakiwa kutekeleza maagizo ya Chama cha Mapinduzi kupitia ilani yake kwamba ni lazima kufanya uhakiki wa mashambaporu yasiyoendelezwa kwa kipindi kirefu na kuyagawa upya kwa wananchi. Sasa eneo hili la eka 2,000 kwa zaidi ya miaka 20 limebaki tu likiwa halifanyiwi kazi...

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Injinia sasa swali.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimimiwa Spika, je Serikali iko tayari sasa kuunda timu maalum kwenda kufuatilia jambo hili kwa nini linachukua miaka mingi bila kupatiwa ufumbuzi huku eneo hili likiwa likitumika kienyeji na baadhi ya watu ikiwa ni pamoja na kuwafanya wananchi walime kwenye eneo hilo katika sehemu ndogo na kuwatoza mazao yanayolimwa katika eneo hilo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi, Mheshimiwa Angelina Sylvester Mabula tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimimiwa Spika, kwanza nikiri wazi kwamba kuna upungufu mkubwa kwa nchi nzima kwa watumishi wa Sekta ya Ardhi. Ukiangalia takwimu za mahitaji tulionayo tunatakiwa kuwa na watumishi 2,957 kwa nchi nzima; lakini mpaka sasa tunao 1,546 na hivyo tuna upungufu wa 1,411. Kwa hali hiyo upungufu uko maeneo mengi na kwa Mheshimiwa *Engineer* Ramo anao watumishi wanne ni kweli ni wachache, lakini kuna halmashauri inawatumishi wawili na nyingine tuliwhali kukuta ina mmoja. Nimuombe tu awe mvumilifu na Waheshimiwa Wabunge wote kwa sababu zoezi hili tumesema tunalipitia upya kwa kuangalia wale tulionao kwa sasa tunaanza kuwapanga upya ili kuweza kuleta uwiano wa kiutendaji katika halmashauri zetu.

Mheshimimiwa Spika, kwa hiyo, nimuombe sana pamoja na kuomba upendeleo nadhani tutaangalia wakati tunapanga tuweze kuona hasa maeneo ya pembezoni

ambapo mara nyingi watumishi wengi wanakwepa kwenda kule. Kwa hiyo, tutaangalia na kuwapa umuhimu wale ambaao tunajua wanayo shida kubwa katika Sekta hii ya Ardhi.

Mheshimimiwa Spika, jambo la pili swalilake la pili amezungumzia kwamba ile kesi pengine ni ya watu wanenai ni tofauti na suala la wanakijiji. Kesi ile imewekwa kwenye jibu la msingi kwa sababu ndiyo hasa ilikuwa imekwambisha katika mambo yote kufanyika pale, na wale walipofungua kesi maana yake hata Kijiji kisingeweza kufanya jambo lolote kwa sababu eneo lilitokuwa linagombewa ni hilo la Kijiji.

Mheshimiwa Spika, lakini tumeshaona hitaji la eneo lile kwamba wananchi wanalamika na bahati nzuri nakumbuka kama siyo mwaka jana nadhani mwaka juzi nilikwenda pale nikafika mpaka kwenye Kijiji nikafika kile killo cha wananchi. Kama Serikali tuliahidi kwamba tutalifanya kazi na baada ya kukuta kuna kesi na maamuzi yalikuwepo tukawa tumefungwa mikono hatukuweza kufanya ile. Lakini kwa sababu pia kuna agizo la Serikali la kuitia mashamba pori yote na kuweza kuyaleta maelekezo yake kwa maana ya kuleta maepndekezo kwa Mheshimiwa Waziri ili yawewe kufutwa jukumu la kufanya hivyo ni la Halmashauri yenye we ya Tunduru, ikisha fanya hivyo pamoja na halmashauri zingine chanzo lazima kianzie kwenye halmashauri husika ndipo wizara itaendeleo.

Mheshimimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe rai kwa mara nyingine tena kwamba suala hili linahitaji kuanzia katika halmashauri zetu mkileta kwa Waziri, Waziri atamshauri Mheshimiwa Rais kuyafuta pale ambapo tunakuwa tumejiridhisha. Na nitoe rai ni marufuku kwa Serikali yoyote ya Kijiji au kwa watu wote wachache kutumia ardhi ya Umma katika kuwafanya watu kuwa kama vibarua kwa sababu unapompa mtu ardhi na kumtoza pesa maana yake wewe tayari umeshakuwa bepari wa kutaka kunyonya wengine. Ni marufuku na kama kuna maeneo watu wanatozwa pesa kwa matumizi ya ardhi kwa maeneo ambayo wameshindwa

kuyaendeleza wenyewe tupate taarifa ili tuweze kuyafanyia kazi.

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda tuendelee na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia swali litauliza na Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mheshimiwa Victor tafadhali.

Na.259

### **Ujenzi wa Chuo cha Veta Chunya**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Chunya ni moja kati ya Wilaya 10 nchini zilizopangiwa kujengewa Chuo cha VETA mwaka 2013.

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo hicho?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya, kwa niaba ya tafadhali.

### **NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-**

Mheshimimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Mwambalaswa Mbunge wa Lupa kama ifuatavyo:-

Mheshimimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Elimu ya Ufundu na Maafunzo ya Ufundu Stadi katika kufikia azma ya Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Katika kutekeleza azma hiyo Serikali ina mkakati wa kuwa na Vyuo vya Ufundu Stadi katika kila Mkoa na Wilaya hapa nchini. Ujenzi huu unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango huu wa ujenzi wa Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi

nchini, Wilaya ya Chunya ni moja kati ya Wilaya za kipaumbele zilizopo kwenye mpango wa ujenzi.

Mheshimimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 40 kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundistiadi kwa Wilaya 25 ikiwemo Chuo cha Ufundistiadi cha Wilaya ya Chunya. Kila chuo kimetengewa kiasi cha shilingi bilioni 1.5

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwambalaswa swali la nyongeza.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimimiwa Spika, nakushuru sana na pia naishukuru Serikali kwa majibu mazuri sana ambayo yanawapa matumaini wananchi wa Wilaya ya Chunya. Halmashauri ya Wilaya Chunya imetenga eneo la eka 10 kwenye Kata ya Mbugani kwa ajili ya chuo hicho.

Je, Mheshimiwa Waziri sasa kwa pamoja na majibu mazuri aliyoniambia Serikali iko tayari kupeleka pesa hiyo bilioni 1.5 kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ili ujenzi uanze katika mwaka huu wa fedha ambao tunaanza? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Eng. Stella Manyanya tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimimiwa Spika, kwanza napenda kuipongeza Halmashauri ya Chunya kwa kutenga eneo hilo, vilevile niipongeze Serikali kwa jinsi ambavyo imendelea kuimarisha, miundombinu ya barabara na maji ambayo sasa itawezesha eneo hilo kuzidi kulifanya kuwa rafiki kwa ujenzi wa chuo hicho. Niseme tu kwamba kama ambavyo nimesema katika jibu la msingi ni kwamba kwa sababu fedha hizo zimeshatengwa muda utakapofikia zitapelekwa mara moja ili ujenzi uweze kuanza.

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge tuendelee, bado tuko Wizara hiyo hiyo ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega Mbunge wa Viti Maalum kwa niaba yake muulizie.

Na. 260

**Walimu Wenye Weledi Juu ya Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MHE. GRACE V. TENDEGA)** aliuliza:-

Walimu wenye weledi wa kuwafundisha Watu Wenye Ulemavu ni wachache sana nchini.

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha Walimu hao ni wa kutosha?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Injinia Stella Manyanya tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA)** alijibu:-

Mheshimimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Grace Victor Tendega Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa Walimu wenye taaluma ya Elimu Maalum. Changamoto hii ina sababishwa na ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu kutokana na mabadiliko chanya ya kimtaalamo na uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa elimu kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimimiwa Spika, mahitaji ya Walimu wa Elimu Maalum nchini ni Walimu 8,882 katika shule maalum na vitengo vinavyopokea wanafunzi wenye mahitaji maalum 706. Hadi kufikia Disemba 2018 Walimu 5,556 wenye taalum ya Elimu Maalum ngazi za Astashahada, Stashahada na

Shahada walihitimu katika Vyuo mbalimbali nchini vikiwemo Chuo cha Ualimu Patandi na Chuo Kikuu Dodoma.

Mheshimimiwa Spika, Serikali imekamilika upanuzi wa Chuo cha Ualimu Patandi ili kuklongezea uwezo wa kudahili. Pia Chuo kimeanzisha kozi ya Elimu Maalum katika ngazi ya Astashahada kwa Walimu tarajali kwa mwaka wa masomo 2018/2019. Hatua hii itaongeza idadi ya Walimu wanaojunga na mafunzo ya Ualimu wa Elimu Maalum ili kupunguza changamoto ya Walimu wenye taaluma ya Elimu Maalum wanaohitajika nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muuliza swali, uliza swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimimiwa Spika, ahsante, kwanza nipongeze nchi za Scandlnavia zillikuwa zikisaidia sana Serikali yetu kupeleka Walimu wa mahitaji maalum kwa muda wa miaka mingi, swali langu la kwanza.

Je, ni lini Serikali itaongeza nguvu ya kipesa kuweza kuwadahili wanafunzi wengi zaidi watakaosomea mafunzo ya alama?

Mheshimimiwa Spika, swali la pili katika Wilaya ya Rungwe kuna shule ya watu wenye ulemavu ya Katumba ambayo ina miundombinu iliyochakaa kwa muda mrefu na ina Walimu wachache wa lugha za alama pamoja na lugha za watu wenye ulemavu, Serikali itatia jitihada gani kuweza kusaidia shule hii ya Katumba kupata mahitaji hayo? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Injinia Manyanya tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimimiwa Spika, ni kwamba suala la watu Wenye Ulemavu ni muhimu sana na Serikali inatambua na kulipa

kipaumbele. Katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na wanafunzi wengi wanaoweza kujifunza lugha ya alama kwa sababu haitoshi tu kila mtu kuongea anavyoolewa ni vizuri kukawa na lugha ambayo kwa yoyote utakayemkuta anaongea lugha ya alama itakuwa ni hiyo hiyo. Wizara tayari ilishashughulikia na kuna vitabu ambavyo vimeshatayarishwa ambavyo vinaweza kuwafundisha watu wengi tukiacha wanafunzi hawa wazazi waweze kuifahamu lugha ya alama.

Mheshimimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuwezeshwa suala hilo. Na kwa upande wa shule ambayo imezungumzwa ya Katumba niseme tu kwamba kwa suala la Watu Wenye Ulemavu hilo ni suala muhimu kwa sababu Tanzania inahitaji kuona kwamba wananchi wote wanafaidika na elimu, iwe mlemavu, iwe asiye mlemavu. Kwa misingi hiyo nikuombe tu Mheshimiwa nitaona kwamba kuna umuhimu wa kutembelea shule hiyo ili iweze kusaidiwa inavyotakiwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa kwa sababu ya muda nawaona kabisa lakini mtaona muda wetu ulivyo, tupate swalii la mwisho, linaloelekezwa Naibu Waziri, linaloelekezwa Wizara ya Nishati litaulizwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Anatropia tafadhalii.

Na.261

### **Bei ya Megawati Moja ya Umeme**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Je, Megawati moja ya umeme inazalishwa kwa bei gani na inauzwa kwa bei gani (*unit cost*)?

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wa Viwanda, na Biashara, Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y.  
WAZIRI WA NISHATI)** aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme Nchini, inagharamia uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme hadi kwa mteja kwa kuweka miundombinu husika ya umeme. Kwa sasa gharama ya kuzalisha uniti moja (*Kwh*) ya umeme kwa kutumia chanzo cha maji ni shilingi 36 na gharama ya kuzalisha uniti moja ya umeme kwa kutumia gesi asilia ni wastani wa shilingi 150. Gharama ya kuzalisha uniti moja kwa mitambo inayotumia mafuta ya dizeli katika maeneo yaliyopo nje ya Gridi ya Taifa ni shilingi 720 kwa uniti moja yaani *Kwh* moja.

Mheshimiwa Spika, bei ya kuuza umeme inatokana pia na gharama za kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme. Kwa sasa bei ya kuuza umeme ni wastani wa shilingi 242 kwa uniti yaani *Kwh*.

**SPIKA:** Haya, ulishapata bei ya umeme. Uliza swali lako Mheshimiwa.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Wanaozalisha umeme ni *TANESCO* na wanaopanga bei ya kuuza umeme ni *EWURA*. Kwa muda mrefu *TANESCO* imekuwa haipati faida, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita ni mwaka 2008 na mwaka 2014 waliweza kuzalisha bila hasara.

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka kuwa inatoa ruzuku ya upungufu wa gharama katika uzalishaji wa umeme pale ambapo *TANESCO* wanakuwa hawapati faida kutokana na mauzo yao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wanunuzi wa umeme wanaoomba kuunganishiwa umeme wakati mwingine hulazimika kununua nguzo na pale maeneo ambako mpango wa Serikali haujaanza, wamekuwa wakitumia

kuanzia 500,000 mpaka milioni kununua nguzo lakini nguzo zinabaki kuwa mali ya *TANESCO*.

Kwa nini wale wanaojinunulia nguzo na kuunganishwa wasiwe wanapewa *units* za umeme sambamba na ile gharama walijotumia kununua nguzo ambazo ni mali ya *TANESCO?* (*Makof!*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia, hili swalii la pili ni muhimu kwelikweli. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kimsingi Shirika la Umeme *TANESCO* ni Shirika la Serikali na kwa kweli kwa mara nydingi sana ingekuwa limeachiwa lijiendeshe lenyewe bila kusalidwa kabisa na Serikali labda sasa hivi lingekuwa limefungwa. Lakini kwa kutambua kwamba hilo ni shirika pekee ambalo pia linachochea uchumi katika nchi yetu kwa maendeleo ya Watanzania kwa ujumla, Serikali lenyewe imekuwa pia ikitoa fedha kwa ajili ya kulisaidia shirika hili pamoja na misaada mbalimbali ikiwemo ya kuanzisha vituo vya kuzalishia umeme, kurekebisha mifumo kwa mfano kujenga *line* ya msongo wa kv 400 ambaao unatoa Iringa mpaka kwenda Mwanza, na sasa hivi unategemea tena kujengwa mwingine wa kv 400 kutoka Iringa mpaka Mbeya, Tunduma, Sumbawanga, Mpanda, Kigoma ambayo ni 400 na kutoka pale kv 220 kwenda mpaka Nyakanazi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuanzisha uzalishaji katika maporomoko ya maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika swalii la pili kuhusiana na kwa nini mwananchi anapokuwa amelipishwa nguzo hiyo nguzo inatakiwa iwe ni mali ya *TANESCO*; sio nguzo tu, hata transfoma, akifungiwa transfoma ambalo amelinunua mwenyewe bado anashauriwa kuwa ni mali ya *TANESCO*. Kuna faida kubwa sana kwa kufanya hivyo kwa sababu nguzo ikishakuwa imejengwa pale utatumia lakini ikitokea imeoza kama umeshairejesha kuwa ni mali ya *TANESCO*

inakusaidia kwamba hata wewe usiweze tena kununua nguzo, ile kazi ya ukarabati inafanyika na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hivyo tu, pale nguzo inapokuwa imefika maeneo hayo inawezesha pia kumfanya mwananchi mwingine aweze kuunganishiwa ikizingatiwa kwamba hatuwezi kuweka nguzo nyingi katika mtaa mmoja. Ile ile *line* moja inayokuwa imenda inasaidia na hata hivyo hizo bei zinakuwa siyo bei kamili, zinakuwa zimezingatia sana kumfanya mwananchi aweze kununua kwa bei anayoimudu.

**SPIKA:** Mtaona Waheshimiwa muda wetu, na leo mambo ya muda yanatupa shida hapa kidogo kuyamanage kwa hiyo tushirikiane, tumalizie hapo.

Wageni tulionao hapa Jukwaa la Spika, tuna wageni 55 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambao ni wanachama wa Chama cha Wanafunzi wanaosoma Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma (*DUPSA*) wakiongozwa na Mwenyekiti wa *DUPSA* ndugu Juma Romala na Katibu wa *DUPSA* ndugu Yohana Emmanuel, karibuni sana *DUPSA*, ninyi mnasoma Sayansi ya Siasa na hapa ndiyo Chuo Kikuu cha Sayansi ya Siasa hapa ndani ya Bunge, kwa hiyo, karibuni sana vijana wetu. (*Makof!*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, mgeni wa Mheshimiwa Omary Mgumba, Naibu Waziri wa Kilimo, ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Wilaya ya Morogoro Vijijiini, ndugu Bohari Magunda; karibu Bohari, yule pale. (*Makof!*)

Mgeni wa Mheshimiwa Julius Kalanga ambaye ni Katibu wa CCM wa Wilaya ya Monduli, ndugu Langael Akyoo; karibu Katibu, yule pale. (*Makof!*)

Wageni 18 wa Mheshimiwa Dkt. Dalali Kafumu ambao ni Makatibu Kata wa CCM kutoka Jimbo la Igunga, Mkoa wa Tabora wakiongozwa na ndugu Salum Mpaki; Makatibu wa CCM wa Kata wa Iguga, karibuni sana, wanapendeza hawa, mko vizuri maana yake, karibuni sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Waziri wa Maliasili na Utalii, anaomba niwatangazie kwamba leo, tarehe 20, Mei, Waziri wa Maliasili na Utalii anawaalika Waheshimiwa Wabunge wote kwenye futari ya pamoja kwenye makazi ya Waziri huyo yaliyoko *Area D*, Eneo la Sengia, Mtaa wa Kyando, nyumba inayotazamana na Ofisi ya Waziri wa Afya.

Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla anawaomba mfike kwenye futari pale *Area D*, Mtaa wa Sengia kwa futari, na mimi nitakuwepo pamoja nanyi Waheshimiwa. Karibuni sana kwenye futari ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla Waheshimiwa Wabunge kuanzia saa 12 kamili na kuendelea, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, juzi, Jumamosi, tarehe 18 nadhani, tuliwawakilisha kwenye shughuli maalum ya uhuisho wa historia ya *Paramount Chief* Daudi Solomona Mazengo Chalula ambaye alikuwa Chifu wa Wagogo, Makao yake Makuu yalikuwa kule Mvumi, kwa hiyo tulikuwa kule. Tulijifunza vitu vingi, kumbe mambo ya machifu yanapoteapotea lakini ni vizuri kuyakumbuka wakati mwingine.

Moja ya vitu ambavyo tulijifunza kule, moja katika vingi ni kwamba kuna wakati kulitokea shida kidogo kwenye utawala wa Chifu Mkwawa kule Iringa ikabidi chifu akimbie, kulikuwa na kama mapinduzi fulani hivi, na akakimbilia kwa Chifu Mazengo ambapo aliihi pale na alipewa na mke, binti wa Kigogo, basi akaishi pale, baadaye Chifu Mazengo akafanya taratibu akafanya usuluhishi kule nyumbani na wakaweza kumrudisha Chifu Mkwawa na akaendelea na utawala wake hadi mnavyojua historia ilivyoenda. (*Makofi*)

Kwa hiyo wajomba zetu Wahehe mna deni bado, sisi tulitoa dada sasa ninyi bado hamjarekebisha ili kuweka sawasawa. Kwa hiyo, historia hizi zinatusaidia sana. (*Makofi/ Kicheko*)

Nashukuru sana, naomba tuendelee kwa sababu ya muda, mambo ni mengi sana hapa Mezani; Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka  
wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Kilimo**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa tunaenda na uchangiaji. Wachangiaji wa CCM wote ni dakika tano na wengine ntawatajia dakika zenu kwa sababu mpo wengi hapa kufuatana na dakika zenu ambazo mmejiwekea.

Tunaanza na Mheshimiwa Nape Nauye, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Umbulla, dakika tano tano, tafadhalii *straight to the point*.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye mapendekezo haya ya Bajeti ya Kilimo. Bahati mbaya sana ni dakika tano na mambo ni mengi kidogo, lakini niwapongeze Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya, Waziri na Manaibu wake, wanafanya kazi nzuri. Ninaamini kwamba mazonge yaliyopo kwenye Wizara ya Kilimo mengi wameyakuta kwa hiyo pengine hayawahu sana isipokuwa wanao wajibu sasa wa kurekebisha tunapotokea hapa kwenda mbele pengine wafanye kazi ile ambayo inakusudiwa. Mengi kwa kweli siyo ya kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ambalo ninataka kushauri Sekta hii ya Kilimo inachukua watu wengi sana lakini bahati mbaya sana ukialinganisha na Makubaliano kwa mfano ya Malabo ya asilimia kumi, sisi bado tuko kwenye *average* ya asilimia 1.2. Nadhani kama lengo letu ni kupambana na umaskini wa watu wengi kwa wakati mmoja, basi lazima tuongeze bajeti kwenye Wizara ya Kilimo, vinginevyo kasi ya kupambana na umaskini itakuwa shida. Kama tunataka kushughulika na

umaskini wa watu wetu lazima tuongeze bajeti maana mtiririko wake kwa kweli ni mbaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, mwaka jana hapa tulifanya mabadiliko madogo kwenye Sheria ya Korosho. Matokeo ya tulichokifanya watu wote tunajua, haihitaji kwenda shule kujua kwamba hali ya tasnia ya korosho sasa hivi ni mbaya sana, ni *almost* iko *ICU*, matatizo ni mengi, mambo ni mengi. Kulikuwa na nia njema ya Serikali, Rais akaweka nia njema, waliokwenda kuitekeleza nia njema ya Rais wamekwenda kugoroga na kuua Sekta ya Korosho.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea, bahati mbaya zoezi lilikumbwa na dhuluma, lilikumbwa na rushwa, lilikumbwa na ubabaishaji mwingi sana na uongo mwingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea Jimbo la Mtama peke yake kwenye vyama vya msingi 11 wakulima ambaao wana korosho chini ya tani 1,500 ambaao wamehakikiwa mashamba yao zaidi ya 1,281 kwa miezi nane toka korosho yao ichukuliwe hawajapata senti tano, 1,281, lakini korosho yao imechukuliwa. Msimu umeanza hawana fedha za kutengeneza mashamba yao, hali ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, sasa mapendekezo yangu; la kwanza; napendekeza tulilete Sheria ya Korosho hapa Bungeni, yote tuipitie upya ili tuokoe zao la korosho. Kile Kipengele tulichokinyofoa kimesumbua sheria nzima, sasa ileteni sheria yote tupitie.

Mheshimiwa Spika, la pili, zoezi hili kwa kuwa lilikumbwa na maneno mengi, mengine ni ya uongo, ninapendekeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aende kukagua atuletee ripoti hapa ndani ya namna zoezi liliwyokwenda ili tuchukue hatua ya kuziba mashimo kwenye yale maeneo ambayo yana shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pendeleko la tatu, kama nilivyosema watekelezaji wa nia njema ya Mheshimiwa Rais

wengi wamekwenda kukoroga mambo. Sasa ni vizuri waliokoroga wawajibike kwa matendo ya kuvuruga tasnia ya korosho. Na hapo ni vizuri tukawa *specific*, si sahihi kuingiza Serikali yote kwenye mambo yaliyofanyika hovyo, watu waliofanya hovyo wanajulikana na kama wasipochukua hatua wenyewe... (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape Nnauye, dakina moja ya kumalizia.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nasema hivi; waliokoroga kwenye jambo la korosho wachukue hatua wenyewe, wasipofanya tutaleta kusudio la kusema jinsi walivyoshiriki mmojammoja na jinsi ambavyo wanapaswa kuchukua hatua kwa sababu waliyoyafanya ni kuhujumu korosho, wananchi, lakini pia wamehujumu uchumi wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo tukiulizana korosho yetu iko wapi, korosho haiwezi kukaa zaidi ya miezi sita hapa nchini ikabaki salama. Mkituambia bado mna korosho sahihi, korosho inayoweza kutumika, huu ni uongo, tukiendelea kusema uongo huu na bado hatuoni aibu tunaendelea kubaki, sio sawa. Ndiyo maana wito wangu, leteni sheria tuipitie upya, CAG aende akakague lakini waliotukoroga wawajibike na msipowajibika tutaleta hoja hapa. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Martha Umbulla, atafuatiwa na Mheshimiwa Benardetha Mushashu, dakika tano tano.

Kwa siku ya leo nikikuita haupo ndiyo imepita hiyo; na kabla hajafuata Mheshimiwa Martha Umbulla kama yupo, niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Maadili mkutane katika ukumbi wenu ule wa kawaida ili sasa rasmi kumhoji Mheshimiwa Stephen Masele ambaye tayari ameshawasili aweze kujieleza kwenye Kamati yenu kama utaratibusi ulivyo.

Tunaendelea, kama Mheshimiwa Martha hayupo tunaendelea na mwininge; Mheshimiwa Benardetha, kama hayupo nashukuru wanankombelea muda hawa; Mheshimiwa Salum Rehani.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, ahsante...

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha yupo?

Mheshimiwa Benardetha, tafadhali ongea nikuita tu, dakika zetu leo ni chache yaani, kila mtu acae...

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wote wawili kwa hotuba nzuri, lakini nawapongeza hasa kwa kuleta mpango wa bima ya mazao. Hii ndio itakuwa mkombozi wa mkulima kwa sababu kukiwa na majanga ya ukame, mafuriko au mashamba yakavamiwa na wadudu kama viwavi jeshi mkulima akapata hasara, hasara hii itaweza kulipiwa na hii bima ya mazao. Nawapongeza sana kwa huo mpango.

Mheshimiwa Spika, msimu uliopta Mkoo wa Kagera tulipata changamoto kubwa sana katika kuuza kahawa. Wakulima waliuza kahawa lakini hawakulipwa malipo yao, lakini na malipo yaliyotolewa ya awali yakawa madogo sana, shilingi 1,000. Ikambidi Waziri Mkoo atoke hapa aje Mkoo wa Kagera akaongea na wakulima, vyama vya msingi, vyama vikuu vya ushirika, viongozi wa Serikali, wafanyabiashara, lakini vilevile akaweza kuhakikisha kwamba wakulima wameanza kulipwa; namshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nampongeza Mkoo wa Mkoo wa Kagera, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Marko Gaguti, wakuu wa wilaya, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika wa Mkoo ambao wamelifanya sasa agenda ya kahawa kuwa agenda ya kudumu kwenye vikao na kila mahali wanapokaa. Matokeo yake ni kwamba sasa kwa msimu uliopita wote walioouza kahawa wameweza

kulipwa, hata zile *arrears* tunazosema malipo ya pili wamepata angalau ni kidogo *KDCU* wametoa shilingi 100 kwa kila kilo, *KCU* wametoa shilingi 150. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tatizo langu kubwa ambalo bado nalion; bei ya kahawa bado ni ndogo sana. Mkulima amepata kati ya shilingi 1,000 na 1,150, kitu ambacho kinamfanya anakata tamaa. Natoa ushauri kwa Serikali kwamba kwanza kabisa tafuta masoko ya kuuza kahawa, nenda nje muingie mikataba na nchi ambazo ni marafiki wakulima waweze kuzalisha kufuatana na mahitaji ya soko, waunganishe na soko waweze kuuza, waruhusu wanunuzi binafsi ambao tayari wana masoko kule nje waweze kuuza, muwape vibali mapema waende kuuza kabla Brazili na Vietnam ambao ni wakulima wakubwa hawajaingiza kahawa kwenye mzunguko. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile ninaomba ukija kuhitimisha utuambie ili yasijitokeze yaliyojitokeza kwenye msimu uliopoita kwa wakulima kahawa; je, kwanza tayari mmeshapata soko la kununua kahawa mwaka huu? La pili, je, kuna utaratibu gani utakaotumika kwenye msimu huu ambao umeanza tena huu mwezi wa tano, ni utaratibu gani utakaotumia katika kuuza kahawa?

Na mwisho, mtueleze, je, bei ya kahawa itaweza kupanda angalau kutoka kwenye 1,000 hadi 2,000 kwa mwaka huu kwa mkulima wa Kagera ili aweze kunufaika?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Nakushukuru mno Mheshimiwa Benardetha Mushashu kwa uchangiaji wa kisayansi na teknolojia; Mheshimiwa Salum Rehani, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmad Katani. Mheshimiwa Salum Rehani.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kupata muda wa kuchangia. Nataka kuiomba Wizara itoe taarifa rasmi hapa kuhusiana na suala zima la Mradi huu wa *SPD* //utaanza lini na kama umeanza, umeanza

wapi na vipi hatuelewi chochote mpaka leo zaidi ya miaka miwili sasa hivi toka umezinduliwa hakuna tunachokiona kinaendelea katika eneo hilo, kwa hiyo, tunaomba Serikali au Wizara itupe maelezo ya *SPD* //na ile mipango iliyokuwepo katika ule mradi inakwendaje.

Mheshimiwa Spika, la pili vilevile kuitaka Wizara hasa kwenye kile kitengo chake cha *Early morning* iweze kuwa inatoa maelezo sahihi kitu ambacho niseme wazi kwamba kimesababisha hasa wakulima wa mikoa zaidi ya nane ndani ya nchi hii kuweza kupata na janga la njaa kidogo yaani upungufu wa mazao kwa sababu kimeshindwa kutoa taarifa sahihi za hali ya hewa au hali ya mvua inavyonyesha au ukame utakavyotoka, kitu ambacho kwa kweli hawatutendei haki kama Watanzania. Kitengo kile kipo kina taarifa ambazo wanazipata kutoka *meteorological agent* lakini hawatoi taarifa wamekaa kimya watu wanalima hawajui hatima yao na watu wanategemea mvua. Kwa hiyo, tunataka utupe maelezo kipi kilichosababisha kwamba mpaka wakashindwa kutoa maelezo safari hii watu mikoa mingine ikaweza kupata upungufu wa mvua.

Mheshimiwa Spika, lakini jingine nilitaka kulizungumza kwamba Serikali au Wizara kwa ujumla wake imeondoa mkono wake kutoka *SAGCOT* zile shughuli ambazo tulikuwa tunazona ambazo zinasadia wananchi kuwekeza katika kilimo hasa mikoa ile ambayo ya Kusini ina mfumuko mkubwa wa uzalishaji lakini leo hii *SAGCOT* tunaiona inaanza kuelekea kulikokuwa siko. Kwa hiyo nitoe angalizo kwa Serikali pale ilipokuwa inaona kwamba imekosea irudi kwenye mstari *SAGCOT* ndio mkombozi ilikuwa kwa maeneo ya mikoa ya Kusini lakini imeelekea sasa hivi mikoa ya Pwani na mikoa mingine tunaihitaji *SAGCOT* irudi kwenye *progress* hali inayokwenda sasa hivi sivyo, hilo lazima tulizungumze. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jingine ambalo tulitaka kuona kwamba Serikali ijikite kwenye mbegu bado Tanzania tumekuwa jalala la mbegu feki mpaka leo kiwango ambacho nchi inaweza kutoa mbegu ndani ya nchi ni asilimia 12,15 mbegu zote zinatoka kwa Belgium, zinatoka South Africa,

zinatoka nchini Kenya na nchi nyinginezo kitu ambacho watu wanatumia nafaasi hiyo kuingiza mbegu feki. Makampuni haa ambayo tunayaita yako hapa nchini ya KIBO, SIDCO sjui mengine ambayo yako Arusha hayazalishi mbegu yanafungasha mbegu ambazo inakaa miaka chungumzima huko kwao na zikiletwa hapa ile *variability* inakuwa imeshapotea kwa hiyo, hazioti na zinawatia hasara wakulima. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Salum Rehani.

**MHE.SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nashukuru sana sasa anafuatiwa na Mheshimiwa Katani Ahmad Katani dakika saba.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwanza kukushukuru, lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Kilimo. Moja niipongeze Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ambayo iko Mtware kwa kiasi kikubwa kwa fedha ndogo ambazo wamepewa wameweza kusimamia vizuri na kuwafikia watu japo tatizo la fedha ya korosho kwa wakulima limekuwa kubwa. Na hili nadhani linafahamika vizuri nilizungumza wakati nachangia Wizara ya Viwanda lakini leo narudia tena kwa Wizara yenye ya Kilimo. Leo tunapozungumza simu yangu hapa nikikuletea ina *message* zaidi ya 700 watu wanalamika hawajapata fedha, tatizo limekuwa ni fedha. Sasa Wizara ya Kilimo mtusaidie mkishirikiana na wenzenu wa Biashara tatizo la fedha ya korosho kwa wakulima lini zitapatikana fedha zikawafikia wakulima wakaweza kupalilia mikorosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niliwaambia leo mikorosho watu wanakodisha shamba la heka 100, heka 80 mtu anakodisha kwa milioni tatu ili mradi tu aone kwamba sasa sina cha kufanya, watu wameshindwa kuwapeleka watoto shule kwa ajili ya fedha ya korosho hakuna, watu wameshindwa kufanya parizi la mikorosho kwa sababu ya fedha hakuna,

lakini kuna shida ambayo naiona, nilisema ukienda maeneo ya Lindi kwa Mheshimiwa Nape, ukienda Kata ya Nachunyu leo korosho zinahitaji kupulizwa watu wale hawana dawa kwa sababu hawana fedha sijui Serikali inataka kutueleza nini wakati mna- *wind up* mtuambie mkakati thabiti wa fedha za wakulima wa korosho zitakwenda lini. Tunajua kazi mnaifanya kubwa kwa sababu jambo lenyewe hamkujiandaa nalo, kazi mnayoifanya kubwa lakini tatizo la fedha ni kubwa kuliko linavyodhaniwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, na hata maelezo na takwimu niliwahi kukwambia Mheshimiwa Waziri kwamba takwimu mnazozitoa mara nyngi haziko sahihi, ukienda Tandahimba *rejection* ya Benki imekuwa kubwa. Kwa hiyo, kitakachozungumzwa kimelipwa ukienda kwenye uhalisia ni tofauti kabisa Watanzania hawa wakulima wa korosho dhamana yao na azma yao ya kupata fedha ni lini? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nikubaliane na mawazo yenu mliyosema kwamba tuweke bima. Bima inaweza ikasaidia kwenye mazingira kama haya tunayokuwa nayo, ingetusaidia sana lakini bahati mbaya sisi Wabunge tuna bima za kila aina lakini kwa wakulima wa korosho ambaa ndio nguvu kazi ya nchi hii hawana bima. Linapotokea anguko la biashara ya korosho kama hili hatuna kwa kukimbilia sasa niwaombe sana muone utaratibu na namna nzuri ambaa mnawenza mkaweka jambo hili sawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nilizungumza Wizara ya Biashara suala la Kangomba na nyie ndio wenyewe korosho wenyewe nataka niwaambie kwenye korosho kule wakati wa korosho kuna wakinamama wanauza mchele wanabadilisha kwa korosho yaani ni *butter trade system* ipo, Mheshimiwa Mgumba umekaa kwenye korosho unayajua haya mnapokaa mkazungumza mambo ya kangomba na nyie watu wa kilimo mpo na mpo mliokaa kwenye korosho Mheshimiwa Omary umekaa kwenye korosho unajua, wakinamama wanapika maandazi wanabadilishana korosho.

Mheshimiwa Spika, kesho akipeleka korosho unatka kuonesha shamba ni kweli haya mambo mnayoyafanya? Haya kweli mnayoyafanya yako sahihi? *Butter trade system* ipo kwenye Mpunga, ipo kwenye Kahawa, ipo kila mahali ambapo mkulima anafanya biashara, sitarajii itatokea miujiza tena ya kukaa mtu ukazungumza Kangomba japo Mheshimiwa Waziri unasema utatafutwa mfumo rasmi wa kurasimisha kangomba iwe jambo ambalo lipo kisheria. Lakini kwenye biashara hii hakuna jambo hilo haliwezekani yaani haupo utaratibu ambao utaupata ukasema hili unataka uliweke kisheria kwa sababu sheria hiyo itakataa tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo ulivyosema kangomba haya huna dawa mkulima asipulize korosho, unataka mkulima asizalishe korosho huna dawa anapatikana tajiri anasema bwana chukua 100,000 anakwenda kununua salfa akienda kununu salfa muda wa msimu yule allyetoe fedha anapewa korosho unamwambia akuoneshe shamba la korosho alitoe wapi wakati ye ye amemsaidia mkulima, nyie Serikali leo mnashindwa kumsaidia mkullima, kama hela yake ya korosho hajapewa unataka alime na nini? Mimi nilikuwa nataka ingewezeekana ufanye uombe siku tatu tu Bungeni hapa kusiwe na posho au kitu gani tuone kama tutajaa humu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Hiyo haikubaliki Mheshimiwa Katani.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, labda tungepata uchungu wa watu wa korosho ukoje siku tatu tusema hamna posho hamna nini viti hapa kama havikubaki vinane hapa, lakini kwa wakulima hawa wana dhambi gani? (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumza)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Katani dakika zako zimeisha dakika saba, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo atafuatiwa na Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante niungane na wenzangu kupongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pamoja na pongezi hizo naomba niende moja kwa moja katika mambo ambayo nakusudia kuyachangia. Nakusudia kuchangia mambo yafuatayo; kwanza kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukianzia ukurasa ule wa 29 mpaka 32 wamezungumzia kuhusiana na suala la zao la korosho. Na zao la korosho katika maeneo yafuatayo;

Mheshimiwa Spika, kwenye ule ukurasa wamezungumzia suala la uzalishaji wa miche ambalo liliifanyika katika msimu wa 2017/2018. Ninachokumbuka kwamba kuititia Bodi ya Korosho walitoa maelekezo kwa halmashauri ili waandae vikundi wazalishe miche ile ya korosho na wote tutakuwa mashahidi miche ambayo ilizalishwa ilipelekwa katika maeneo mengi katika na wameeleza ni mikoa 17 ambayo ilipelekwa miche ile.

Mheshimiwa Spika, mpaka hivi ninavyosimama hapa wako wanavikundi ambao waliingia mikataba na Bodi ya Korosho hawajalipwa pesa zao niombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja alizungumze hili kuona namna gani kwa sababu tunapozungumzia wanavikundi tunagusa jamii zetu na ni watu ambao wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu sasa walifanya hii kazi lakini mpaka leo unapozungumza hawajalipwa. Nikuombe Mheshimiwa Waziri utakapokuja kutoa ufanuzi tueleze ni kwa nini hawajalipwa na vinginevyo nitashika shilingi kwa mara ya kwanza nakusudia kushika shilingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo nakusudia kuzungumza ni suala la ujenzi wa maghara, nafahamu kwamba yako maeneo ambayo tulikuwa tunaendelea kujenga maghara napozungumza maghara ni yale maghara ambayo tunafikiria kwa ajili ya uhifadhi wa korosho. Kuna Mkuranga na kuna Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru na tayari ujenzi huuulianza lakini ninapozungumza sasa hivi ujenzi huo umesimama, niombe Mheshimiwa Waziri atueleze tutamaliza lini yale majengo.

Mheshimiwa Spika, nimeshawishika kulisema hili kwa sababu hivi tunavyoendelea tunaingia katika mfumo wa ununuzi wa Ufuta na tu na tunapozungumza sasa korosho nyingi ziko maghalani, sasa sjui itakuwaje kwenye hili jambo kwamba Ufuta unatakiwa uingie kwenye maghala lakini maghala yamejaa korosho mpaka korosho hazijaondolewa, kwa hiyo niombe Mheshimiwa Waziri utakapokuja pia utuambie ule ujenzi utakamilika lini, kwa sababu tulipanga sisi kupitia Serikali yetu lakini bado hatujakamilisha ujenzi wa maghala likiwemo ghala lile katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru lilitengewa pesa ilitoka pesa kidogo na sasa ujenzi umesimama. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine naomba nizungumze suala la Maafisa Ugani, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamelisema lakini pia naomba niliseme tunazungumza kulima kilimo cha kisasa. Naomba niseme kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu wako wakulima wetu mpaka hivi tunavyozungumza hawajui hata namna ya matumizi ya hizi pembejeo sasa ili waweze kutumia pembejeo ni pamoja na kuwepo Maafisa Ugani katika vijiji vyetu ili waendelee kuwaekeleza wakulima wetu katika kulima kilimo bora na chenye ufanisi.

Mheshimiwa Spika, nimelazimika kushawishika kuyasema haya kwa sababu ni mionganoni mwa Wabunge wanaotoka katika Mkoa wa Ruvuma na sisi Ruvuma ina wakulima tunalima kilimo cha chakula, lakini pia tunalima kilimo cha biashara ili tuwasaidie wananchi wetu ni pamoja na kuwapeleka Maafisa Ugani na hii ni sera kabisa lazima wawepo Maafisa Ugani, kwa hiyo suala la Maafisa Ugani kwanza ikumbukwe tunao wachache lakini hata wale tuliokuwa nao hawafanyi kazi ipasavyo, wengine wanageuka kuwa wanasiasa, lakini kuna sintofahamu katika ya Afisa Ugani anayeshughulika na masuala ya uvuvi na anayeshughulika na masuala ya kilimo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye vijiji vyetu akimuono Afisa Ugani anayehusika na masuala uya uvuvi ana amini kwamba anaelewa na masuala ya kilimo, sasa niombe

kupitia hii Wizara na masuala ya mifugo niombe kupitia Wizara tuone uwezekano wa kuwapeleka Maafisa Ugani ili waendelee kuwasaidia wakulima wetu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Sikudhani.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja mambo ni mengi lakini muda mchache ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga dakika 10 wao ni zile za kwao za upande wao wamegawana dakika 10 atafuata Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe. Mheshimiwa Haonga tafadhali.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia nitagusa baadhi ya maeneo kwa mfano nitagusa eneo la kwanza linalohusu zao la Kahawa, pia eneo la pili nitagusa Korosho na kama muda utaruhusu pia nitazungumzia suala la Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kwanza suala la zao la Kahawa, ni kwa muda mrefu sasa bei ya kahawa imekuwa ikishuka miaka hadi miaka na msimu huu kahawa ndio imeendelea kushuka imekuwa bei ndogo kuliko wakati mwингine wowote ule.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo naomba nijiulize kidogo na naomba labda tusaidiane kidogo Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atusaidie, kwa nini nchi ambazo zinatuzunguka wanaolima kahawa sawa na sisi kwa mfano nchi kama Uganda pamoja na nchi nyingine ambazo zinalima kahawa Kenya na nyingine kwa nini hawalalamiki sana kuhusu suala la bei ndogo ya kahawa? Na ushahidi unaonyesha kwamba hata kahawa ya Tanzania inatoroshwa kupeleka Uganda kwa maana ya Kahawa ya Kagera inapelekwa Uganda, lakini pia kahawa kutoka Kigoma inatoroshwa na maeneo mengine ya mpakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kwamba hawa wenzetu kwa sababu tunaamini kahawa inauzwa tuna soko la dunia je wao soko lao liko wapi? Kwa nini kahawa yetu sisi imeendelea kushuka wakati soko la dunia ni moja? Kwa kweli nadhani shida kubwa hapa nayoiona shida kubwa sio soko la dunia hiyo sio shida kubwa, shida kubwa ni utashi wa viongozi wa Serikali hii ya Awamu ya Tano ambao wamepewa dhamana kutuongoza ndio tatizo linaanza hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo kwa mfano ukiangalia kuna suala la Uganda pale wao hawana kitu kinaitwa vyama vyaa msingi vyaa ushirika hawana lakini bei ya kahawa ni nzuri, hawana kitu kinachoitwa hizi tozo karibu zote zimeshaondolewa imebaki tozo moja tu yule anayekuja kununua kahawa analipa ile tozo ya mwisho anapokuwa anasafirisha kahawa anapoondoka, sasa sisi bado kwenye kahawa kuna tozo nydingi sana hilli ni tatizo kubwa sana, sasa huyu mkulima wa kahawa kama angeweza kuachwa kwa mfano tukamfutia tozo zote ali pe kodi anaponunua saruji kwa sababu ataenda kujenga, ali pe kodi anapoenda kununua batii kwa sababu ataenda kujenga, huko ndiko ambako sasa tungeweza kupata kodi kwa njia kama hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri Wizara iangalie namna ya kuondoa tozo na kodi zote kwenye zao la kahawa kama wanavyofanya nchi ya jirani ya Uganda ili mwisho wa siku nchi yetu tuweze kuwasaidia wakulima wa kahawa. Hata eneo tunalolima kahawa ni eneo kubwa sana lakini tija ni kidogo, leo tunaambiwa kwenye takwimu hapa kwamba msimu tulipata zaidi ya tani 60,000 na miaka ya nyuma ilikuwa tani 40 na kidogo 40,000 nakadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia Uganda wanalima zaidi ya tani wananaapata zaidi ya tani 300,000 wanapolima mara moja zaidi ya 300,000 tunaingia mara sita kwa Uganda, kwa hiyo tija kwenye zao la kahawa pia hapa kuna shida, tuna mashamba makubwa lakini tija ni ndogo. Kwa hiyo, ni vizuri tukatafuta muarobaini kwa nini wenzetu ambao wanalima kahawa wana mashamba madogo kuliko

ya kwetu lakini wanapata kahawa nyingi kuliko sisi shida iko wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungume jambo la pili ambalo ni jambo la kuhusu suala la korosho. Aliyevuruga suala la korosho au biashara ya korosho huyu tumchukulie kama alivyokuwa wahujumu uchumi wengine, kwa sababu leo ukiangalia zao la korosho kwa takwimu ambazo tunazo mwaka jana korosho fedha za kigeni tulilingiza dola za Marekani milioni 367 ukichukua zao lilitofuatia ilikuwa ni Tumbaku ambalo ilikuwa ni dola za Marekani milioni 222, na kahawa ilikuwa dola za Marekani milioni 134, lakini ukichukua mazao yote kama Karafuu, Katani, Chai, Pamba unaona mazao yote haya ukijumlisha bado hayawezi kufikia kwenye zao la korosho. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa leo tunaweka watu kwenye magereza zetu tumewajaza watu ambao wanasema ni wahujumu uchumi kwa vitu vidogo lakini kuna watu waliochezea zao la korosho tunacheke na, tunakula na, tunakunywa na, tunawaangalia. Leo tulitegemea kwamba watu hawa wangkuwa magereza lakini tunacheke nao tunawaangalia tu. Sio mtabiri wala sio Nabii kama Mbunge wa Arusha Mjini Mheshimiwa Lema lakini Rais ajaye sijui atakuwa nani aidha upande wa CCM au CHADEMA au CUF ninaamini atakuja kufanya jambo kwa sababu naamini kwa upande huu kipindi hiki ni kwamba ni nani amfunge paka kengele inawezekana ndio shida inaanzia hapo. Lakini kwa hawa wanaotuingizia hasara Taifa letu kwa kweli lazima wachukuliwe hatua kama wahujumu uchumi wengine ambavyo wamekuwa wakifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo zao hili tumepoteza *export levy* mwaka jana ilikuwa zaidi ya bilioni 300 *export levy* leo hatujapata hata shilingi hatujapata kwenye *export levy* kwa sababu ya watu wachache tu walioamua kutufanyia mambo ambayo kwa kweli sio mazuri hata kidogo. Leo halmashauri zinazolima korosho Tandahimba maeneo yote yanayolima korosho hawajapata ushuru unaotokana na zao la korosho. Leo halmashauri hizi zinaendaje kuendesha mambo yao?

Kwa sababu kuna watumishi ambao wanaajiriwa na halmashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo tunaambiwa kwamba hawatapewa fedha kwa maana ya ushuru wa korosho maana yake hawa watu wameporwa ushuru wa mabango, wameporwa ushuru wa majengo, leo unaenda kuwapora na ushuru wa korosho tafsiri yake ni kwamba hizi halmashauri zinaenda kufa, sasa kama zinaenda kufa mwisho wa siku itakuwa sasa mwisho wataenda kuzifuta tu kwa sababu sasa hivi shida kuendesha mambo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo bado nisisitize kuna hana najua Mheshimiwa Waziri wewe ni mgeni lakini kuna haja ya waliohusika wote waweze kufunguliwa kesi za uhujumu uchumi ili mwisho wa siku tuweze kupeana adabu na mwisho wa siku mambo yaweze kwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo noamba nizungumzie kidogo ni suala la kuhusu Maafisa Ugani, kwa takwimu tulizo nazo Tanzania tuna vijiji zaidi ya 15,000 vijiji tulivyokuwa navyo lakini Maafisa Ugani ambao tunao ni 7,974. Juzi hapa uliongea kwamba unapozungumzia kwa mfano suala la uchumi wa viwanda huwezi ukaiacha kwa mfano Bandari ile ya Bagamoyo ukaiacha ni sawa na ng'ombe anakuwa nyuma halafu mkokoteni unakuwa mbele, wakati ng'ombe anatakiwa akae mbele avute mkokoteni. (*Makofii*)

Sasa leo kama inafika mahali Maafisa Ugani wako wachache namna hii ambao ni 7,964 tu, lakini na vijiji zaidi ya elfu 15 ni sawasawa na mfano uliotoa ule kwamba, unapeleka mkokoteni mbele halafu ng'ombe wanaovuta wanakaa nyuma. Sasa jambo hili Mheshimiwa Waziri atueleze wakati atakapokuwa anahitimisha, je, wana mpango gani kuhusu kuajiri Maafisa Ugani? Kwa sababu, hatuwezi Maafisa Ugani ni wachache. Hata hawa waliopo utakuta yuko mmoja, huyohuyo wanampa kazi ya utendaji, mara watampa sijui kazi ya nini; hawa ni wacache, lakini wanapewa na majukumu mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, hawa Maafisa Ugani waliopo tunaomba waweze kuajiriwa na wengine ili wawe wengi zaidi, lakini pia waweze kupewa motisha. Leo maeneo mengine ya nchi ambazo zimeendelea huko ambazo ziko *serious* kwenye masuala ya kilimo Maafisa Ugani hawa amepewa angalau mtu anapewa, hata kama hawesi kupewa gari, basi mpe hata pipipiki ili aweze kufanya kazi kwenye mazingira mazuri. Maana kilimo chetu sasa tunakitegemea kwamba, inapofika mwaka 2025 twende kwenye uchumi wa katii, hatuwezi kuwa na uchumi wa katii ikiwa Maafisa Ugani ni wachache namna hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwenye kilimo ambalo naomba nigusie, ni kilimo cha umwagiliaji. Mwaka jana, bajeti ambayo tunaenda kuimalizia sasa kwenye suala la umwagiliaji, tulitenga kama bilioni 24 hivi, lakini mwaka huu tumetenga billioni nane tu; tunavezaje kuwa na nchi ya viwanda kama tumetenga billioni nane kwenye umwagiliaji? (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumza)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja ya Upinzani.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, dakika tano,tano.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika hotuba hii. Kwa sababu muda ni mchache, naomba niende moja kwa moja kwenye mchangano wangu.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye Fungu 05 - Tume ya Umwagiliaji ambapo katika maelezo ya hotuba inaelezea kujenga na kuboresha na kukarabati skimu za

umwagiliaji. Nakuja kwenye Mkao wa Katavi, Serikali katika hotuba yake imesema itakarabati skimu 16 na nyingine kujenga tano, nafikiri hii ni Tanzania nzima kama sikoseli, maana hawaajielezea vizuri. Hata hivyo, ukirudi katika Mkao wa Katavi skimu ambazo hazifanyi kazi ni skimu sita, skimu ambayo inafanya kazi ni skimu moja na hii skimu nafikiri ni ile ya Urwira, iko katika Kata ya Urwira, Jimbo la Nsimbo ambayo nafikiri inafanya kazi kwa sababu tu iko chini ya usimamizi wa Kanisa Katoliki.

Mheshimiwa Spika, narudi ambazo hazijajengewa miundombinu ziko 84, ambazo zimejengwa baadhi ya miundombinu ziko 35, jumla ya skimu Mkao wa Katavi ni 126 na inafanya kazi moja. Je, kweli, tuna nia ya dhati katika kuleta mapinduzi ya kilimo ambayo mazao yake ndio sasa yanayoenda kutumika katika viwanda ambayo tunasema uchumi wa viwanda, naomba tuwe *serious* katika hilli ndugu zangu.

Mheshimiwa Spika, narudi sasa mimi, katika skimu hizo hizo naona zisizofanya kazi Skimu za Mwamapuli na Skimu ya Kilida hazimo kabisa. Skimu ya Mwamapuli katika bajeti ya mwaka juzi iliwekwa kwenye mpango mkakati wa Serikali, wa Taifa. Sasa nauliza na hela ile ilitengwa karibu bilioni mbili, sasa sielewi zilikwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, huu mradi ninaosema Skimu ya Mwamapuli katika Kata ya Mwamapuli, Jimbo la Kavuu, nauongelea huu mradi kwa heshima kubwa ya Mheshimiwa Mstaifu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda. Alitujengea pale mradi mkubwa wa kinu kikubwa cha kuchambulia mchele kwa kutegemea kwamba, hii skimu sasa ingelisha kwenye hiki kinu, lakini mpaka leo hii, kile kinu kinaoza, hakifanyi kazi yoyote, wakulima wamejiandaa pale, tuna mbuga kubwa sana pale na skimu hiyo ni kubwa. Nashangaa kwa nini, na kwenye Wizara ya Maji nimeiongelea, nashangaa kwa nini haichukuliwi hatua? Naomba Serikali sasa inipatie majibu kwa nini skimu hii imeachwa haimo kwenye bajeti kabisa? Skimu ya Mwamapuli na Skimu ya Kilida. Skimu ya Kilida ni matengenezo tu inahitaji, lakini na

yenye hawajaiweka kabisa. Kwa hiyo, naomba sasa watakapokuja waje na majibu wanieleze kwa nini skimu hizi mbili hawajaziweka kabisa? Pia kwa nini Mkoa wa Katavi iko skimu moja tu wakati tuna skimu 126, skimu moja tu ndio inayofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe sana, narudi kwenye Jimbo langu la Kavuu, nataka wanieleze kwa nini Mradi wa Skimu ya Mwamapuli pamoja na Kilida haumo kwenye bajeti? Je, hauna umuhimu kwa wananchi? Je, ilikuwa haifanyi kazi? Miradi yote hii ilikuwa inafanya kazi. Sasa naomba waniambie kwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la pembjeo, hasa kwenye upande wa mbegu. Nataka nijiulize, nimekaa nikijiuliza sana kwani ni lazima kila mwaka mwananchi anunue mbegu? Je, katika zile mbegu wanazokuwa wamezileta mwaka huu, je, mkulima amelima, mimi nakumbuka zamani tulikuwa tukilima, mnachagua mahindi ambayo ni mazuri mnayahifadhi kwa mbegu; je, hizo mbegu zikihifadhiwa zikatumika kwa mwaka unaofuata hazifai? Naomba niulize swali hili kwa sababu, tumekuwa na ucheleweshaji wa mbegu ambazo sasa wakulima wanakuwa hawapati. Nilikwishesha maeneo mbalimbali yana mvua tofauti, kwa mfano katika Jimbo langu la Kavuu mimi kuanzia mwezi wa 11 mvua zinaanza kunyesha, pembejeo wanaanza kuleta mwezi wa Tatu, sasa je, mtu akihifadhi mbegu alizolima mwaka huu akahifadhi akapanda mwaka kesho, hizo mbegu hazifanyi kazi? Nawauliza kupitia kitengo chao cha utafiti? Maana tunataka kujua kwa sababu, hata hizo wanazoleta kila mwaka bado hazioti na hazifanyi vizuri. Kwa hiyo, naomba watufafanulie katika hayo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Wananchi wangu wamenisikia. Nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa John John Mnyika ajiandae.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hoja hii ambayo iko mbele yetu. Napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote kwa kuitayarisha hoja hii vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, nataka niongelee zao la tumbaku peke yake. Nchi ya Malawi ilikuja Tanzania kuja kuomba mbegu ya tumbaku mwaka 1966, ilichukua mbegu kwetu, sasa hivi Malawi wanazalisha tumbaku karibu kilo milioni 200; sisi ambaao walichukua mbegu kwetu tumewahi kufika mwaka 2010, tulifika kilo milioni 120, sasa mwaka huu tunategemea kilo milioni 54 kutoka kwenye milioni 120 mpaka kilo 54. Kuna tatizo gani? Kwa nini uzalishaji unashuka namna hii wakati ardhi tunayo Watanzania? Watu ni walewale na watu tunaongezeka?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningetegemea kwamba, uzalishaji ungekuwa unaongezeka, uzalishaji unashuka, ina maana kuna tatizo tena tatizo kubwa. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, naomba tutumie Chuo Kikuu cha Sokoine, tutumie SUA; wenzetu Afrika hii, wenzetu duniani wanatambua umuhimu wa wataalam waliopo hapo Sokoine. Wanawaita, wanakwenda Ethiopia, wanakwenda *Southern Africa* huku kwenda kutoa taaluma yao. Naomba tutumie Chuo Kikuu cha Sokoine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kuna miradi mingi ambayo huko Wizarani wamepata fedha kwa mfano Miradi ya Sumu Kuvu ambayo wameipata. Wawatumie wataalam wa Chuo Kikuu cha Sokoine ili tuweze kujua kwenye tumbaku kuna tatizo gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, zao la tumbaku mwaka huu, Mheshimiwa Waziri anajua, kuna makampuni ambayo, tuna makampuni kama manne au matano ambayo yananunua tumbaku hapa nchini. Kampuni moja imeamua kujitoa, nadhani limetoa nia ya kujitoa, kwa hiyo, hawajatoa makisio mpaka sasa. Kwa hiyo, kuna Vyama vingi vya Msingi Wilayani Chunya, Tabora, Mpanda, Songea ambavyo havina kwa

kuuza tumbaku ya mwaka kesho. Mheshimiwa Waziri anajua, naomba isije ikawa korosho ya pili, naomba Mheshimiwa Waziri achukue hatua stahiki tupate kampuni nyingine za kuja kununua tumbaku kwa wakulima ili tuweze kuinua kipato cha wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana *Senator Victor Mwambalaswa*. Mheshimiwa Ritta Kabati. (*Makofi*)

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya kilimo. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu wote Mawaziri wa Wizara hii kwa kazi nzuri sana ambayo wamekuwa wakiifanya kwa kipindi kifupi ambacho wamekuwa katika Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda kuwa mchache, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja. Kwanza kabisa nichangie kuhusiana na changamoto katika vituo vya utafiti. Kwa kweli mimi ni mijumbe, tumetembelea katika hivi vituo, hali ya vituo ni mbaya mno. Ningombaa Serikali sasa itambue umuhimu wa vituo vya utafiti, ili sasa tuweze kufanya utafiti wa uhakika katika mbegu, magonjwa, dawa za tiba, viuatilifu, udongo, ili tuweze kutenda haki kwa wakulima wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia, nzungumzie kuhusiana na *NDC*, inafanya kazi nzuri sana za kuwakopesha wakulima zana za kilimo za kisasa. Je, wakulima wanatambua kuhusiana na haya matrekta kwa sababu, ni bei rahisi na tunategemea kwamba, kama wakulima watapata matrekta yatasaidia kulima kilimo cha kisasa ambacho kitaleta tija katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini moja kwa moja niende katika Mkoa wangu wa Iringa kuhusiana na zao la pareto. Hili ni

zao la biashara katika Mkoa wetu wa Iringa, linatuingizia pato katika mkoa wetu na katika nchi hii, lakini kuna kiwanda ambacho kiko katika Wilaya ya Mufindi. Vilevile tushukuru kwamba, katika hiki kiwanda kinahitaji kama tani 5,000 za maua ya pareto, lakini kuna walanguzi ambao wamekuwa wakija kuwarubuni wakulima katika hili zao la pareto kwa sababu, sasa hivi kiwanda kinapata maua kama tani 2,500 tu na kiwanda tushukuru kwamba, wamekuwa wakiwa-support wakulima kwa kuwapa pembejeo na utaalam, tuwapongeze sana, lakini sasa je, Serikali inalindaje viwanda kama hivi na inalindaje wakulima?

Mheshimiwa Spika, inalindaje kuhakikisha kwamba, walanguzi hawaji kulangua malighafi katika maeneo ambayo wakulima wanafanya maana tunaelekeea kwenye uchumi wa viwanda. Sasa kama Serikali itakuwa haina mpango mzuri, mkakati wa kuhakikisha kwamba, inalinda hivi viwanda bado tutakuwa tunapiga *mark time*. Sasa niombje je, hakuna sheria inayolinda viwanda ambavyo vinawekeza katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, vilevile nizungumzie kuhusiana na masoko. Tatizo kubwa la mkulima ni masoko. Nyanda za Juu Kusini tunalima mahindi, pareto, parachichi, viazi, lakini mkulima leo hii anapolima hajui soko atalipata wapi, lakini kuna Bodi ya Mazao Mchanganyiko ambayo tulikuwa tunategemea kwamba, sasa itatusaidia kututafutia masoko, lakini bado unaona kwamba ina changamoto kubwa sana, haipatiwi fedha za kutosha kuhakikisha kwamba, inafanya kazi inayotakiwa; sasa je, Serikali mmejipangaje? Maana bila soko bado wakulima wetu wamekuwa maskini.

Mheshimiwa Spika, mkulima wa leo hawezi hata kumsomesha mtoto. Mkulima wa leo yani analima, lakini wanaofaidika ni wale walanguzi. Sasa ifike sehemu Serikali hii imwezeshe mkulima, ili ajisikie kama wakulima walivyo katika nchi nyiningine wanapata heshima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie Benki ya Kilimo; Benki ya Kilimo tulikuwa tunategemea itusaidie katika kuhakikisha

kwamba, mkulima anakopesheka, kwa sababu, mkulima wa sasa hivi hakopesheki kutokana na *risk* kubwa ambazo anazo. Tuombe kwamba, bima ya mazao iwekewe udhibiti, ili aweze kukopesheka, lakini tuombe benki hii iongezewe mtaji wa kutosha...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumza)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati. Mheshimiwa John Mnyika, dakika 10, atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kutoa pole kwa Chama cha Mapinduzi, hususan Chama cha Mapinduzi Zanzibar kwa kifo cha Mzee wetu Shamhuna, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema na msiba wake unaendelea kutukumbusha kwamba, sisi wote ni udongo na tutarudi kuwa udongo. Kwa sababu hiyo, tuenende kwa unyeyekevu na hekima. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pili, nieleze tu kwa sababu nina dakika 10 kwamba, naunga mkono Mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu zao la korosho kuanzia aya ya 80 mpaka aya ya 92 na mapendekezo yote hayo kuanzia ukurasa wa 23 na 26, yahesabike vilevile kama ni sehemu ya mchango wangu ili nijielekeze kwenye nini sasa tufanye baada ya kadhia nzima ya korosho ambayo kwa ukubwa wake, hii kashfa ya korosho inafanana na *EPA*, inafanana na *Escrow*, inafanana na *Richmond*, inafanana na kashfa zenye sura ya namna hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya namna hii tunapaswa turejee kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania ambapo Ibara ya 63(20), imetamka kwamba, Bunge ndio chombo kikuu ambacho kwa niaba ya wananchi kina wajibu, sio tu wa kuishauri Serikali bali pia, kuisimamia Serikali. Hapa tunahitaji kuisimamia Serikali na kutaka uwajibikaji wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa tunapotaka uwajibikaji wa Serikali Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni, kwa Katiba ya nchi yetu, Ibara ya 52 inamtamka kwenye Ibara Ndogo ya (2) kwamba, ni Waziri Mkuu na Ibara Ndogo ya (1) inasema, sio tu hapa Bungeni Waziri Mkuu atakuwa na madaraka juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku kwa kazi za shughuli za Serikali za kila siku.

Mheshimiwa Spika, sasa kama hili suala la korosho kwa siku zote hizo limeendelea na kashfa ya uozo wa namna hii, ni wakati sasa Waziri Mkuu katika majumuisho ya Wizara hili afike Bungeni atangaze kujuzulu yeye mwenyewe nafasi yake kabla hajawajibishwa. Hii ndio italinda dhana ambayo Mheshimiwa Mwakyembe alisimama siku chache zilizopita akimjibu Mheshimiwa Msigwa wakati aliposema Waziri Kabudi anatakiwa kujuzulu, Waziri Mwakyembe alisimama kwa niaba ya Serikali, kwa niaba ya Waziri Mkuu akasema jambo hili ni la uwajibikaji wa pamoja, sasa uwajibikaji wa pamoja uonekane ukitanguliwa na Waziri Mkuu mwenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hili la uwajibikaji wa pamoja linaongozwa na Katiba yetu, Ibara ya 53(2), nitanukuu inasema:

*"Serikali ya Jamhuri ya Muungano chini ya mamlaka ya Rais itakuwa ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za Serikali kwa ujumla na Mawaziri," Mawaziri nasisitiza, "Mawaziri chini ya uongozi wa Waziri Mkuu watawajibika kwa pamoja Bungeni kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali. (*Makofii*)*

Mheshimiwa Spika, sasa kadhia hii imewagusa Mawaziri wengi kidogo, imewagusa wale walioondolewa mwanzoni, wakati Rais alipotoa kauli akafikia hatua mpaka

kusema wale mashangazi kule Kusini watapigwa, wakaondoka baadhi ya Mawaziri. Wakaingia wengine, lakini hawa walioingia badala ya kurekebisha tatizo wamelikuza na kuliendeleza tatizo mpaka hivi sasa tunavyozungumza. Ndipo yanapokuja masuala kama ya *Indo Power* ambayo pamoja na kuwa Mheshimiwa Profesa Kabudi ndio anaonekana kwenye picha pale mbele, mstari wa mbele, Mawaziri wanaohusika ni Waziri wa Fedha ndio maana Gavana wa Benki alikuwepo, anatakiwa awajibike, Waziri wa Viwanda na Biashara anatakiwa awajibike, Waziri wa Kilimo naona tunamkwepakwepa Waziri huyu eti kwa sababu ni mpya wakati mkataba umesainiwa yeye akiwepo anatakiwa kuwajibika, Waziri wa Mambo ya Nje anatakiwa kuwajibika, Waziri wa Utawala Bora ambaye Usalama wa Taifa uko chini yake wenye wajibu wa kuishauri Serikali anatakiwa kuwajibika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mzigo wote huu wa uwajibikaji, lazima Waziri Mkuu ndio awe minara wa kwanza wa kuwajibika kutangaza kujiuzulu nafasi yake ya Uwaziri Mkuu. Waziri Mkuu akishajiuzulu maana yake... (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa John Mnyika kwa mtu ambaye hajui nini kimekuwa kikiendelea, ikiwa ni pamoja na mimi mwenyewe, tungependa kujua wawajibike kwa sababu gani? Endelea tu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na hili la *Indo Power* ambalo mnataka kusema *as if* kwa sababu, hawajauziwa korosho sio shida. Kwenye uchumi kuna kitu kinaitwa *opportunity cost*, gharama ya fursa; yaani kwamba, walituhidi kununua korosho laki moja na tukasaini na hawakununua na korosho zikakaa kwenye maghala mpaka zimeoza, tunavyozungumza hivi sasa tumekosa mapato ya nje. Hii gharama ni kubwa ni ya yale makosa yanayopelekwa Mahakamani unasikia, huyu awajibike kwa uzembe na kuisababishia hasara Serikali kwa uhujumu uchumi, hao wanatakiwa kuonesha uwajibikaji, ili sasa wale walioishauri Serikali vibaya, kama kuna watu nyuma

walioishauri ukiondoa hawa Mawaziri, nyuma ya Serikali hawa nao wanapaswa kuwajibika.

Mheshimiwa Spika, hili ni suala la Kikatiba tena...

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Mnyika, tupokee Taarifa.

Mheshimiwa Abdallah Ulega, Naibu Waziri wa Mifugo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nataka kupata kujua maana ya neno kuoza ni nini? Maana Mheshimiwa Mbunge anayezungumza anasema korosho zimeoza, korosho zilizooza ni korosho zipi na kuoza ni kitu gani?

Mheshimiwa Spika, maana asipotoshe, akang'ang'ana kusema kuoza, kuoza maana yake ni *decay*. *Decay* maana yake ni *process* ya kibailojia inayoleta wadudu. Korosho gani katika nchi hii alizoziona yeze Mheshimiwa Mbunge zinatoa wadudu hivi leo kama sio upotoshaji?

**SPIKA:** Mtunzieni dakika zake

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, bahati nzuri nazungumza nikiwa nimetoka Ruvuma, Mtwara na Lindi kwenye shughuli za chama na nimekutana na wakulima. Wanapozungumzia korosho huwa zina muda wake, muda ukipita korosho zinasinyaa, zikishasinyaa zinakosa soko na ndio maana Serikali...

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** imeanza kuwarudishia wananchi, naomba niendelee...

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, taarifa unapewa Mheshimiwa Mnyika.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mnyika kwamba hadi jana korosho ambazo anasema yeye kwamba zimeoza zinaendelea kubanguliwa kwenye viwanda vilivyopo Tunduru na Mtwara. Sasa yeye ni korosho zipi ambazo anasema zimeoza ambazo haziwezi kubanguliwa? (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, mimi naomba niendelee kwa sababu anani...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika pokea taarifa hiyo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** ...wananipotezea tu muda wangu.

Mheshimiwa Spika, ninachokisema ni kwamba kuna wakulima wanarudishiwa korosho zao wanaambiwa Serikali haizitaki tena zipo chini ya kiwango kwa sababu Serikali inajua haziuziki nje inaanza kuwarudishia wakulima. Kuna wakulima hawajalipwa, kuna mambo mengi nisipotezwe nje ya mstari naomba niendelee...

**MHE. KATANI A. KATANI:** Taarifa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Katiba ya nchi...

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa...

**SPIKA:** Naomba tumuache aendelee, endelea Mheshimiwa...

**MHE. KATANI A. KATANI:** Tuweke *clarification* hili...

**SPIKA:** Dakika zako zitavurugika, endelea.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Nilitaka nijibu korosho wapi zimeoza maana najua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Katani muachie, za kwako ulizitumia vizuri, ungeongea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Katiba ya Nchi yetu Ibara ya 54 inayozungumza kuhusu Baraza la Mawaziri ibara ndogo ya 3 inasema bila kuathiri masharti yaliyomo Ibara ya 37 ya Katiba hii, Baraza la Mawaziri litakuwa ndicho chombo cha kumshauri Rais juu ya masuala yote yanayohusika na utekelezaji wa madaraka yake. Inaendelea mbele, kwa ajili ya muda nisiinukuu yote.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba huu uozo wote wa korosho, kuanzia ushauri wa kwanza wa kumshauri Rais kwamba korosho zikusanywe na zibebwe na jeshi na kuleta azimio hapa Bungeni la kumpongeza Rais; huu uamuzi Baraza la Mawaziri lilmshauri Rais vibaya, Baraza la Mawaziri linastahili kuvunjwa. Mpaka uamuzi wa kwenda mbele kuitafuta hiyo Kampuni ya Kenya ya Indo Power kwamba itanunua korosho...

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L BASHUNGWA):** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** ...za laki moja. Baraza la Mawaziri limemshauri Rais vibaya, Baraza la Mawaziri linastahili kuvunjwa na ili livunjwe Waziri Mkuu ajiuzulu...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** ...na kama hajiu zulu tutaleta hoja ya kutokuwa na imani naye ili kuiwajibisha Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika pokea taarifa ya Mheshimiwa Innocent.

## TAARIFA

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA – NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyika tunamsikiliza lakini ukiangalia...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika bado dakika zako, hii ni kengele ya kwanza eeh, endelea.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA – NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ukiangalia hoja anayojenga Mheshimiwa Mnyika anai-*deduct* kutoka kwenye kuoza kwa korosho. Taarifa tumempa kwamba hakuna korosho iliyoza kwa hiyo kwa sababu ana-*deduct* hoja yake kutoka... (*Makof!*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA – NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** kwenye kuoza kwa korosho na si kweli, hoja yake haipo-*valid* ni *void*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilitaka nimpe taarifa, una-*derive* hoja yako kutoka kwenye kuoza kwa korosho lakini hakuna korosho ambayo imeoza.

**SPIKA:** Ahsante sana, wanasemea neno kuoza, Mheshimiwa Mnyika unapokea hiyo taarifa? Bado dakika zako mbii.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Hivi mtu akileta korosho yenyе kiwango halafu hiyo korosho ikawekwa kwenye maghala ikaharibika ikawa chini ya kiwango, anarudishiwa amefanya nini?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee. Hoja yangu siyo ishu ya kuoza peke yake na kuna taarifa hapa...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mbona taarifa za huku unazikataa, taarifa za huku unazikubali? Hiyo ni *double standard*, mkaribishe tu huyu anatoka kwenye eneo la korosho aseme kama korosho haziozi au la atoe ufanuzi. (*Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** naomba umpe taarifa basi, pokea taarifa hiyo kuhusu korosho kuoza kutoka kusini.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuendelea. Hoja siyo jambo la korosho tu kuwa chini ya kiwango ambayo tunakubaliana na kwamba CAG akachunguze tasnia nzima ya korosho...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** ...lakini hoja nyingine hapa kadhaa...

**SPIKA:** Subiri Mheshimiwa Mnyika. Nilikuwa nalinda dakika zako, nakulinda wewe mwenyewe nikiamini una cha kusema. Nilifanya hivyo kwa sababu huyo unayetaka atoe taarifa amepata dakika zake saba za kuzungumza hapa, unanielewa eeh?

Eeh subiri, amepata dakika zake za kuzungumza. Kuna kuhusu utaratibu huku sijui upande gani, Mheshimiwa Naibu Waziri.

## KUHUSU UTARATIBU

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwa Kanuni ya 64(1) (a); kuhusu kudanganya. Kwanza mimi ni mkulima wa korosho, ye ye si mkulima wa korosho. Korosho ina utaratibu wake, ina muda wake maalum unaofikiwa na kuitwa kwamba imesinyaa, tulisema na tukaiweka katika utaratibu uka itwa unyaufu. Katika muda huo ambao tumezikusanya korosho mpaka hii leo, hamna uwezekano wa kusema korosho imeoza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, narudia tena, mimi ni mkulima wa korosho, ninazo kwangu korosho na ninazo za kwangu mwenyewe pia vilevie korosho. Kwa hiyo suala la kusema kwamba korosho imeoza, huo ni uongo mkubwa na aache kupotosha na urongo wake huo. (*Makofi*)

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Mheshimiwa Selasini nimekuona *Chief Whip*.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe ukishamuona Mheshimiwa Selasini amesimama au unashinda naye? Kaa Mheshimiwa Selasini aongee Mheshimiwa Mwambe. (*Kicheko*)

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Mheshimiwa Selasini ni bosi wako bwana anaposimama mnatakiwa kuheshimiana kidogo, ahsante Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, tumemuomba.

Mheshimiwa Spika, tusipotoshe hili jambo, tukiwa sisi kwenye kamati tumeletewa malalamiko, wanasema kwamba wanaomba kujenga maghala ya kuhifadhiya korosho kwa sababu *storage facilities* zetu ni *transit*. Kwa hiyo, korosho ukiweka muda mrefu kwenye hayo maghala zinaharibika, *they go bad*. Na kwa kuthibitisha hili *SIDO* Mtwara waliamua kutunza korosho zilizobanguliwa ili wapate ile *room temperature (AC)* walikuwa wanawasha, wamewatoa wafanyakazi wote wakawa wanawasha AC, ninaweza kuthibitisha ndani ya hili Bunge na tulipowaambia wakazitoa. Wanasema wanajenga maghala ya kuhifadhiya korosho zilizobanguliwa Dar es salaam, Kurasini, kazi hiyo hajafanyika. Ndiyo maana tunaomba *CAG* aende akakague aje atueleze hapa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe tumeshakusikia. *Issue* ni kwamba anasema waliambiwa kwenye Kamati kwamba ukiweka korosho kwa muda mrefu katika maghala zinaweza kuharibika, kitu chochote ukikiweka katika muda mrefu kitaharibika. Anachosema ni kwamba katika muda huu tangu zimechukuliwa mpaka sasa hazijaharibika, katika muda huu, lakini katika muda mrefu huo mnaosema inaweza hilo likatokea.

Na kinachozungumzwa hapa ni *terminology* tu ya neno kuoza, kwa hiyo msemaji anaweza akarekebisha neno lake akaweka sawa na kwa sababu hakuna zilizooza, kwa hiyo maana yake hoja ya Mnyika imekufa, ndiyo wanachosema wenzako. Nakurudishia umalizie maana bado dakika moja tu hapo. (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. NYIKA:** Mheshimiwa Spika, kama hilo neno linawakera sana naliondoa lakini hoja yangu mimi si suala la kuoza peke yake; nimesema kuhusu mkataba wa *Indo Power*, kuhusu Serikali kukosa mapato nje (*forex*), kukosa mapato kwa ujumla wake ambayo tungeyapata kwenye mauzo ya korosho. Mambo ni mengi kweli kweli ambayo kwa pamoja yanataka kama *CAG* hamumruhusu kuchunguza basi Kamati Teule ya Bunge iundwe iende kuchunguza na hatua zichukuliwe. Wakati tukiendelea na uchunguzi wa

Bunge, Serikali iwajibike Waziri na Mawaziri wajiu zulu na kama hawajiuzulu tutaleta hoja ya kutokuwa na imani na Serikali, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mnysika, Mheshimiwa Ezekiel Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Joel Mwaka dakika tano tano, Mheshimiwa Magolyo.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi nichangie mada iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kwa kuipongeza sana Serikali kwa hatua zinazofanyika katika kuboresha sekta ya kilimo. Zimekuwepo kero nyangi kwa miaka ya nyuma lakini hivi sasa unaona kabisa kwamba hatua zinazochukuliwa zinatatua kero hizo. Kama tunakumbuka kwa wale ambao tumekuwa kwenye Bunge hili muda mrefu, shughuli kwa mfano ya bei na usambazaji wa pembejeo za kilimo limekuwa ni tatizo la muda mrefu, lakini utasikia kwa sasa na hata miaka ya baadaye, hatua ambazo zimechukuliwa za ununuzi kwa mfano wa mbolea kwa pamoja unafanya vizuri; na hii ni hatua nzuri sana ambayo kwa kweli naipongeza sana Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nipongeze vilevile Serikali kwa zao la pamba; uzalishaji unaongezeka sana, tunategemea mwaka huu kuvunja rekodi ya zaidi ya miaka mitano nyuma. Hizi ni jihada za Serikali yetu. Mimi nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Waziri na Naibu Mawaziri wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kazi hii kubwa inayofanyika wote tunaamini kwamba inatakiwa ilenge katika kuweka uhakika wa chakula katika nchi kwa ujumla wake, pia inatakiwa kuwa ni chachu katika dhana nzima ya Tanzania ya viwanda. Mimi mchango wangu upo kwenye haya maeneo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, *food security* kwa Tanzania bado kwenye baadhi ya maeneo tunapata changamoto. Kwa huu mwaka wa kilimo ambao tunaenda nao, kuna baadhi ya

maeneo ambayo hayajapata chakula vizuri kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi na hali ya hewa kusababisha mvua kutokunyesha vizuri; lakini kuna maeneo ambayo yamepata chakula. Nini *solution* ya suala hili? Kwa ujumla tumekuwa tukishauri kwamba ni vizuri tukajikita kwenye *scheme* za umwagiliaji ili kutunza maji yanayopatikana kwa muda mrefu. Suala hili kwa Mkoa wetu wa Shinyanga tumekuwa tukilizaungumza kwa muda, tukiamini kwamba si vizuri Mkoa kila wakati tukisema kwamba tuna matatizo ya njaa basi tunaomba chakula cha msaada. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013, tulipendekeza katika *RCC* kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu na Halmashauri ya Shinyanga Vijiji kwa maana ya Jimbo la Solwa na Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, maeneo yake zaidi ya asilimia 80 yanafaa kwa kilimo cha mpunga. Kwa hiyo mkoaa ubuni mpango wa kufanya kilimo cha umwagiliaji kwenye maeneo hayo. Zimekuwepo jitihada katika mkoaa lakini inaonekana kama vile kuna mawasiliano hafifu baina ya Serikali Kuu, kwa maana ya Wizara na Mkoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Msalala kwa mfano miaka miwili iliyopita tulipendekeza *scheme* zaidi ya sita. Tulipendekeza kuwepo *scheme* kwenye Bonde la Kashishi, kuna eneo linaitwa Kashishi kule, ni kubwa tu ambalo likifanyiwa kilimo cha umwagiliaji tunaweza kupata mazao vizuri. Kuna Bonde la Kabondo, Bonde la Buva, Bonde la Chela kuna *scheme* ilianza mwaka 2008, haikufanya vizuri; na kuna Bonde la Mwalugulu. Kwa bahati mbaya maeneo yote haya ambayo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji jitihada ambazo zimekuwa zikifanyika kwenye ngazi za halmashauri, hazioneshi kuungwa mkono na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikuombe sana rafiki yangu, mhasibu mwenzangu, Mheshimiwa Waziri hebu fika Msalala uyaone haya maeneo, uone jitihada ambazo tunafanya katika halmashauri ili uone namna ya kusukuma jitihada hizi ili tuwe na uhakika wa chakula. Tunaamini kabisa jitihada hizi za Wilaya na Mkoa zikiungwa mkono, tutakuwa na uhakika wa chakula. Tunataka maeneo haya ndiyo yawe

ghala la mpunga kwa mkoa mzima na tuweze kuzalisha na kuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile kama nilivyosema, kwa upande wa kuunganisha na biashara, kwenye zao la pamba viwanda vinavyoendana na zao hilo bado havijasukumwa sana. Nilitaka kuiomba Serikali kwa maana ya Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Viwanda hebu jaribuni kukaa pamoja ili kuangalia namna ya kuboresha zao la pamba kutoka zao...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Malizia Mheshimiwa

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** ...hadi linapoweza kutengeneza nguo pamoja na mafuta.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, jitihada zinazofanyika na Serikali ni kubwa na zinaonekana, naiunga mkono bajeti hii. Nimuombe sana tu Mheshimiwa Waziri aje aone jitihada zetu na tuunge mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsate sana Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige. Mheshimiwa Joel Mwaka atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate. Mheshimiwa Mwaka.

**MHE. JOEL M. MWAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, niipongeze Wizara kwa maana ya Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara kwa bajeti yao nzuri waliyotuletea safari hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kwa sababu ya muda, niende tu moja kwa moja kwenye jambo mahsusini

ambalo ningependa kuongea leo. Kilimo kwa Kanda ya Kati, sehemu kubwa tutegemee kilimo cha kumwagilia. Suala la mvua hapa Dodoma ni tatizo kubwa sana, Dodoma ina *register* mvua nyingi sana lakini zinazokuja bila mpangilio unaoweza kuwezesha mazao kukua na kutoa mazao yanayotegemewa. Kwa hiyo njia peke yake ni kulala kwenye kilimo cha umwagiliaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikizungumza suala la kilimo cha umwagiliaji, maana yake tunahitaji mabwawa. Tunayo mabwawa ya zamani ambayo yapo tayari lakini bado kuna mipango ya kuweka mabwawa mapya; hivi ndiyo vitu vya Serikali kuweza kuvishughulikia kwa ukaribu kabisa katika eneo letu hili la kati.

Mheshimiwa Spika, mabwawa ya zamani, nimebahatika mara mbili hivi kwenda na Mawaziri kwenye maeneo ya mabwawa kwenye Jimbo langu la Chilonwa. Nimekwenda kwenye Bwawa la Bwigiri, Bwawa la Ikoa na Waziri, wakati Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Kamwele, lakini na juzi nimekwenda na Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Ommary Mgumba. Hoja ya wananchi kwamba mabwawa yanafukulika ilichukuliwa na Serikali na kusema kwamba wanayafanyia kazi hatuoni mrejesho wowote juu ya mabwawa haya.

Mheshimiwa Spika, ninalomba Serikali, iwasaidie wananchi wa eneo hili ili waondokane na tatizo hili wanadolizungumza Waheshimiwa Wabunge wengine waliopita, la kila wakati kulia njaa ilhali Dodoma ina ardhi nzuri inayokubali mazao yote, Dodoma unalima kila aina ya zao.

Mheshimiwa Spika, nimeshangaa, sasa hivi Jimboni kwangu wanavuna pamba, sikuamini wakati tunaambiwa tupande pamba lakini sasa hivi wanavuna pamba, maeneo ya Segala kule, nimekwenda nimeshangaa na macho yangu. Kwa hiyo kila zao linakubali ila shida ni maji. kwa hiyo, tunaomba sana masuala ya mabwawa haya, hebu yapate

mrejesho unaoeleweka ili wananchi wawe na uhakika wa kulima. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, niende pia kwenye suala la mafunzo kwa wakulima hawa. Wakulima wanahitaji kupewa mafunzo ya nini cha kufanya kwenye maeneo yao mbalimbali. Si kila ardhi inakubali kila zao, basi wapewe elimu ya eneo hili hapa wajue afya ya udongo wa eneo walilopo inakubali mazao gani ili waweze kupanda hayo mazao. Vilevile, hata ikibidi watumie mbolea basi watumie mbolea gani katika udongo ule badala ya kutumia kila mbolea kwa kila zao kila sehemu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda basi nichukue nafasi hii kwa heshima na taadhima niunge mkono hoja kwa asilimia 100, ahsante sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana kwa kunitunzia muda. Mheshimiwa Innocent Bilakwate atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Kilimo. Kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Kilimo na Naibu Waziri kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kwenye sekta hii. Pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuwa msaada mkubwa sana kwa wakulima wetu wa Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, moja kati ya maeneo muhimu sana ambayo nilitaka nichangie kwa maslahi ya muda ni uelewa ambao tunatakiwa wote tuwe nao. Moja, Mheshimiwa Waziri ujue kwamba hakutakuwa na Mapinduzi ya viwanda nchini kama hatutakuwa na Mapinduzi ya kilimo ni kwa sababu asilimia 65 ya malighafi yanayokwenda viwandani yanatoka kwenye kilimo. Pili, hatutakuwa na mapinduzi ya kilimo kama hatutakuwa na mapinduzi kwenye mfumo wa kufikisha pembejeo kwa wakulima wadogo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anafahamu vizuri, wakulima wetu wengi wapo vijjini, na pembejeo za kilimo kwa maana ya mbolea, mbegu bora na viuatilifu vinapatikana mjini. Ili huyu mkulima aweze kuzalisha kwa tija ni lazima atumie mbolea nzuri, mbegu bora na atumie viuatilifu. Kama hivi vyote vinaendelea kupatikana mjini maana yake huyu mkulima mdogo ni lazima asafiri kupata hii huduma, na unamuongeza gharama za uzalishaji. Akishazalisha zao Lake, anakuja kuliiza kwa gharama kubwa kwa sababu anataka kufidia gharama.

Mheshimiwa Spika, mfumo ambao Serikali unaufanya ni mzuri, wa kuhalikisha kwamba vijjini kunakuwa na maduka madogo madogo ya wauza pembejeo. Maduka haya vijjini yatauza mbolea, mbegu bora na viuatilifu.

Mheshimiwa Spika, changamoto tunayoipata kwenye hii sekta ya kilimo ni gharama za kufungua haya maduka vijjini, wajasiliamali wengi vijjini wamejengewa uwezo na uelewa wa umuhimu wa kuuza pembejeo vijjini ili mkulima mdogo aweze kupata huduma kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, sasa vyeti vinavyotokana na kupata hicho kibali ni gharama kubwa sana. *TOS/C* peke yake wanataka 100,000, *TFRA* wanataka pia fedha lakini *TPRA* wanataka 320,000, *TFDA* wanataka 100,000, kabla hujafungua duka la pembejeo kijjini, lazima uwe na shilingi zaidi ya 600,000; hapo hujaweka shelves dukani, hujanunua bidhaa. Sasa mjasiri amali gani wa kijjini atakuja kuwekeza kwenye hii biashara ili kumsaidia mkulima mdogo kupata huduma kwenye sekta hiyo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, ili tupate mapinduzi ya kilimo, Mheshimiwa Waziri azipitie tena hizi tozo na gharama, ikiwezekana aziondoe, kama haiwezekani basi zipunguzwe kwa kiwango ambacho kitamsaidia mjasili amali mdogo aweze kuwa msaada kwenye hii *value chain* ya *inputs* kwa maana ya pembejeo, tusipofanya hivi tutaendelea kuwatesa wakulima na hatutapata majibu. Ninayo mifano halisi, Kigoma peke yake zaidi ya wajasiri amali

159 wamejengewa uwezo lakini wameshindwa kufungua maduka kwa sababu hawajakidhi viwango vyta kuwa na yeti kwa sababu ya gharama.

Mheshimiwa Spika, ukienda Mkoa wa Kagera wakulima 461 wamejengewa uwezo kupitia Shirika la *Agra*, lakini ni wakulima 139 tu wameweza kulipia gharama hizi na kufungua maduka vijijini, tutapata wapi mapinduzi ya kilimo kama hatutaki kuwekeza kwenye mfumo wa pembejeo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Joseph Mhagama, unachangia kisayansi kweli kweli. Sasa Mheshimiwa Rehema Migilla upande wa *CUF*, una dakika saba.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi nami nichangie kidogo kwenye hii Wizara. Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu wataala*, kwani bila yeze sisi hatuwezi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba moja kwa moja nijikite kwenye mada. Ni ukweli uliowazi kwamba sekta ya kilimo inachangia kwa asilimia kubwa sana katika kutoa ajira kwa watu wenye elimu na hata wasiokuwa na elimu. Hata hivyo, sekta hii imekumbwa na changamoto kubwa sana hususan kwenye changamoto ya masoko *especially mazao* ya biashara.

Mheshimiwa Spika, nitajikita zaidi kwenye zao la tumbaku. Mkoa wa Tabora kama ilivyo mikoa mingine inayolima tumbaku umekumbwa na tatizo kubwa kabisa la zao la tumbaku kuwa linadorora siku baada ya siku. Yote hii inasababishwa na kauli mbalimbali kwamba zao hili linasababisha kansa na kauli nydingine mbalimbali ambazo hazina tija kwa mkulima. Mimi naona tatizo kubwa sio hizi kauli, tatizo kubwa lipo kwenye Serikali na nini kinasababisha, kinachosababisha mpaka hili zao kuzorota ni kupotea kwa

hawa wanunuzi wa zao la tumbaku baada ya kuwa kuna milolongo mingi ya kodi na tozo zisizokuwa na faida kwa hawa wanunuzi.

Mheshimiwa Spika, mfano, ni hii *export levy*; sasa hivi *export levy* imepanda kutoka 0.25% mpaka 1% kwenye *export value* sasa kama hii tozo inapanda kwa kiasi hicho inamkandamiza sana na kumuumiza huyu mnunuzi hali inayopelekea mpaka aamue asinunue mazao yetu. Hii *impact* yake ni nini? Tumeona kuna kampuni moja ya kununua tumbaku sasa hivi imefunga oparesheni kutokana na kwamba imeshindwa ku-*afford* hizi gharama.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Serikali kushindwa kurudisha hii *VAT returns*, suala la *VAT returns* ni suala ambalo lipo kisheria na kikatiba na inapaswa kila mwaka lirejeshwe kwenye haya makampuni ya *net exporters*, lakini sasa hivi kwa miaka kama mitatu mfululizo huko nyuma hii *VAT returns* hairudishwi. Sasa tunajuliza kama huko nyuma *VAT returns* ilikuwa inarudishwa nini kimesababisha mpaka dakika hii *VAT returns* ambayo ndiyo ilikuwa inawa-*bust* hawa wanunuzi waweze kununua tumbaku kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaomba Wizara ituambie je, hii *export levy* ambayo imepanda kwa kiasi hicho itairudisha lini lakini vile vile hii *export value* na yenye we itarudishwa lini na *VAT* kwa sababu tunaona wakulima wetu hawajui hatima yao ni nini, leo makampuni ambayo yanafunga operesheni zao tunaona kuna *redundancy* kubwa ya wafanyakazi, lakini tunaona pia halmashauri nyingi mfano Tabora Mjini, Urambo wapi zinakosa cess, lakini pia wakulima sasa hivi mpaka wanapewa *limitation*, badala ya kulima kama walivyokuwa wanalima zamani sasa hivi anaambibiwa lima tani kadhaa au kilo kadhaa kitu ambacho kinaikoseshwa hata Serikali yetu mapato ya *forex*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwenye korosho; korosho ndiyo limekuwa zao mbadala kwa Mkoa wa Tabora baada ya kuonekana zao la tumbaku linasuasua kwa kiasi kikubwa sana. Hata hivyo, zao hili linapelekwa kisiasa siasa

zaidi hali ambayo inawakatisha tamaa wakulima kuingia kwenye hicho kilimo cha korosho. Naomba sasa hii Wizara ili zao hili liweze kulimwa na wengi na liwe lenye tija basi kwanza tunaomba elimu itolewe juu ya zao la korosho. Pia suala lingine hii miche kule kwetu inauzwa sasa kama inauzwa watu wanashindwa kununua badala ya kupewa bure, leo wanauziwa mche mmoja ni shilingi 1,000. Kwa hiyo tunaomba hii kama inawezekana wapewe bure ili waweze kupata *moral*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni vitambulisho nya wakulima na hii bima ya wakulima. Hili suala ni zuri sana kwani litawawezesha wakulima wetu kuwa na wenyewe wanatambulika juu ya kilimo chao, lakini tunaona tu kuna *story story* tu kwenye hiki kitabu cha Waziri kwamba mpaka dakika hii hakuna kanzidata inayoonesha ni wakulima wangapi wa tumbaku ambao wamesajiliwa kwenye hiyo kanzidata yake.

Mheshimiwa Spika, pia suala lingine ni kwenye hii bima ya wakulima. Tunaelewa kabisa kwamba sasa hivi kuna mabadiliko makubwa sana ya hali ya hewa, mafuriko yamekuwa ni mengi, ukame umekuwa wa kutosha, sasa hivi wakulima wetu wanalima kilimo cha mashaka mashaka sana. Kama kweli hii bima itatolewa kwa hawa watu wetu basi nina uhakika kabisa hili suala ni zuri na namwomba Waziri waliendeleze ili wakulima wetu sasa pindi wanapolima wawe wana uhakika kwamba hata ikitokea janga Fulani, basi wawe na uwezo wa kufidiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ni kwenye suala la pembejeo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rehema Migila. Mheshimiwa Deusderius Mipata atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Kishimba.

**MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima, lakini pia niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa hotuba nzuri sana hii walijotuletea, lakini pia kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mchango wangu utakuwa katika maeneo mawili.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni juu ya upatikanaji wa pembejeo na bei zake, sijaridhishwa sana na jinsi mbolea au pembejeo za kilimo zinavyopatikana kwa wakulima bado kuna changamoto nyingi. Mbolea hazipatikani kwa wakati, pembejeo za mbegu na madawa feki ni nyingi kupita kiasi na wakulima wanakula hasara sana na kwa sababu ni shughuli ambayo na sisi wenyewe tunafanya Wabunge nami ni mmojawapo, nashuhudia kwa ushahidi mimi mwenyewe wakati mwengine unanunua madawa yatafanya kazi na wakati mwengine hayafanyi kazi kabisa. Kwahiyo bado kuna changamoto kubwa sana katika suala la utafiti na wataalam wetu waweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo hayo nataka niwe na mchango ufuatao, kwamba, vituo vya utafiti viimarishwe, tusitegemee sana vituo vya utafiti au mbegu na pembejeo za kutoka nje, hizi zinatusumbua na zinaleta hasara kubwa sana kwa wananchi wetu. Pale kwetu Rukwa pale kuna kituo cha Utafiti cha Mirundikwa kina changamoto nyingi sana, tuna ardhi ya kutosha lakini hawana wafanyakazi wa kutosha, hawana fedha, hawana matrekta, wakisaidiwa hawa watasaidia wakulima wa Mkoa wa Rukwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nafikiri ni muhimu sana katika hii ni pembejeo. Matrekta tumeambiwa yapo hapo Bagamoyo yapo matrekta mengi, lakini hii habari haijafika vizuri kwa wakulima wetu, hawajui, utaratibu uliowekwa na Serikali ni mzuri sana, lakini watu hawana *information* ya kutosha juu ya namna ya kupata hayo matrekta na kwa utaratibu uliowekwa na Serikali ni mzuri kabisa. Kwa hiyo, bado kuna habari ya hamasa ifike kwa wakulima. Kule kwetu kuna vikundi vingi sana hasa Mkoa wa Rukwa vikundi vingi sana vinajihuisha na kilimo, Nyanda

za Juu Kusini kwa ujumla wake, lakini hawajapata habari kwamba kuna trekta zipo ambazo wakijiunga kwenye vikundi vikiandikishwa wanaweza wakapata na wakaboresha kilimo chao. Kwa hiyo niipongeze Serikali kwanza kwa uamuzi huo, lakini natoa wito kwa Serikali wataalam wetu watoe wito na elimu zaidi kwa wakulima namna ya upatikanaji wa hizo trekta ili waweze kunufaika na wazo hili zuri la Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni masoko ya mazao; Nyanda za Juu Kusini sisi ni maarufu wa kulima nafaka, lakini siku zote katika miaka miwili mitatu hii yamekuwa ni mateso. Watu wanalima na wanaendelea kukata tama, kwa sababu hatuoni soko la mazao, tunajua wazi kwamba Serikali si wajibu wake kutafuta kununua mazao ya kilimo kama wanavyotusaidia *NFRI* lakini ni wajibu wa wataalam wetu kuhakikisha kwamba mazao yanayolimwa na wakulima wetu yanapatiwa masoko nje na ndani ya nchi yake. Hakuna sababu kufunga mipaka, mwaka huu ni mbaya sana, nafaka inaweza kuwa kidogo, lakini wazo watakalokuwa wanalfikiri sasa hivi watu wa Serikali ni kufunga mipaka badala ya kuacha watu wanufaikie na uzalishaji ambao sasa umetolewa kwa muda mrefu. Naomba kabisa kabisa mwaka huu msithubutu kufanya jambo hilo. Wawaacie watu wanaofanya kazi waweze kunufaika na mazao yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mipata. Nilikwishakutaja Mheshimiwa Jumanne Kishimba, dakika tano, utafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Kilimo. Kwanza nawapongeza Manaibu Waziri na Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa wanayofanya kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, leo suala langu ni gumu kidogo ingawaje kabla sijaanza watu wanaanza kucheka. Mimi nakuja na suala la bangi, nchi nne za Afrika sasa hivi

zimeruhusu kilimo cha bangi kwa ajili ya matumizi ya dawa za binadamu. Ni vizuri wakati wowote wakati dunia inapopata nafasi...

**SPIKA:** Hebu Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, yanapoongelewa mambo ya maana na muhimu tunasikiliza, Katibu weka vizuri dakika zako hebu anza vizuri, Mheshimiwa Kishimba endelea.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Spika, ni vizuri sana wakati dunia inapopata kitu kipyaa na sisi Watanzania kuwa wa kwanza kuwahi kama wenzetu wanavyowahi. Ninavyoongea gazeti la Mwananchi la tarehe 18 mwezi wa Tano Jumamosi, nchi ya Uganda imekwisharuhusu kulima bangi kwa ajili ya dawa za binadamu. Dawa nyingi za maumivu hasa za kansa Mheshimiwa Waziri wa Afya, Naibu Waziri wa Afya Mheshimiwa Ndugulile anafahamu vizuri kwamba nyingi kwa asilimia 80 zinatokana na bangi.

Mheshimiwa Spika, nashangaa kwa nini wataalam wetu wa *TFDA* wangkuwa wameshachukua sampuli muda mrefu wakati wanaziangalia kwenye maabara, wangetujulisha kwamba ndani ya hizi dawa kuna bangi na wangemuuliza *supplier* hii bangi unapata wapi. Maana yake sisi wenyewe tunayo bangi na ukiangalia vizuri bangi tunayoona kila siku inakamatwa kukatwa ukweli bangi hiyo siyo kwa ajili ya kuvuta, bangi hiyo imekuwa ikienda kwenye dawa za binadamu. Ushahidi ninao Lesotho na Zimbabwe wameruhusu na mimi nimefika kwenye kiwanda cha Zimbabwe ambacho kinatengeneza dawa za binadamu kwa kutumia *material* ya bangi.

Mheshimiwa Spika, gunia moja la bangi leo Tanzania ni shilingi milioni nne mpaka milioni nne laki tano, lakini Lesotho na Zimbabwe ni dola elfu saba, karibu milioni ishirini na bangi yote hii ya Tanzania yote inakwenda kwenye madawa ya binadamu ambayo sisi tunaletewa kuja kutumia kwenye hospitali zetu. Sasa kuna ubaya gani Serikali ikaanza kutoa *permit* au vibali watu kwenye maeneo mbalimbali na

kuhalalisha watu waanze kulima bangi hiyo ili tuweze kupata faida na kuondoa mgogoro mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siwezi kuungana na Mheshimiwa Musukuma kwenye suala la kuvuta, suala la kuvuta sheria iendelee palepale kwamba watu hawaruhusiwi ,lakini kwa kuwa sasa ni halali kwa ajili ya madawa ya matumizi ya dawa za binadamu, tuna sababu gani ya msingi sisi kutowahi hilo soko? Hata kama tutakataa leo, baada ya miaka minne wakati bei itakuwa imeanguka hata tukiruhusu haitatusaidia. Ni vizuri Waziri wa Kilimo awasiliane na Waziri wa Afya waone namna gani watafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ilivyo bangi ni zao ambalo kwanza haliliwi na wadudu, hakuna wadudu wanaokula bangi na eka moja ya bangi unapata gunia sita. Kama ni gunia sita kwa bei ya millioni 20, ni millioni 120 lakini leo wananchi wetu wanauza milioni nne na ndiyo zao peke yake Tanzania kwa leo ambalo mkulima akiwa amepewa *advance*, Mheshimiwa Heche naona ametoka. Kwa hiyo badala ya kuendelea na mgogoro huu tunaomba Wizara ya Kilimo wafikirie *contract farming* ya bangi ambayo sasa inaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi ya Canada imeruhusu, yenewe imeruhusu kuvuta, lakini Canada ni mionganii mwa nchi saba tajiri na Mheshimiwa Waziri wa Fedha nafikiri anatarajia kuomba pesa huko akipewa pesa za bangi atakataa na atazijuaje kwamba hizi ni za bangi. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri ni vizuri sana, tumeona tumepoteza vitu vingi sana kwa ajili ya kuchelewa. Tulikuwa hapa meno yetu ya tembo yanakwenda Burundi kwa miaka 30, mpaka mwishowe biashara ya meno ya tembo imekwisha. Tumeshuhudia dhahabu zetu zikienda tunachelewa sana sana kufikiri, juzi hapa kwenye Uwanja wa Ndege wa Entebbe tarehe 11 Machi zimekamatwa tani saba za dhahabu. Ukiangalia tani saba za dhahabu Uganda haina dhahabu, dhahabu hizo zimetoka Tanzania, lakini namna hii

hii tunachelewa baadaye dunia inabadilika si tunaendelea kulima matikiti maji. Tunaomba na uzuri kama Waziri wa Kilimo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali yuko hapa kama watapitisha hili na Wabunge nafikiri watakuwa watu wa kwanza kabisa kujisajili na hali yetu kama unavyoijua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, huyu anaitwa Professor Jumanne Kishimba. Sasa niwape siri Waheshimiwa Wabunge mnaojiandikisha kuzungumza mnatakiwa muwe mnaongea kama Kishimba. Yaani kwamba siku unapoamua kuongea unakuja na kitu chako fulani sio unajiandikisha tu ili mradi utumie dakika zako tano unapigapiga kelele, hii hoja ni nzito sana hii, magazeti yasije yakaandika Ndugai ameunga mkono lakini kwa kweli ni hoja nzito. (*Kicheko*)

Naamini Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Jenista Mhagama hii ameipigia mstari. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Timotheo Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Selasini ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, lakini na kazi wanayoifanya yeye na Manaibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, nina mambo machache sana leo ya kuzungumza, mambo kama mawili tu. Jambo la kwanza ningombwa kuchangia kwenye kilimo cha mkonge, kwa mwaka 2014 - 2018 kwenye mkonge tumezalisha tani 190,649. Katika hizo Mkoa wa Tanga peke yake umezalisha tani 106,221 na katika Mkoa wa Tanga Wilaya inayoongoza kwa kuzalisha mkonge ni Wilaya ya Korogwe hasa Halmashauri ya Korogwe. Hata hivyo, tumekuwa na changamoto kadhaa kwenye zao la mkonge, changamoto kubwa ya kwanza ni usimamizi usioridhisha wa taasisi inayosimamia zao la mkonge. Pia ushiriki mdogo wa taasisi zetu za utafiti kama ile ya pale Mlingano kwenye kusaidia kuendeleza zao la mkonge.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumekuwa na wakulima wadogo wengi kule Korogwe na Mkoa mzima wa Tanga, lakini tuna changamoto kubwa sana. Wakulima walio wengi hata mbegu wanaokota kutoka kwenye mashamba ya mkonge ya muda mrefu kwenda kupanda kwenye mashamba yao. Mbegu hizi zinafanya mkonge huu usiweze kuwa na muda mrefu wa kuvunwa lakini tungeweza kuvitumia vizuri vyuo vyetu vya utafiti na taasisi za utafiti kama pale Mlingano tungeweza kuwa na mbegu bora na wakulima wetu wangelima na wangeweza kuvuna mkonge kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, inawezekana changamoto kubwa inayotusumbua ni fedha. Kwenye zao la mkonge kwa miaka mingi tunapata *service levy* 0.3%, lakini kwa mujibu ya Sheria ya Fedha kwenye mazao haya ya biashara tunapaswa pia kuwa na ushuru wa mazao *produce cess* lakini kwa mujibu wa Sheria ya Fedha *produce cess* anayepaswa kuilipa ni mnunuzi.

Mheshimiwa Spika, sasa wakulima hawa wakubwa wa mikonge ambao wanazalisha singa wenyewe mnunuzi wanamkuta nje, ambapo kule nje wanamkuta wakala hakuna nani ambao; kwa hiyo ni vigumu sana kupata *produce casse* wanapoleka mkonge kule nje; na hata halmashauri zetu zimekuwa zikikosa sana mapato kwa sababu hii.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia vizuri kama tungekuwa tunapata *produce cess* 2014 mpaka 2018 tungepata zaidi ya bilioni tisa kwenye *produce cess* peke yake. Kwenye *service levy* tumeypata takriban shilingi milioni sita na kitu. Nilikuwa naiomba sana Serikali tuangalie namna, hapa hatuombi kuibua kodi mpya, hii kodi ipo kwa mujibu wa sharia. Changamoto tuliyonayo ni namna ya kupata fedha hizi; kwa sababu mnunuzi anayepaswa kulipwa yuko nje ya nchi na hajumo ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tuna mfumo mpya sasa hivi; na ninampongeza sana Mheshimiwa Mkuu wetu wa Mkoa wa

Tanga, ametusadia sana na ametusaidia kupata haki na faida kwa wakulima wadogo wa mkonge. Tuna wakulima wadogo wa mkonge ambao wanauza mazao yao ya mkonge kupitia vyama vyao via ushirika na mnunuzi anapatikana kwa kushindanishwa kwenye mnada. Sasa tunapopata mnunuzi anayeshindanishwa kwenye mnada ananunua mazao ya wakulima hawa wadogo wa mkonge yule mnunuzi analipa *produce cess* kwa sababu ye ye anakuja kununua ndani; lakini hawa wakulima wakubwa wanaopeleka nje hawalipi, hatimaye hii ita-*discourage* hawa wanunuzi wanaokuja kununua mazao ya wakulima wadogo...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, heeeee naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Janet Mbene atafuatiwa na Mheshimiwa Selasini na Mheshimiwa Taska Mbogo ajiandae.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Napongeza, hotuba ni nzuri ya kimkakati na naamini itaenda kujibu hoja nyingi ambazo zilikuwa zimeleta wasiwasi mkubwa sana katika sekta hii. Bado nasikitika tu kuwa Wizara hii bado inapewa bajeti ndogo ukilinganisha na mahitaji, na hasa ukichukulia kuwa ni sekta ambayo kwa kweli ingetutoa katika umaskini kabisa katika nchi yetu. Mimi ninaamini hivyo na nafikiri hata *data zinaonesha* kuwa kweli hii Wizara hata ingepata trioni moja tu ingefanya mambo makubwa sana kwa sababu ndio inayoajiri asilimia kubwa sana ya watanzania wakiwemo akina mama na vijana. Vilevile ndiyo inayolisha taifa zima na ingeleta fedha nyingi sana za kigeni ambazo zingetuwezesha sasa kufanya mambo mengine makubwa zaidi ya miundo mbinu na kadhalika, hayo ndio maoni.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi nataka kuzungauamzia sana suala zima la kilimo chetu, kwamba kimejikita sana kwenye mvua; na kama tunavyoja mvua huwezi kuitegemea kiasi hicho. Tumekuwa na *scheme* nyangi sana za umwagiliaji lakini kwa bahati mbaya *scheme* hizi zote zilikuwa zinasimamiwa kwa kiasi kubwa na fedha za nje, na hata hao wahisani wenyewe kuwa ndio waliokuwa wanaweka wakandarasi kuja kuendesha hizo *scheme* na nyangi hazikufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuomba sana Serikali ihakikishe kuwa inaweka fedha ya kutosha katika *scheme* za umwagiliaji; lakini vilevile waangalie ni kwa jinsi gani wanaweza kuwasaidia wananchi wakulima wadogo wadogo katika kuanza utaratibu wa kuvuna maji ya mvua. Mvua huwa inanyesha nyangi sana kwa vipindi tofauti nchi kwetu lakini inaishia chini. Kama wananchi wangekuwa wanafundishwa jinsi kuvuna maji ya mvua kwa sehemu zao wenyewe walizopo ingesaidia hata kwa kiasi kikubwa sana kukidhi mahitaji ya maji katika maeneo yao na wengeweza kumwagilia, kufuga na kufanya shughuli zile zingewaletea kipato.

Mheshimiwa Spika, nataka nije kwenye suala zima la mazao ya kimkakati. Kuna mazao makubwa ya kimkakati ambayo yametajwa na katika mkoa wangu wa Songwe na hasa Wilaya ya lleje; kuna mazao matatu ya kimkakati katika Tanzania lakini Wilaya yangu inayalima kwa wingi ikiwa ni pareto, kahawa, alizeti na bado kuna fursa ya kuzalisha mazao mengi kwa sababu ya hali hewa, udogo uliopo kule na watu wenyewe wanajituma sana katika kufanya kazi. Tatizo letu kubwa ni huduma za ugani. Huduma za ugani ni ndogo, tunahitaji wataalamu wengi sana wa kutuongoza katika kila kijiji.

Mheshimiwa Spika, vilevile suala lingine ni masoko; bado masuala ya masoko hayajakaa vizuri. tunajua Serikali imefanya makubwa sana na kwa kweli wametusaidia kwa kiasi kikubwa sana katika kuonyosha ule mfumo mzima wa soko lakini bado haujakamilika, bado kuna changamoto

nyingi, kuna tozo nyingi na bado kuna tatizo la miundombinu ya kuyafikia masoko yale.

Mheshimiwa Spika, tungependa kuona sana Serikali ikihakikisha kuwa katika hata maeneo ambayo yana fursa nzuri za uzalishaji kama lleje, Mbozi na Mkoa mzima wa songwe basi inaturahisishia miundo mbinu ambayo itawawezesha wananchi kufikisha mazao sokoni.

Mheshimiwa Spika, Vilevile Kuhusu Elimu Pamoja na Pembejeo Bora. Tuna matatizo makubwa ya pembejeo za kuwezesha mazao yetu kuwa na ubora na uzalishaji mwingi. Bado tuna fursa kubwa sana katika soko la dunia kwa kahawa na pareto. Pareto kwa Afrika tunaongoza sisi Tanzania, hiyo ingekuwa fursa kubwa sana kwetu kuhakisha kuwa tunawekeza nguvu zaidi katika zao hili kwa sababu tayari sisi tuna hilo fursa kitaifa. Kwenye kahawa vilevile kuna masoko maalum ambayo tungeweza kuyalenga kwa mfano masoko ya *organic*, masoko ambayo yangeweza kuwa...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Malizia Mheshimiwa dakika moja.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo ningependa sana kuona Wizara hii ikijikita kimikakati katika yale maeneo ambayo yana mazao ambayo tayari yanadvantage ya kuzalishwa kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Janet, ahsante sana tunakushukuru Mheshimiwa Joseph Roman Selasini dakika kumi.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika wangu katika mambo ambayo utakumbukwa kuyafanya kwenye Bunge hili ni pamoja nakutengeneza Kamati ya iliyochunguza fujo zilizotokana na gesi kule kusini. Kamati iliyochunguza

madini ya Tanzanite na kamati iliyochunguza madini ya Almasi.

Mheshimiwa Spika, nimetazama picha Mheshimiwa Rais akiwa ameshika pajili uso anaonyesha kutafakari sana. Picha ile inaonesha amezeeka kuliko alivyoapishwa. Inaonekana Mheshimiwa Rais ana mawazo mengi. Sasa kutokana na hiyo hilo nillosema kwanza na hili la Mheshimiwa Rais naomba niseme yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Bunge hili kuishauri Serikali, kazi ya Bunge hili ni kuisimamia Serikali. Tunafanya makosa makubwa sana kufanya siasa ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niseme nimekuwa msafirishaji wa korosho kwa miaka mingi. Maana Wabunge hapa hawajaambiwa waeleze vitu wanavyofanya. Wapo watu wanasmama hapa wanatetea mambo mabaya yanayofanyika kwa sababu tu wanalima korosho. Mimi nimesafirisha korosho, na kutokana na hilo nataka niwambie, karosho inaoza kama vitungu. Korosho iliyoza maji maji yake yakigusa korosho nytingine inaoza.

Mheshimiwa Spika, nimetangulia kukusifu kwa kutengeneza hizi kamati kwa sababu nataka nikuombe; kama kuna ubishi ndani ya Bunge hili kwamba korosho zimeoza au hazijaoza tengeneza kamati ya watu wachache waeendee wakakague kwenye maghala. Nataka nikwambie korosho imeoza kwa asilimia 30, na hakuna ubishi. Narudia; kama kuna ubishi, Mheshimiwa Spika wetu, Mheshimiwa Spika wangu, sisi ndio tunaosimamia Serikali tengeneza watu waende wakaone wakuletee taarifa. Kwa sababu tukizubaa zikiendelea kuoza hata hizo zilizopo tutapata hasara kubwa zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Gazeti la *Nation* la Kenya la tarehe 12 Mei lilikuwa na kichwa cha habari kinachosema *President Magufuli* aingizwa chaka na lilikuwa tunazingumza juu ya hii kampuni ya *Indo Power* kwamba hii kampuni ni ya kitapeli sasa tunazungumza kampuni ambayo ilisimama kama *middle*

men ikaja ikaidanganya nchi, ikaidanganya Serikali yote kwamba ina uwezo; na Serikali yetu, ya nchi yetu ikaingia mikataba na kampuni ambayo kumbe haina uwezo ilikuwa inaenda kutafuta kampuni nytingine.

Mheshimiwa Spika, ulikuwepo wakati wa sakata la *Richmond* na Mheshimiwa Mwakyembe ndiye alikuwa Mwenyekiti katika kuchunguza sakata lile. Kampuni ya *Richmond* haikuzalisha umeme; ilionekana kwamba haina uwezo, viongozi waliwajibika hapa. Kampuni ya *Indo Power* imekuja kutudanganya hapa, tumeingia hasara, hapo ndipo inaingia hoja ya Mheshimiwa Mnyika. Hakuna sababu ya taarifa, hakuna sababu ya miongozo; sisi kama Wabunge tuna wajibu wa kuangalia ni wapi tulipokosea.

Mheshimiwa Spika, sakata la korosho litadumu kizazi hata kizazi kwa sababu maghala sasa yamejaa, msimu unakuja, hakuna maghala ya kuweka korosho, wakulima wanadai, kwa hiyo kutakuwa na hasara mfululizo katika jambo hili, na hii inaenda kuwa kashfa kama za *EPA, ESCROW* na *Richmond*. Ndiyo maana sisi tunasema, kwa unyenyekevu wote, suala hili la korosho kama tulijikwaa, kama tuliteleza tusiendee kuvutana bila sababu ya msingi taifa likaendelea kupata hasara na wananchi wakaendelea kupata hasara; kwa sababu ukweli wa tatizo upo. Ndiyo maana naungana na wanaosema Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali kama Mheshimiwa Spika utaona haifai uchague watu wachache wakaangalie basi Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali aende akachunguze ili aje aliambie Bunge fedha zilizopelekwa kwenye utaratibu huo ni kiasi fulani zimetumika hivi watu fulani hawakutumia vizuri fedha zilitoka wapi na tumepata hasara kiasi gani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninasikitika sana kuwa suala ambalo linahusu maslahi ya taifa kulifanyia siasa. Bunge linapotoka kabisa, na Spika una uwezo, na umeshafanya mambo mazuri nayakaleta matokeo mazuri. Hili lipo mikononi mwako tusiache wananchi wetu wakateseka tu na majibu kwa sababu watu tunataka kufanya siasa.

Mheshimiwa Spika, baada yakusema haya ninakuomba sana nizungumze pia habari ya kahawa. Zao la kahawa limefanya mambo mengi mazuri katika nchi hii. Wale mlosoma Sekondari ya Lyamungo ilijengwa na KNCU kwa sababu ya kahawa; wale ambao wanaosoma sasa Chuo cha Ushirika Moshi na waliosoma Chuo cha Ushirika Moshi kilijengwa na wakulima wa kahawa; kilijengwa kutokana na mapato ya kahawa. Hoteli ya *KNCUpale* Moshi, *Moshi Curing* yote kahawa ilifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini zao la kahawa Mkoa wa Kilamanjaro linakufa na linauawa kwa sababu ya ushirika. Ushirika wa KNCU uliingia kwenye kashfa ya namna mbalimbali. Mali za ushirika zilifujwa, mashamba ushirika yalifujwa, wananchi walidhurumiwa na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini yapo matatizo mengine yanayotokana na kwanini zao la korosho linakufa. Bei ni ndogo kwa sababu hatuna masoko ya nje hatuna ya ndani mazuri, na kwa sababu hiyo wakulima wanakata tamaa. Katika Wilaya ya Rombo katika Jimbo langu la Rombo baadhi ya wakulima wamekataa tama. Wanang'oa ile mibuni wanapanda makabichii, nyanya na kadhalika; jambo ambalo si zuri kabisa kwa sababu hata mimi nimesoma kwa kahawa na juu thamani ya kahawa.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaiomba Serikali, jinsi ilivyopeleka nguvu kwenye zao la korosho, jinsi inavyopeleka nguvu kwenye zao la pamba iwakumbuke wakulima wa kahawa wa Rombo na wa Mkao wa Kilimanjaro na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, tuna shida ya Maafisa Ugani; ni wachache na ajira zao zinatoka kwa kusua sua. Wapo wazee wetu ambao wamestaafu wapo kule vijiji ambao wanaweza wakaletwa sasa kwenye mfumo. Wapo vijana ambao wamemaliza shule ambao kwa bahati mbaya hawajaajiriwa bado pia wanaweza wakaletwa kwenye mfumo kwa kujitolea. Wakati mwininge wakulima wale wakiwalipa wao

wenyewe; Serikali iangalie namna ya kutengeza progamu ili wawalete hawa watu ili waweze kulisaidi lile zao.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna hoja ya pembejeo kuwa ghali, madawa yako juu na kadhalika na kadhalika. Liangaliwe hilo ili Serikali isaidie pembejeo ziwe naafuu wananchi waweze kununua pembejeo vizuri waweze kuamsha lile zao la kahawa.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya mwisho ni kuhusu umwagiliaji. Tunapoteza maji mengi sana katika nchi hii. Mvua inayonyesha maji...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Malizia Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** ...maji yanapotea. Kwa hiyo nilikuwa naomba Serikali na Wizara ingalie uwezekano wa ku-*tap* haya maji ya mvua ili yaweze kuwasidia wananchi katika kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninakushuru, ahsante sana, na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, Mheshimiwa Taska Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Mtuka. Mheshimiwa Taska!

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu na kumpongeza Waziri Hasunga na Manaibu wake Mheshimiwa Mgumba na Mheshimiwa Bashungwa kwa jitihada zenu za kubadilisha kilimo nchi Tanzania.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye Mkoa wangu wa Katavi. Mkoa wangu wa Katavi sisi asili yetu ni wakulima. Mkoa wa Katavi una *Squire* mita 47,586 ambapo

asilimia 58.6 ni misitu pamoja na Mbuga za wanyama na asilimia 44 tunatumia kwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wangu huu wa katavi una mapungufu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, pungufu la kwanza hatuna Maafisa Ugani. Mkoa unahitaji Maafisa Ugani 248; kwa sasa una Maafisa Ugani 164. Tuna upungufu wa Maafisa Ugani 16 Mleleji DC, 42 Mpanda DC, 34 Mpanda DC, 41 Nsimbo DC na 31 Mpimbwe DC; jumla tuna upungufu ya Maafisa Ugani 164. Ninaomba Wizara ya Kilimo mtuletee maafisa ugani.

Mheshimiwa Spika, mkoa wetu una changamoto za miundombini; tukipata maafisa ugani wataweza kwenda vijijini; na mkoa wetu pia vijiji vyake havipo karibu; umbali wa kutoka kijiji kimoja kwenye kijiji kingine ni umbali kama wa kilometra 10 mpaka kilometra 20 ndipo unakuta kijiji kingine. Nikuombe Mheshimiwa Waziri utupatie Maafisa Ugani ili waweze kuusaidia mkoa wetu wa katavi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ninalotaka kuomba pia; kwa sababu mkoa ni mpya naomba Wizara ya Kilimo muutupie jicho la huruma, muwapatие Maafisa Ugani hawa vitendea kazi ili waweze kusafiri; angalau pikipiki au hata baiskeli; ukilinganisha na umbali kati ya kijiji na kijiji.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwamba Mkoa wetu wa Katavi hauna Maafisa Kilimo, tunauhitaji wa Maafisa Kilimo kama 4, lakini Mkoa wa Katavi una Afisa Kilimo mmoja. Hii yote inasababisha afisa kilimo mmoja hawezи akazunguka mkoa mzima kwenda kuangalia shughuli za kilimo. Niombe Wizara iuangalie mkoa huu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia; mwaka jana wakulima wa Mkoa wa Katavi walipata hasara sana ya mazao yao. Walipotaka kuyauza waliambiwa mahindi yao hayanya ubora. NFRA walipofika kule katavi waliangalia yale mahindi wakawaambia hayana

ubora. Hii yote ilisababishwa na ukosefu wa Maafisa Ugani ambao hawakuwafundisha mahindi yenye ubora ni mahindi ya namna gani, kwa hiyo wakulima waliishia kula yale mahindi bila kuyauza.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la hawa Maafisa Ugani wa Mkoa wa katavi. Kuna mazao mapya yameenda kule Katavi, zao la pamba na korosho. Maafisa Ugani waliopo Mkoani wa Katavi hawana uzoefu na haya masuala. Ningeomba kupitia bodi za korosho na bodi za pamba haya maafisa ugani wapewe elimu ya pamba na korosho ili waweze kuwafundisha wananchi wa Mkoa wa Katavi kwa manufaa ya zao hili na manufaa ya wananchi wa mkoa huo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia mwaka jana Serikali ilitoa tozo...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Taska malizia unga mkono hoja.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja nilitaka kusema kwamba Serikali ilitoa tozo la asilimia tano kwenda asilimia tatu kwa mazao ya biashara na asilimia tatu kwenda asilimia mbili kwa mazao ya chakula, lakini wakulima hawajanufaika, nataka kuuliza swali, aliyenufaika hapa ni mfanya biashara au mkulima?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Taska Mbogo. Mheshimiwa Daniel Mtuka, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Masala. Mheshimiwa Mtuka.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii walau ya dakika tano. Ninayo tu mambo machache sana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, niende moja kwa moja kwenye hoja yangu, kaka yangu Mheshimiwa Mwaka, Mbunge wa Chilonwa, yeye alizungumzia hali ya hewa katika eneo la kati ya nchi hii ni kame. Naunga mkono hoja yake na mazungumzo yake, ni kweli kabisa tuko kwenye eneo kame, lakini kuwa na ukame maana yake sio kwamba hatuna udongo au hauna rutuba. Udongo wetu una rutuba ya kutosha, Mkoa wa Singida na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia hali ya Manyoni kwa mfano, bonde la ufa, limeimega Manyoni pamoja na Dodoma, kwa hiyo tumeshirikiana ule ukame. Kwa upande wangu bonde la ufa, hali ni ngumu sana kwa mfano kwa mwaka huu hatuna chakula, lakini nije na pendekeso la Mkakati kwa maana ya kupunguza sasa au kuondokana na hali ya njaa.

Mheshimiwa Spika, sisi Manyoni, tuna eneo linaitwa Bwawa la Tope la Bahi, Bwawa hili lina mito miwili mikubwa, ambayo inatoka ukanda wa Kaskazini, Manyara inamwaga maji kwenye lile bonde, ni bonde lina rutuba kubwa ya kutosha. Naomba Wizara hii ya Kilimo itusaidie, kukomesha njaa kwenye bonde hili, kwa upande Dodoma kwa maana ya Bahi na upande wa Manyoni. Tuwekeeni Bwawa kubwa la mkakati kwenye bonde hili, tunayo mito miwili mizuri inaleta udongo wenye rutuba ambao umetoka kule juu.

Mheshimiwa Spika, maji yapo ya kutosha na uwezekano ni mkubwa, hebu tusaidieni sana, walete wataalam, wafanye utafiti, watuchimbie bwawa la kutosha. Tunazo ekari zaidi ya 50,000 nzuri zenye rutuba tukaweka bwawa pale, watakuwa wametusaidia kabisa lakini tatalisha na sehemu zingine za nchi hii ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tuna kabwawa kamoja si ka mkakati ambako tayari andiko limeshakamilika liko Wizarani, mwaka jana ilikuwa iwekwe kwenye Bajeti ianzé kwa sababu utafiti, upembuzi yakinifu ulishafanyika, usanifu wa kina umeshafanyika, kila kitu kiko tayari ni kujenga tu. Mwaka jana ilikuwa iingizwe kwenye bajeti wakasema tutaingiza mwaka

huu, nimeuliza maswali karibu mara tatu katika Bunge hili, Bwawa la Mbwasa, lakini nimeangalia Bajeti tena halipo, sijui tatizo ni nini? Njaa itatuua jamani na mimi sioni aibu, nitaomba tu chakula kwa sababu lile bonde halina chakula sasa, lakini wakitujengea kabwawa haka, ile njaa nitakuwa nimeondokana nayo, hebu tusaidieni tuna maji ya kutosha, tusaidieni jamani.

Mheshimiwa Spika, naomba waangalie, Bajeti Kuu bado haijasomwa, waangalie bwawa hili, waliingize kwenye Bajeti ya mwaka huu, tuchimbiwe bwawa pale Mbwasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Singida tumejinasibu kwamba tunalima alizeti na ndiyo *brand* yetu sisi, lakini bei ya mbegu lko juu sana hii ambayo imefanyiwa *research* kwa maana ya *hybrid*. Kwa mfano kilo moja tu ya mbegu inaitwa *hysun F124* inauzwa kwa wastani wa shilingi 35,000 kilo moja. Wakulima wangu wale wa Manyoni wale, Singida yote ni wachovu, kilo moja shilingi 35,000 watalima wapi? Nani atanunua hiyo mbegu? Watuletee angalau ruzuku basi watunyanyue nyanyue ili tupandishe zao hili la alizeti, hii bei si rafiki kwa maana kwamba Singida tuwe ma-giant wa uzalishaji wa alizeti na mbegu hii, hapana.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, malizia. (*Makofii*)

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Spika, baada ya machache hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Daniel Mtuka. Mheshimiwa Hassan Masala atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Nagu. Hayupo? Mheshimiwa Mary Nagu pia? Yupo, karibu Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na Mheshimiwa Justin Monko ajiandae.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana na vilevile niseme kwamba hii ni sekta ambayo inatoa chakula kwa asilimia mia moja kwa Watanzania na inatoa ajira kwa asilimia 65. Inatoa malighafi kwa Viwanda kwa asilimia 65, jamani sio Sekta ya kupuuza, lakini leo napenda sana kujielekeza kwenye suala moja tu kama ulivytuelekeza ni suala la umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, suala la tabianchi kubadilika linajulikana kwa kila mmoja na nafikiri ni muhimu sana kwa Waziri wa Kilimo kulifahamu hilo, bila kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hili suala la chakula, suala la kupata malighafi kwa viwanda, suala la ajira ya watu wengi na mambo mengine ambayo sitayasema sasa hivi litakuwa halina maana yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sina hakika, labda mimi mwenyewe sijaiona, suala la umwagiliaji halijapewa umuhimu unaotakiwa kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, naomba atueleze kwa nini ni kwa sababu tu ndiyo imehamia kwake. Pamoja na hilo sisi watu wa Hanang, tuna miaka kumi tuliomba kuchimbiwa Bwawa la Gidahababieg ambalo linakusanya maji ya Mlima Hanang yote kwenye eneo ambalo ni kavu na hawana uhakika wa chakula, kwa nini Mheshimiwa Waziri hajaorodhesha miradi ambayo katika bajeti hii itapewa hela ningeweza kujua kama Gidahababieg ipo au haipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana na Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Hanang ni moja ya Wilaya ambayo ina udongo mzuri sana, ndiyo Wilaya ambayo inalima sana, lakini mvua siyo za uhakika. Kwa hiyo masuala ya Mabwawa ni muhimu sana, pamoja tunajua kwamba kuna upungufu kwenye maeneo mengine ya kilimo, lakini naomba leo niseme kwamba, kama tunataka tutumie udongo huo mzuri wa Hanang na Mkoa wa Manyara kwa ujumla, hatuna jambo lingine isipokuwa kukazania mabwawa ili watu wapate maji lakini vilevile kilimo kipate maji na mifugo vilevile ipate maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya yetu ya Hanang ukiangalia tukichimba hata mita 200 ya visima hatupati maji. Kwa kweli ni mabwawa yanayotakiwa ni makubwa, wananchi wetu wanajitahidi hata wanachimba wenyewe mabwawa lakini wanahitaji kwa kweli msaada wa Serikali kwa mabwawa makubwa kwanza kwa kufanya *survey*, lakini kwa kuchimba mabwawa kwa namna ambayo inatakiwa kwa ufundi. Kwa hiyo naomba sana, naunga mkono hotuba hii na naunga mkono bajeti hii na ukiangalia Waziri katengeneza kitabu kizuri sana, lakini kitabu hiki basi kiweze kuwasilisha manufaa kwa wananchi. Kwa mwaka huu kwa Wilaya ya Hanang ni kujua kwamba Bwawa la Gidahababieг litachimbwa na sisi tuweze kunufaika na Mwenyezi Mungu ambariki sana Mheshimiwa Waziri katika kazi yake hiyo mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono bajeti hii na yote ambayo anayafanya Waziri. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu. Mheshimiwa Justin Monko, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**MHE. JUSTIN J MONKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami ya kuchangia katika hotuba ya Bajeti hii ya Wizara ya Kilimo. Natambua kabisa kilimo kwa nchi yetu ya Tanzania ni sehemu muhimu sana kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengine waliotangulia ndio inayoajiri zaidi ya wananchi asilimia 65 na kuhakikisha kwamba inaleta chakula kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukijaribu kupitia katika Bajeti hii ya Kilimo ni ukweli usiopingika kwamba fedha zilizotengwa kwenye Bajeti ya kilimo ni ndogo sana, ni chache sana. Tunajua liko tatizo la Kibajeti na maeneo mengi ni ya kipaumbele, lakini tuiombe Serikali sana ifanye maamuzi ya makusudi kuongeza fedha katika Bajeti hii ya Kilimo. Kwa utaratibu huu tunaokwenda, hizi bilioni mbili, bilioni mia mbili na hamsini na tatu, kwenye Sekta hii yote ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika hazitoshi kututoa hapa tulipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia wananchi zaidi ya asilimia 65 na ukiangalia kwenye fedha za maendeleo, huko tena ndiyo kumekuwa hakufai zaidi, kwa sababu fedha nyingi ambazo zimetengwa kwenye upande wa maendeleo zinatoka kwa wafadhili, tunategemea wafadhili kwa zaidi ya asilimia 38, ukienda kwenye umwagiliaji zaidi ya asilimia 91 ya fedha zilizopangwa kwenye umwagiliaji zinatoka kwa wafadhili wa nje, siyo mapato yetu ya ndani, wakati sisi, kwenye Sekta yenye ya Kilimo inazalisha kwa zaidi ya asilimia 28 ya pato la Taifa. Kwa hiyo, naiomba sana, Serikali kwa utaratibu huu tunaokwenda nao kwa kutumia fedha za nje, tunaweza tukapata fedha kwa wakati ambao siyo muafaka na matokeo yake kilimo chetu kikaendelea kudidimia na Wizara hii isifanye vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwenye upande wa umwagiliaji, kwa kweli Sekta ya Umwagiliaji imetengewa fedha kidogo sana shilingi bilioni thelathini na saba. Ni fedha kidogo sana ukiangalia na bilioni ishirini na tisa ndiyo zinapelekwa kwenye upande wa maendeleo. Nimejaribu kuangalia hakuna mradi wowote katika Mkoa wa Singida, ambao upo kwenye umwagiliaji, iko miradi michache sana ambayo itatekelezwa kwa fedha hizi kidogo ambazo zipo. Sasa, sisi tunataka kuongeza uzalishaji, wakati huo huo, tunahangaika sana na kujaribu kuona namna ambavyo tunaweza tukahifadhi mazao mengine. Nadhani tungewekeza kwenye Kilimo cha Umwagiliaji na tukawa tunalima mwaka mzima, hata tusingetumia nguvu kubwa sana katika kuhifadhi mazao ambayo tutayahitaji wakati ambao wananchi wanatafuta chakula wakati ambao kimehifadhiwa kwenye maghala, ambao wakati mwingine yako mbali sana na maeneo waliyoko wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka niombe, Serikali ifanyi juhudii ya makusudi, wamesema Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwenye upande wa umwagiliaji zipatikane fedha angalau zaidi ya bilioni mia tano ambazo zinaweza zikaenda kwenye maeneo mengi ya kuhuisha pamoja na kujenga miundombinu. Kule katika Jimbo langu, yako mabwawa mengi, liko Bwawa la Suke, liko Bwawa la

Mgori, liko Masoghweda, liko Kisisi, liko Ntambuko, yako ni maeneo mengi ambayo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji hata na miradi ya maji. Hata hivyo, hatujaona kwamba tumechukua hatua za makusudi za kutumia maji haya ambayo tayari Mungu ameshatupa bure ili kuweza *ku-develop* kilimo cha umwagiliaji na kuongeza uzalishaji wetu kuititia huku.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni upande wa masoko; naipongeza na kuishukuru sana Wizara kwa kuweka Kitengo cha Masoko katika Wizara hii ya Kilimo. Kwa sababu tumekuwa tukitegemea sana Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, ambao wakati mwingine hawajui hata ubora wa bidhaa ambazo Wizara ya Kilimo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JUSTIN J MONKO:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana na naunga mkono hoja, lakini waangalie sana suala la umwagiliaji. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua kuwa kilimo ni uti wa mgongo kwa nchi yetu, kwa nini wananchi zaidi ya asilimia 70 ni wakulima. Ambao wengi wao ni waelewa wa uwezo wa kati wa kuwa na maeneo makubwa na uzalishaji kuwa wa wastani, ni dhahiri wanahitaji kupewa elimu na kufanyiwa utafiti wa udongo kwa mazao yao, kutokukana na uchovu wa udongo wao. Hivyo Taasisi yetu ya *TARI* inahitajika kupatiwa fedha za kutosha kwani, hivi sasa tunahitaji utaalim wao zaidi ndani ya nchi yetu, hasa Mkoa wa Rukwa kwani mwaka 2018/2019 baadhi ya wakulima wamepatiwa mbegu zisizo bora na pembejeo kuwa feki na kumpatia hasara kubwa mkulima wetu.

Mheshimiwa Spika, nasikitika ndani ya ukurasa 20-23, *TAR*/wameandaa nyenzo tatu za kumsaidia mkulima kufanya uamuzi wa kuboresha uzalishaji wa zao la mhogo, hakuna maeneo ya Mkoa wa Rukwa katika kufanikiwa na utafiti huo wa *TAR*/kwa wakulima wetu wa mhogo - mwambao wa Ziwa Tanganyika, Kala, Wampembe, Kisumba-Kasanga, Karogwe, Kabwe, Kirando, Kipili, Mpombwe na kadhalika. Tunahitaji msaada wa zao hilo, kwani hatuna Maafisa Ugani wa kutosheleza mahitaji.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa Watafiti na Maafisa Ugani tulishughulikie katika ajira yao ili tuboreshe kilimo chetu. Vijiji zaidi ya elfu 15, Maafisa Ugani ni elfu saba ni kujidanganya wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ndani ya ukurasa wa 25, kuhusu mazao ya jamili ya mikunde, inalimwa kila pande ya nchi yetu na wananchi hutumia kama mboga kwenye chakula kikuu kwa kila upande. Uzalishaji wake unashuka pamoja na kutumika eneo kubwa la kuzalishia ni ukosefu wa mbegu bora. Bado uwezo ni mdogo wa *TAR*/kuzalisha mbegu bora, si sahihi kwa wakulima 10,160,577 tu ndiyo wanufaika wa mbegu bora za aina ya mikunde. Ni vema nguvu ya rasilimali fedha kuandaliwa upya kwa maslahi ya wakulima wa nchi hii. Kuinua tija kwa wakulima wetu, hatuwezi kuwa tegemezi wa ukulima wetu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba uwepo utaratibu maalum wa ujenzi wa maghala makubwa na vihenge vikubwa vyta kutosha kwenye maeneo ya uzalishaji mkubwa. Majengo hayo ya Serikali yanapohifadhiwa mazao hayo hakuna uharibifu mkubwa, kuliko tunavyohifadhi wakulima wenyewe mazao uharibika na kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, utafiti na ukaguzi wa karibu zaidi wa pembejeo za kuhifadhi mazao, nyingi ni *fake*. Asilimia 14.5 ya utekelezaji wa vihenge nchini, ni wa hali ndogo sana ambayo inakatisha tamaa kwa wakulima wanapoharibikiwa mazao yao. Tuongeze nguvu na usimamizi wa karibu. Pia Mkoa wa Rukwa tufikirie kuletewa hivyo vihenge vyta

kututosha. Tunasisitiza tujipange hasa na ujenzi wa maghala makubwa, kwa ajili ya stakabadhi ghalani ni zoezi limpatialo mkulima faida kwa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. HASNA S.K. MWILIMA:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuchangia kwa maandishi. Kwanza niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara. Zao la michikichi ni zao linalolimwa Mkoa wa Kigoma na ndiyo asili ya zao hili, japo kwa siku za hivi karibuni, mikoa mingine ya Tanzania nayo inalima zao hili la michikichi. Zao hili linatupa mafuta ya mawese, tunapata mafuta ya mise, tunapata chakula cha mifugo, tunapata na sabuni. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameamua kwa makusudi kulisimamia zao hili, binafsi nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa namna ambavyo amewekeea mkazo zao hili la michikichi.

Mheshimiwa Spika, ombi kwa Serikali, naomba Wizara isituletee pesa bali itununulie miche ya michikichi ya miaka mitatu ili wananchi wapewe miche na kuanza kupandikiza miche hii ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, ombi la pili kwa Serikali kuititia Wizara hii ya kilimo, tunaomba mbege kwa kuwa wakulima wa zao hili hawana pesa, wala hawana namna ya kupata hizo mbegu, miche ya michikichi.

Mheshimiwa Spika, ombi la tatu, mashine za kuchakata mafuta ya mawese, kwani kwa sasa wanatumia magogo kukaa watu wanne na kuzunguka hadi jasho jembamba kuwatoka ndiyo wapate mafuta ya mawese. Natambua *SIDO* wanazo *machine* za kuchakata mafuta, ni bora wapewe *machine* kwa mkopo watarejesha pindi watakapopata pesa kwa kuuza mafuta yao. Sambamba na mashine za kukamua mafuta safi na salama ya mise pamoja na machine za kuchakata sabuni, kwa kufanya hivyo Tanzania ya viwanda itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Nguruka ni Tarafa yenye wakulima wengi wa za la tumbaku lakini zao hili limekuwa na changamoto nyingi sana, ikiwepo changamoto ya wakulima kubambikiziwa madeni na vyama vya msingi kuwalazimisha wakulima kuchukua mikopo hata kama hawataki siku *bank* wakiendelea kumdai aliyekopa wanawafilisi wote hata wale wasiokopa.

Kwa hoja, hiyo niombe Waziri au Naibu Mawaziri kupanga ziara ya kuja Uvinza na kusikiliza kilio cha wakulima wa tumbaku, pamoja na changamoto ya kukosa mbolea, mbegu na madawa ya viuatilifu ya kuulia wadudu. Natambua hivi karibuni Wizara ya Muungano chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais imepiga marufuku mifuko ya *plastic* ifikapo 1/7/2019, Kigoma tunalima mihogo Mkoa wote. Tunaomba Wizara ituletee mbegu ili basi wananchi walime mihogo kwa wingi, kuwezesha viwanda vya kutengeneza karatasi vifunguliwe kwa wingi kwani malighafi zitapatikana.

Mheshimiwa Spika, Uvinza tunalima alizeti, kahawa na ufuta lakini tatizo ni mbegu na pembejeo zote kwa ujumla. Niombe Wizara ya Kilimo kutuletea mbegu za alizeti, ufuta, kahawa na mpunga tunayo mabonde mengi yanayolimika mwaka mzima hata kama hakuna mvua. Sambamba na ombi la pembejeo na mbegu, tunatambua Wizara ina mpango wa *ASDP* unaowezesha kujenga maghala, tunaomba Halmashauri ya Uvinza tupatiwe maghala *Vijiji* vya Kashagulu, Mgambazi, Nguruka, Mganza, Basanza na llagala.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huu, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu mawakala wa pembejeo kwa msimu wa mwaka 2015/2016; Serikali hajjawalipa fedha wasambazaji pembejeo na kila mwaka Wizara ya Kilimo inapitishiwa bajeti, ndani ya miaka minne bado Serikali imeendelea kuhakiki, kama siyo uonevu kwa mawakala hawa. Niombe wakati Waziri anakuja kuhitimisha nipate kauli ya Serikali kwa bajeti ya mwaka 2019/2020 italicipa madai hayo.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kwa upatikanaji wa mbolea kwa wakati na isiyo bora; ni kwa muda mrefu sasa ndani ya nchi yetu mbolea inachelewa kupatikana kwa wakati ili mazao yaweze kupatikana. Azma ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda haiwezi kutimilika kama kilimo kitafanyiwa mzaha.

Mheshimiwa Spika, asilimia 75 ya Watanzania ni wakulima, wanatakiwa wapate mazao ya kutosha ili waweze kusomesha, kujitibu na kadhalika, lakin wakulima hawa wanalima bila msaada wa Maafisa Ugani, Serikali haioni kuwa imewaacha wananchi walime kilimo cha mazoea kisicho na tija, kwa kufanya hivyo hatuwezi kushindana na nchi za Umoja wa Afrika Mashariki, ina maana Tanzania tutabaki nyuma.

**MHE. JOEL M. MWAKA:** Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kilimo cha umwagiliaji pamoja na wakulima wenyewe. kilimo cha umwagiliaji kwa Mkoa wa Dodoma na Kanda ya Kati kwa ujumla kinategemea mabwawa. Mabwawa ya zamani sasa yanaelekea kutoweka kutokana na kujaa tope. Nimepata bahati mara mbili kuwapeleka Mawaziri kuyaona na kuzungumza na wananchi wanaolima. Kwanza nilikwenda na Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji wakati huo, Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe*; pili, nilikwenda na Naibu Waziri wa Kilimo na Umwagiliaji sasa, Mheshimiwa Omary Mgumba. Ahadi zilizotolewa za kuyarekebisha Mabwawa ya Buigiri na Ikowa bado hazina mrejesho kwa wananchi, naomba mrejesho. Mabwawa mapya; ujenzi wa Mabwawa ya Membe na Kwahemu bado hakuna maendeleo mazuri, naomba mrejesho au taarifa.

Mheshimiwa Spika, mafunzo kwa wakulima; ili wananchi walime kwa tija kunahitajika elimu; elimu ya kilimo chenyewe, elimu juu ya afya ya udongo, ili waweze kulima mazao yanayostahili na ikibidi kutumia mbolea basi waweke mbolea inayostahili na elimu ya kilimo hai (*organic agriculture*). Naomba kuwe na vituo vya mafunzo ya kilimo kwa wakulima angalau kila kata au hata kila kijiji ambapo wanalima kilimo cha umwagiliaji kila baada ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ESTHER M. MMASI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa napenda kutoa pongozi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Hasunga pamoja na Manaibu wake kwa wote wawili Mheshimiwa Bashungwa pamoja na Mheshimiwa Ommary Mgumba kwa juhudini zao katika kuinua wakulima wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nitapenda kujielekeza mchango wangu juu ya ushiriki wa vijana kwenye kilimo cha biashara kama ajira mbadala na hatima ya ustawi wa kipato cha mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 sambamba na rasimu ya mwaka 2017 ya Sera ya Taifa ya Ajira ikisomwa pamoja na mkakati wa Kitaifa wa kuwezesha vijana kwenye sekta ya kilimo (2016 – 2021) *instruments* zote hizi zimetia mkazo wa kutosha juu ya umuhimu wa kuwezesha vijana kujihusisha na shughuli za kiuchumi ikiwemo shughuli za kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na miongozo tajwa ya kisera na kisheria ikumbukwe kuwa kwa sasa nchi yetu ya Tanzania inazalisha *graduates* zaidi ya 700,000 kwa mwaka na kwa bahati mbaya *graduates* si zaidi ya 40,000 sawa na asilimia (6 – 10) ndio wanaoingia kwenye soko la ajira rasmi, lakini haitoshi Serikali imekuwa iki-*spend* takribani shilingi bilioni 427 kugharamia elimu ya vijana vyuo na vyuo vikuu kupitia *HESLB*.

Sambamba na hili pia, Serikali imekuwa iki-*spend* takribani kati ya Shilingi bilioni 20 mpaka 23 kwa mwezi kwenye utekelezaji wa sera ya elimu bure. Nguvu zote hizi ni vyema zikaakisiwa kwenye ukuaji wa uchumi hasa tunapoangalia ushiriki wa vijana katika muktadha mzima wa ajira kwani kwa kufanya hivi ndivyo tunavyoweza kushabihisha uwekezaji mkubwa wa Serikali kwenye elimu na ujuzi wa vijana wetu na uchumi endelevu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaandika hapo juu, juu ya sera ya mikakati ya kushirikisha vijana kwenye sekta ya kilimo ni dhahiri kwamba, bado tuna changamoto kubwa sana katika kutengeneza ajira za kilimo cha biashara kwa kundi kubwa la vijana. Changamoto tulizonazo kwa mantiki hii ni pamoja na yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kukosekana kwa mitaala ya somo la kilimo kwenye elimu ya awali, sekondari na hata kwenye baadhi ya vyuo vikuu visiviyokuwa na mchepuo wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, pili, kukosekana kwa usimamizi mzuri juu ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana chini ya Halmashauri zetu. Fedha zinazotoka (41%) kwa baadhi ya Halmashauri zetu zimekuwa zikitoka kama sehemu ya utamaduni na hakuna *mechanism* nzuri ya kuona fedha hizi zinakwenda kwenye kusudio la kuondosha tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana wetu. Mafungu haya yangeelekezwa kwenye kilimo cha biashara na hata usimamizi ukawekwa vizuri, naamini vijana wengi wangeondokana na adha ya ukosekanaji wa mitaji na hata wangeweza kushiriki kwenye shughuli za kilimo cha biashara.

Mheshimiwa Spika, tatu, kwenye Bajeti ya Wizara ya Ardhi ya 2016/207 Wizara ya Ardhi chini ya Mheshimiwa Waziri Lukuvi alielekeza Wakurugenzi wote wa Mipango Miji kutenga maeneo maalum na mahususi kwa ajili ya vijana wetu ili waweze kushiriki kwenye kilimo. Pamoja na maelekezo na mikakati ya Wizara ya Ardhi katika kuona vijana wanapata maeneo ya kilimo, lakini bado hakuna kilichotekelzeza mpaka sasa. Vijana wamekosa hatima ya ajira zisizo rasmi pamoja na maneno mazuri ya baadhi ya waajiri.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018/2019, Wizara ya Viwanda na Biashara ilitenga fedha kupitia Mfuko wa *NEDF* kiasi cha shilingi bilioni 17, ili kusaidia wajasiriamali wadogowadogo kama *startup capital*, lakini hakuna kilichotoka hata tunapokwenda mwisho wa mwaka wa fedha 2018/2019. Vijana wamekosa fedha za kushiriki kwenye

sekta ya kilimo cha biashara kupitia Mfuko huu. Hata hivyo, vijana wamekosa kutumia fursa mbalimbali za kilimo biashara, mfano mwaka 2016/2017, Wizara ya Viwanda na Biashara ilitangaza kufungwa dirisha maalum kwa kundi la akinamama na vijana kushiriki kwenye zabuni za Serikali.

Mheshimiwa Spika, zipo taasisi mbalimbali za Serikali zinazonunua biashara za mazao mfano *FNRA* na hata Taasisi za Ulinzi na Usalama, Jeshi na Magereza ambazo zimekuwa zikitangaza tenda mbalimbali kwa kuwa vijana wetu hawajaandalowi inakuwa ni vigumu vijana wetu kuweza kutumia fursa mbalimbali. Fursa za *AGOA* pia bado hazijatumiwa kutokana na kukosekana na mipango madhubuti ya Wizara ya Kilimo katika kushirikisha vijana kwenye masuala ya kilimo cha biashara.

Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni sehemu ya ushauri wangu kwa Serikali:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, mradi wa kuwainua vijana kupitia mradi wa kilimo cha vizimba (*greenhouse*) chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ipitiwe upya na badala yake mradi huu ulenge zaidi katika kilimo shirikishi cha biashara. Pia mradi utoe dira na mwelekeo sahihi juu ya masoko ya bidhaa inayolengwa kufundishwa kupitia mradi huu.

Mheshimiwa Spika, mradi ulenge kutoa elimu ya mnyororo wa thamani ya mazao ya kilimo biashara, mradi ulenge kutoa ajira za kudumu kwa kuelekeza vyanzo vya fedha ambazo ni tengeo la vijana kwenye Wizara mbalimbali, mfano, Mfuko wa Vijana wa Taifa, fedha za vijana kupitia halmashauri zetu (4%). Serikali kupitia halmashauri zetu ielekeze kila halmashauri itoe sheria ndogo itakayotaka halmashauri zetu kutenga sehemu maalum ya ardhi ili vijana wapate mahali pa kuendesha shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Elimu iandae mtaala maalum wa kilimo na vijana wetu

wafundishwe nadharia ya kilimo cha biashara kutokea ngazi ya chini ya elimu.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara iharakishe katika kutoa mkakati wa kitaifa wa kuhusisha vijana kwenye Sekta ya Kilimo. Mkakati huu bado unasomeka kama rasimu na siyo mkakati rasmi wa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache naomba kuunga mkono hoja ya bajeti Wizara ya Kilimo. Ahsante.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, mchango wa Sekta ya Kilimo ni mkubwa na muhimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, 30% ya Pato la Taifa; 30% ya bidhaa zinazouzwa nje; 65% ya malighafi za viwanda; 65.5% ya ajira; na 100% ya chakula kudhibiti mfumuko wa bei. Hivyo kilimo ni muhimu katika kuifikisha Tanzania yetu kwenye Dira ya Tanzania ya 2025 kuwa na uchumi wa kat, Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, ikiwa hivyo ndivyo ilivyo, inabidi kuimarisha kilimo na upatikanaji wa chakula uwe na uhakika. Namna ya kuimarisha kilimo kwa kufanya utafiti wa kweli wa udongo, mazao na teknolojia sahihi ili kuwa na masoko ya uhakika na kuwa na bei ambayo inafanya wakulima wapate faida ya kukuza kilimo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kilimo kinakuwa kwa 3.1%; Malaba ilitaka kilimo kikue kwa 6% na uwekezaji wenye kilimo ufikie 10% ya Pato la Taifa. Sasa uwekezaji kwenye kilimo ni chini ya 5%, Serikali isaidie. Tatu, wakulima wanahitaji Wagani kwa kila kijiji watosheleze mahitaji yao. Sasa hivi kuna vijiji vingine havina Wagani, naomba Serikali Wagani wote waliofuzu waajiriwe kuongeza nguvu ya wakulima ya kuzalisha mazao.

Mheshimiwa Spika, nne, kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna. Sasa upotevu wa mazao unafikia

kati ya 30% - 40%. Hii inawaletea wakulima hasara na hata Taifa. Najua Serikali inajitahidi kupunguza upotevu lakini bado jitihada inatakiwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, tano, suala muhimu ni kuimarisha na kuongeza miundombinu ya umwagiliaji kutohana na mabadiliko ya tabianchi. Hanang iliomba kujengewa bwawa la Gidahababieg. Tumeomba bwawa hili ili kusaidia eneo la Gidahababieg kupata fursa ya kulima kwani ni eneo lenye uhaba wa mvua. Vilevile, bwawa hili linajengwa katika eneo ambalo maji yote ya mvua kutoka Mlima Hanang yangekusanywa. Huu ni mwaka wa kumi toka watu wa Hanang kupitia kwa Mbunge wameomba kujengewa bwawa. Nataka kujua kwa nini tumecheleweshewa bila kupata maelezo ya kuchelewesha ujenzi wa bwawa hili, itabidi nitoe shilingi.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri inayofanya na Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri kama timu ya pamoja wamekuwa wakifanya maamuzi yenye tija katika mazao ya chakula na kibiashara. Wilaya ya Meatu imechaguliwa kuwa Wilaya itakayozalisha mbegu mama ya pamba na tayari kazi hiyo inafanyika katika Kata ya Mwabusalu.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 5/2/2019 Baraza la Madiwani lilitataa taarifa ya Bodi ya Pamba kuwa Wilaya nzima kuwa ya kilimo cha mkataba tena Bodi ilichelewa kuwaandaa wakulima na pamba iikuwa imechanganya na magugu ya msimu uliopita.

Mheshimiwa Spika, ushauri, kwa msimu huu 2019/2020, pamba haifai kuwa mbegu mama isipokuwa ya Kata ya Mwabusali. Kuruhusu wanunuzi wanaotaka kununua pamba Wilaya ya Meatu ili kuwepo na ushindani wa bei na mkulima anufaiki. Katika msimu ujao wanunuzi watakaotakiwa kununua pamba mbegu watapatiwa kwa taratibu za uzabuni, taratibu za Serikali ili kuondoa mazingira ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali itengeneze mazingira ya kuwa na bei nzuri ili isitofautiane na bei ya pamba katika wilaya jirani ambayo itawafanya wakulima wasitoroshe pamba wilaya jirani, hivyo kuikosesha halmashauri ushuru wa pamba na kuwavutia wakulima katika kulima kilimo bora. Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wakulima wa pamba Meatu kuwa wanalima pamba mbegu mama.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu na kinaajiri zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita zaidi katika suala la ardhi na changamoto zake kwa wakulima wetu. Suala la kupima na kujua hali ya udongo kabla ya kutumia mbolea ni jambo la msingi sana, lakini kwa bahati mbaya sana wananchi wamekuwa hawapati huduma za kitaalam kupima *acidity* na *alkalinity of soil* kutohana na kutokuwa na vituo vya kupimia udongo na ubora wake. Nashauri Serikali ianzishe vituo vyenye kujitosheleza kwa wataalam na vifaa vya upimaji ili kujua ubora wa udongo na aina ya mbolea inayofaa kwa wakulima kulingana na mazingira husika na ikiwezekana kila wilaya au tarafa au kata viwepo vituo vya kupimia ubora na aina ya udongo na mbolea inayofaa kwa ajili ya kurutubisha na kushauri aina ya mbegu inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya mbolea pamoja na viuadudu pia viuatilifu ni vema vikawekezwa zaidi nchini ili kuhakikisha wananchi wanapatiwa huduma hizi kwa bei nafuu ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya chakula na yale ya biashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na viwanda vya kuongeza thamani kwenye mazao ya kilimo ni jambo la msingi sana, hivyo basi naishauri Serikali kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji katika Sekta hii ya Viwanda. Viwanda kwa ajili

ya kuongeza ubora na thamani vinatakiwa kuwekeza katika Viwanda vya Nguo, Viwanda vya Kubangua Korosho, Viwanda vya Kukamua Mafuta ya Alizeti, Michikichi, Karanga, Pamba. Aidha, viwanda kwa ajili ya kuchakata matunda pia ni vema vikaongezwa ili kuwakomboa wakulima wa matunda.

Mheshimiwa Spika, suala la vipimo kwa ajili ya mizani ya kupimia uzito kwa ajili ya wakulima wetu bado kuna shida kubwa hasa kutokana na wanunuzi mara zote ndio huwa ni wamiliki wa mizani ambayo siku zote huichezea kwa lengo la kuwapunja wakulima, hivyo basi ni vyema Serikali ikaweka mkazo kuhakikisha kwamba wakulima wanamiliki mizani yao wenyewe na Mamlaka au Wakala wa Vipimo nchini kuihakiki mizani hiyo mara mara ili kuепusha wakulima kupunjwa.

Mheshimiwa Spika, suala la mabadiliko ya tabianchi; iko haja kwa Serikali kuwekeza zaidi katika Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa kwani kwa sasa utabiri wa hali ya hewa nchini unafanyika kwa kubahatisha na matokeo yake wananchi wanapata hasara kwa kutokupata taarifa sahihi na matokeo yake wananchi wanapambana na ukame au mafuriko na hivyo kuathiri wakulima kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uharibifu mkubwa wa mazingira unaathiri moja kwa moja Sekta ya Kilimo kwa vile uharibifu wa mazingira kwa kukata miti husababisha ukame na mmomonyoko wa udongo, naishauri Serikali kuwekeza katika uhifadhi wa mazingira kwa kupanda miti na kuwashauri wakulima kutokata hovyo miti basi wahakikishe wanaacha baadhi ya miti mashambani.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nachangia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, umuhimu wa uwekezaji katika utafiti; ni muhimu sana kuwekeza katika utafiti hasa kubaini aina ya udongo na kutambua/kushauri ni aina gani ya mazao yalimwe na kupandwa kwenye eneo husika. Jambo hili litasaidia kufanya kilimo chenye tija na mazao

mengi yatakayotokana na ushauri wa kitaalam. Mfano, Visiwa vy'a Ukerewe vyenye eneo la kilomita za mraba 6400, ni asilimia 10 tu ambayo ni nchi kavu. Kwa sababu ya kilimo cha kujirudiarudia hatimaye sasa ardhi yake imechoka na haina rutuba tena. Zao kuu ambalo ni muhogo halistawi tena pamoja na mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Wizara pamoja na maeneo mengine inatakiwa ipeleke wataalam wake visiwani Ukerewe ili wafanye utafiti wa kisayansi kubaini aina ya udongo na kushauri yapandwe na kwa utaratibu upi. Jambo hili itasaidia eneo letu dogo litumike kwa ufanisi na kwa tija na kuondoa tatizo la upungufu wa chakula kwenye Visiwa vy'a Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji na umuhimu wa umwagiliaji, ni jambo lilio wazi kwa kuwa zama za kufanya kilimo cha kutegemea mvua kimepitwa na wakati. Kwa kuwa nchi yetu imebahatika kuwa na vyanzo vingi vy'a maji ni vizuri sana kuwekeza zaidi kwenye kilimo cha umwagiliaji tukitumia vyanzo hivi vy'a maji. Mfano, Visiwa vy'a Ukerewe ambavyo vimezungukwa na maji havitakiwi kuwa na shida ya chakula na vingeweza kuhudumia maeneo mengine kwa chakula kama tu Wizara ingewekeza kwenye umwagiliaji. Mradi wa umwagiliaji wa Miyogwezi na Bonde la Bugorola umesimama kwa sababu ya kukosa fedha.

Mheshimiwa Spika, ushauri, Wizara ifufue mradi wa umwangiliaji Miyogwezi na Bungorola ili kutumia rasilimali maji yaliyopo Ukerewe na kuifanya Ukerewe kuwa wazalishaji wakubwa itakayofanya wajitoshereze kwa chakula na ikiwezekana kuhudumia maeneo mengine kwa chakula.

**MHE. MARGRET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana kwa kazi kubwa Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake, hongera kwa kazi nzito wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, kwa niaba ya wananchi wa Urambo, naomba wafanyie kazi kwanza

upatikanaji wa pembejeo kwa wakati, hususan mbolea. Kwa mfano, sisi tunaolima tumbaku inabidi tupate mbolea kabla ya mwezi Agosti na kwanza, bei ipunguzwe. Pili, ili wakulima walime zaidi masoko ya mazao yawe ya uhakika na tatu, wanunuzi wawe wengi ili ushindani wa bei uwepo kwa manufaa ya wakulima wetu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nina maswali yafuatayo:-

Kwanza, kwa kuwa kampuni ya *TLTC* ilikuwa mnunuzi mkubwa wa tumbaku kwa tani zipatazo milioni 14 kwa msimu; je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kuwa iwapo kampuni hii itajitoa wakulima wasikose makisio msimu ujao na wakiondoka pengo lao litazibwa na nani?

Pili, je, kuna makubaliano yoyote kati ya *BAT* (*British American Tobacco*) katika kuwa wanunuzi wa tumbaku?

Tatu, je, Serikali ina mpango gani kuhusu bima kwa wakulima na mazao yao?

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa niaba ya wananchi wa Urambo tunaomba mtaalam wa zao la alizeti aje atuambie mbegu ipi ni nzuri kwa ardhi yetu.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe wa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii. Pili, napenda kumpongeza kwa dharti Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na kuwasilisha hotuba hii kwa ufasha mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutoa mchango wangu katika hotuba hii, napenda kuchangia kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Vyuo na Vituo vya Mafunzo ya Kilimo; naipongeza Serikali kuititia Wizara hii kwa kuweka utaratibu mzuri wa kutoa mafunzo ya kilimo kwa vijana wetu nchini. Hili jambo ni jema ambalo litatupelekea

kulima kwa mtindo wa kisasa badala ya ule wa kufanya kazi kwa mazoea.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Wizara ni kwamba, iweze kuwatumia wataalam wanaohitimu kwenye vyuo vyetu ili walete mafanikio. Wataalam hasa Mabwana/ Mabibi Shamba wawezeshwe ili waende vijijini badala ya kukaa mijini/maofisini. Wakulima wetu wa vijijini hasa wale wa kipato cha chini wanahitaji maelekezo ya kitaalam sana ili kufanikisha kazi zao.

Mheshimiwa Spika, pili, pembejeo za kilimo, Serikali yetu inajitahidi sana kutafuta miundombinu ya pembejeo. Kilimo ni uti wa mgongo hasa katika nchi yetu ambayo inaelekeea kwenye siasa ya uchumi wa viwanda, bila ya kilimo hakuna viwanda, hivyo ni vyema Serikali ikawawezesha wakulima kwa kuwapatia pembejeo hizo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika suala la pembejeo kwa Serikali kuweka bei wezefu ambazo wakulima wetu wa chini wataweza kununua/watamudu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa na nzuri wanazofanya kwa nia ya kukuza na kuendeleza sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuishukuru Serikali yetu siku na kibinagsi na kwa niaba ya wananchi wa Longido namshukuru Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Magufuli kwa maagizo yake ya kuwapelekea chakula wananchi wa Wilaya ya Longido waliokumbwa na uhaba wa chakula cha nafaka ya mahindi kufuatia ukame wa muda mrefu. Rais alitoa maagizo na Serikali kuititia Waziri wa Kilimo waliwatenglea na kuwapeleka wananchi wa Longido mahindi ya bei nafuu ya Serikali jumla ya tani 10,000 ambayo yatawatosha hadi msimu ujao wa mvua.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi na shukurani hizi, naomba sasa nijielekeze kwenye kuchangia hoja ya bajeti ya Wizara ya Kilimo iliyoko mezani mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu kilimo chenye tija; kwa kuwa bado kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu, iko haja ya Serikali kuwekeza katika masuala ya msingi ambayo yakizingatiwa, wakulima wa Tanzania ambao wengi ni wakulima wadogo wadogo wanaotumia zana duni kama majembe ya mkono na plau, zana ambazo kamwe hazitatoa na kutupeleka kwenye mapinduzi ya kilimo chenye tija. Ili tuondokene na kilimo duni, Serikali iongeze bajeti na kuwekeza kwa nguvu zote katika maeneo yafuatayo:-

- (a) Kuhakikisha kila Kijiji kina Afisa Ugani;
- (b) Kutoa ruzuku ama mikopo ya kuwezesha wakullma kupata na kutumia zana bora za kilimo kama vile *power tillers* na matrekta na hivyo kutokomeza kabisa matumizi ya majembe ya mkono na plau kama zana za msingi za kilimo; na
- (c) Kusambaza pembejeo za kilimo (mbegu bora, mbolea na madawa bora) kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi; kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi yamekuwa yakiathiri kwa kiwango kikubwa kilimo kinachotegemea mvua. Nashauri Serikali iongeze bajeti ya kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Tanzania tuna maeneo mengi yenye rutuba yanayofaa kwa kilimo isipokuwa changamoto ni vyanzo vyya kudumu vyya maji ya kuendeshea kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kufanya usanifu wa kujenga mabwawa ya umwagiliaji na kuboresha skimu za umwagiliaji ili kukuza kilimo chenye tija katika nchi yetu. Hili liende sambamba na kufundisha wataalam wa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, katika Kata yangu ya Tingatinga Wilayani Longido kuna maombi ya muda mrefu ya bwawa la umwagiliaji kwenye nyanda za chini katika eneo linapotawanyika mikondo ya Mto Simba unaotoka Mlima Kilimanjaro. *Survey* zilifanyika tunachoomba ni bajeti ya kujenga bwawa hilo.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kushauri Serikali kuwekeza katika kufanya utafiti na usanifu wa skimu bora za umwagiliaji kwa kutumia maji ya Mto Ngarenanyuki ambayo hufaa sana kwa kilimo cha nyanya, vitunguu, viazi na mboga za aina mbalimbali. Matumizi yasiyo ya kitaalam ya maji ya mto huu kwa sasa yamesababisha maji kutowafikia wakazi wa Vijiji vya Mwendo wa chini hasa wa Kijiji cha Ngareyani kilichopo Wilaya ya Longido.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ijenge matanki makubwa ya maji ya umwagiliaji yapitishwe kwenye mabomba hadi kwenye mashamba badala ya mifereji inayotumiwa kwa sasa ambayo huchapusha maji toka mtoni bila kurudisha na kupelekea kukauka kwa mto na uharibifu wa mazingira wa nyanda za mto huu muhimu.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhusu uwekaji wa chakula cha akiba; pamoja na mpango mzuri ulioko tayari wa Serikali kuwa na maghala mikoani kwa ajili ya kuhifadhi chakula cha akiba, naomba niendelee kusisitiza kwa Serikali kuendelea kuona umuhimu wa kuwekeza zaidi katika kuhifadhi chakula kingi zaidi cha akiba (hasa nafaka) kwa ajili ya kukabiliana na uhaba unaoweza kutokea wakati wowote kutokana na kuongezeka kwa kasi ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, namalizia kwa kutamka kuwa naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu vikwazo vya kufikisha pembejeo (mbolea, viatilifu na mbegu bora) kwa wakulima wadogo vijijini na hivyo kupoteza tija; wakulima wengi wadogo wapo vijijini ambako ndiko pia

shughuli za kilimo zinafanyika. Maduka ya pembejeo kwa sehemu kubwa yapo mijini. Tanzania mkulima mdogo apate pembejeo ni lazima asafiri hadi mijini kununua. Hili linaongeza gharama za uzalishaji kwa mkulima mdogo.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza tija haina budi maduka ya pembejeo yasambae hadi vijiji ambako wakulima wapo. Katika maeneo mengi wajasiriamali vijiji wanafanya jitihada za kufungua maduka ya pembejeo ili kufikisha huduma karibu na wakulima. Jitihada hizi zinakwamishwa na gharama kubwa za vyeti vinavyotakiwa. Vyesti ni kama ifuatavyo:-

- (1)  $TOSCI = 100,000.$
- (2)  $TPRI = 320,000.$
- (3)  $TFRA = \text{gharama ya chakula wakati wa mafunzo.}$
- (4)  $TFDA = 100,000.$
- (5) Leseni = 71,000.

Jumla ni 591,000

Mheshimiwa Spika, gharama hizi ni kubwa sana, zinakatisha tamaa kwa wajasiriamali. Wapo wengi wameshindwa licha ya kushiriki mafunzo na kujengewa hamasa bado wameshindwa kufungua maduka. Mifano halisi ni, katika Mkoa wa Kagera wajasiriamali 461 walijengewa hamasa na kupata mafunzo ya biashara hiyo kuititia Shirika la AGRA matokeo yake ni kama ifuatavyo:-

<b>WALIOPATA MAFUNZO</b>	<b>Cheti TOSCI</b>	<b>Cheti TFRA</b>	<b>Cheti TPRI</b>	<b>WALIOFUNGUA MADUKA</b>
Waliopata mafunzo na kujengewa hamasa ni 461	82	108	17	139

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Kigoma, kati ya Wajasiriamali 704 walijengewa hamasa na kupatiwa mafunzo ya biashara na Shirika la AGRA ni wajasiriamali 389 tu ndio wamefungua maduka. Aidha, wajasiriamali 159 walipata mafunzo na TFRA Mwezi Oktoba, 2018 lakini hadi leo hawajapata vyesti vya TFRA ili kuwezesha kuanzisha

maduka ya pembejeo vijijini. Utaratibu huu kama hautabadiilika, ukuaji wa sekta hii utaendelea kudorora.

Mheshimiwa Spika, ushauri; Serikali iangalie upya ada hizo (*TOSCI, TFRA, TPRI, TFDA*) ziangaliwe upya au Serikali ibebe huo mzigo ili kuwezesha ufikishaji mbolea, viatilifu, mbegu bora kwa wakulima wadogo.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze na kumpongeza Waziri Mheshimiwa Japhet Hasunga, Naibu Mawaziri Mheshimiwa Bashungwa na Mheshimiwa Mgumba pamoja na Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha hotuba ya bajeti hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kupongeza Serikali kwa usajili wa wakulima; jambo hili ni jema sana. Ni imani yangu sasa zoezi hili la usajili wa wakulima nchini Serikali itaweza kutambua:-

- (i) Ardhii itakayotumika katika kilimo
- (ii) Mahitaji halisi ya wakulima kama mbolea, mbegu, madawa na viuatilifu, upangaji wa bajeti utarahisishwa.

Mheshimiwa Spika, lakini naitaka kujua, je, hili la usajili litachukua muda gani kukamilika na linafanyikaje? Je, uelewa wa wakulima katika kujisajili ukoje?

Mheshimiwa Spika, miradi ya umwagiliaji; hadi kufikia mwaka 2017, jumla ya skimu 2,942; skimu zilizoendelezwa zipo 960 tu na skimu ambazo bado hazijaendelezwa zipo 1,987 na katika Mkoa wetu wa Iringa una jumla ya skimu 58 za umwagiliaji. Hapo ni lazima tukiri Tume ya umwagiliaji haikufanya vizuri katika kipindi kilichopita. Hivyo, niipongeze Serikali kwa kuona umuhimu wa kuondoa baadhi ya watendaji katika Tume hiyo na kuunda Tume mpya. Ni vyema sasa Serikali ingefanya upembuzi yakinifu wa miradi ile iliyokaribia kumalizika au miradi yenye tija ili ipatiwe kipaumbele kupatiwa pesa kuliko kutoa pesa kidogo kidogo katika miradi mingi matokeo yake huwa inakuwa miradi

haikamiliki mingi na pesa inapotea bila tija yoyote. Pia Benki ya Kilimo na Mfuko wa Pembejeo watoe asilimia 20 kusaidia miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Ugani; asilimia 25 ya wakulima wadogo nchini ndiyo wanapata mbegu bora na asilimia 10 ya ardhi inayolimwa ndiyo inatumia mbolea, lakini uajiri wa Maafisa Ugani na mazingira ya kazi vimekuwa ni changamoto kubwa sana nchini. Mfano, kati ya mwaka 2014 - 2016, Maafisa Ugani waliopata mafunzo na kuhitimwa walikuwa 3,189 lakini kati ya hawa, asilimia 20 tu ndiyo walipata ajira. Upungufu wa vituo vya kuwapatia maarifa wazalishaji wadogo na uwezo mdogo wa rasilimali (wataalam wa teknolojia). Je, nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha Maafisa Ugani wanaajiriwa?

Mheshimiwa Spika, Benki ya Kilimo; tunapongeza kwa kuzindua Benki ya Kilimo. Benki hii itakuwa ndiyo mkombozi kwa wakulima nchini na vizuri Serikali itoe ruzuku ya kutosha kwa Benki hii kwa sababu kushuka kwa mikopo sekta ya kilimo kulinganisha na sekta nyingine, hii inatokana na taasisi za fedha kuchukua kilimo kama sekta hatarishi (*risk*) na uanzishwaji wa Bima ya mazao utasaidia wakulima wetu kukopesheka kama kutakuwa na ukame, mafuriko, uvamizi wa viwavi jeshi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, changamoto katika vituo vya utafiti; tulifanya ziara katika vituo vya utafiti hali ni mbaya sana. Bila Serikali kuona umuhimu wa kutenga pesa ya kutosha ili tafiti ziweze kufanyika hata sera yetu ya uchumi wa viwanda itakuwa kazi bure sababu viwanda vyetu vitakosa malighafi ya uzalishaji. Mfano, mbegu tu ya mahindi ni asilimia 65 kutoka nje, mboga mboga asilimia 99 kutoka nje. Serikali ingewekeza katika Taasisi ya ASA wakawekewa miundombinu ya umwagiliaji, matrekta na zana za kilimo, hiki kituo Kingeweza kuzalisha mbegu za kutosha.

Mheshimiwa Spika, zao la pareto; hili ni zao la biashara katika Mkoa wetu wa Iringa. Pia kipo kiwanda katika Wilaya ya Mufindi. Kiwanda kina uhitaji wa maua ya pareto kiasi cha

tani 5,000, lakini wakulima wana uwezo wa kuzalisha tani 2,500 tu. Tunawapongeza sana wamiliki wa Kiwanda cha Pareto kwa kuwapatia wakulima pembejeo na utaalami, lakini mbaya zaidi kuna walanguzi wanaokuja kuwarubuni wakulima maua yao. Je, Serikali inalinda vipi viwanda vyetu nchini dhidi ya hawa walanguzi? Hata tulipofanya ziara katika mashamba ya parachichi Mkoa wa Njombe kulikuwa na changamoto ya walanguzi toka nchi jirani kuwarubuni wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze Wizara kwa juhudhi kubwa wanazofanya kuinua kilimo nchini. Naomba kujua mkakati wa Serikali kuboresha upungufu. Kutambua na kupima hekta 147 za Mto wa Mbu na Migungani, Selela, Engaruka. Naomba kuboreshewa sehemu ya Mahande, kusakafia mifereji katika Skimu za Mahande, Jangwani, Selela, Engaruka Juu inatakiwa shilingi milioni 200. Hii itasaidia kuinua umwagiliaji. Naamini Serikali itatusaidia kutenga fedha za ukarabati *schemes* zetu.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naipongeza Wizara kwa ujumla katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na changamoto ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejenga skimu ya umwagiliaji ya Itete katika Wilaya ya Malinyi (2011-2013). Toka skimu hiyo kukamilika na kukabidhiwa kwa wananchi katika Vijiji vya Minazini, Alabama na Itete, skimu hiyo haitumiki kwa kikamilifu kutokana na changamoto za upungufu wa maji, mitaro mibovu na ukosefu wa barabara kuelekea katika mashamba ya skimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali mwaka 2015 na 2016 ilikiri kabisa kwamba skimu hiyo imejengwa chini ya kiwango stahiki na kuahidi kuifanyia marekebisho upya ili skimu itumike kikamilifu. Naiomba Serikali itekeleze ahadi ya ukarabati au

marekebisho ya skimu hiyo katika bajeti ya mwaka huu 2019/2020 kama ilivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Malinyi bado ina fursa kubwa ya ujenzi wa skimu zingine katika Mito ya Lwasesa, Sofi, Furua, Mwatisi na mingineyo. Je, ni lini Serikali itafanya utaratibu wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mito hiyo minne ili ititirishe maji ya uhakika masika na kiangazi ili ujenzi wa skimu za umwagiliaji uanzé. Ahsante.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, m Konge; pamoja na mchango wangu wa kuzungumza naomba nishauri Serikali kwa Wizara ya Kilimo na Fedha kukaa pamoja ili kuweka kwenye *Finance Bill*/kipengele cha namna ya kutoza *produce cess* kwa wakulima wote wakubwa wanaosafirisha nje m Konge ili tuisiwavunje moyo wanunuzi wanaokuja kununua m Konge wa wakulima wadogo. Pia fedha hizi zitasaidia utatuzi wa changamoto za zao la m Konge.

Mheshimiwa Spika, chai; kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa pembejeo kwenye zao la chai. Jambo linalowalazimisha wakulima kukopa pembejeo kwa wenye viwanda na kuwaathiri kwenye bei. Ushirika katika chai uimarishwe , pia tuanzishe soko au mnada wa chai hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, umwagiliaji; ili kuwaondoa katika umaskini wananchi wa kata 10 za Tarafa ya Mombo ni kutekeleza Mradi wa Umwagiliaji wa Bonde la Mto Mkomazi. Bwawa linaloweza kusaidia kilimo cha umwagiliaji kwenye hekta zaidi ya 5,000.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya M Konge, kumekuwa na udhaifu mkubwa wa usimamizi wa m Konge kwa sababu ya uwezo mdogo wa Bodi ya M Konge. Nashauri bodi iangaliwe upya. Pia Serikali ifuutilie utaratibu uliotumika kutoa mashamba ya m Konge. Pia namna mali za Bodi ya M Konge zilivyouzwa au kugawanywa ili kujua Bodi ilikuwa na mali gani, zimekwenda wapi na kwa utaratibu upi?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Serikali imetangaza dhamira yake ya kuanzisha Bima ya Mazao ili kukabiliana na majanga. Ni wazo zuri na naliunga mkono japo litazamwe kwa makini isije kuwa ni gharama kwa mkulima na faida kwa makampuni ya bima. Hata hivyo, napenda kurudia wito wangu kuwa kuna haja ya kuwa na Skimu ya Hifadhi ya Jamii kwa Wakulima. Bima ya Mazao yaweza kuwa moja ya mafao yatakayotolewa na mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, nasaha yangu kwa Serikali ni kuanzisha Skimu ya Hifadhi ya Jamii ya Wakulima ili kuwavutia kuweka akiba, kupata bima ya afya, Fao la Bei na mikopo nafuu ya pembejeo. Fao la Bei husaidia bei ya mazao ikianza kushuka. Kwa sasa bei za mazao zikishuka wakulima watarudi kwenye umaskini kwani hawana fidia ya bei kushuka (Fao la Bei). Kukiwa na *price stabilisation* mkulima anakuwa na hakika hata bei ikishuka chini ya kiwango cha gharama zake za uzalishaji Skimu ya Hifadhi ya Jamii itamfidia na hivyo kuendelea na shughuli zake msimu unaofuata.

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari, 2018 niliandika Kuhusu Skimu hii kwenye zao la korosho, nanukuu:

*"Mwaka huu peke yake iwapo wakulima 600,000 wa korosho wangekuwa kwenye hifadhi ya jamii, wangeweza kuweka akiba ya TZS 144 bilioni (14% ya Mapato yote ya korosho katika msimu mpaka sasa). Ingekuwa tumefanya hivi tangu 2015/2016 na 2016/2017, leo skimu ya Hifadhi ya Jamii ya Wakulima wa Korosho peke yake ingekuwa na thamani ya zaidi ya shilingi 300 bilioni. Hizi zingeweza kuwekezwa kwenye biashara ya pembejeo za kilimo, kuboresha mashamba, viwanda vya kuongeza thamani (processing factories). Pia ingetatua kabisa tatizo la afya kwa kuwapa wakulima wote Bima ya Afya bila kuathiri akiba zao." Mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Spika, kuititia Skimu wakulima wanaweza kuingia kwenye mpango wa nyumba bora kwa kupewa mikopo ya muda mrefu ya nyumba na hivyo kufuta kabisa umaskini. Mkulima wa Tanzania anaathiriwa sana na mitaji

ya pembejeo, uhakika wa bei za mazao yao na gharama za matibabu wanapoumwa wao na familia zao. Yote haya yanajibowi na hifadhi ya jamii. Zaidi ya yote mkulima anakuwa na akiba ya uezemi, pale ambapo hataweza tena kulima anakuwa analipwa pensheni ya kila mwezi. Haya ndio mapinduzi tunayoyataka kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nawasihi Wabunge kulitazama hili na kufanya kazi na Serikali ili kuleta mabadiliko makubwa kwa wananchi. Serikali ianze na wakulima wa baadhi ya mazao kama vile tumbaku, kahawa, pamba, karafuu, chai na mkonge. Baada ya kutekeleza na kujifunza kwa wakulima hawa tunaweza kupanua wigo kwenda kwa wakulima wote nchini.

Mheshimiwa Spika, skimu ya namna hii pia yaweza kutekelezwa kwa wafugaji na wavuvi pia. Mfano wakulima wa korosho wapatao 600,000 nchini wakiwa kwenye Hifadhi ya Jamii (kwa kutumia ushuru wa korosho - *exports levy*), tutaweza kufikia watu 3.6m wenye Bima ya Afya katika mikoa yote inayolima korosho amba ni sawa na wananchi wote wa Lindi, Mtwara, Tunduru na baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Pwani. Kupitia Skimu na mafao yake wakulima hawatakopwa mazao yao, pembejeo zitafika kwa wakati na wakati wa hali mbaya ya bei, watafidiwa gharama zao za uzalishaji.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, Utafiti wa mbegu mpya na *TARI-GMO* ya Malindi katika Kituo cha Makutupora Dodoma. Napongeza hatua hiyo Iakini kumekuwa na kauli kinzana Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo alinukuliwa akisema Serikali imepiga marufuku majaribio ya *GMO*, huku hotuba ya Waziri ikionesha kuwapongeza Wizara imegundua mbegu mpya za mahindi inayostahimili magonjwa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara ya maendeleo inayoombwa na Wizara ya kiasi inayopelekwa ni asilimia 48.74. Hata nusu ya asilimia hamsini haifiki kama nchi, kilimo sio kipaumbele na hii inajidhirisha kutokana na bajeti ndogo iliyopelekwa na hata hii inakiuka makubaliano ya Malabo

kuna bajeti ya kilimo lazima itengwe na kufikiwa kwa asilimia 10 ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, ASA; Serikali iongeze nguvu kusaidia utafiti wa mbegu katika vituo vya utafiti. Sasa hivi mbegu nyingi zilizopo nchini hazitoshalezi badala yake makampuni binafsi kama *SEDICO*, *Pannerna* kadhalika ndio makampuni yanayosambaza mbegu nchini. Ikumbukwe kuwa *Harb za makampuni* haya ya nje zipo nje ya nchi hivyo ikitokea siku wakagoma ku-*supply* mbegu nchini hatutakuwa na *sustainable agriculture*, lazima Serikali ifikirie.

Mheshimiwa Spika, kuwekeza kwenye uzalishaji wa mbegu mfano Kenya ilivyofanya kwamba *Agricultural Institute* zinatengewa bajeti ya kutosha na kuwekeza nguvu kwenye utafiti wa mbegu za kilimo, mbogamboga matunda.

Mheshimiwa Spika, kodi nyingi kwenye kilimo, mfano kilimo cha tumbaku zimezidi mfano (*Cess/city service, skills development levy*, tozo ya Bodi za Kusindika, tozo Bodi ya Kununua Zao Mbichi, *export levy, radiation levy*, ushuru wa ushirika, ushuru wa *research*, halafu mkulima alipwe malipo ya pili *all on top of the price*, nchi nyingine mkulima analipwa bei anahangaika na kodi kwani ye ye sio mnunuzi.

Mheshimiwa Spika, Viwanda vya Tumbaku Morogoro vinapunguza ununuzi wa tumbaku kutokana na Serikali kushindwa kulipa 25 bilioni *returns VAT*; iko haja Wizara ya Kilimo na Viwanda na Biashara kufanya kazi kwa pamoja maana viwanda vikifa wakulima hawatakuwa na wanunuzi wa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, upotevu wa mavuno (*post harvesting*) wakulima wengi wanapoteza mazao yao kutokana na ukosefu wa maghala ya kuhifadhi mazao. Hali hii ya kukosekana maghala kunasababisha wakulima kulazimika kuuza mazao yao kwa bei ya kutupwa/bei ya hasara. Ushauri, Serikali ifikirie kujenga maghala makubwa katika maeneo ambayo yana kiwango kikubwa cha mazao.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya matrekta kwa wakulima; bila kufanya utafiti wa kutosha wakulima wengi wanashindwa kurejesha mikopo. Mfano wakulima waliopo milimani wamekopeshwa matrekta hawawezi kuyatumia hali inayosababisha wakulima kupaki matrekta juu ya mawe, mfano wakulima wa Mgeta, Mvomero Mkoani Morogoro ni vyema utafiti wa kina wa matumizi ya matrekta hayo ukafanyika kabla ya kutoa mikopo hiyo.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nipongeze uongozi mzima wa Wizara kwa jitihada wanazofanya kukabiliana na changamoto mbalimbali katika sekta ya kilimo pamoja na ufinyu wa raslimali walizonazo.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kufanya mapinduzi ya kilimo katika Taifa letu ni lazima tuamue kama Taifa kwa makundi kuwekeza vya kutosha katika kilimo na hususani katika Nyanja ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Moshi Vijijiini kwa miaka mingi tulishaingia katika kilimo cha umwagiliaji na kwa bahati nzuri tulipata mradi mkubwa wa umwagiliaji kwa ushirikiano na nchi ya Japan Mradi unaoitwa *Moshi Irrigation Scheme*. Mradi huu umekuwa ni mkombozi mkubwa kwa watu wetu hasa katika Kata za Mabogini, Arusha chini na Old Moshi Magharibi.

Mheshimiwa Spika, mradi huu sasa unakabiliwa na changamoto kuu tatu.

(i) Maji hayatoshi hivyo zinahitajika fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu iliyopo katika mradi huu kuepusha maji mengi kupotea na kulinda vyanzo vya maji hayo.

(ii) Wakulima wa mpunga katika mradi huu wameunda ushirika wao na kwa muda mrefu wamekuwa wakiomba wakabidhiwe vifaa vilivyoachwa wakati wa kuanzishwa kwa mradi huu ikiwa ni pamoja na mashine ya kukoboa mpunga mpaka leo hawajakabidhiwa mashine.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri afanye kila linalowezekana wakulima hawa wajibiwe kilio chao.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya tatu ni barabra inayoingia katika mradi huu inayoitwa Funga Gate – Mabogini – Chekereni – Kahe; kipindi kirefu cha mwaka barabara hii haipitiki kabisa jambo ambalo linaathiri sana ustawi wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa kuendeleza kilimo awamu ya pili zipo fedha zilizoainishwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika miradi ya umwagiliaji. Naiomba Wizara iratibu vizuri fedha hizi na kwa kushirikiana na *TARURA* ili barabara hii iweze kutengenezwa ikiwezekana kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifereji ya asili huko nyuma imekuwa ikisaidiwa katika ukarabati wake na Serikali kuititia Ofisi ya Kanda ya Tume ya Umwagiliaji. Kwa muda mrefu *support* hii imekoma matokeo yake ni kwamba mifereji mingi imeanza kufa jambo ambalo ni hatari sana kwa ustawi wa watu wa Moshi Vijijini. Mifereji kama Makeresho wa Kata ya Kibosho Magharibi, mfereji wa Makupa, Metro na mingine mingi karib kata zote 16 inahitaji ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Wizara irejee utaratibu wake wa zamani wa kusaidia mifereji hii kwa kuwa mahitaji ya sasa wananchi hawawezi kuyamudu kwa nguvu zao wenyewe.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi. Aidha, nimshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa iliyofanyika katika kufufua zao la tumbaku Wilayani Namtumbo, pamoja na kutuletea soko la Stakabadhi Ghalani kwa mazao ya ufuta, soya, alizeti na dengu. Nimpongeze pia Mheshimiwa Rais kwa kumwona mchapa kazi, Waziri Mheshimiwa Japhet Hasunga na

kumkabidhi Wizara hii ngumu ya Kilimo na Umwagiliaji. Yeye ni msikivu bila kujali aina ya hoja anazoletewa, anatusikiliza kwa unyenyekevu, ahsante sana.

Hata hivyo, kama mwakilishi wa wananchi wa Wilaya ya Namtumbo ambayo wakazi wake ni wakulima wadogo wasio na kipato cha uhakika, naomba aendelee kupokea hoja zifuatazo na kuzifanyia kazi:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Benki ya Kilimo iwahudumie wakulima. Itoe mikopo kwa wakulima wadogo kupitia Vyama vyao vya Ushirika kama vile *AMCOs* zinazounda Chama Kikuu cha *SONAMCU*. *SONAMCU* inalazimika kukopa kwenye benki za kibiashara kwa ajili ya pembejeo na hivyo kutozwa riba kubwa inayomwongezea mkulima mdogo umaskini.

Mheshimiwa Spika, pili, Mfuko wa Pembejeo nao uwahudumie wakulima wadogo. Changamoto kubwa ya wakulima wadogo ni upatikanaji wa mbegu bora na mbolea. Pembejeo sio matrektu, tukopeshwe vile vile kwenye upatikanaji wa mbegu na mbolea.

Mheshimiwa Spika, tatu, tunampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa maamuzi ya kijasiri ya kununua korosho baada ya soko la zao hilo kuvurugwa na kutaka kumuumiza mkulima. Kwa Namtumbo, tunayo Tarafa moja ya Sasawala ambayo wakazi wake hutegemea zaidi zao la korosho. Wapo walioanza na kulipwa lakini wapo wakulima 76 waliouza jumla ya tani 104.485 za korosho hawajalipwa kabisa hadi hivi leo. Nimwombe Mheshimiwa Waziri ahakikishe wakulima hao wanalipwa haraka ili wapate nguvu ya kuendelea na kilimo cha korosho cha msimu mpya ambao umeshaanza na palizi na upuliziaji wa *sulphur*.

Mheshimiwa Spika, nne, kuna vikwazo vingi vinavyoathiri soko na uzalishaji wa zao la tumbaku na mazao wengine ya kimkakati. Tozo ni nyingi mno na utekelezaji wa kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*) hauko sawa. Marejesho

ya kodi hiyo hayafanyiki kwa wakati na hivyo kuathiri mtaji wa kufanya kazi *working capital* kwa wanunuzi na wachakataji wa mazao hayo hususan zao la tumbaku. Hebu Mheshimiwa Waziri amshawishi Waziri wa Fedha na Mipango na Wajumbe wa Baraza la Mawaziri waelewe madhara ya kutolipa VAT return kwa wakulima wetu. Soko la mazao hayo litakufa na watakaoathirika ni wakulima wetu maskini.

Mheshimiwa Spika, tano, taasisi za udhibiti katiba sekta ya kilimo ni nydingi mno na zinafanya kazi zinazofanana. Ukienda kwenye tumbaku, sukari, korosho, chai ama pamba hali ya utitiri wa tozo inafanana. Viwango vyta za taasisi za udhibiti ni vikubwa mno, vinaongeza gharama za uzalishaji na kuzifanya bidhaa zetu zishindwe kushindana kwenye soko huria.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa asilimia mia moja na naomba majibu chanya ya maeneo matano ya hapo juu.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoa na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku. Pia pongezi hizi pia ziwafikie watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, maoni au ushauri wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, fedha zinazopangwa na kupitishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya kilimo zitolewe kwa wakati ili kuweza kutekeleza miradi hiyo na kuleta tija katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali itafute masoko ya uhakika ya mazao yetu nje ya nchi ili kuweza kupata fedha za kigeni, pia wakulima kuweza kulima zaidi na kupata kipato cha kujikimu.

Mheshimiwa Spika, tatu, pindi wakulima wanapolima na kuvuna mazao yao na kuamua kuyauza Serikali wakati wa kuuza isilingilie kati kwa kuwapangia bei ya kuuza kwa sababu wakati wa kulima walitumia jitihada za wenyewe bila kupata msaada wowote wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali kwa kutumia wataalam wetu wa kilimo itoe elimu ya kutosha kwa wakulima wetu jinsi ya kutumia mbegu bora, mbolea na madawa ya kuua wadudu ambao wanaathiri katika ukuaji wa mazao ili kuweza kulima kisasa zaidi na kupata mazao bora na yenye tija.

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali ihamashe wakulima kulima zao la mpira katika mikoa mingine kama ilivyofanya katika zao la korosho ili kuweza kupata malighafi ya kutosha katika Kiwanda cha *General Tyre* kilichopo Arusha maana kinategemea malighafi kutoka mikoa miwili tu Tanzania nzima; Tanga na Morogoro na hii wakati mwingine husababisha kiwanda kusimamisha uzalishaji kutokana na ukosefu wa malighafi.

Mheshimiwa Spika, sita, Serikali ihamashe wananchi (wakulima) walime mazao ambayo yatatumika kama malighafi katika viwanda vyetu vya hapa nchini, hivyo kuweza kujihakikishia soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, saba, Serikali iwalipe kwa wakati wakulima ambao mazao yao yanauzwa katika vyama vya ushirika, pia mazao ambayo Serikali imeamua kuyanunua hususan zao la korosho kuwalipa fedha zao ili wakulima hao waweze kupata fedha za kuandaa mashamba yao pindi msimu wa kilimo ukifika, pia waweze kupata fedha zao na kuweza kuzitumia katika kuhudumia familia zao.

Mheshimiwa Spika, nane, Serikali iboreshe mnyororo wa thamani wa mazao yetu ili kuweza kuuza katika soko la dunia kwa kuwa ubora wake utakuwa umeongezeka.

Mheshimiwa Spika, tisa, Serikali katika maeneo ambayo wakulima wanatumia zaidi kilimo cha umwagiliaji, iwawezeshe wakulima hao kuwapatia vifaa mbalimbali ambavyo vitasaidia katika umwagiliaji wa mazao yao maana wakulima wengi hutumia njia za kienyeji, mfano, kuchimba mifereji katika kumwagilia mazao yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawaombea afya njema na umri mrefu katika kutekeleza majukumu yao Waziri na Naibu Mawaziri wake pamoja na watendaji wote wa Wizara.

**MHE. RHODA S. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo inachangia 29.1% ya Pato la Taifa endapo tutaongeza juhudhi katika uzalishaji huenda Sekta ya Kilimo ndio ikaleta mageuzi makubwa nchini. Changamoto tuliyonayo ni kufeli kwa mipango ya Serikali yetu kufungamanisha miradi mikubwa ya kiuchumi na Sekta ya Kilimo sambamba na mikakati ya kuongeza thamani kwenye uzalishaji wa Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa takwimu za hifadhi ya chakula nchini tangu 2015 mpaka 2019 zinaonesha kiwango cha uzalishaji wa chakula kimeshuka kwa asilimia kubwa na inatisha. Nimeangalia takwimu zilizotumiwa na Benki Kuu Aprili, 2019 hifadhi ya chakula imeshuka kwa 82.7 kutoka mwezi Machi, 2019. Ukiangalia takwimu hizo utaona Machi, 2015 hifadhi ya chakula ilikuwa tani 452,054.0 lakini kufikia Machi, 2019 hifadhi ya chakula imeshuka mpaka 78,336.0.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya ardhi kuongeza uzalishaji. 53.3 ya ardhi yetu ni misitu na 15.4 iliyobaki ni ardhi yenye rutuba. Sehemu kubwa ya ardhi yetu hapa nchini inafaa kwa kilimo ila uzalishaji wetu umeendelea kushuka siku kwa siku. Kumekuwa hakuna utoshelevu wa kutosha wa chakula ili hali tuna ardhi yenye rutuba isipokuwa tuna maarifa duni ya kuongeza kiwango cha uzalishaji. Endapo tungekuwa na utoshelevu wa kutosha wa chakula basi hata ujenzi wa reli ya *standard gauge* unapaswa kutumika

kusafirisha chakula Afrika Mashariki, DRC Congo, Burundi na Uganda na Rwanda.

Mheshimiwa Spika, takwimu za uagizaji chakula nje ya nchi na bei za vyakula; Bei zimeshuka na kuumiza wakulima. Uagizaji umeongezeka kutoka dola milioni 13.3 mwezi Machi, 2018 mpaka kufikia dola millioni 15 Machi, 2019.

Katika mazao sita makuu mazao manne bei zimeshuka, Machi, 2018 gunia la mchele 185.735.4 na sasa 168,520.5 kwa 9.3. Maharage ilikuwa 170,140 na zaidi imefika 165,3000 na zaidi kwa 2.8%. Uwele gunia kutoka 76,712.1 sasa ni 75.677.4 kwa 1.3%. Gunia la viazi 67033.8 imeshuka kwa 1.9 mpaka 68,302.9. Mtama 148.8371 mpaka 134,724.3 hatujafanya juhudhi za kutosha kutumia sehemu ya ardhi yenye rutuba.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu ni kama ifuatavyo:-

(a) Ifanyike juhudhi ya kuongeza thamani ya mazao kama matunda kwa kufanya *packaging* na *processing* ya matunda *juice*.

(b) Kuweka mazingira bora ya kisheria na kisera kwa sekta binafsi kujenga viwanda na kuchakata korosho.

(c) Kuweka mazingira bora ya kisera na kisheria kwa sekta binafsi ili kujenga viwanda vya kukamua mbegu za mazao kama alizeti.

(d) Kuweka mazingira bora ya kisera na kisheria kwa sekta binafsi kujenga viwanda vya utengenezaji wa nguo *textile industries* pamba inayozalishwa nchini ni nyingi 20 peke huchakatwa nchini.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Japhet Hasunga kwa wasilisho zuri asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa saba wa kitabu cha Mheshimiwa Waziri, kinaelezea kuhusu Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Wananchi wa Wilaya ya Mafia wameitikia wito wa kuanzisha Vyama vya Ushirika na Akiba na Mikopo lakini kwa masikitiko makubwa maombi ya Msajili wa SACCOShaiba SACCOSyamepokelewa na Afisa Ushirika tokea tarehe 18 Machi, 2019 na hadi naandika hapa, Afisa Ushirika Mkoa wa Pwani hajatoa usajili kwa kisingizio cha kuwa anafanya uhakiki wa wanachama.

Mheshimiwa Spika, sheria inamtaka afisa kutoa usajili au kukataa ndani ya siku 60 na muda huo unamalizika kesho, Jumamosi, huku hakuna matumaini yoyote kwa SACCOS hii kusajiliwa. Naomba nichukue fursa hii kumwomba Mheshimiwa Waziri aingilie kati mchakato huu kurahisisha usajili.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 11 wa kitabu cha Mheshimiwa Waziri unazungumzia upatikanaji wa mbegu bora za mazao. Nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Bajeti tulibahatika kutembelea Kiwanda cha Kusindika Mafuta ya Alizeti cha *Mount Meru* kilichopo Mkoani Singida. Moja ya changamoto kubwa inayokikabili kiwanda hiki ni upatikanaji wa alizeti kutoka kwa wakulima. Uzalishaji wa alizeti hautoshelezi kulisha kiwanda hiki kutokana na wakulima kutumia mbegu duni za kizamani ambazo zinatoa alizeti kidogo kwa ekari moja.

Mheshimiwa Spika, nilete ombi kwa Serikali kuagiza mbegu bora za kisasa kutoka India zenyet tija kubwa kwa ekari. Mbegu hizi bora zitasaidia kulisha viwanda vyetu vya ndani na kuondokana na tatizo la kuingiza mafuta ya kupikia kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mafia inalima zao la nazi kwa wingi sana. Naomba kuishauri Serikali yangu kutuletea mtaalam wa kilimo na mbegu bora ili zao hili liweze kuwa na manufaa kwa wananchi wa Mafia na nchi nzima kwa ujumla. Nakushukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, pongezi kubwa kwa Serikali ya Awamu ya Tano. Niongelee utafiti. Bila utafiti wa magonjwa ya mazao, bila utafiti wa mbegu bora, bila utafiti wa masoko ya chakula na mazao ya biashara, bila utafiti wa wataalam wa kilimo ili kutambua ni wataalam wangapi waliopo na wako wapi na wanaleta tija gani katika maeno ya wakulima hapa nchini haya yote yasipozingatiwa na umakini mkubwa, na kikubwa bila kutenga bajeti ya kutosha katika maeneo yote hayo. Narudia tena kuiomba Serikali kutenga fedha za kutosha kwenye bajeti katika maeneo hayo na mengine ya kitaalam ambayo yanakuwa ni kikwazo na kurudisha nyuma sekta hii nyeti ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, maafisa ugani; maafisa ugani ni wachache na hata wale waliopo hawaonekani. Hii ni kutokana na ukosefu wa vitendeakazi kama magari, plkipiki, vifaa vyta kunyunyizia dawa ya kuulia wadudu waharibifu wa mazao n.k kwenye maeneo ya kata mbali mbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha muhogo; kilimo cha zao la muhogo ni chepesi na ni rahisi zaidi na kinastahimili ukame, lakini pia kina tija kubwa kwa wakulima wengi, hasa wadogo wadogo na wa kati. Hata hivyo pia kuna wawekezaji wakubwa na wa kati wameanzisha viwanda vyta kuchakata zao hili la muhogo kama kule Mkoa wa Lindi na Handeni (Tanga) ili viwanda hivi viweze kuzalisha kwa kiasi kikubwa zao hili la muhogo na ikizingatia kuwa wawekezaji hawa wametumia fedha nydingi kwa kuja hapa nchini kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda kama ilivyo malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano (Serikali ya Viwanda). Wawekezaji hawa pia wangepewa maeneo makubwa ya kulima kilimo cha muhogo kama walivyopewa maeneo wawekezaji wa kilimo cha miwa amba wanazalisha miwa na kisha kusindika (sukari), viwanda vyta kuchakata mpunga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji hawa wanalima mashamba yao na pia wananunua mazao mengine kwa wakulima wadogo wadogo (*outgrowers*).

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naiomba Serikali iwapatie maeneo makubwa wawekezaji wenyewe viwanda vyatia kuchakata mazao ya kilimo kama muhogo na mazao mengine ambao wamewekeza kwa kujenga viwanda hapa nchini. Kwa mfano kiwanda cha kuchakata zao la muhogo mkoani Lindi wanahitaji eneo kubwa la kulima zao hili. Wamepewa kiasi kidogo ili kuwapa moyo na kuvutia wawekezaji wengi, ni vyema wakapatiwa eneo la ziada ili kukidhi haja na tija kwa kiwanda na wakulima wengi Tanzania kwa mkoa wa Lindi na mikoa mingine ambayo inalima mihogo. Kiwanda cha Lindi ni muhimu sana, kiongezewe eneo.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji ndiyo suluhisho la kumkomboa mkulima wa Kitanzania na kupata ziada kuza mazao nje ya nchi. Nchi ifanye jitihada kubwa kujenga miundombinu ya kukinga maji ya mvua ambayo yatasaidia kunywesha mifugo, kufuga samaki, kumwagilia mazao ya kilimo na matumizi ya nyumbani. Je, eneo hili la kukinga maji ya mvua kwa kutengeneza mabwawa makubwa ya kuhifadhi maji ya mvua na kuweka miundombinu ya kutiririsha maji hayo kwenvye maeneo ya kilimo yanahitaji fedha za kigeni na wataalam kutoka nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, Ombi. Wizara ya Fedha itenye fedha za kutosha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Wataalam wetu katika Wizara ya Kilimo watambue unyeti wa Wizara hii na kwa uchumi wa nchi yetu, na watekeleze kwa kuhakikisha wanashirikisha na Wizara nyingine kama Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano) n.k.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SUSAN A. KOLIMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza sana Serikali kuitia Wizara ya Kilimo kwa juhudini kubwa wanayoifanya katika kuhakikisha

wanatatua changamoto zinazojitokeza katika sekta hii muhimu kwa taifa, sekta ya kilimo; ikiwemo utafutaji wa masoko kwa mazao ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi naomba kuishauri Serikali kutafuta masoko ya mazao ndani na nje ya nchi yetu. Mazao hayo ni pamoja na zao kama mahindi, viazi, maparachichi, mananasi matunda mengine kama maembe, *apples*, nk yanayolimwa katika Mkoa wetu wa Njombe.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali (Wizara ya Kilimo) kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya TAMISEMI ili kufanya utafiti katika Mikoa ili kujua wapi wamezalisha zao gani kwa wingi na mikoa ipi ina uhitaji wa zao hilo. Kwa mfano Njombe wanazalisha mahindi kwa wingi na mara nyingi wakulima wanavuna wanapata changamoto kubwa ya kuuza mahindi hayo ilhali kuna mikoa au wilaya nyingine zina uhitaji mkubwa wa chakula kama mahindi, maharage n.k. Kwa mfano mwaka jana Wilaya ya Longido walikuwa na uhitaji mkubwa wa chakula ikiwemo wananchi wa wilaya ya Ludewa/Njombe walikuwa na mahindi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Masoko Nje ya Nchi. Naipongeza Serikali kwa kupata masoko ya nje ya nchi. Kuna baadhi ya mazao kama mihogo, maparachichi n.k; naendelea kuishauri Serikali kuitumia Wizara ya Mambo ya Nje kupitia mabalozi walioko ndani na nje ya nchi ili kuweza kupata masoko ya maparachichi, mahindi, maharage na viazi; nchi kama vile Sudan Kusini, nchi za Falme za Kiarabu, nchi za SADC na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa Pembejeo. Naomba kuipongeza Serikali kuweka mikakati ya upatikanaji wa pembejeo ikiwemo mbegu, mbolea na viuatilifu vilivyowafikia wakulima kwa wakati. Niishauri na kuiomba Serikali kuhakikisha mbegu bora ikiwemo mbegu za mahindi, viazi mviringo, maharage na maparachichi kwa Mkoa wa Njombe vinasambazwa kwa wakati na kusimamiwa vizuri ili kuwafikia wakulima kwa wakati sahihi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali/Wizara kwa kutoa mafunzo ya uongozi wa mbolea kwa maafisa kilimo kutoka Mkoa wa Njombe ili kuweza kuleta tija katika kilimo. Naomba Wizara itoe mafunzo kwa wafanyabiashara wa mbolea wa Njombe kama ilivyofanya katika mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Japhet N. Hasunga (Mb) na Naibu Waziri Mheshimiwa Omary T. Mgumba na Mheshimiwa Innocent L. Bashungwa kwa kazi nzuri ya kuiongoza Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, nimependa nichangie kwa sababu naona nchi yetu inapoteza fursa kuboresha mazao na kuzalisha mazao mapya.

Mheshimiwa Spika, moja kwa kutotenga fedha za uhakika katika utafiti wa mazao na kilimo kwa ujumla. Mbili, kupiga marufuku utafiti na *controlled test* ya uhandisi jeni (*genetic engineering*). Katika eneo la utafiti, fedha tunazotenga katika *agricultural research* zinapaswa ziongezeke ili kukabiliana na changamoto za kuboresha mazao hasa kuongeza uzalishaji kuangalia udongo, kukabiliana na wadudu fungi, virusi na *nematodes*.

Mheshimiwa Spika, aidha, kumekuwa na kupanua marufuku ya *genetically Modified Crops (GMO's)*. Awali sheria ilikataza majaribio ya *GM crops* katika mashamba au kuzalisha mazao hayo ya majaribio katika mashamba. Jambo hili lilizui li kisheria kwa kuweka *strict liability clause*. Tangazo la Katibu Mkuu wa Wizara hii Mhandisi Mathew J. Mtigumwe likapiga marufuku kabisa utafiti wote, kwenye maabara, kwenye utafiti nje ya maabara na shambani. Jambo hili limefanywa bila kujali kuwa Tanzania ndiyo nchi ya kwanza Africa katika utafiti huu (tulikuwa mbele ya nchi zote Afrika katika kutafiti wa *GMO*). Tumefunga maabara na kuwatawanya wanasayansi na watafiti wetu.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inasikitisha na kurudisha nyuma sana. Hakuna kubisha kuwa tabianchi imebadilika kwa haraka na inaendelea kubadilika. Mazao tunayotumia ikiwa hatutayabadili kuweza kuendana na mabadiliko hayo, keshokutwa tutakuwa taifa lenye njaa sana. Wakati huo, tutakuwa hatuna majibu ya changamoto ya mvua kidogo, mvua inayonyesha kwa wiki tatu badala ya miezi mitatu, ongezeko la joto (*evaporation*) ongezeko la aina ya wadudu na idadi yao, virusi na visumbufu vingine, upungufu wa unyevu kwenye hewa na kwenye udongo.

Mheshimiwa Spika, maamuzi yetu yanatuchelewesha sana. Nchi yetu imefanya utafiti tayari na kuwa na mbegu yake ya *GMO cotton* (inaitwa *Bt cotton* Duniani). Hii ni kwa kuwa takriban nchi zote duniani zinazolima pamba zinazalisha na kutumia *Bt cotton*. Mfano wa nchi hizo ni India, Pakistan, China, Russia, USA, Brazil, Uganda, Kenya, Sudan, Egypt, Nigeria, Niger , Mali, Burkina Faso n .k. Ukiangalia ni Tanzania tu ambayo inakataza wakulima wake kutumia mbegu za *Bt. Cotton*.

Mheshimiwa Spika, *Bt cotton* inatoa *longer lint* (hivyo bei bora); inazalisha 3,000 kg *cotton/ha* ukililinganisha na mbegu za kienyeji tunazotumia. Inakinzana na wadudu na visumbufu vyta pamba hivyo huhitaji kupulizwa dawa (viuatilifu) mara tatu badala ya mara sita mpaka saba kwa msimu, na huhimili upungufu wa unyevu kwenye udongo. Aidha, kwa Tanzania ni muhimu kutumia *Bt cotton* kwa kuwa inakinzana na *red american ball worm*, hivyo kwa kutumia *Bt cotton* hatuna haja ya kuzuia kilimo cha pamba katika Wilaya ya Chunya, Rufiji, Lindi, Mtwara, na Wilaya zingine za Kusini.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Spika, kilimo kinaajiri zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania na hivyo ni vyema sekta hii ambayo ndio imeajiri watu wengi wa hali ya chini iangaliwe kwa umuhimu mkubwa na ipelekewe fedha za kutosha. Upelekaji wa fedha kwenye Wizara hii bado uko chini sana.

Mheshimiwa Spika, kama nchi tunatakiwa kujitafakari juu ya hali isiyotia matumaini ya baadhi ya mazao nchini. Wakulima wa katani/mkonge wamekata tamaa, kahawa nao wamekata tamaa, alizeti, mbaazi, mahindi, hali ni mbaya, korosho ndiyo hiyo inayoyoma.

Mheshimiwa Spika, ni vyema tuijulize tumekosea wapi? Hivi mkulima wa Tanzania alime nini ili apate kunufaika?

Mheshimiwa Spika, mahindi ni zao linalolimwa kama chakula na biashara. Mbegu bora ya mahindi inauzwa ghali sana na hivyo kufanya wakulima wengi kushindwa kuzipanda. Serikali iangalie namna bora ya kuwapatia wakulima mbegu bora. Huko nyuma tulikuwa na mashamba ya kuzalisha mbegu kuititia kampuni ya *TANSEED* ambayo yalizalisha mbegu tena katika mazingira ya kwetu. Mbegu kwa sasa nyingi zinatoka nje na ndiyo maana zinauzwa ghali.

Mheshimiwa Spika, zao la mbaazi nalo lina hali mbaya sana. Mwaka jana zao hili lilipoteza thamani na halikuuzika mwanzoni na baadaye liliuzwa kwa bei ndogo sana. Serikali iwatafutie masoko ya mbaazi.

Mheshimiwa Spika, kama kweli kilimo kinathaminiwa Serikali iwaajiri maafisa wengi wa ugani ili wakulima wapate mafunzo na ushauri wa kitaalam kwa karibu sana.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii muhimu katika maendeleo ya uchumi wa taifa letu. Ninaipongeza Wizara ilioongozw na Mheshimiwa Waziri Japhet Hasunga, Naibu Waziri Mheshimiwa Omary Mgumba, Naibu Waziri Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Katibu Mkuu wa Wizara na watendaji wa Wizara kwa hotuba nzuri ya kimkakati ambayo itaenda kutatua changamoto nyingi zilizoko katika Wizara hii. Ni matumaini yangu kuwa, timu hii itaibadilisha kabisa tija ya sekta hii nchini.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa mazao ya kimkakati, yaani kahawa, pareto, pamba, tumbaku, alizeti,

parachichi, mbaazi, kunde, choroko, dengu, soya, kwenye mazao mchanganyiko Mkoa wa Songwe unazalisha kwa wingi kahawa tena ya arabika, pareto, cocoa, mpunga, parachichi, soya, mahindi, maharage, viungo na mboga. Fursa za kuendeleza mazao haya, hususan pareto, kahawa, cocoa, viungo na alizeti ni kubwa sana. Wakulima wamehamasishwa sana na wameitikia wito na wanazalisha kwa wingi hasa katika Wilaya ya lleje.

Mheshimiwa Spika, iko haja ya Serikali kuwa na mkakati wa kuzingatia hatua zote za mnyororo mzima wa thamani katika kila zao muhimu na la mkakati, liwe la chakula au la biashara. Hii ni pamoja na uzalishaji, usafirishaji na uhifadhi. Soko linahitaji aina ya bidhaa, kiasi na ubora na kwa hivyo iko haja ya kuwekeza katika kukuza uzalishaji mkubwa. Uzalishaji mkubwa unahitaji teknolojia na matumizi bora ya pembejeo, mbegu bora, miche, mbolea, dawa, pamoja na kuimarisha shughuli za ugani, ili kulinda ubora na wingi wa uzalishaji mazao husika.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la ugani kuna changamoto kubwa ya upotevu mkubwa wa mazao wakati wa kuvuna na wakati wa kuhifadhi. Upotevu huu wa mavuno unatokana na changamoto ya uhifadhi, maghala, kwamba hayatoshelezi na kwa hivyo hata ile dhana ya kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani unashindikana, na kwa hivyo, kumfanya mkulima kukosa bei nzuri na huduma muhimu za kumlinda dhidi ya hasara na umasikini wa kipato.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya yangu ya lleje mazao yanayozalishwa ni pamoja na kahawa ya arabika, pareto, alizeti na kwa kiasi kidogo cocoa na korosho ambayo imeanza kulimwa. Eneo linalolimwa kahawa limeongezeka kutoka hekta 5,859 hadi hekta 6,229 ambapo jumla ya kata 10 zinajihusisha na kilimo cha kahawa. Uzalishaji kwa lleje upo kati ya tani 550 hadi tani 800 kwa mwaka. Mwaka 2017/2018 tulipata tani 707.9, mwaka 2018/2019 tumeweza kupata tani 549.9. Kushuka huku kumesababishwa na hali ya hewa ilioyathiri kipindi cha kuchuma maua. Lleje na Mbozi ni wilaya mbili zinazozalisha kahawa ya arabika, kahawa hii inafanya

vizuri kwa sababu, ya hali nzuri ya hewa, rutuba na mvua ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, masoko ya kahawa bado ni changamoto japo bado mahitaji ya kahawa ni makubwa katika masoko ya nje kama Japan wanaonunua *gourmet coffee* kwa bei kubwa sana kwa sababu ni kahawa inayozalishwa bila kutumia kemikali (*organic*), Ulaya, Canada, India, China na kadhalika. Masoko haya yanatupa fursa ya kuona umuhimu wa zao hili, ili kuwekeza zaidi kuhakikisha tunaingiza fedha nyingi ya nje kujenga ajira za wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali katika kurekebisha mfumo wa vyama vyaya ushirika; hii imesaidia sana, lakini bado elimu ya kutosha inahitajika kwa wananchi kuielewa hii dhana, hasa baada ya historia mbaya iliyojengeka huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, tunaishauri Serikali iendelee kufanya kazi suala la masoko. Kilimo hai kiendelezwe kwenye kahawa, hii itasaidia wakulima kupata bei nzuri. Serikali itueleze itaweka mkakati gani wa kuendeleza hili. Ugani kwenye kilimo cha kahawa unahitajika sana ili kuwawezesha wakulima kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, zao la pareto ni miongoni mwa mazao ya kipaumbele kwa Wilaya ya lleje na ndani ya Mkoa wa Songwe. Zao linalimwa katika hekta nne vijiji 12 wakulima 3,500. Wakulima wanahitaji elimu zaidi, miche bora na utaalamu kuzingatia ubora wa zao wakipeleka sokoni, ili wapate bei nzuri. Serikali isaidie katika kuwasaidia wakulima kutengeneza makaushio bora na yanayozingatia utunzaji wa mazingira. Jumla ya tani 397 za mauwa ya pareto zilikusanywa mwaka hadi Aprili, 2019.

Mheshimiwa Spika, tunashauri Serikali ifanyie kazi changamoto zinazolikabili zao hili. Suala la masoko liendelee kufanyiwa kazi ili kupata masoko ya bei nzuri kwa wakulima. Kuboresha miundombinu ya hifadhi ya mazao (maghala).

Vyama vyta ushirika kuwezeshwa kiuchumi/mitaji, ili kuwawezesha wanachama wao kuendesha shughuli za maandalizi ya zao hili.

Mheshimiwa Spika, parachichi ni zao linaloongezeka kwa umuhimu katika Wilaya yetu. Hili pamoja na pareto na hata kahawa bado vinaingiliwa sana na walanguzi, hasa kutoka Kenya. Je, Serikali inafanya nini kuzuia hili jambo ambalo linawanyonya wakulima na kuwanufaisha wakenya?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuipongeza Wizara kwa jitihada kubwa wanazofanya katika kukuza kilimo nchini.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa changamoto ya ahadi wanazopewa wakulima lakini zinageuka kuwa vilio. Mfano ni Mkoa wa Tanga; mwaka 2018 walipewa ahadi wakalima mihogo kwa kiwango kikubwa sana mwisho wake ikageuka hasara kubwa kwao. Hamasa hii ilitoka kwa baadhi ya viongozi wa Serikali na mashirika yasiyokua ya kiserikali. Tatizo hili liliwapata pa wananchi wa Tunduma kwenye kilimo cha mbaazi. Niiombe Serikali illangalie hili tatizo na kuona inazuiaje lisijirudie, na pia kuwasaidia wale wanaokumbwa na hasara hii kwa kuwafidia walau kwa kiwango fulani ili wasikate tama maana kilimo ndio uti wa mgongo kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia niiombe Serikali ione umuhimu wa kuwaelimisha na kuwapa hamasa hasa vijana ambaio ndio wana nguvu kujunga sana na kilimo kwa kuwasaidia pembejeo, elimu na maeneo ili kuwavutia wasizagae tu mitaani kwa kukosa ajira rasmi hatimaye kujajiri katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, vilevile wakulima wa mbogamboga wengi wao wanalima katika mabonde ya maji machafu, labda ni kwa kukosa elimu ya afya au kukosa maeneo hivyo kupelekea matatizo ya kiafya kwa watumiaji wa mboga hizo ikiwemo kuumwa matumbo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wanalima tu kimazoea bila kuwa na elimu ya kilimo bora. Serikali ione umuhimu wakuwaelimisha wakulima kwa ngazi za vijiji maana si wote wana uwezo wa kusikiliza kuititia redio au televisheni.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya kumalizia niiombe Serikali iwasaidie sana wakulima pembejeo za kilimo kwa wakati. Naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER CHIZA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuleta hotuba nzuri na kuibua changamoto.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, atakapohitimisha hoja yake naomba atoe maelezo kuhusu maeneo matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali illeta muswada wa Sheria (mwaka 2013) ulioweka muundo wa Kitaasisi (Tume ya Umwagiliaji) uliolenga kugatua madaraka na huduma za umwagiliaji kutoka ofisi ya kanda na kuanzisha ofisi za mikoa na kwenye halmashauri za wilaya.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuomba wataalam/wahandisi wa umwagiliaji hawatoshi kusambazwa wilayani haina nguvu. Wataalamu wanaendelea kuzalishwa na wengine wanastaifu kila mwaka. Hata *extension officers* hadi leo hawatoshi lakini huduma za ugani zipo wilayani. Nashauri utekeleze yaliyomo katika Sheria ya Umwagiliaji kwa sababu Wabunge waliipitisha Sheria ya Umwagiliaji na Muundo wa Tume.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali; na Wizara ilianzisha mchakato wa *Price Stabilization Fund* kwa kuanzia na mazao ya tumbaku, kahawa, korosho na pamba. Mchakato huu umekwamia wapi? Je, bado kuna nia ya kuanzisha *Commodity Exchange Market* kwa ajili ya mazao ya kilimo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya katika kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kuzuia uuzaji wa Chakula/Nafaka ya chakula nje ya nchi kwa kuwa nchi yetu mwaka huu maeneo mengi yamekumbwa na ukame.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuishauri Serikali kuongeza Bajeti ya Wizara hii kutokana na kwamba sekta hii huchangia zaidi ya asilimia 25 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa maafisa ugani tunaomba sana Serikali iajiri maafisa ugani walau hata kwa ngazi ya Kata kote nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua za makusudi kupata fursa ya kuokoa mauzo ya korosho ili hata hasara itakayotokea iwe ndogo. Sote tunafahamu lengo la Serikali lilikuwa ni kukomesha hujuma walizokuwa wanafanyiwa wakulima wa korosho.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu nia hiyo njema ya kumwezesha mkulima kupata faida kuitia kilimo cha korosho.

Msheshimiwa Spika, mwisho naomba Wizara kupita wataalam wake wafanye ziara katika Jimbo la Mbulu Mjini. Tulikuwa na bwawa la Tlawi, katika Kijiji cha Tlawi. Bwawa hili la Tlawi limefanyiwa usanifu wa kina mwaka 2005 na kuombewa fedha kuanzia mwaka 2009 mpaka sasa. Hata hivyo nampongeza sana Mheshimiwa Isack Kamwelwe alifanya ziara ya kutembelea eneo lilitotarajiwaa mwaka 2017 na kuahidi kulitafutia hela. Kwa kuwa bwawa hilo ni muhimu

na wananchi wa Kijiji cha Tlawi tayari wamepeleka mawe lori hamsini (50) katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, naomba Mheshimiwa Waziri kama tulivyo kubaliana ufanye ziara kwa ajili ya ufumbuzi wa suala hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga hoja asilimia 100 kwa maslahi mapana ya taifa.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo kupata fursa ya kuchagia na kunipa afya njema.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu pia kutupa Baraka zake nchini na kutupa amani.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Rais wetu wa Awamu ya Tano Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli pamoja na Mawaziri wake hasa katika Wizara ya Kilimo, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa taasisi mbalimbali chini ya Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nashauri suala la bajeti, kwa maoni yangu kila mwaka bajeti ya Wizara hii hushuka kidogo kidogo. Maeleo tunayopewa ni kupanda kwa bajeti ya Wizara nyingine zinazopeleka pia bajeti zao kwa maendeleo ya wakulima. Mimi binafsi nikipiga hesabu kutokana na Bajeti kuu ya Shs. trillion 33, hiyo mikataba tulioingia kama nchi, ya Malabo na Maputo kufanya asilimia 10 ya bajeti tatu kwa sekta ya kilimo, bado hatujafikia asilimia 10 ya trillion 33, ni trillion 3.3. Hata ukijumlisha fedha zote za Wizara mtambuka kama TAMISEMI, Ardhi, Mifugo na Uvuvi, (Barabara za vijiji) uchukuzi, Maliasili na Utalii, Maji, Mawasiliano, Elimu, Afya, Fedha zinazokwenda vijijini tulipo wakulima haziendi trillion 3.3 (chukua, Bajeti za REA, TARURA, RUWASA, Afya, Elimu, TAMISEMI)

Mheshimiwa Spika, pia ukilinganisha Bajeti za Kilimo kwa miaka mitatu au mitano, badilisha kwa bei hiyo ya Dollar ya Marekani (\$USD) utanona bajeti inashuka.

Mheshimiwa Spika, pili nashauri Serikali itekeleze "*Blueprint*" ili kuondoa tatizo la urahisi wa kufanya biashara (*Fair Competition in Trade*). Leo hii tumeona sekta isiyokuwa rasmi inakua kutokana na sekta rasmi kutozwa kodi, Ada, Tozo na ushuru mkubwa na kwa idadi kubwa kutoka kila taasisi ya udhibiti (*Regulatory Bodies*).

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iangalie namna ya kuboresha sekta ya umwagiliaji. Nipongeze Serikali kurudisha sekta ya umwgiliaji. Niipongeze Serikali kurudisha Tume ya Umwagiliaji kutoka Wizara ya maji kurudi Wizara ya Kilimo. Naamini Wizara hii itaitendelea haki sekta ya umwagiliaji tangu Tume kuanzishwa hadi leo haikupangiwa au kupewa fedha za maendeleo katika umwagiliaji. Nashauri Serikali isibaki kujaribu kufanya peke yake bali iweke mazingira wezeshi na rafiki ili sekta binafsi pia ichangie. Nashauri Serikali iondoe kodi katika mitambo ya kuchimba maji na mitambo ya kutengeneza mabwawa, pamoja na kodi ya *Pump* za Sola za umwagiliaji na vipuri vya zana za umwagiliaji. Pia Benki ya TADB na Mfuko wa Pembejeo watenge asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, nashauri kila Mkoa upewe angalau mitambo ya kuchimba mfereji na mabwawa badala ya kutoa tenda ya kuchimba maji na kutengeneza mabwawa.

Mheshimiwa Spika, napongeza juhudhi ya kuwa na Sera na Sheria ya Kilimo, ndiyo njia pekee ya kusonga mbele. Hapa nashauri ardhi ya kilimo italindwa na mijini mashamba ya kilimo yataendelea.

Mheshimiwa Spika, nashauri TARI ipewe kipaumbele kwa kupewa bajeti ya kutosha ya ndani ili wenyе kufanya utafiti vizuri wa mbegu, viuatilifu vizuri vya mbegu, viuatilifu vya magonjwa na pia ugani katika kilimo. Bila kuwekeza katika taasisi yetu ya TARI kilimo chetu itabidi kuwa cha

kubabaisha na duni bila tija. Tuna vituo 17 na vyote vinahitaji kuboresha miundombinu, vifaa nya kisasa kufanya kazi zao vizuri na zana nyingine kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Nashauri Chuo Kikuu cha SUA kiwe chini ya Wizara ya Kilimo ili kuboresha tija katika chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, nashauri ASA iongezewe mtaji ili kuzalisha mbegu bora na zenye viwango kwa kutosheleza mahitaji ya nchi. Nje ya bajeti wao wakopeshwe zana za Kilimo, matrekta na zana nyingine, vifaa nya umwagiliaji nya aina mbalimbali kutokana na shamba husika, vifaa nya kuchakata na kusafisha mbegu na kuweka dawa ya kuhifadhi na kutunza mbegu na hapo hapo TASTA pia ipewe watumishi wa kutosha na wapate mfumo wa TEHAMA kwa ajili ya kusafirisha mbegu za ndani na nje ili kuwa na udhibiti wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, pia na shauri *TFS* wafanye uhakiki wa aina mbalimbali za mbolea na kuishauri Serikali kuondoa vikwazo katika baadhi ya vipengele kwenye Sheria ya Mbolea.

Msheshimiwa Spika, nashauri Serikali na Wizara ishirikiane na taasisi nyingine kuboresha *TPR/iliyopo* chini ya Wizara ya Kilimo na kuiboresha pia Miundombinu, vifaa nya kisasa kuifanya kazi yao. Wafanye utafiti wa mabaki ya sumu tunayotumia sisi walaji wa mazao (*No pesticide Residuals*) na kushauri nini kifanyike.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Benki ya Kilimo na Mfuko wa Pembejeo ziongezewe mtaji ili Serikali ifanye yale yake na sekta binafsi zifanye juhudhi kuendeleza kilimo na umwagiliaji.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa fursa hii na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendani wote.

Mheshimiwa Spika, swalilangu linahusu zao la kahawa Mkoa wa Kilimanjaro. Serikali ina mpango gani kushirikiana na wakulima wakubwa ili watoe msaada wa pembejeo, elimu na hata kuwatafutia soko wakulima wadogo? Naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Naishauri Serikali ione haja ya kufanya kazi maoni ya Kambi Rasmi kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ningependa niishauri Serikali kuweka mkakati madhubuti wa kujenga mabwawa ya umwagiliaji na majosho ili kuepuka kilimo cha kubahatisha. Mfano ni Jimbo la Mlimba, shughuli kubwa ni kilimo cha mpunga, pia ndizi, cocoa, ufuta, mahindi, miti, maparachichi na kadhalika. Kila zao linastawi lakini Jimbo zima lina mradi mmoja tu wa umwagiliaji ambao hauna tija ingawa unatumia hela nydingi.

Ombi na kilio cha wananchi wa Njagi ni kujengewa bwawa ambalo litawawezesha kulima kwa mwaka mzima, tofauti na sasa hulima wakati wa mvua tu, mara moja kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, pia kwa kuwa Jimbo la Mlimba lina mito mingi inayotiririka mwaka mzima na maeneo makubwa yaliyokuwa yanatumiwa kwa kilimo yamechukuliwa na Maliasili kwa mradi wa bwawa la umeme Rufiji. Hivyo basi kuna umuhimu mkubwa wa Serikali kupeleka fedha kwa uchimbaji mabwawa na malambo ili wananchi wapate kilimo bora katika maeneo machache yaliyobakia vijijini ambapo itawezesha kupata ufanisi katika kilimo. Hivyo ningependa kupata majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Jimbo la Mlimba kuwa ni eneo la kilimo lakini kuna uhaba mkubwa wa wataalam wa kilimo; hivyo napenda kupata majibu ya Serikali; Je, ni lini Serikali itaatiri waghani na kuapeleka Jimbo la Mlimba ili wakulima hao wapate tija katika mazao yao?

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Mlimba wana upungufu mkubwa wa mitambo ya kilimo. Mfano Gereza la Idete la kilimo pamoja na kuwa na maeneo makubwa ya kilimo lakini Serikali imewapatia trekta moja tu na kuwafanya washindwe kuyalima mashamba yote. Pia mitambo ya kuvunia ili kuwezesha kupata mazao bora na kuondosha upotevu wa mpunga kwa kutumia wafungwa kuvuna. Je, Serikali iko tayari kupeleka matrekta na *harvester* gereza la Idete? Je, Serikali iko tayari kupeleka matrekta katika Halmashauri ya Kilombero ili wakulima waweze kukopa na kuongeza mazao yao?

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Mlimba wanalima sana lakini mazao yao yanakosa soko kutokana na ubovu wa barabara. Kukosekana kwa soko, vikwazo vyta Serikali kuweka zuio la kuuza nje ya nchi isipokuwa ndani ya nchi tu inamkandamiza mkulima kwani anatumia garama kubwa na kuuza bei ndogo hivyo kumuongezea umaskini. Nashauri Serikali isiwe inamzuia mkulima huyo kuuza mazao yake nje ya nchi kwa faida, ahsante.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo ambayo kimsingi ni uti wa mgongo wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Wakulima wa Miwa. Kumekuwa na kilio cha muda mrefu sana cha wakulima wa miwa wa bonde la Ruhembe Jimboni Mikumi ambao ni wakulima wa miwa wa nje (*out growers*) katika ukanda wa Bonde la Ruhembe ambapo malalamiko yao ya muda mrefu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, idadi ya miwa inayoingizwa kiwandani kutoka kwa *outgrowers* bado imekuwa ndogo sana hivyo tunaomba sana Wizara iliangalie suala hili kwa kuwa tumewashauri sana wakulima na watu wengine walime miwa kwa wingi, lakini miwa inayochukuliwa na kiwanda ni kidogo. Hali hii inasababisha miwa mingi ya wakulima wa nje kutochukuliwa na kiwanda, hasa ukizingatia pia kuwa kiwanda nacho kina mashamba yake.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Mzani. wakulima wa miwa wamekuwa wakilalamikia sana mzani unaotumika na kiwanda cha Illovo kwa kuwa mzani ni wa Illovo na wanaopimia ni watu wa llovo hivyo wakulima wanakosa wawakilishi wa kuwawakilisha ili kuhakikisha kuwa kiwango cha miwa na utamu kweli vinaendana na uhalisia. Hivyo wakulima wanaomba sana wapate mzani wao au wawe na uwakilishi wa kutosha katika mzani unaotumiwa na kiwanda cha sukari cha llovo.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utamu wa Muwa (*sucrose*). Kumekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa wakulima wa miwa kwamba kwa kuwa hawana wawakilishi wakati wa upimaji wa utamu wa sukari, basi wamekuwa wanapewa takwimu ambazo si sahihi, hivyo kuwafanya walipwe pesa kidogo sana kutokana na vipimo vya sukari vinavyoonesha kuwa miwa yao ina utamu kidogo tofauti na uhalisia. Kwa kuwa kuna wakati wanaambiwa miwa yao ina *sucrose* mpaka nne (4), kitu ambacho wataalamu wanasema hakuna kiwango hicho kwa miwa ya bonde la Ruhembe, bali inakuwa kwenye 10 -11 na si hizo takwimu ambazo wanaambiwa na watu wa kiwandani.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Mabaki (Maganda ya Miwa – *Bagasse*). Wakulima wameendelea kulalamika kuwa wanalipwa utamu tu wa miwa na hawalipwi mazao mengine yanayotokana na miwa kama mashudu (*bagasse*) ambazo zinatengenezewa umeme na nytingine zinatumika kama mbolea. Pia wamekuwa hawalipwi *molasses* ambazo zinatumika kwa ajili ya kutengeneza *sprit*, hivyo kilio kikubwa cha wakulima kwa Serikali ni kuhakikisha wakulima hawa wa miwa wanalipwa na vitu vingine vinavyotokana na miwa kama *bagasse* na *molasses* sambamba na *sucrose* (utamu) ili kuuinua uchumi wa wakulima wetu wa nje.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Pembejeo. Kama Kambi Rasmi ya Upinzani ilivyoshauri, kilio kikubwa cha wakulima ni ukosefu wa pembejeo kwa wakati. Ili tupate kilimo bora ni vema sana Serikali ikahakikisha kuwa upatikanaji wa pembejeo unapatikana kwa wingi na kwa haraka

iwezekanavyo. Kwa mfano kwenye Wilaya yetu ya Kilosa pia tumekuwa na ucheleweshaji mkubwa sana wa pembejeo. Pia zimekuwa na tatizo la kupatikana kwa bei ya juu sana na inapanda kila mwaka na kufanya wakulima wetu wa Wilaya ya Kilosa kushindwa kulima kwa tija ilhali wilaya yetu imebarikiwa sana kwa kuwa na ardhi nzuri ya kilimo na ni moja ya wilaya bora kabisa hapa nchini kwetu kwenye sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba sana Serikali ili wakulima wetu waweze kulima kilimo bora na cha kisasa, ihakikishe upatikanaji wa pembejeo, usambazaji wa pembejeo na matumizi yake. Pembejeo zinazohitajika sana kwa wakulima wetu wa Wilaya ya Kilosa ni mbegu bora, mbolea na madawa, ahsante sana.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia hoja hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kushika kalamu na kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi. Kwanza nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote watatu pamoja na Makatibu wote kwenye Wizara hii bila kuwasahau Wakuu wa Taasisi zote zilizopo kwenye Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya kwa kipindi kifupi walichopewa kufanya kazi kwenye Wizara hii. Kwa kweli sasa tumeanza kuona matunda ya kazi zenu kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Liwale ni mionganoni mwa Wilaya zinazolima zao la korosho na mazao mengine ya chakula na biashara kama vile ufuta, mbaazi, mtama na muhogo. Tatizo kubwa la wakulima wa Liwale ni upatikanaji wa masoko ya mazao hayo, Wilaya ya Liwale haina soko la uhakika la mazao ya biashara. Shida nyiningine kubwa sana katika kilimo ni uhaba wa maghala ya kuhifadhiya mazao hasa inapokuja kwenye msimu wa korosho. Mwaka huu korosho kwa mfano zimekaa muda mrefu sana kwenye maghala madogo ya vyama vya msingi, maghala ambayo hayana ubora hivyo kuharibu ubora wa mazao husika. Hivyo naiomba Serikali kuipatia ujenzi wa maghala kwenye halmashauri yetu.

Mheshimiwa Spika, malipo ya korosho kwa Wilaya ya Liwale bado si wa kuridhisha kwani wakulima wote wakubwa bado hawajapata malipo yao japokuwa uhakiki ulishakamilika. Naiomba Serikali kuangalia malipo haya japo msimu wa maandalizi wa mashamba umeshapita na wakulima hao hawajui hatma ya mashamba yao. Pamoja na kauli ya Mheshimiwa Rais alipokuwa ziarani Mtwara kuamuru wakulima wote walipwe, jambo hili kwa halmashauri ya Liwale halijatekelezwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, Skumu ya Umwagiliaji ya Kata ya Ngongowele Wilayani Liwale ni ya muda mrefu sana. Hatma ya mradi huu hadi leo hatujui hatma yake licha ya kutengewa fedha kila mwaka; fedha za awali zaidi ya milioni 700 zimeliwa bila mafanikio. Naiomba Serikali kuja na timu maalum ili kufanya ukaguzi ili kuona namna mrdai huu ulivyoohujumiwa.

Mheshimiwa Spika, idara ya kilimo katika halmashauri ya Liwale pamoja na changamoto nyingi lakini uhaba wa watumishi wa kada hii ni mkubwa; sambamba na uhaba wa vitendea kazi kama vile magari na pikipiki kwa ajili ya maafisa ugani. Kulikuwa na mradi wa upandaji wa Miche ya mikorosho, vikundi mbalimbali vilihamasishwa kuanzisha vitalu vya Miche ya mikorosho lakini hadi leo vikundi hivi bado havijalipwa malipo ya upandaji wa Miche hii. Watu hawa walichukua mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha hivyo sasa watu hawa wako kwenye hatari. Naiomba Serikali kuwalipa watu hawa madai yao.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Liwale inapakana na Pori la Akiba la Selous hivyo kuna changamoto kubwa sana ya wanyama waharibifu kuharibu mazao ya wakulima. Wanyama hawa ni kama vile nyani, nguruwe, viboko na tembo. Hivyo naiomba Wizara ikisaidiwa na askari wa wanyamapori kuja na mkakati maalum wa kuwasaidia wakulima hawa namna ya kuanzisha vikosi vya misako ya mara kwa mara, misako ambayo inahitaji msaada wa vifaa kama bunduki ndogo, nyavyu za kusakia na zana nyingine za kusaidia kupunguza athari za uharibifu huo.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuondoa umaskini bila kuigusa sekta inayoajiri Watanzania wengi, hivyo basi, napendekeza kuondoa kodi kwenye Uwekezaji katika sekta ya kilimo ili kuboresha na kukuza uchumi kupitia sekta hii.

Mheshimiwa Spika, wananchi walio wengi wanaojishughulisha na kilimo wameachwa na Serikali kujitegemea wenyewe. Serikali ingewekeza angalau asilimia 40 katika sekta hii, itasaidia katika kuboresha na kuimarisha/ kukuza mnyororo wa thamani (*Agricultural value chain*), na kwa jinsi hii itaweza kutengeneza ajira nyingi katika ngazi mbalimbali (vitongoji – wilaya – mikoa) na itakuwa na *major impact* katika nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali haijaweka wazi mikakati ya wazi ya kufungamanisha sekta ya kilimo, na sekta ya viwanda. Ni wakati sasa suala hili likaangaliwa katika upana wake.

Mheshimiwa Spika, Suala la Pembejeo Katika Ujumla Wake. Kuna uhaba na ucheleweshwaji wa kusambaziwa kwa Wakulima, ubora hafifu, kutokufika kwa wakati (msimu), bei kuwa juu kwa baadhi ya maeneo na kukosekana mfumo thabiti kuzuia pembejeo zisizo na ubora kwenye soko kwa kuzingatia haya. Wizara ifanye tathmini na kutengeneza mikakati mahsusii ya kuboresha haya.

Mheshimiwa Spika, Raslimali Watu Katika Sekta ya Kilimo. Kuna upungufu mkubwa wa wataalamu na maafisa ugani katika sekta hii. Hata kwa wafanyakazi waliopo (*especially* maafisa ugani) wanafanya kazi katika mazingira magumu kwa ukosefu wa vitendea kazi. Wizara ilifanyie kazi suala hili.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Mazao Baada ya Kuvunwa (*Post-Harvest Losses*); hii husababishwa na:-

(i) Wakulima kuwa na elimu ndogo na miundombinu hafifu ya kutunza/ku-store mazao yao (na hata wakati

mwingine kusababisha kutokea kwa *aflatoxins*) na (kuhatarisha afya za binadamu na mifugo);

(ii) Idadi ndogo sana za maghala za kuhifadhi (kati ya vijiji 13,000, kuna maghala mangapi?);

(iii) Teknolojia zinazotumiwa wakati wa kuvuna na kusindika ni duni sana, hii husababisha upotevu mkubwa wa mavuno (n20% ya mazao hupotea baada ya mavuno).

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha na Kuboresha Mfumo wa Masoko (Ndani ya Nje ya Nchi). Changamoto ni nyingi na kusababisha hasara na ugumu wa maisha (hususan kwa wakulima wadogo). Wizara/ Serikali ijifanyie tathmini ili kuboresha suala hili.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara ya Kilimo na kumpongeza Waziri na Manaibu wote wawili. Ombi langu ni kuhusu Skimu ya Umwagiliaji ya Lwafi iliyopo Jimboni Kwangu Katika Kata ya Kipili na Kirando. Skimu hii imegharimu pesa shilingi bilioni moja na mia nane milioni, kubwa sana hajasaidia wakulima wa mpunga wa kata hizo kabisa na wakandarasi wamepewa fedha zote hizo.

Mheshimiwa Spika, Skimu hiyo ilikuwa isaidie sana wakulima wetu, leo hii skimu hiyo ni bomu kubwa. Kusema kweli fedha iliyotumika hailingani na kazi, inaonesha wataalamu wetu hawakusimamia sawa au hawana utaalamu wa kutosha na kusababisha kupoteza pesa bilioni 1.8 bure. Naomba uchunguzi ufanywe na skimu ikamillike.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri sana, wanayoifanya ya kusimamia na kutekeleza majukumu waliyopewa.

Mheshimiwa Spika, Zao la mahindi, halijapewa kipaumbele licha ya kuwa Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa mikubwa minne inayozalisha mahindi kwa wingi

sana na zao hili bado halijawekewa mkakati madhubuti wa soko na mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara ina mpango gani wa kufanya utafiti wa mbegu bora ambazo zitaleta tija kwa mkulima kulingana na aina ya mbegu na udongo unaostahili kulimwa mahindi, na utafiti huo utachukua muda gani ili kuharakisha utekelezaji huo ili kuokoa nguvu za wakulima zinazopotea bure kwa uzalishaji usio na tija?

Mheshimiwa Spika, zao la tangawizi linalimwa sana katika Wilaya ya Songea Vijiji ni katika Halmashauri ya Madaba maeneo ya Mkongotema, Mahanje, Madaba, Wino na maeneo mengine. Tangawizi ni chakula, tangawizi ni dawa na imekuwa ikitumika sana katika mapishi mbalimbali. Je, Serikali ina mpango gani katika kuwekeza zao hili ambalo limekuwa linakuza uchumi katika nchi yetu ya Tanzania?

Mheshimiwa Spika, lakini, pia limekuwa likiuza ndani ya nchi yetu tu ilhali ziko nchi mbalimbali ambao wamekuwa wakitumia tangawizi kama chakula na dawa. Ninaomba Serikali ilete wataalamu katika maeneo yaliyotajwa hapo juu ili kuendelea kutoa elimu elekezi kwa wananchi. Ni imani yangu kuwa kwa kufanya hivyo itasaidia sana kuongeza tija katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Masoko, soko la mahindi ni tatizo kubwa sana, ningependa Serikali itafute soko la uhakika la mahindi. Halikadhalika ninaomba Serikali itafute soko la tangawizi, mbaazi, mahindi na mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Mawakala wa Pembejeo. Mawakala wa pembejeo hawajalipwa pesa zao kwa muda mrefu sana. Je, tatizo ni nini? Siku zote majibu ya Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha ni juu ya suala la uhakiki, je uhakiki huo utaisha lini? Mimi sioni kama mawakala wote walifanya udanganyifu kwa Serikali bali ninaamini kuwa katii yao wapo waliofanya vizuri. Sasa ni kwa nini hao waliofanya vizuri wasilipwe? Ninachelea kusema kuwa Serikali haiwatendei

haki mawakala wa pembejeo, ninaomba mchango wangu hansard.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Scheme* ya Umwagiliaji ya Mtula. Baada ya umwagiliaji kuhamishiwa Wizara ya Kilimo, ninaomba Serikali ione uwezekano wa kukamilisha *Scheme* ya Umwagiliaji ya Kijiji cha Mtula ambayo ni msaada mkubwa kwa kilimo na uchumi wa wananchi wa Mafinga.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa viwanda, msingi wake ni kilimo; jitihada za kujikwamua na uhaba wa sukari, zitafanikiwa ikiwa tu Wizara ya Kilimo itaongeza jitihada za Kilimo cha miwa hasa kwa *small scale* na hasa kwa kufanya ubia katи ya Serikali (halmashauri na sekta binafsi).

Mheshimiwa Spika, naambatisha haya maelezo ya Kaimu Mwenyekiti wa Chama cha Wakulima wa Miwa, Dkt. George Mlingwa, na wenzake. Pamoja na kuwa andiko hili ni la mwaka 2016/2017 bado ninaamini *module* hii ambayo wenzetu Brazil wametumia inaweza kuwa suluhisho la uhaba wa sukari ambao msingi wake ni kilimo cha uhakika cha miwa.

Mheshimiwa Spika, maelezo kwa ufupi kuhusu sukari, kuna maeneo mengi nchini ambayo tunaweza kujenga viwanda vidogo na vya katи, (tani 10,000 mpaka tani 30,000 kwa mwaka). Kila mkoa una maeneo kama haya. Kwa mfano Kilosa tani 10,000, Manyara tani 10,000, Mara tani 30,000, Ruvuma tani 10,000, Dodoma Chamwino tani 10,000, Kigoma Bonde la Malagarasi tani 30,000, Pwani – Rufiji tani 30,000 na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa viwanda vidogo unachukua muda mfupi, miezi nane mpaka kumi. Gharama zake ni za chini USD milioni tatu hadi kumi ukilinganisha na vile vikubwa USD milioni 100 hadi milioni 300 ambavyo huchukua miaka miwili hadi mitano. Viwanda vidogo viko karibu na wananchi, bei ya sukari yake ni nafuu kutokana na gharama kuwa chini. halmashauri za wilaya husika zinaweza

kuingia ubia na wawekezaji wazalendo katika maeneo yao. Miradi hii inaweza kuziingizia mapato halmashauri zetu.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Pembejeo. Kwa kuwa wakulima wamelima mazao, kwa nguvu zote na kwa ari lakini pembejeo ni gharama sana matokeo yake wananchi wanapanda mazao bila utaalam wa kutumia mbolea na dawa za wadudu, mazao yamekuwa kidogo. Niishauri Serikali kupunguza gharama ya pembejeo ili wananchi walime kitaalam na kuwa na mavuno yenye tija.

Mheshimiwa Spika, Ukosefu wa Masoko ya Mazao. Pamoja na kwamba wakulima wanajituma kuzalisha mazao hata kwa gharama kubwa lakini mwisho wa yote hakuna soko la mazao. Naishauri Serikali kutafuta masoko kwa mazao ya wakulima wetu. Pia Serikali itoe elimu kwa wananchi juu ya usindikaji wa mazao mbalimbali kama vile mahindi ili kuongeza thamani ya mazao yetu, hii itasaidia kupata masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Tafiti. Kwa kuwa tuna tatizo kubwa la kukosa soko la mahindi, naomba watumike watafiti kutafiti kwenye nchi yetu na kubaini maeneo ambayo yana chakula cha kutosha na yale ambayo hayana chakula cha kutosha, na kisha kupeleka chakula hicho kutoka maeneo ambayo hayana chakula.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umwagiliaji wa Suga uliopo katika Kata ya Suga Wilayani Ulanga umejengwa miaka mingi lakini umeshashindwa kufanya kazi hivyo kuitia Serikali hasara.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Mradi wa Minepa. Mradi huu upo Kata ya Minepa na umeshaanza kazi, lakini gharama

za mradi na ubora wake haviendani kabisa na kuna malalamiko mengi kutoka kwa mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Mradi Mkubwa wa Lupiro. Huu ndio mradi utakaolikomboa eneo la Wilaya ya Malinyi, Ulanga na Kilombero. Tayari tafiti zilishafanyika na thamani ya mradi ni bilioni 52, hivyo tunaomba fedha.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ulinzi wake kwetu sote. Ninaomba sasa na mimi nitoe mawazo yangu katika Wizara hii mumhimu ambayo ndio uti wa mgongo wa taifa. Pamoja na umuhimu mkubwa uliopo ndani ya Wizara hii iliyobeba asilimia zaidi ya 65 ya wananchi wa Tanzania. Bila Wizara hii uhai wetu unakuwa mashakani kwani hii ndiyo Wizara ya chakula. Hivi karibuni imethlibitika kuwa hata mazao tuliyokuwa tunayatambua huko nyuma kama mazao ya chakula kama maharage, mahindi na mpunga sasa yamekuwa sehemu ya mazao ya biashara. Kama ndivyo basi naomba nishauri Wizara yafuatayo;

Mheshimiwa Spika, kuongeza idadi ya Maafisa Ugani ili waweze kuwasaidia wananchi kulima mazao haya muhimu kwa tija. Kutoa elimu juu ya kilimo cha kisasa ya mazao haya muhimu. Kujenga maghala ya kutosha ya kuhifadhiya mazao haya. Njia pekee ya kujihakikishia usalama wa chakula nchini ni kufanya kilimo cha umwagiliaji. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sana huko ndiko ambako Serikali haipeleki fedha za kutosha ambazo zingeweza kutekeleza azma hiyo. Kama hili halitoshi wakulima wamekuwa wakicheleweshewa pembejeo, jambo linalowasababishia hasara kubwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa sisi wote tunahubiri suala la Serikali ya Viwanda. Zaidi ya asilimia 60 ya malighafi ya viwanda hivi tunategemea kutoka mashambani. Ni vyema sasa tuone umuhimu wa kuanzisha vituo vya ushauri na kuondoa changamoto zote zinazowakwaza wakulima wetu ili tuweze kufanikiwa kama taifa kufikia uchumi wa viwanda

ifikapo 2025. Kwa kuwa Wizara hii ndiyo Wizara pekee ya kututoa mahali tulipo ili kufikia malengo ya Serikali ya Viwanda tuliyojiwekea ni dhahiri kuwa bajeti ambayo imekuwa ikitengwa imekuwa ndogo sana kiasi cha kutotosheleza mahitaji makubwa yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii pia ina changamoto kubwa ya upungufu wa watumishi, jambo ambalo limekuwa kikwazo katika utekelezaji wa kazi nyingi katika Wizara hii. Ni rai yangu sasa Serikali ione ni kwa njia gani tunawekeza katika Wizara hii ya Kilimo ili kuweza kufikia malengo tuliyojiwekea ya kuondokana na uhaba wa chakula pamoja na kupata malighafi toshelevu kwa ajili ya viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, nipende kuishauri Serikali yangu kuwekeza katika kilimo cha mazao mkakati kama kahawa, Pareto, tumbaku na kadhalika ili tuendelee kujenga uchumi wetu lakini pia kujipatia fedha za kigeni.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuwepo mahali hapa nami niweze kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo ya Mwaka 2019/2020. Vilevile nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri, hotuba hii inakwenda kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuhakikisha sekta nzima ya kilimo inaendelea kuimarika kama ilivyoainishwa hasa ukizingatia nchi yetu ina uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuanza kwa kutoa pongozi zangu kubwa kwa Serikali, hakika Serikali imeendelea kuweka jitihada za kutosha katika sekta nzima ya kilimo. Hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa 2017/2018 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2018/2019 imeendelea kuimarika kutokana na hali nzuri ya mvua katika maeneo mengi ya nchi, kuongezeka kwa tija na uzalishaji. Uzalishaji wa mazao ya chakula umefikia tani milioni 16.89 ikilinganishwa na mahitaji ya chakula ya tani milioni 13.57. Hivyo nchi ina ziada ya chakula ya tani milioni 3.32 za

mazao yote. Hii ni hatua nzuri na ya kujivunia kwa usalama wa chakula ni usalama wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingine kwa Serikali ni Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (*ASDP II*). Tarehe 4 Juni, 2018 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (*ASDP II*). Programu hiyo inalenga kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo; kwa maana ya mazao, mifugo na uvuvi; ili kuongeza uzalishaji na tija, kufanya kilimo kiwe cha kibiashara na kuongeza pato la wakulima, hususan wakulima wadogo kwa ajili ya kuboresha maisha na usalama wa chakula na lishe, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa *ASDP II*.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeimarisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*TADB*) ili kuwa benki mama itakayoongoza mipango inayolenga kutatua changamoto ya ukosefu wa mitaji kwa wakulima, wafugaji na wavuvi nchini. Lengo la Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ni kuifanya *TADB* kuwa benki ya mfano na ya kisasa katika kuleta mapinduzi ya kilimo nchini kutoka katika kilimo cha mazoea cha kujikimu kwenda katika kilimo cha kibiashara na uzalishaji wenye tija katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kujivunia sana, hadi kufikia Februari, 2019 *TADB* imetoa mikopo ya shilingi bilioni 100.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 10 mwaka 2017. Mikopo hiyo imewanufaisha zaidi ya wakulima na wafugaji milioni moja nchi nzima. Aidha, *TADB* tayari imeshafungua ofisi mbili za kanda Jijini Dodoma na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa menejimenti na Bodi ya *TADB*ni kukamilisha ufunguzi wa ofisi zilizopangwa kwa wakati ili kutatua changamoto za upatikanaji wa pembejeo na miundombinu duni ya uzalishaji, usafirishaji, uchakataji wa mazao na masoko zinazokabili wakulima wadogo nchini; kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyotangulia kuzungumza katika hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao makuu ya biashara ya kimkakati yakiwemo chai, kahawa, korosho, pamba na tumbaku umeimarika kutokana na juhudzi zinazofanywa na Serikali ikiwemo kuimarisha ushirika. Kwa mfano, uzalishaji wa zao la pamba uliongezeka kutoka tani 132,934 mwaka 2017/2018 hadi kufikia tani 222,039 mwaka 2018/2019, wakati uzalishaji wa zao la kahawa uliongezeka kutoka tani 45,245 hadi kufikia tani 65,000.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa mazao hayo na mengine kwa kuwa ndiyo mhimili wa kutoa malighafi za kuendesha viwanda na yana myororo mpana wenye fursa ya kutoa ajira nyingi na kuliingizia taifa fedha za kigeni. Mfano, katika mkakati wa uzalishaji wa zao la chikichi Serikali kwa kweli imekuwa ikitumia fedha nyingi za kigeni kwa ajili ya kununua mafuta ya kula kutoka nje ya nchi. Aidha, uzalishaji mdogo wa zao la chikichi ni mionganini mwa sababu za kushindwa kujitosheleza kwa mahitaji ya mafuta ya kula nchini. Kutokana na changamoto hiyo Serikali imeamua kuweka nguvu kubwa kwenye uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta ili kuondokana na utegemezi na kuokoa matumizi ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, sina budi kuendelea kuishukuru Serikali kwa kuchukua hatua mbalimbali za kutatua changamoto za wakulima jimboni kwangu. Hata hivyo bado kuna baadhi ya maeneo kumeendelea kuwepo changamoto za migogoro ya wakulima na wafugaji. Migogoro hiyo baadhi yake imekuwa ikilalamikiwa na wakulima kwa baadhi ya maamuzi yanayochukuliwa na kuonekana kesi nyingi zikiwapendelea wafugaji.

Naiomba Wizara kuchukua hatua madhubuti hasa katika kipindi hiki kwa kuangalia namna gani itaweza kutatua migogoro hiyo kwa kuhakiki mipaka ili maeneo ya wakulima na wafugaji yajulikane. Kufanya hivyo kutasaidia kumaliza tatizo kubwa lilitopo jimboni kwangu la migogoro hii. Aidha, kuna madai ya muda ya wakulima wa zao la korosho wa Soga, Kikongo na kadhalika. Wakulima hawawana madai yao kwa Serikali, ni fedha za malipo kwa ajili ya zao la

korosho. Sasa namuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akihitimisha hotuba yake anipe majibu ya changamoto hizi ili wananchi wangu wapate kujua hatma ya maswali wanayojilizila.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika kuna tatizo katika mradi wa Shamba la Umwagiliaji la Mongomole, Kwala. Mradi huu umetumia fedha nyingi na inasemekana kuna ubadhirifu mkubwa umefanyika. Nakuomba Mheshimiwa Waziri atupe majibu juu ya mradi huu na tuhuma hizi. Je, Serikali inatambua hilo na hatua gani za haraka itakwenda kuzichukua, kwani mradi huu umetumia fedha nyingi na umekuwa hauna tija kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, dakika tano. Atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**NAIBU WAZIRI ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami nichangie hoja hii ambayo iko mezani ya Wizara ya Kilimo, na nianze kwa kuunga mkono. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa na machache ambayo yanakwenda kusaidia katika hatua ambayo Serikali inajaribu kuchukua katika kuhakikisha kwamba katika uboreshaji wa kilimo na namna ambavyo tunawezesha Wakulima wetu kuweza kupata ardhi ya kutosha na kuweza kuzalisha kama ambavyo wengi wanassema kilimo kinachukua karibu zaidi asilimia 65 kwa maana ya wanaohusika na kilimo hicho.

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwa kusema kwamba nia na dhamira njema ya Serikali katika kuhakikisha kwamba tunakipa kipaumbele kilimo, tumeanza na ile hatua ya kuanza kunyang'anya yale mashamba ambayo yametelekezwa ili baadaye yaweze kupangiwa matumizi mazuri katika kilimo kama ambavyo Serikali imekusudia.

Mheshimiwa Spika, tuna mashamba zaidi ya 45 ambayo yamebatilishwa na mashamba haya ambayo tayari yamebatilishwa baadhi yake yameshapangiwa pia shughuli hiyo tukianza na shamba namba 217/1-6 la Mkulazi ambalo limetengwa kwa ajili ya kilimo cha miwa. Pia tunalo shamba lingine la Makurunge Bagamoyo namba 3561/1 nalo limetengwa kwa ajili ya kilimo cha miwa.

Mheshimiwa Spika, pia hatukuwaacha nyuma wananchi wetu ambao nao pia wamekuwa na tatizo kubwa katika suala zima la ardhi. Wote ni mashahidi kwamba katika Mkoa wa Morogoro nadhani unaongoza katika migogoro ya ardhi ambayo sehemu kubwa ni masuala ya maeneo ya kilimo. Kule nako katika yale mashamba yaliyofutwa tumefuta shamba namba 32, 33, 34, 35, mpaka 36, yaliyoko Mvumi pamoja na mashamba namba 4, 5, 8 na 10 yaliyoko Msowelo lakini, mashamba haya yamerejeshwa kwa wananchi ili waendelee na kilimo kwa sababu lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba tunazalisha kwa wingi. Tunapozungumzia Tanzania ya Viwanda pia tuweze kupata malighafi itakayokwenda katika viwanda hivyo. Haya yanafanyika ili kuweza kuona ni jinsi gani tunaweza tukapeleka nguvu zaidi katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi maelekezo ya Serikali pia yalishatoka kwenda katika Halmashauri zetu zote, waliombwa kutenga maeneo kwa ajili ya kilimo na hasa kwa ajili ya vijana ambayo yangeweza kutumika kwa kilimo na masuala mengine, lakini mpaka dakika hii ninapoongea ni Halmashauri chache ambazo zimeweza kuzingatia hilo. Hili lingeweza kusaidia zaidi katika kuwawezesha vijana, lakini pia kuwaweka katika maeneo hayo wangeweza kulima kilimo chenye tija. Kwa sababu wengi tunaotegemea mbali na *graduates* ambao wanamaliza, lakini pia hata wale walioko katika maeneo yetu ya Halmashauri, wengi wamekuwa wakiwezesha na Wizara husika, Wizara ya Kazi, ambayo imekuwa pia ikisaidia katika kuhakikisha kwamba vijana wengi wanapewa elimu kwa ajili ya kilimo, kwa ajili ya ufugaji na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, niziombe pia Halmashauri zetu, zizingatie maelekezo ya Serikali yanapotolewa, kwa sababu lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunainua kilimo. Kilimo kina mambo mengi ndani yake, kama hujawatambua wakulima wako kama ambavyo mtoa hoja amesema, utashindwa pia kujua wanahitaji pembejeo kiasi gani, utashindwa kujua mkwamo wao uko wapi, lakini utashindwa kujua pia, *scale* ya kilimo ambacho wao wanafanya, wanafanya kilimo cha biashara, wanafanya kilimo cha chakula au wanafanya kilimo gani. Ukipishawatambua maana yake ni kwamba pia utakuwa unawatolea huduma kwa hao Maafisa Ugani tunaowazungumza, tunaweza kujua Afisa Ugani mmoja anahudumia wakulima wangapi? Sasa kama usipojua idadi ya wakulima, *obvious* hata kujua idadi ya Maafisa Ugani wanaotakiwa inaweza ikawa ngumu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kikubwa hoja ya Serikali ya kuanza kuwasajili wakulima inasaidia pia katika kuwatambua na kujua mahitaji yao ya ardhi ni kiasi, lakini pia katika suala zima la kuona kwamba tunaongeza ardhi ya kilimo, tunao wawekezaji ambao tunasema ni wawekezaji kama ambao wameshindwa, ambao wametelekeza mashamba yao, wako zaidi ya mia moja, lakini wengi wao pia wamekopea mashamba hayo. Wamekopea mashamba lakini wameenda kuendeleza maeneo mengine.

Sasa Serikali pia inapitia hawa wote kuweza kujua ni wangapi na wako wapi ili tuweze kuwanyang'anya yale mashamba yaweze kufanya kazi ile iliyokusudiwa halafu wao watafute dhamana nytingine ya kuweza kuweka katika mikopo yao.

Mheshimiwa Spika, hayo yote yanafanyika katika dhamira njema ya kuhakikisha kwamba Sekta hii ya Kilimo inaimarishwa na inakuwa pia ni chachu katika mwelekeo wa Serikali wa Tanzania ya Viwanda ili tuweze kuwa na maeneo ya uzalishaji yalio mengi na yanayozalisha kwa tija.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Angeline Mabula. Sasa ni Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji dakika tano pia, Mheshimiwa Kakunda.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe pole kwa Wanzazibari kwa kufiwa, kwa kuondokewa na Viongozi wawili muhimu, Mheshimiwa Ally Juma Shemuhuna, na Mheshimiwa Ally Fereji Tamimu, Mwenyezi Mungu awaweke mahali pema.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri kwa hotuba nzuri na nizungumze machache tu katika hii Sekta ya Kilimo kwamba ukiacha malighafi ya mazao ambayo wenyе viwanda pia wana mashamba kama viwanda vya sukari ambavyo kuna mashamba ya miwa, viwanda vya chai na mashamba makubwa ya mpunga ambayo yana viwanda vyake kama yale ya Kapunga kule Mbarali na viwanda vya maparachichi, tumekuwa tunapata matatizo makubwa kwenye mnyororo wa thamani kwenye viwanda vya mazao ambayo hayana mashamba kama korosho, viwanda vya nguo, viwanda vya kukamua mafuta, alizeti, pamba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nizungumze machache tu katika hii sekta ya kilimo, kwamba ukiacha malighafi ya mazao ambayo wenyе viwanda pia wana mashamba kama viwanda vya sukari ambavyo kuna mashamba ya miwa, viwanda vya chai, na mashamba makubwa ya mpunga ambayo yana viwanda vyake kama yale ya Kapunga kule Mbarali na viwanda vya maparachichi.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunapata matatizo makubwa kwenye mnyororo wa thamani kwenye viwanda vya mazao ambayo hayana mashamba kama korosh, viwanda vya nguo, viwanda vya kukamua mafuta, alizeti, pamba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni kweli nikiri kwamba tunahitaji uchambuzi wa kina ambao utafanywa na Serikali

kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine ili hatimaye tuweke mfumo wa uhakika wa kuhakikisha kwamba viwanda vyetu hivi, hasa ambavyo havina mashamba vinakuwa na uhakika wa kupata malighafi; na hiyo ndiyo itatupatia *sustainability* ya viwanda vyetu ambavyo vimekuwa vinaathiriwa sana.

Mheshimiwa Spika, ushindani wa bei kwenye soko umekuwa mkubwa kiasi ambacho viwanda vyetu vimekuwa vikipata shida kushindana bei na makampuni mengine ambayo yamekuwa yanatoa bei kubwa sana kwenye soko na matokeo yake viwanda vimekuwa vinakosa malighafi na hivyo kufa. Ukiangalia katika kipindi cha miaka mitano hadi 10 iliyopita viwanda vingi vya korosho vimekufa kwa sababu ya ushindani wa bei kwenye soko na hivyo kukosa maghafi.

Mheshimiwa Spika, kama nchi suala la kuendelea kuza malighafi yetu kwenye nchi nyingine ni sawa na kuendeleza viwanda, ajira na faida kwenye nchi nyingine, kwa sababu bidhaa hizo a mbazo huzalishwa viwandani baadaye zitarudishwa tena kwenye nchi yetu na kuuzwa na kunuliwa na Mtanzania kwa bei ya juu zaidi. Endapo tutaeendelea mtindo huo hatutajikomboa kiuchumi. Watu wetu wataeendelea kukosa ajira na hata faida za kiuchumi zitakuwa kidogo. Kwa hiyo Serikali inalichukulia suala hili kwa uzito mkubwa ili kuanzia mwaka ujao tuwe na mfumo mzuri utakaohakikisha viwanda vyetu vinapata malighafi ya kutosha kwa mwaka mzima na hivyo kulinda ajira na faida zaidi kwa Watanzania na wakati huo huo wakulima waendelee kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la mapendekezo hapa. Wenzetu wamekuwa wanazungumzia mashtaka kwa wahujumu uchumi. Mimi niseme tu kwamba suala hilo ni suala la kisheria na sheria zina utaratibu wake ikiwemo kuwa na ushahidi wa kutosha kukamilisha taarifa za uendeshaji wa mashtaka. Sasa wakati tunamuachia Mwanasheria Mkuu wa Serikali mambo kama hayo tunatambua jambo moja la muhimu kwenye sekta ya korosho; kwamba kabla Mheshimiwa Rais hajachukua uamuzi

wa Serikali kumkomboa mkulima kwa kumlipa shilingi 3,300 kwa kila kilo hakuna kampuni ya ununuzi hata moja ilikuwa imefikia *offerya* bei hiyo ambayo Mheshimiwa Rais aliamua kuitoa kwa ajili ya kumkomboa mkulima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini ajabu ni kwamba mara baada ya Serikali kuanza kuwalipa wakulima shilingi 3,300 kila kilo baadhi ya makampuni yalijitokeza kusema kwamba sasa tupo tayari kulipa hiyo bei ya 3,300 au zaidi. Kwa hiyo hapo kama uchunguzi utaelekeea kwenye mambo kama hayo mimi nadhani hapo tutaunga mkono wala hakutakuwa na shaka. Kwa hiyo kama tutachunguza kwa mwelekeo huo, si vibaya.

Mheshimiwa Spika, lakini si afya sana kuwekeza kwenye uchunguzi wa aina hiyo badala ya kuwekeza kwenye ufumbuzi wa kudumu wa matatizo yetu, hususan kuhakikisha viwanda vinapata malighafi na pia wakulima wanapata bei nzuri; kwa maana ya kuweka vizuri mfumo wa masoko ya mlighafi na mfumo wa masoko ya bidhaa za viwandani ili twende vizuri kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu *Indo Power...*

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, dakika zimeisha.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, dakika moja tu. *Indo Power* ni kampuni halali ambayo imesajiliwa kwenye orodha ya makampuni ya Kenya, na hii ilithibitishwa na Balozi wa Tanzania nchini Kenya na Balozi wa Kenya nchini Tanzania kwa barua rasmi ambazo zipo. Kwa hiyo kampuni hii inafanya kazi kihalali. Sasa kushindwa kuelewana na benki yake kwa ajili ya kutoa fedha za kununua korosho isitangazwe kwamba hiyo ni kampuni ya kitapeli. Ninataka kuthibitisha Bungeni hapa kwamba kampuni hiyo mpaka jana imeendelea kufanya biashara nchini Kenya, Afrika Mashariki na Dunia nzima. Kwa hiyo tumeachana na

mkataba huo tunaendelea na kampuni nyingine, korosho zitauzwa na tutatangaza hapa Bungeni kabla Bunge halijaisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana tunakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, dakika tano pia.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Nalbu Mawaziri wake wawili kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha kilimo chetu kinanyanya.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme mambo mawili makubwa, na jambo la kwanza ni ambalo limesemwa kwa kiwango kikubwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, lile la kufikia asilimia 10 ya bajeti yetu kupelekwa kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inatambua sana umuhimu wa sekta ya kilimo katika kufikia dhima ya mpango wetu wa pili wa maendeleo wa miaka mitano. Hakuna viwanda bila kuwa na malighafi na hakuna malighafi bila kuwa na kilimo.

Mheshimiwa Spika, nimeanza kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, mchango wa kilimo chetu, kwenye uchumi wetu wa taifa unaonekana sasa na unaendelea kukua; mwaka huu *ime-register* ukuaji mzuri tu na mimi nawapongeza sana. Hiyo yote imetokana na Serikali kuwekeza katika kilimo chetu. Ndiyo maana pamoja na mambo mengi ambayo Serikali inayo ya kufanya, kwa mfano tunaangalia uhalisia wa mapato yetu kwa mwaka husika ukilinganisha na mahitaji ya lazima yanayohitajika ili mambo

mbalimbali yaweze kutendeka. Kwa mfano ulipaji wa Deni letu la Taifa ambalo lilitumika kwa kiwango kikubwa kwa ajili ya miradi yetu ya maendeleo. Vilevile tunatakiwa kuhakikisha watumishi wetu wanalipwa mishahara yao kwa wakati, jambo ambalo Serikali yetu inatenda sasa tangu imeingia madarakani.

Mheshimiwa Spika, pia Waheshimiwa Wabunge tuisahau kwamba tunavyowekeza kwenye kilimo siyo ile pesa inayokwenda moja kwa moja kwenye Wizara ya Kilimo. Tunaweza tukapeleka pesa nyingi kwenye kilimo lakini kama hatuna miundombinu hatutaweza kuleta athari chanya kwenye kilimo chetu, na ndiyo maana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli tangu akiwa Waziri wa Ujenzi aliimarisha sana miundombinu. Mikoa yetu yote imeunganishwa na sasa tunaenda kukamilisha Mkoa wetu wa Kigoma kuunganisha na mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunataka kuhakikisha tumbaku inayozalishwa Tabora, pamba inayozalishwa Mwanza inasafirishwa kwa siku moja kufika Dar es Salaam. Hata kama ni viwanda vyetu vya nguo vinavyoenda kuanzishwa kule Bariadi – Simiyu, tunataka kuhakikisha nguo zile zinafika ndani ya siku moja Dar es Salaam. Tunaenda kuwekeza kwenye *SGR* ili kuhakikisha kilimo chetu kinaleta tija kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, tunaposema Tanzania ya Viwanda, nimesema huwezi kuwa na viwanda bila kuwa na malighafi. Moja ya malighafi ni umeme wa bei nafuu ambaou upo unapatikana kwa wakati wowote, ndicho Serikali ya Awamu ya Tano inafanya, kuhakikisha kilimo chetu kinaleta tija katika mnyororo mzima wa thamani wa mazao yetu ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo hayo, hatujaisahau Wizara ya Kilimo na bajeti nzima ya maendeleo, ndiyo maana mwaka huu tukiangalia kitabu hiki cha bajeti ya kilimo kwenye bajeti ya maendeleo tumeongeza bajeti ya maendeleo kwa asilimia 46. Hii ni kwa sababu tunajali na

tunathamini kilimo chetu kwenye mnyororo mzima kuanzia uzalishaji mpaka kwenye mazao yake ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulisemea mchana wa leo ni kuhusu *VAT refund*. *VAT refund* sote tunafahamu kwamba Taifa letu liliumizwa kwa kiwnago kikubwa, tunaendelea kulipa madeni haya ya *VAT refund*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Malizia Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naomba niseme tu kwamba tayari deni la bilioni 20.8 limeshahakikiwa na linalipwa ndani ya mwezi huu na billoni 28.8 nalo pia tunamalizia uhakiki wake tunaenda kuwalipa Watanzania na ambao wanatudai ndani ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba nirejee kusema naunga mkono hoja na nashukuru sana kwa nafasi hii. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Dkt. Ashatu Kijaji. Sasa naanza kuingia Wizarani, naomba tuanze na Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Omary Mgumba, nakupa robo saa, dakika 15.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)**  
Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya na uzima tumeipata nafasi hii ya kuchangia katika sekta hii muhimu kwa Watanzania, sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, pia natoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu na nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli, kwa kuniamini na

kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Kilimo katika kumsaidia katika majukumu kwenye sekta hii ya kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, natoa pia shukrani za pekee kwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Japhet Hasunga (Mb) kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Vile vile ninamshukuru Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Naibu Waziri mwenzangu kwa ushirikiano mmkubwa anaonipa katika kuwatumikia Watanzania; tunafanya kazi hii kwa pamoja kama timu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao. Aidha, nawashukuru wapiga kura wangu kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano wa kutosha pale ambapo ninapokuwa katika Bunge hilli na sehemu zingine kuwawakilisha. Nipo hapa kwa sababu yao, niko hapa ndiyo sauti yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia nachukua nafasi hii kukishukuru chama changu Chama Cha Mapinduzi kwa ushirikiano mkubwa kinachonipa katika kutekeleza majukumu haya hasahasa kusimamia llani ya Chama Cha Mapinduzi kwenye Sekta hiyo ya Kilimo. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wa Wizara ya Kilimo na taasisi zilizokuwa chini ya Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya na ushirikiano wanaonipa katika kutimiza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, ninaomba sasa nichangie hotuba yangu ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa kutoa maelezo na ufanuzi wa hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika sehemu kuu mbili ambazo ni umwagiliaji na zao la kahawa na kama nitapata muda nitaenda kwenye miwa pia na mbegu za mafuta kwenye mafuta ya kula.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza na hoja hizo mbili, sisi kama Serikali niishukuru sana michango ya Wabunge. Wengi wamezungumzia kuhusu bajeti kwamba bajeti ya

sekta ya kilimo ni ndogo. Pamoja na ukweli huo wengi wana-refer azimio la Malabo na lile la Maputo. Ni kweli lakini tuna maazimio mengi ambayo tumeingia kama nchi. Tutoe mfano tu, afya tunatakiwa tutenge asilimia 15, elimu asilimia 20, kilimo asilimia 10, tuna asilimia 45 kwa mambo matatu tu; lakini ukiangalia vipaumbele tulivyokuwa navyo viko vingi. Kwa hiyo hii bajeti kwa mazingira tuliyonayo na hasa uchumi wetu ni vizuri kwamba tukazingatia badala ya kujielekeza kwenye maazimio ambayo hayaendani na hali halisi ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, pia bajeti hii ya sekta ya kilimo tunaitekeleza kwa kupitia mpango wetu wa *ASDP II*. Kama tulivyoeleza bajeti hii kwenye *ASDP II* asilimia 40 ndiyo Serikali na asilimia 60 itatekelezwa na sekta binafsi. Kwa hiyo sekta binafsi nayo ina mchango mkubwa sana katika kuendeleza kilimo katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni kipana, ni kilimo mazao, kilimo mifugo, kilimo mifugo, kilimo uvuvi, na kilimo misitu, Kwa hiyo bajeti yake huwezi kuiona tu kwenye Wizara hii moja ya Kilimo, utaiona kwenye Wizara zote hizo zingine pamoja na Wizara zile za Kisekta. Kama mnavyokumbuka bajeti hii ni mwendelezo wa mipango wa Serikali tangu mpango ule wa mwanzo.

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana kama Serikali, mpango wa mwanza ulikuwa kwanza kuondoa vikwazo vyakimaendeleo na ndiyo maana sasa hivi bado Serikali tunaendelea kuondoa vikwazo vyakimaendeleo ili kumkwamua mkulima; ndiyo maana tunaboresha hiyo miundombinu ya barabara, reli, pamoja na ndege, yote ni ili kuwezesha mazao ya wakulima ili yaweze kufika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Hoja Mahsusni Kuhusu Mambo ya Umwagiliaji. Kulikuwa na hoja kutoka kwenye Kamati yetu ya Kilimo lakini pia Kambi Rasmi ya upinzani na pia katika michango ya Wabunge mbalimbali. Ni kweli eneo la umwagiliaji kama nchi bado ni dogo sana ambalo eneo linalofaa kwa umwagiliai tuna hekta zaidi ya milioni 29 lakini mpaka sasa tumeendeleza hekta 475,000.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga ndani ya miaka 10 tuweze kuongeza eneo la uzalishaji kutoka hekta 475,000 mpaka hekta 1,000,000. Kama nilivyosema awali hiyo sisi kama Serikali pamoja na kushirikiana na Sekta Binafsi pia na Serikali za Halmashauri na kupitia Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo na Benki nyingine kwa sababu tukisema kwamba tunategemea hela za kibajeti, maeneo haya ya umwagiliaji yote hatutaweza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo na Benki nyingine za kibiashara kama *CRDB*, *NMB*, *Azania*, Benki ya Posta na zingine zote, hizi sasa tunesema kwamba kwa sababu tunaenda kwenye kilimo cha biashara, zinakwenda kwa maelekezo ya Serikali na mipango hiyo kwamba Serikali tunakwenda kudhamini asilimia 50 ya fedha zote zilizotolewa na benki hizi za biashara ili kwenda kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji katika nchi hii badala ya miradi yote ya umwagiliaji kusubiri pesa za kibajeti kwa udhamini wa Serikali kwa kushirikiana na Serikali za Halmashauri za Wilaya pamoja na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ambao wao watahusika kwa ajili ya kutoa utaalam kwa ajili ya ramani na kusimamia ujenzi ili halmashauri hizi na miradi hii tuweze kuchukua mikopo ya masharti nafuu kuiendeleza miradi hiyo ili tuwe na kilimo cha uhakika cha umwagiliaji katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutakuwa kweli na miradi itategemea fedha za kibajeti lakini pia tutakuwa na miradi ya kibiashara ambayo itapata fedha kutoka kwenye taasisi zetu hizi za fedha kwenye benki hizo ambazo nimeziainisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na mkopo huu utalipwa ndani ya miaka mitano mpaka miaka 15; na mingine iwe ni fursa kwa wafanyabiashara wakubwa kuchukua ardhi kwenda kuwekeza miundombinu ya umwagiliaji, baadaye tutaweza kuwakodisha kwa wakulima na wanufaika wengine utawezwa kulipa tarayibu mpaka pale ambapo pesa itakaporudi. Mpango huu tunauweka katika ile mpango wetu wa

kwamba jenga, endesha, baadaye unakabidhi baada ya malipo ya ujenzi ule kurudi.

Mheshimiwa Spika, la pili kwenye umwagiliaji, tumeona baada ya Wizara hii kuja kwetu cha kwanza ambacho kama Serikali tulichokifanya kwa pamoja ni kuiielekeza mhasibu (*CAG*) kufanya ukaguzi maalum kwenye miradi yote ya umwagiliaji nchini.

Mheshimiwa Spika, na nikiri, baada ya taarifa hiyo ambayo tulishai-*table* hapa kwenye Bunge lako Tukufu, tutajadili vikao vijavyo baada ya Bunge la Bajeti ambapo tumeona madhaifu mengi sana katika miradi hii; na ndio maana sehemu nyingine miradi kwamba imemalizika, maji haitoi au miradi imejengwa chini ya kiwango. Yote hayo sisi kama Serikali tumeyapokea na tumeshaanza kuyafanyia kazi hata kabla hatujaanza mjadala hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza, tumeunda timu maalum ya kiuchunguzi kwenda kuyathibitisha yale ambayo aliyoyagundua *CAG* kwa mujibu wa sheria ili sasa wale wote ambao waliotufikisha hapo kwanza tuwachukulie hatua lakini kubwa zaidi ni kujifunza wapi tulifanya vibaya ili kuja na mikakati ya kuweza ku-*address* tatizo liliokuwepo na kwenda kuwa na kilimo cha uhakika cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, pia, katika suala la umwagiliaji sasa tunataka kufanya mapitio ya kimuundo. Badala ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kuwa tu kwenye kanda, sasa tunataka tuishushe mpaka kwenye ngazi ya kata, vijiji mpaa ngazi ya halmashauri. Kwa hiyo tutakuwa na wataalam Makao Makuu kwenye Tume ya Taifa ya Umwagiliaji lakini pia tutakuwa na wataalam wa umwagiliaji kwenye kanda, tutakuwa na wataalam wawili kwenye mkoa na baadaye tutakuwa na wataalam wengine kwenye wilaya. Baadaye tutawajumuisha pamoja na wale wa halmashauri ili miradi hii isimamiwe maalum. Kila mradi ambao utasimamiwa, utakuwa na Meneja maalum au Mhandisi maalum wa kuusimamia mradi huo, badala ya sasa miradi mingi ilikuwa inasimamiwa na *Engineers* wa Kanda ambao wanaishi

Makao Makuu Dar es Salaam, kitu ambacho kimechangia miradi mingi kujengwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na hoja za Wabunge mbalimbali, ambao wamezitoa. Kwa mfano, Mheshimiwa Deo Ngalawa, alikuwa anazungumzia mkakati wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji badala ya kutegemea mvua. Ni kweli, hoja yake ni ya msingi, lakini katika kilimo hiki cha umwagiliaji kama nilivyosema katika maelezo yangu, kwa sababu kilimo tunategemea mvua, tunategemea maji ya ardhini kwa kuchimba visima, lakini pia kwa ajili ya kuvuna maji kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa. Sisi kama Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili kuwawezesha wakulima hawa wadogowadogo, mpaka sasa tuliagiza mitambo ya kuchimba na kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji na mitambo hiyo imeshafika na imeshafika hapa Dodoma. Lengo kwa wale wandarasi wa ndani wadogo wanaopewa, ambao uwezo wao wa vifaa ni mdogo, watakodisha kwa bei nafuu mitambo hii ili kurahisisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile kulikuwa na Mheshimiwa Neema Mgaya, alikuwa anasema kwamba Serikali iwekeze kwenye malambo, mabwawa ili kuongeza uzalishaji. Kama nilivyosema katika maelezo yangu kupitia mapitio ya mpangi kabambe, ambao tayari tulishauhaulisha, mpango wa umwagiliaji, yote lengo ni kwenda kujibu hoja za wananchi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, ni suala la kahawa, ni kweli, kwenye suala la kahawa, kama walivyosema Wabunge wengi na Kamati yetu ya Kilimo, walikuwa wanataka kujua mkakati wa Serikali wa kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa soko la kahawa. Kwanza, tulichofanya katika msimu huu unaokuja, cha kwanza tumeyatambua makampuni yote ya ndani ambayo yananunua kahawa zetu kwa ajili ya kuwapa vibali Vyama vyote vya Ushirika na wakulima na makampuni yanayonunua hapa kahawa, kuuza moja kwa moja bila kupitia mnadani. Hilo limeonesha mafanikio makubwa zaidi, kahawa zaidi ya asilimia 80 tunavyoongea, tayari zilishakuwa kwenye makubaliano ya kuweza kuuzwa moja kwa moja kwa

wale wanunuzi wa kahawa wa uhakika ambao wanakwenda kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, la pili, tuliona kwamba ni busara, kwa sababu kahawa ni zao la muda mrefu, tunawahimiza wakulima wetu walime kahawa, lakini hii fursa inaangaliwa na nchi mbalimbali duniani. Wanavyoona bei ya kahawa inavyopanda au bei ya mazao mengine, nao wanaangalia. Cha pili, tumeona kwamba ni vizuri kuingia makubaliano maalum na nchi zile za walaji katika nchi mbalimbali ili tuwe na soko la uhakika. Kahawa hii tunawahimiza wakulima walie, tunakwenda kuiuza kwa nani, kwa bei gani na kipindi gani ili tupate mikataba ya muda mrefu kati ya miaka mitano mpaka 20 ili tusije kuzalisha kahawa kwa wingi, baadaye inafika kule muda unakuwa umekwisha. (*Makofii*)

Watu wengi hapa walikuwa wanajiliza kwa nini Kenya ni kubwa na Uganda...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu...

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):**  
Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie dakika moja tu.

**SPIKA:** Ahsante, malizia dakika moja.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):**  
...wanasema kwa nini Kenya bei ni kubwa na Uganda, sababu ni hiyo, wenzetu walishakuwa na *bilateral*/sisi tulikuwa bado, ndiyo maana kwamba wenzetu walikuwa wanapata mikataba mizuri kabla ya sisi na sisi sasa tumeamua tunafanya hivyo ili kuboresha bei ya mazao yetu nchi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Omary Mgumba. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Bashungwa, tutakupa robo saa pia.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja ya Waziri wangu wa Kilimo. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya njema nikaweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja hii. Pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Rais wa Watanzania, kwa kunteua, kuniamini na namhakikishia kwamba nitaendelea kumsaidia kwa kushirikiana na Mheshimiwa Waziri wangu na Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu katika kutimiza majukumu ambayo Mheshimiwa Waziri wetu Japhet Hasunga, anatuongoza katika kuyatimiza. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, namwombea kwa Mwenyezi Mungu amjalie afya njema ili azidi kusukuma gurudumu la Watanzania la maendeleo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Japhet Hasunga kwa hotuba nzuri iliyosheheni mikakati ambayo tunakuahidi pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba tutaisimamia katika kuhakikisha inatimiza yale malengo ambayo tumewaaahidi. Vile vile nitumie nafasi hii tumshukuru sana Naibu Waziri mwenzangu, pacha wangu, Mheshimiwa Omary Mgumba, kwa ushirikiano anaonipa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya katika kutimiza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuishukuru sana familia yangu, mke wangu Jennifa Bash, *a.k.a* mama Araska, pamoja na watoto wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nishukuru sana vilevile michango ya Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji, tunashukuru sana kwa michango yenu mizuri, ushauri na kwa namna ambavyo wanaendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara yetu na tunaahidi tutazidi kuwapa ushirikiano kwani Kamati ni *extension* ya Bunge na Kamati ndiyo *think tank* inayoshauri Wizara. Kwa

hiyo, tunawashukuruni sana kwa michango na ushauri wenu.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwashukuru sana Kambi Rasmi ya Upinzani, tumesikia ushauri na maoni yao na naamini watatuunga mkono katika kupitisha hii hoja ili tuweze kwenda kufanya kazi ule ushauri ambao wameipatia Serikali. Vile vile nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Wabunge wote ambao wamechangia hoja yetu ya Wizara, Waheshimiwa Mawaziri, tunawashukuru sana kwa michango na ushauri wetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho katika shukurani, nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Karagwe kwa namna wanavyoendelea kuniamini na kunipa ushirikiano nami naendelea kuwaahidi kwamba sitawaangusha katika jukumu langu la kuwakilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, sasa niende kuchangia kwenye maeneo ambayo yalikuwa *cross cutting* na nianze na suala la bei za mazao. Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia mazao mbalimbali lakini kwenye suala la bei kuwa chini. Nipende kuwakumbusha tu kwamba suala la bei tunaangalia matokeo, lakini pia lazima tuangalie mchakato unaotupeleka kwenye bei, ni mchakato gani ambao tunatakiwa kushirikiana kuufanya kazi, ili bei za mazao ya wakulima wetu ziweze kupanda.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia suala la bei, ni suala la *factors* kadhaa, kuna suala la kodi na tozo, Serikali sikivu ya Awamu ya Tano, katika Bunge hili la Kumi na Moja tayari tumeshatoa tozo na kodi kero nyangi katika mazao. Kwa vile kodi na tozo siyo *factor* peke yake ambayo inasaidia bei kupanda, Serikali tunaendelea kufanya jitihada kuhakikisha, kupita ushirika, tunazingatia kanuni za ubora wa mazao, tunawapa elimu wakulima ili kupitia ushirika tuweze kusimamia suala la ubora kwa sababu bei, ukiondoa kodi kero na tozo, lakini suala la ubora ni suala muhimu sana katika kuhakikisha mazao yetu yanapata bei nzuri na namna pekee ya kusimamia suala la ubora ni kupitia ushirika.

Mheshimiwa Spika, kuna takwimu zinaonesha kwamba hata kwenye upande wa pamba, upande wa kahawa, upande wa chai, ushirika ume-*prove* kwamba ndiyo namna bora ambayo tunaweza tukasaidia kuwaelimisha wakulima wetu wazingatie ubora ili mazao haya tunapoyapeleka kwenye masoko, suala la ubora au *quality* liweze kuwa zuri na kuweza ku-*attract* bei ya mazao yetu. Kwa hiyo, ushirika katika *models* ambazo zipo za kusaidia wakulima wadogowadogo katika *peasant setting*, ushirika ndiyo ume-*prove* kuwa mfumo mzuri ambao tunaweza tukautumia kuwasaidia wakulima wakazingatia suala la ubora.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge *concern* yao kubwa ni kukosa uadilifu na utawala bora katika mfumo wa ushirika na sisi Wizara tuwahakikishie, hili ni jukumu ambalo wametupa, tutaendelea kufanya kila liwezekanalo kuhakikisha tunapata viongozi wazuri katia *AMCOS* zetu, tunapata viongozi katika *Unions* zetu ili viongozi hawa tuweze kuwasimamia na kupita huu mfumo wa ushirika, tuweze kuzingatia ubora wa mazao ili mazao haya yanapokwenda sokoni yaweze kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, katika bei pia kuna suala la *supply and demand*, yaani unapopeleka zao sokoni, inategemeana na wingi wa mazao uliyokuta katika soko ukoje. Hilo suala liko nje ya mkakati kwa sababu ni *exogenous factor* lakini tunaendelea kujitahidi kupitia kuzingatia ubora na katika ushirika, tunataka kuhakikisha tunasheheni mambo mengi, si tu katika kuzingatia ubora, lakini ushirika utatusaidia kupata takwimu, kwa sababu wakulima wanakuwa *organized* katika mfumo *AMCOS*, ni rahisi sana kujua *AMCOS* x katika wilaya fulani ina wakulima wangapi. Kwa hiyo, kama ni suala la pembejeo, kama ni suala la mafunzo ya uzingatiaje wa kilimo bora, kupita ushirika, kwa sababu tunaweza tukapata takwimu kirahisi, itatusaidia sana kwenye mambo ya kutoa *extension services* kwa ajili ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii ni sababu nyingine ambayo inaonyesha kwa nini ushirika ni mfumo mzuri, kwa

hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tuwaombe waendelee kutupa ushirikiano katika suala zima la kuboresha ushirika kwa sababu kuna faida nyingi ambazo tunaweza tukazipata katika kuhakikisha tunalinda na kuboresha maisha ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, pia katika ushirika, mikakati ambayo hotuba ya Mheshimiwa Waziri imesheheni likiwemo suala la bima za mazao, ni rahisi sana kutoa huduma hii katika mfumo wa ushirika ambao umekuwa *organized* vizuri. Pia hata suala la mambo ya *kangomba, butula*, baada ya kuwa na ushirika imara, ni rahisi ndani ya *AMCOS* au *Union*, kukawa kuna Mfuko au *SACCOS*, ambayo itasaidia kutoa *advance* kwa wakulima wetu wakati wa kulima ili mkulima huyu asingie katika majaribu ya kukutana na mtu ambaye anataka amnyonye kwa sababu ya shida.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hata rafiki zangu akina Mwambe ambao wanasesma tuhalalishe suala la mfumo wa *kangomba*, tunaweza tusihalalishe mfumo wa *kangomba*, lakini katika kuimarisha ushirika, tukaweka mfumo wa *SACCOS* ndani ya *AMCOS*, kutoa *advance* kwa wakulima ili waweze kuondokana na zile changamoto na shida ambazo zinawapeleka kwenye *kangomba, butula*, na mambo ya namna hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulichangia, limejitokeza sana katika michango ya Waheshimiwa Wabunge ni suala zima la uzalishaji na usambazaji wa mbegu. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kama mlivyoona, sisi Serikali tumejipanga kuhakikisha tunakuwa tuna mkakati ambao pia tunausimamia kuutekeleza na mkakati huu ni kuhakikisha, sasa hivi tatizo lilitopo ni kwamba, mzalisha mbegu na mkulima wanategemea mvua wote kwa wakati mmoja. Mkakati wa Serikali, ni kwamba, huyu anayezalisha mbegu *ASA, TARI*, wakati wa kiangazi, tutatenga fedha kwa ajili ya kumwezesha *TARI* na *ASA* waweze kuzalisha mbegu wakati wa kiangazi ili mbegu hizi ziwepo, ziwe tayari wakati wa msimu mkulima anapozihitaji.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo, tutaondokana na hii changamoto ambayo Waheshimiwa Wabunge walio wengi wameichangia kwamba mbegu hazipatikani, zilizo bora, zinazostahimili ukame, zinazostahimili magonjwa, lakini tuna Taasisi ya ASA na TARI ambazo Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha wakati wa kiangazi wanatumia *pivot irrigation* badala ya kusubiri mvua ili mbegu ziwe tayari mkulima wetu mvua inapoanza basi aweze kupata hizi mbegu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge waunge mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wetu kwa sababu mambo haya yote baada ya kuitisha tutakwenda kwenye utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo napenda kulzungumzia ni suala la masoko kwa sababu ni mtambuka, linahusu mazao yote ya kimkakati na mazao mchanganyiko. Tayari, chini ya uongozi wa Waziri wetu Mheshimiwa Japhet Hasunga, tumeshakaa na wenzetu upande wa Wizara ya Viwanda, ku-/lnk kilimo na viwanda. Tumekaa na *breweries*, kwa sababu *breweries* nyingi zinatumia ngano, zinatumia mahindi, zinatumia mtama na zinatumia zabibu. Tumekaa nao na hivi ninavyozungumza tunakaribia kusaini *partnership* ambayo mahitaji yao wameshayabainisha na tumewaomba wa-project kwa miaka mitano, kama ni zabibu watahitaji kiasi gani, kama ni mtama watahitaji kiasi gani, kama ni mahindi watahitaji kiasi gani ili tuweze kwenda kwa wakulima sasa katika wilaya na mikoa ambayo inalima haya mazao kwa wingi na kuhamasisha kwamba, limeni kwa sababu soko lipo na ni la kiasi hiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *breweries* tumeshakaa nazo, na tumeshakaa hata na viwanda ambavyo vinatengeneza *soft drinks*. Ukiangalia maembe, machungwa, wana *import concentrate* kutoka nchi za jirani na wakati wakulima wetu ukienda kule Tanga, wakati wa msimu machungwa yanaiza. Kwa hiyo, tumeshakaa na hizi *soft drinks*, viwanda vinavyotengeneza soda hizi na sasa hivi kwa sababu ya watu kuzingatia afya, viwanda hivi vinaanza kutengeneza *juice* sambamba na *distribution* ya soda. Sasa zile *juices* ambazo wanatengeneza zenye *flavor* ya

*pineapple*, zenye flavor ya *mango*, zenye flavor ya *orange*, wanaagiza *concentrate*. Sasa sisi tunataka kwa sababu tumeshakaa nao, tujuue mahitaji yao, twende tukahamasishe kilimo cha maembe, kilimo cha machungwa, kilimo cha nanasi ili badala ya ku-*import concentrate*, viwanda hivi viwe vinanunua malighafi hii ya wakulima hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo, tayari Wizara yetu tumeshakaa na hawa *International off-takers*, ninyi mashahidi, tulikaa na *WFP*, (*World Food Program*), tumeingia nao mkataba wa muda mrefu kupita *NFRA* watakuwa wanakusanya mahindi na sasa hivi si mahindi tu, ukienda *South Sudan* wanahitaji mtama.

Kwa hiyo pia kupitia *NFRA* tutakuwa tunawahamasisha wakulima walime mtama halafu *NFRA* au *aggregate*, lakini *WFP* anakuwa anachukua hapa Tanzania kupita *NFRA* na wanunuzi binafsi, kupeleka kwenye nchi ambazo hazina ardhi yenye rutuba, hazina amani kama Tanzania. Kwa hiyo, sasa ni muda sahihi wa kuhakikisha wanaunga mkono bajeti ya Kilimo ili tuweze kuipeleka kwenye utekelezaji na kuchukulia hii *geographical comparative advantage* tuliyonayo katika nchi za Afrika Mashariki na *SADC* kwa sababu tunaweza tukazalisha kwa kiasi kikubwa na tukaweza kuondokana na hii changamoto ya wakulima wetu kulima, lakini masoko yakawa yanakosa.

Mheshimiwa Spika, tunawahakikishia Waheshimiwa Wabunge wakiunga mkono bajeti hii haya mambo yote tunayowaambia tutaweza kupeleka kwenye utekelezaji na matokeo makubwa watayaona kwa muda mfupi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala ambalo Mheshimiwa pacha wangu Mheshimiwa Omary Mgumba amelizungumzia, tukizungumzia mambo ya umwagiliaji mara nyingi tunafikiria ujenzi wa mabwawa makubwa, fedha nyingi, lakini niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Mheshimiwa Mgumba, kupitia halamshauri zetu...

**SPIKA:** Dakika moja umalizie.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Suala la mabwawa kwa mfano kwenye mpunga, hauhitaji skimu kubwa, tunaweza tukaangalia jinsi ya *ku-rain harvest*, yaani kwa uchimbaji mdogo tu unakinga unapata maji kwa ajili ya kilimo cha mpunga na mazao ya bustani badala ya kusubiri kwamba mpaka mradi mkubwa uje uletwe na Tume wa Umwagiliaji kwenye wilaya husika, sasa sisi ndani ya Serikali tutakaa na halmashauri, Wakuu wa Mikoa, kuhakikisha suala la *rain harvest* linakuwa sambamba na uchimbaji wa mabwawa tunayozungumzia.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bashungwa. Sasa ni Mheshimiwa Mwakyembe, kwa dakika tano, karibu tafadhali.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa fursa. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika sekta hii. Nami naunga mkono hoja moja kwa moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nitumie nafasi hii vilevile kutoa pole kwa Watanzania wote wakiwemo wananchi wa Kyela, kwa matatizo makubwa waliyoyapata hasa baada ya mvua hizi kubwa kunyesha, kupata mafuriko, wamepoteza mazao, wamepoteza watu, wamepoteza maisha na vilevile miundombinu kuharibika. Leo hii ninavyoongea wasaidizi wangu wako Jimboni Kyela wakigawa chakula kwa walioathirika sana. Kwa hiyo, hata Waheshimiwa Wabunge ambao wanawenza wakapata huruma kidogo basi tunapokea michango tutaifikisha hapo kwa waathirika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pengine niongelee kitu kifupi sana maana dakika tano siyo nydingi, kuhusu suala la ushirika ambalo aliongelea Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani,

kwamba ushirika ni tabu tu kwa wakulima, lakini pengine kwa mazao mengine, lakini naomba niongelee zao la kokoa kwamba, ushirika ndiyo mkombozi kwa wakulima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sana sisi Kyela tunazalisha sehemu kubwa ya kokoa nchini. Kokoa haijawahi kupanda bei zaidi ya Sh.3,000 kwa kilo, hiyo ni bei kubwa sana, lakini kuanzia Novemba, tulipoanzisha huu mfumo, tumeweza, kuitia hii minada, kupata bei nzuri ya kuanzia Sh.4,500, haijashuka imeendelea kuwa Sh.5,000, ikaenda Sh.5,600, tunaelekea kwenye Sh.6,000 sasa hivi kwa kilo. Vilevile mfumo huu umetufanya tuweze kuelewa pia unyonyaji mkubwa unaoendelea, hasa kutokana na wenzetu hawa wa katikati hawa, kwingine wanaitwa *kangomba*, sisi tunaita *njemke*.

Mheshimiwa Spika, kule kwetu kilo moja, lakini wala siyo kilo, ni kitini kimoja kinaitwa sado, ni Sh.800 analipwa mkulima, lakini hicho hicho kitini kimoja kinaitwa sado, kina kilo tatu ndani yake. Kwa hiyo, mkulima analipwa Sh.800, yeye akienda kwenye soko, anapata zaidi ya shilingi elfu 16, ni unyonyaji mkubwa sana! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nafurahi kwamba Serikali imeshatunga Sheria ile ya *Microfinance Act* ya 2018 ambayo inatupa msingi sasa wa sisi kuweza ku-regulate hii, hatuwafukuzi hawa watu, lakini kuwa-regulate sasa, kwa sababu chini yah ii sheria tunaweza kabisa tukatunga kanuni ambayo inaendana na zao kwa zao. Kwa mfano, mimi mwenyewe, nitakuwa wa kwanza katika kukimbilia kwa hii fursa kwamba tuwe na kanuni kwa zao la kokoa kwa kuwaelewesha ili hao wenzetu *njemke* wasipate faida kupitiliza, angalau nusu ibakie kwa mkulima na yeye nusu ifidie gharama zake za kwenda huko na kule. Kwa kweli ni kazi ambayo inawezekana kabisa ikafanyika na ikaleta tija katika soko.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni suala ambalo tuliliongelea juzi, aliliongelea Mheshimiwa Mwambe hapa la *Ministerial responsibility*. Alisema lazima Waziri anapofanya

kosa sisi tuliseme hapa, ni kweli kabisa hakuna tatizo kabisa kuhusu *Ministerial responsibility*. Nilichokuwa nalalamikia mimi ni kwamba kuna suala ambalo, haliihusu hiyo Wizara yenye, lakini linahusu Mawaziri watatu, wanne, si sahihi ukam-single out Waziri mmoja huyo huyo kwa kumrushia mawe. Sasa inakuwa kama una kitu fulani kwake, ndiyo maana nikasema, chini ya Ibara ya 53, sisi ndani ya Bunge, chini ya Waziri Mkuu, tunawajibika kwa Bunge kwa pamoja, (*collectively*), kwa hiyo, ndiyo hicho nilitaka kufafanua tu waelewe kwamba sasa kama kuna Mawaziri wawili, watatu wanahuksika, mmoja tu ukiendelea kumtupia mawe siyo sahihi hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hili ni suala letu, hata mimi mwenyewe ukinilaumu, mimi mwenyewe nitaitetea Serikali hapa kwa sababu ni suala la kiserikali na hakuna ambaye amelikimbia na bado ulivyomsikia Waziri wa Viwanda na Biashara, ameeleza vizuri sana, hoja nyingi sana hapa zinaweza kuyeyuka kama mshumaa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, na Waheshimiwa Manaibu Waziri, Waheshimiwa Wabunge wote, ambao tumepata fursa japo ya muda mfupi kujadili hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ya jambo muhimu sana ambalo ndilo asilimia kubwa ya watu wetu wanashughulika na kilimo, wapiga kura wetu wengi sana ni wakulima na maisha yetu Watanzania bado kwa kiasi kikubwa yamejikita kwenye kilimo. Kwa hiyo, tumefika wakati sasa wa kwenda mapumziko kidogo na tutarudi hapa saa kumi kamili jioni, ambapo sasa tutamwita mtoa hoja kwa sababu hoja hizi ni nyingi, tutampa saa moja ili aweze kuhitimisha kwa nafasi kuliko kukimbia kimbia. Baada ya hapo tuaendelea na utaratibu wetu wa vifungu na kadhalika tuweze kuitendea haki hoja hii. Nawaombeni tuwahi kurudi kusudi tusikilize majibu yote tukiwepo, badala ya kuwa umeshajibiwa halafu tena baadaye unasi mama na kadhalika, inakuwa inasaidia.

Nawakumbusha tena saa kumi kamili jioni tukutane hapa, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2019/2020  
kwa Wizara ya Kilimo**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano yetu, sasa nimwite Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Japhaet Ngailonga Hasunga ili ahitimishe hoja yake. Mheshimiwa Hasunga, tafadhalii.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuhitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo ya hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge niwatambue Waheshimiwa wote waliochangia kwa maandishi na kwa kuongea. Hoja hii imechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 89 wakiwemo Waheshimiwa Wabunge 47 waliochangia kwa kuzungumza humu ndani Bungeni na Waheshimiwa Wabunge 42 waliochangia kwa maandishi. Nitambue kipekee mchango uliotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, nawashukuru sana kwa maoni yao mazuri na mapendekezo yote na ushauri ambao wameshautoa. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwani wametoa hoja nzuri

zenye malengo ya kuimarisha utekelezaji wa majukumu katika Wizara yangu na kuharakisha Mapinduzi ya Kilimo chetu hapa nchini. Hii inaonesha umuhimu wa kilimo katika usalama wa chakula, lishe, ukuaji wa uchumi, na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba (Mb) na Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa (Mb) kwa kuchangia hoja hii na kutoa ufanuzi wa hoja mbalimbali zilizotolewa na Wabunge, nawashukuru pia Katibu Mkuu Mhandisi Methew John Mtigumwe, Naibu Katibu Mkuu Profesa Siza Tumbo, na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano na ushauri wanaoendelea kunipa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Michango iliyotolewa ni mingi sana na yote ni muhimu sana. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa muda nitafafanua baadhi ya hoja zilizotolewa ambazo ni muhimu Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla wakapata ufanuzi wa moja kwa moja. Ninawahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba majibu ya hoja zote zilizotolewa yataandaliwa na kukabidhiliwa kwa Waheshimiwa Wabunge kabla ya kumalizika kwa mkutano huu wa Bunge la Bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kujibu hoja ya Waheshimiwa Wabunge kwa kueleza mwelekeo wa Serikali katika kuleta mapinduzi ya kilimo hapa nchini. Sote tunatambua umuhimu wa kilimo katika usalama wa chakula, lishe, ukuaji wa uchumi, malighafi za viwandani na kupunguza umaskini. Sote tuko hapa kwa sababu tumepata chakula tumekula, ama kama hatujala muda huu tutakula jioni au usiku; kwa hiyo sisi wote ni wadau katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, vilevile Tanzania kama sehemu ya dunia imesaini makubaliano ya kimataifa kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu, (*Sustainable Development Goals – SDG*). Chini ya makubaliano hayo ya kimataifa lengo namba moja linahusu kutokemeza umaskini na lengo namba mbili ni kukomesha njaa ifikapo mwaka 2030. Malengo hayo yanamaana kubwa kwenye kilimo kwani kama tunataka kutokomeza umaskini na kukomesha njaa ni lazima tuwekeze

kwenye kilimo kwa kufanya mapinduzi yenyewe kuongeza tija na uzalishaji, kuwa na uhakika wa kuzalisha mazao bora kwa ajili ya malighafi za viwandani na masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa Mapinduzi ya Kilimo na kama nilivyowasilisha kupitia hotuba yangu Serikali inatekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya pili *ASDP II*. Programu hii inalenga kuleta mageuzi makubwa ya sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo. Sisi sote ni mashahidi tunaona tija ilivyo ndogo sana katika maeneo mengi kwenye kilimo chetu. Tunakusudia kufanya kilimo kiwe cha kibashara zaidi na kuongeza Pato la Taifa kwa wakulima wadogo kwa ajili ya kuboresha maisha yao. Pia tunahitaji kuwa na uhakika na usalama wa chakula na lishe na kuchangia katika Pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, historia inatuonesha kuwa nchi nydingi duniani zimepiga hatua kubwa kwa maendeleo kutokana na mchango wa sekta ya kilimo. Nchi kama Uingereza, China, Malaysia, Canada, Korea, Indonesia na nchi nydingi nydingi zimeendelea kwa sababu ya mchango mkubwa wa kilimo katika uchumi wao. Nchi nydinge hizo uchumi wao ulianza kwenye Mapinduzi ya Kilimo na kuelekea kwenye Mapinduzi ya Viwanda. Tunaona kabisa kwa mfano Uingereza ilianza na *Agrarian revolution*, ambayo ilikuwa ni *agricultural revolution* ikaja *industry revolution* na baadaye wakaenda kwenye *commercial revolution* na *political revolution* na hatimaye sasa hivi wako kwenye teknolojia ya maendeleo kabisa. Kwa hiyo kwa kweli kila nchi mchango wa kilimo ni mkubwa sana katika hatua ambayo wamefikia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeona nchi nydingi sasa hivi zimefikia kwenye ugunduzi mkubwa wa kuboresha, yaani kuwa na huduma nzuri yaani *service industry* na sasa nydingi zimeingia katika uzalishaji wa teknolojia. Nina uhakika hatuna namna ya kukwepa kama taifa, na ndiyo maana katika hotuba yangu nilibainisha baadhi ya maeneo muhimu yanayohitaji msukumo wa kipekee na maboresho kuanzia

mwaka 2019/2020. Maeneo hayo ni pamoja na maboresho ya sera, na Sheria, kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo, masoko ya uhakika ya mazao na bidhaa za kilimo, na kuwakinga wakulima na majanga kuititia Mfumo wa Bima ya Mazao. Ndiyo maana tumeanza mapitio ya sera ya kilimo ya mwaka 2013, mapitio ya sera ya ushirika pia ya mwaka 2002, pia tumeanza mchakato mkubwa wa kuanza mchakato wa kutunga Sheria ya Kilimo na kuandaa utaratibu wa Bima za Mazao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili mabadiliko ya kweli ya kilimo yaweze kutokea lazima tuchukue hatua za kusimamia matumizi endelevu ya ardhi kwa kuwa na sera nzuri, na sheria ya kusimamia matumizi ya ardhi ya kilimo, ikiwa ni pamoja na kupima afya ya udongo ili kuwezesha wakulima kuongeza virutubishi vya udongo ardhini kulingana na mahitaji ya udongo. Vilevile matumizi endelevu ya maji ni muhimu sana katika kuongeza uzalishaji na tija ikizingatia mabadiliko makubwa ya tabianchi yanayotokea duniani na nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya kweli pia yanahitaji uzalishaji wenye tija na faida katika minyororo ya thamani ya mazao yote; katika eneo hili Serikali imejipanga kuongeza matumizi ya pembejeo bora za kilimo ikiwa ni pamoja na uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za mazao kama vile mahindi, mtama, ngano, ulezi, uwele, maharagwe, na jamii nydingine ya mikundi, alizeti, michikiti, ufuta, karanga, muhogo, parachichi na miwa. Mazao mengine ni kahawa, pamba, pareto, tumbaku, korosho, viazi mviringo, ndizi na zabibu.

Mheshimiwa Spika, tumeanza kuona mabadiliko katika ukuaji wa sekta ya kilimo. Takwimu rasmi za ukuaji wa kilimo zinaonesha kuwa sekta ya kilimo ilikuwa kwa asilimia 6.9 kwa mwaka 2014 na hizi takwimu ni baada ya kubadilisha ile *re-base* na Kambi Rasmi ya Upinzani ilitoa takwimu namna uchumi ulivyokua, sasa takwimu halisi ambazo ndizo sahihi zinaonesha kuwa kilimo kilikua kwa asilimia 6.9 kwa mwaka 2014, asilimia 5.4 kwa mwaka 2015, asilimia 4.8 kwa mwaka

2016, asilimia 5.9 kwa mwaka 2017 na asilimia 5.3 kwa mwaka 2018. Hizi ndizo *official*/takwimu zinazoonesha ukuaji wa sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, ukuaji huu mzuri wa sekta ya kilimo umetuhakikishia usalama wa chakula nchini kwa muda wa miaka minne iliyopita. Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu utoshelevu wa chakula kwa mwaka 2018/2019 ni asilimia 124. Hata hivyo kuna dalili za kutokea upungufu wa chakula katika baadhi ya maeneo kutokana na upungufu wa mvua na mvua kuchelewa katika badhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, hivyo tuendelee kuhifadhi chakula katika ngazi ya kaya na Serikali kuititia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula itanunua chakula cha kutosha na kuhifadhi kwa ajili ya kukabiliana na upungufu unaoweza kujitokeza. Hata hivyo niwahakikishie wananchi kwamba Serikali haitarajii kuzuia wakulima na wafanyabiashara kuuza mazao yao nje ya nchi, narudia hata hivyo niwahakikishie wananchi kwamba Serikali ya Awamu ya Tano haitarajii kuzuia wakulima na wafanyabiashara kuuza mazao yao nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuongeza matumizi sahihi ya mbolea viuatilifu mbalimbali kama *copper*, *sulfur*, na matumizi ya teknolojia za kilimo. Pia tutaboresha matumizi ya dhana za kilimo na kuimarisha huduma za ugani, utafiti na mafunzo. Sanjari na kuongeza uzalishaji suala la masoko ya uhakika wa mazao yanayozalishwa limepewa na litaendelea kupewa kipaumbele kutoka na kuwepo kwa ongezeko la uzalishaji hapa nchini na mahitaji katika masomo ya ndani nje ya nchi. Masoko yataimarika zaidi kwa kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya mazao yakiwemo mazao kama kahawa, mahindi, mbaazi, korosho, parachichi, pareto, tumbaku, mkonge matunda na mbogamboga. Aidha, tutaimarisha ukusanyaji wa takwimu za kilimo, huduma za fedha zinazotolewa kama mikopo na vitu vinginevyo, Bima ya Mazao, usafishaji, utunzaji wa mazao na kujenga uwezo wa wataalam wetu katika maeneo mbalimbali ili waweze kutoa huduma zile zinazohitajika kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya jumla naomba nitoe ufanuzi wa maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingi ambazo zimetolewa kama nilivyosema kwamba sitaweza kuzijibu zote zingine tutazijibu kwa maandishi. Hata hivyo naomba nianze na hoja namba moja ambayo ilikuwa imetolewa; kwamba hoja hii inahusu ushuru wa usafirishaji wa korosho ghafi nje ya nchi yaani *Export Levy* kurudishwa kwa wakulima kwa ajili ya kuendeendeleza zao la korosho. Hoja hii ilichangiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge, pia Mheshimiwa Cecil Mwambe naye alichangia hoja hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nikumbushe kwamba Bunge lako Tukufu limeifanyia marekebisho Sheria ya fedha ya mwaka 2018, kifungu cha 17 (a). Kwa mujibu wa marekebisho hayo fedha za ushuru wa usafirishaji wa korosho ghafi nje nchi zitaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa sasa tasnia ya korosho inahudumiwa moja kwa moja na Serikali kuititia Wizara ya Kilimo, na Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, tulikaa wote hapa tulipitisha ile kwa pamoja. Kwa hiyo hilo sasa suala hilo tena halipo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili iliyotolewa ilikuwa inahusu Serikal iondoe ushuru kwenye Pembejeo za Kilimo kama mbolea, mbegu na viuatilifu. Hoja hiipia ilichangiwa na Mheshimiwa Neema Mgaya, naomba niseme mchango ulikuwa mzuri sana tunaipokea.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya ushuru wa forodha wa Afrika Mashariki (*The EAC Customers Management Act of 2004*) na Sheria ya kodi ya ongezeko la thamani *VAT Act of 2014*, pembejeo za kilimo ikiwemo mbolea, mbegu na viuatilifu havitozwi kodi wala ushuru wowote. Naomba nirudie, pembejeo za kilimo ikiwemo mbolea, mbegu na viuatilifu hazitozwi kodi wala ushuru wowote. Aidha, Serikali inaendelea kufanya maboresho ya tozo, ada, ushuru na kodi mbalimbali katika sekta ya kilimo

kwa lengo la kuvutia wawekezaji na kuwaongezea wakulima kipato.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi miaka mitatu kuanzia mwaka 2015 Waheshimiwa Wabunge mlifanya kazi nzuri sana katika mjadala, mkasema kuna kodi nydingi sana ambazo ni kero ambazo ni tozo kwenye kilimo mkaalagiza na kuishauri Serikali iziondoe. Nyote mnakumbuka kwamba kuanzia mwaka 2015 jumla ya ushuru tozo na ada 105 zilifutwa kati ya kodi 146 zilizokuwa zinatozwu na kubainika kuwa kikwazo katika maendeleo ya sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa pembejeo Serikali katika mwaka 206/2017 ilifuta jumla ya tozo na ada saba katika tasnia ya mbegu, nne katika tasnia mbolea na moja katika mfuko wa pembejeo. Aidha, Serikali imefanya marekebisho ya kanuni zillzoanzisha tozo na ada hizo kwenye pembejeo ili kuwezesha utekelezaji wake kuwa mwepesi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imefanya marekebisho ya Kanuni ya Sheria ya Mbolea ya Mwaka 2011 (*The Fertilizer Regulation of 2017*) ambapo gharama za uhakiki wa ubora wa mbolea imepunguzwa kutoka dola 30,000 hadi kuwa dola 10,000, na muda wa majaribio umepunguzwa kutoka miaka mitatu hadi msimu mmoja katika maeneo mawili ya ikolojia tofauti. Wizara pia ilitunga Kanuni za Kusimamia Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja [*Fertilizer Bulk Procurement System (BPS)*] ambapo imekadiliwa kupunguza bei ya mbolea kwa mtuamiaji wa mwisho kati ya asilimia 10 mpaka asilimia 40 ya bei.

Mheshimiwa Spika, hapa naomba nitoe maelezo kwa undani. Sasa hivi katika utafiti ambao tumeufanya na kuangalia bei ya mbolea nchini na maeneo yote duniani inaonekana kwamba mbolea gharama kubwa ya mbolea inaanzia pale mbolea inapowasili bandarini, kuanzia pale bandarini, gharama za kuitoa pale kuweka kwenye mifuko na kusafirisha mpaka kwa mkulima. Kwa utafiti uliofanyika unaonesha kwamba gharama zile ziko kati ya asilimia 40 mpaka asilimia 60. Kwa hiyo ina maana kwamba tukifanyia

kazi vizuri katika hili eneo kuna uwezekano mkubwa mbolea zikashuka bei na zikawa na bei ambayo mkulima anaweza kufaidika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunakusudia kufanya marekebisho hayo na ndiyo maana tunaupitia upya huu mfumo na hivi kesho tumeita kikao cha wadau wote wanaonunua na kuagiza mbolea nchini wanakuja hapa Dodoma tuna mkutano nao kwa ajili ya kukaa na kujadiliana vizuri kuangalia gharama zote za uendeshaji ili kusudi ikiwezekana mbolea hii ambayo inaagizwa basi ipunguzwe bei na wakulima wetu wapate mbolea ambayo ni sahihi na ile yenye bei nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya tatu ambayo ilikuwa inahusu kuteua Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Korosho kwa mujibu wa Sheria. Hoja hii ilchangiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, pia Mheshimiwa Abdallah Chikota amechangia vizuri sana na wengine waliochangia.

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya uteuzi zimeanza uundaji Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Korosho Tanzania kwa mujibu wa sheria ya tasnia ya korosho namba 18 ya mwaka 2009 na kanuni za korosho za mwaka 2010. Kazi hii itakamilishwa na Serikali baada ya muda mfupi ujao. Naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu tayari tulishamteua Kaimu Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Korosho ana takriban wiki mbili alisharipoti kazini na wiki hii tunakamilisha uundaji wa Bodi Wajumbe watatangazwa. Kwa hiyo ninauhakika sasa jukumu lile ambalo wanalo lile la kisheria la kuhakikisha wanasimamia zao la korosho wataendelea kusimamia jukumu hilo moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nitoe angalizo na utofauti uliopo. Kulikuwa na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, bodi ile ilikuwa haisimamii zao, ilienda kama mnunuzi, na kama wanazo fedha wataendelea kununua wakishindana na wafanyabiashara wengine watanunua na

kuendelea kuuza. Lakini Bodi ya Korosho itasimamia taratibu zote kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne ilikuwa ni wadau mbalimbali wa korosho hususani halmashauri bado hawajalipwa fedha na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao. Hoja hii pia ilichangiwa na Wajumbe wengi na Waheshimiwa Wabunge wengi akiwemo Mhandisi Edwin Ngonyani, pia Mheshimiwa Chikota alichangia na wengine wengi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imelipa jumla ya bilioni 26.3 kwa watoa huduma mbalimbali walioko kwenye mnyororo wa thamani wa korosho. Watoa huduma hao ni pamoja na wasafirishaji, *AMCOS* Vyama Vikuu vya Ushirika, waendesha maghala na gharama za magunia. Kwa kuwa uwamuzi wa Serikali wa kununua korosho kullenga kumnufaisha mkulima hivyo baadhi ya gharama zimebebwa na Serikali zikiwemo Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachotaka kusema ni kwamba katika wale wadau ambao bado hawajalipwa sasa hivi tukishapata fedha tutahakikisha kwamba nao basi wanalipwa; lakini lazima tukumbuke kanuni inayoelekeza; Serikali moja haiwezi kuitoza kodi Serikali nyengine. Kwa hiyo ukisema Serikali Kuu ilipe Serikali za Mitaa kidogo kwa mujibu wa kanuni na sheria za kodi ni tofauti. Kwa hiyo hapa tunapozungumzia tunazungumzia wale wadau wengine wote waliotoa huduma ambao si Serikali, hao wote tuna uhakika watalipwa bila tatizo lolote.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na hoja kwamba wakulima wengi bado wanadai, naomba nikiri kabisa kweli kuna wakulima mpaka sasa hivi hatujamaliza kuwalipa, zaidi ya bilioni 100 za malipo ya korosho bado zinadaiwa, na mimi nakubaliana kabisa na Waheshimiwa Wabunge, wameliongelea suala hili kwa uchungu mkubwa na mimi kama Waziri wa Kilimo linaniumiza sana, nakosa hata usingizi kwa sababu mimi tungependa wakulima wetu wapate fedha kwa wakati ili waendelee kulima; hatutaki kuona wakulima

wanahangaika. Kwa hiyo hili kwa kweli sote linatusumbua, lakini tatizo limekuwa ni upatikanaji tu wa fedha za kutosha za kuhakikisha kwamba tunalilipa.

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inaendelea kufanya malipo kwa wakulima kulingana na uhakiki uliofanyika; hadi kufikia Mei mwaka 2019 Serikali ilikusanya jumla ya tani 222,830.5 za korosho ghafi zenyе thamani ya shilingi bilioni 722,775,186,000, katи ya hizi fedha jumla ya shilingi bilioni 623,680,510,416 zimelipwa kwa wakulima moja kwa moja ambayo hii ni sawa na asilimia 86 ya madai yote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli Serikali tumejitahidi hatukutegemea kwanza halikuwa lengo kwamba zile fedha labda tutachelewa, tulidhani kwamba baada ya kukusanya tukiiza, tungezungusha zile fedha wakulima wote wangekuwa wamelipwa. Mpaka sasa hivi hatujauza lakini Serikali imelipa zaidi ya bilioni 623, tumejitahidi. Hii haina maana kwamba tunabeza wale ambao hawajalipwa kwa sababu moja ya watu ambao hawajalipwa ni wale wakulima wakubwa ambao mimi nataka walipwe ili waendelee kulima zaidi na kuhudumia kilimo. Kwa hiyo hili tutaendelea kulifanyia kazi na kwa muda mfupi nina uhakika Serikali tutaliangalia na kuhakikisha kwamba tunapata fedha kwengine hata kwa kukopa ili wakulima hawa walime waendelee kupalilia korosho zao na waendelee kuzalisha, kwa hiyo hili tutaendelea kulishughulikia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine kwamba tujikite kwenye ubanguaji, wawekezaji kwenye viwanda vya Serikali walioshindwa kuviendoeleza wanyang'anywe. Nakubaliana kabisa na maoni ya Waheshimiwa Wabunge, nchi yetu ni kubwa wala hatuwezi kulinganisha na nchi nyingi, ni nchi iliyobahatika kuwa na ardhi nzuri yenyе uwezo mkubwa, yenyе watu wengi wenye utaalam mkubwa. Sasa hivi Msumbiji wanabangua korosho zao kwa asilimia 75, sisi nchi kubwa yenyе wataalam wengi, korosho zetu zote tunauza zikiwa ghafi. Hii haikubaliki na ndio maana hata viwanda tulivyokuwa navyo vyote, Mheshimiwa

Baba wa Taifa marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alianzisha viwanda 12, tukavibinafsisha, tukawauzia watu, baadhi ya watu waliochukua wameshindwa kuviedeleza wala havifanyi ile kazi, ndio maana kwa sababu hiyo Serikali tumeamua kuvirudisha baadhi ya viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe takwimu, viwanda vinne sasa hivi tumeshavirudisha mikononi mwa Serikali ili kusudi tuwekeze, viendelee na kazi ya kubangua, kusudi korosho zetu zote zibanguliwe hapa nchini. Kwa hiyo tumechukua Kiwanda cha Kubangua Korosho cha Lindi kile cha Buko, wote mnajua. Pia tumechukua kiwanda cha Newala yaani *Agrow Focus* nacho tumekitaifisha, tumeshakirudisha, tumemnyang'anya yule mwekezaji. Vile vile Kiwanda cha Mtama yaani kile cha Lindi *Farmers* tumekichukua, Kiwanda cha Nachingwea nacho tumekichukua. Kwa hiyo, viwanda vyote hivi tumeshavirudisha, sasa hivi tunatafuta wawekezaji wapya ili wawekeze na wahakikishe kwamba kwa kweli hivi viwanda vinabangua.

Mheshimiwa Spika, najua kulikuwa na tatizo kubwa ambalo walikuwa wanalisema, walikuwa wanasema wanashindwa kushindana kwenye soko kwa sababu wanakosa malighafi, lakini nataka nilihakikishie Bunge tumejipanga vizuri kuangalia upya sera yetu ya uuzaji ili kusudi viwanda vyote vitakavyoanzishwa vihakikishiwe kupatiwa malighafi ili vitoe ajira na kuongeza thamani. Kwa hiyo, hiyo sera itakuwa nzuri sana.

Aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha wawekezaji wanye viwanda vyta kubangua korosho ili kuongeza uwezo wa ndani wa ubanguaji na kukuza ajira. Serikali itaendelea kutafuta wanunuzi wa korosho zilizohifadhiwa kwenye maghala ili kutoa nafasi ya kuhifadhi korosho kwa msimu ujao. Nitumie fursa hii kuwaomba hata Waheshimiwa Wabunge, wanaweza wakaunda *SACCOS* ya kwao wakaanzisha viwanda, hebu tuongoze kwa vitendo, tunaweza tukaanzisha viwanda viwili, vitatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna viwanda pale vyatubangua korosho unaweza ukaanzisha kwa Sh.1,000,000,000. Nina uhakika kabisa Waheshimiwa Wabunge tulioko hapa haviwezi kutushinda, kinachohitajika ni dhamira ya kweli ya sisi wenye kwamba tunataka kweli tujenge viwanda, tunaweza, hili linawezekana, ukilinganisha na mikopo ambayo huwa tunakopa. Tukiwekeza nina uhakika nchi hii itasogea mbele na tutasogea sana.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu mawakala ambao hawajalipwa wale ambao walisambaza pembejeo mwaka 2015/2016. Nakubaliana kabisa kwamba kulikuwa na mawakala wengi lakini tulipofanya utafiti, tulipofanya uchunguzi imebainika karibu kila wakala alidanganya, mawakala wote walidanganya. Sasa kama wamedanganya, takwimu ni feki unamlipaje?

Kwa hiyo, sisi tulichokifanya sasa hivi katika hili suala tulipoona kwamba wote kila mtu ana udanganyifu, tumechukua takwimu zao zote tumepeleka TAKUKURU, wanaendelea na uchunguzi, ukikamilika wale watakaobainika kwa kweli hawakudanganya hao wote tutawalipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja Serikali kupelekea pembejeo kwa wakulima kwa wakati, bei nafuu na kuweka mfumo mzuri wa upatikanaji wake. Hoja hili imechangiwa na Wabunge mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Pia Mheshimiwa Ngalawa, Mheshimiwa Semesi, Mheshimiwa Kakoso na wengine wengi wamechangia hii hoja. Wizara inakamilisha mapitio wa mifumo ya uzalishaji, uagizaji na usambazaji wa pembejeo ili kuandaa mfumo madhubuti utakaohakikisha kwamba pembejeo zilizozalishwa au kuagizwa nje zina ubora na zinapatikana kwa wakati na kwa bei nafuu kwa mkulima. Aidha, Serikali itahamasisha na kusimamia usambazaji wa pembejeo kwa kuzingatia kalenda ya kilimo katika maeneo mbalimbali nchini kulingana na kanda za kiikolojia za kilimo ili pembejeo zifike kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeliagiza Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) kutoa kipaumbele cha kusafirisha mbolea kwenda mikoa yenyе miundombinu ya reli kwa kuwa gharama za usafirishaji kwa njia ya reli ni nafuu ikilinganishwa na usafiri wa barabara. Hili mpaka kuanzia bandarini pale, bandarini pia tumeongea na wenzetu wa bandari kwamba watoe kipaumbele mbolea zinapowasili ziweze mara moja kupakuliwa na kupelekwa katika maghala na ziweze kusafirishwa ziende kule zinakohitajika. Tunajua misimu inatofautiana, kwa hiyo, tumetoe hicho kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na suala linahusu bajeti ya kilimo kwa kuzingatia Maazimio ya Malabo na Maputo. Hoja hii imechangiwa sana na Kamati ya Kudumu ya Bunge na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imelisema na Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema kwamba bajeti ya kilimo ni ndogo. Naomba nitoe ufanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kusema bajeti tu haitoshi, ni kweli haitoshi na hakuna siku ambayo tutasema bajeti inatosha, lakini upangaji wa bajeti na vipaumbele unategemeana na nchi moja na nchi nyingine, lakini tunazingatia majukumu ya Serikali ni nini katika hiyo. Kwa mfano katika nchi yetu, Serikali haiendi kulima mashamba, Serikali kazi yake ni kutengeneza miundombinu ili sekta binafsi zikalime, wakawekeza, wakafanye biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunachosema sisi ni kwamba, Serikali ndio unawenza ukaiangalia bajeti ya kilimo lakini kitaalam zaidi bajeti ya kilimo haipimwi kwa hela zilizowekwa kwenye Wizara ya Kilimo peke yake, fedha zote ambazo ziko TAMISEMI kwa asilimia kubwa zile ambazo ziko *TARURA* zote zinatengeneza barabara zinazohudumia kilimo. Fedha zilizoko Wizara ya Uvuvi, fedha zilizoko kwenye Wizara mbalimbali, kwa mfano sasa hivi Wizara ya Nishati wanasantaza umeme vijijini, ule umeme ni kwa ajili ya kuhudumia wakulima. Kwa hiyo yote hiyo tunaita ni bajeti ya kilimo. Barabara mbalimbali zinajengwa barabara kubwa, reli zinajengwa, viwanja vya ndege vinajengwa, vyote hivyo ni kwa ajili ya kuhudumia wakulima. Kwa hiyo ukitaka upate

bajeti ya kilimo peke yake ni vigumu, zote hizo zichukue, angalia, sasa ndio unaweza ukakokotoa ukapata bajeti ya kilimo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba hatuwezi kusema tunaweza kutekeleza hiyo kama ilivyo lakini lazima tuiangalie kwa vipaumbele ambavyo tunatekeleza na nina imani bajeti zilizotengwa kwenye Miundombinu, Nishati, Mawasiliano, Uvuvi, TAMISEMI zote ni kwa ajili ya kuhudumia kilimo chetu na hivyo nina uhakika kabisa kwamba bajeti ni kubwa na itatosheleza katika kutekeleza majukumu ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara na Taasisi mbalimbali kama vile Viwanda, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Maji, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Nishati zinachangia katika utekelezaji na ukuaji wa Sekta ya Kilimo. Kwa mfano Wizara ya Ardhi, ardhi yote hii ikipimwa na tunasema kwamba ikipimwa ikaeleweka ardhi ya kilimo ni hii tayari watakuwa wamechangia na itakuwa ni bajeti ya kilimo. Pia kuna ASDP //inatekelezwa na Wizara za Kisekta ikiwepo Wizara ya Kilimo, lakini kuna Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maji, TAMISEMI, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Uwekezaji na kadhalika. Zote hizo ukiangalia shughuli zao kwa asilimia karibu 80% zote zinashughulikia masuala ya kilimo. Kwa hiyo kilimo, nasema ni suala mtambuka na hivyo bajeti yake bado ni kubwa na inatosheleza.

Mheshimiwa Spika, wapo Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kuhusu masoko na wamezungumza kwa undani sana. Hoja hii ilchangiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mifugo na Maji, Kambi Rasmi ya Upinzani walisema, lakini pia baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walichangia sana kuhusiana na masoko. Serikali inaendelea kutafuta masoko ya uhakika ya mazao mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kwa kuanzia tumeanzisha Kitengo cha Masoko katika Wizara ya Kilimo ambacho hakikuwepo ili kihakikishe kwamba kwa kweli kinafanya *market intelligence*, kitafute masoko nje, kitafute masoko ndani na hata ndani hapa

masoko bado ni makubwa bado hatujayatumia vizuri. Kwa hiyo, kwa kupitia kitengo hiki ni imani yangu kwamba tutajitahidi sana kuhakikisha hili tunalfanya.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutangaza fursa za masoko ya wakulima, kuingia mikataba ya kibiashara baina ya Tanzania na nchi mbalimbali na kuanganisha wakulima moja kwa moja na wanunuzi kama nitakavyowaeleza hapo baadaye. Aidha, Wizara ya Kilimo inaendelea kutoa vibali vya kuuza na kusafirisha mazao nje ya nchi. Kwa mfano, katika mwezi Januari, 2019 na Aprili, 2019; jumla ya tani 22,201 za mbaazi zimesafirishwa kwenda nchi za Qatar, Dubai, Oman, Pakistan, Bangladesh, Malaysia, Kuwait, Indonesia, *United Emirates Republic* na Ureno. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya tani 80,648 za mahindi ziliuzwa nchi za Rwanda, Uganda, Congo, Kenya, Burundi, Malawi, Oman, Sudan ya Kusini na kadhalika na vilevile makampuni yaliyosajiliwa yamenunua mhogo mkavu katika tani 254.52 kwa ajili ya kusafirisha kwenda nchini China na kuna kampuni kama tano ambazo zimeshapata vibali vya kusafirisha mhogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachotaka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, hizi jitihada tuendelee nazo. Tutaendelee kuzungumza na nchi mbalimbali, tutaendelea kutafuta wanunuzi mbalimbali wa mazao yetu yote, yale ambayo tunayo na yale mengine tunayoweza kuanzisha ili kuhakikisha kwamba kilimo kinachangia kwa kiwango kikubwa katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye tafiti kwa zao la parachichi kuendana na hali halisi ya mabadiliko ya teknolojia. Nakubaliana kabisa na hoja hizi zilizotolewa na Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Neema Mgaya wamechangia kweli, lakini Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (*TARI*) inafanya utafiti wa kuzalisha mbegu pamoja na miche bora ya parachichi na kuisambaza kwa wakulima. Vilevile Serikali imepeleka taarifa muhimu za kisayansi zinazohitajika kwa ajili ya masoko ya parachichi katika nchi

ya China na nchi za Ulaya. Taarifa hizo zimefungua majadiliano kwa lengo la kuweka makubaliano ya kibiashara baina ya Tanzania na nchi hizo. Ni imani yetu kwamba tukishaweka makubaliano yatasaidia sana katika kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinakwenda mbele na tunapata masoko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulitolewa hoja nydingine kwamba kipaumbele kitolewe kupeleka fedha katika Vyuo vya Mafunzo na Taasisi za Utafiti. Hoja hii imechangiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Serikali imekuwa ikiongeza fedha kwa ajili ya utafiti mwaka hadi mwaka na hilo ndio lengo letu kwa sababu utafiti ndio uhai wa kilimo, bila utafiti hakuna kilimo. Katika mwaka 2018/2019, jumla ya Sh.697,905,309 zilitengwa kwa ajili ya ukarabati wa maabara za kibaiolojia na bioteknolojia za *TARI* Tengeru ambapo ilitengewa Sh.399,999,630 na maabara ya kusindika mvinyo ya *TARI* Makutupora ambayo ilitengewa Sh.297,906,300 kupitia *COSTECH*. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara imetenga Sh.9,224,033,150 katika bajeti ya fedha ya maendeleo na matumizi ya kawaida. Aidha, *TARI*/Naliendele imetengewa Sh.5,610,547,100 kwa ajili ya kuimarisha na kuendeleza utafiti wa zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, zipo hoja nydingi ambazo zimetolewa, lakini kulikuwa na hoja kuhusu utafiti wa udongo na kwamba Serikali ikamilishe kwa haraka. Naomba nilitarifu Bunge lako Tukufu na hoja hii imechangiwa na watu wengi sana. Tathmini ya udongo hadi sasa imefanyika katika mikoa 16 kati ya 26 ya Tanzania Bara na baadhi ya ramani zimeshatolewa kwa vipimo vya aina mbalimbali. Tumeshamaliza katika kanda zote kama nilivyoahidi kwenye Bunge la mwezi wa Pili kwamba tunafanya tathmini katika kanda zetu zote kuweza kubaini udongo uliopo na kuangalia virutubishi ambavyo vinakosekana katika ule udongo.

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kazi hii imekamilika na tayari tunayo ramani inayoonesha nchi nzima, ninazo hapa ramani zinaonesha ni

aina gani, udongo wetu una nini, vitu gani vinakosekana, vipo hapa na ramani kubwa tunazo tumeziacha pale chini. Ramani zimekamilika, kwa hiyo tuna uhakika, hii kazi imekamilika lakini tunaendelea sasa kwenda mkoa kwa mkoa ili tukipata mkoa kwa mkoa tutajua mkoa huu unahitaji nini na kinakosekana nini.

Mheshimiwa Spika, lengo la hii yote ni nini? Lengo hasa ni kutaka kujua kwamba wanapotumia mbolea tuweze kuwaambia mbolea ambazo ni sahihi kulingana na mahitaji ya udongo na wakati mwengine watu wanunua mbolea unakuta kwamba labda hiyo mbolea vile virutubisho vilivyopo mle ndani havihitajiki. Kwa hiyo ndio maana tumeamua kwamba kuanzia mwaka huu tunafanya jitihada na wawekezaji ili wajenge kiwanda cha kuchanganyia mbolea. Baada ya utafiti huu tuwe na kiwanda sasa ambacho tumekubaliana kinajengwa pale Dar es Salaam, tunatumia magodauni ya pale Dar es Salaam kichanganywe mbolea yaani ile *blending plant*, tunaweka mwaka huu, ili kusudi wakulima wakisema mahitaji ya udongo wangu yako hivi, basi tunajua mbolea anayohitaji inatakiwa hii na hii. Nina imani kama hilo litafanyika tutaendelea vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhus uzalishaji wa mbegu za mafuta, lakini pia uzalishaji wa mbegu hapa nchini bado hautoshelezi. Nakiri kabisa kwamba tuna changamoto kubwa kwenye uzalishaji wa mbegu tunazozihitaji na mpaka sasa hivi uwezo wa nchi kuzalisha mbegu ni karibu asilimia 64 tu ya mahitaji yote, lakini tumeamua kuweka jitihada na kuweka mikakati ya kutosha kuhakikisha kwamba tunapata mbegu zile ambazo tunazihitaji. Kwa hiyo Serikali imeamua kuwekeza vyta kutosha katika uzalishaji wa mbegu za mafuta ili kujitosheleza kwa mafuta ya kura na ziada kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia Wizara imeanza mkakati wa kundeleza zao la mchikichi unaolenga kuzalisha mbegu bora za michikichi kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2018/2019 mpaka 2021/2022. Katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine

wakiwemo JKT na Magereza itazalishwa miche ya michikichi 5,000,000 kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa zao hilo. Mkakati huu unatekelezwa sambamba na kuwapatia wakulima teknolojia bora za kuongeza thamani kuitia *SIDO*, *TADB*, *CAMARTEC*, *NDC* na *UNIDO*.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa kwamba kwa kweli tunahitaji mbegu zilizo bora na kama nchi lazima tuwekeze kwenye mbegu zilizo bora. Hili tuna imani kabisa tutalifanyia kazi vizuri na nitumie fursa hii kuziomba taasisi zingine hapa tumesema JKT na Magereza lakini nina uhakika taasisi zingine zinaweza zikawekeza kwenye uzalishaji wa mbegu, taasisi binafsi, taasisi za umma hasa wanawekeza lakini bado haitoshi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunahitaji mbegu za kutosha kwa upande wa michikichi? Nchi ya Malaysia ambayo miaka ya nyuma ilichukua mbegu za michikichi kutoka Tanzania inazalisha mafuta, inazalisha mafuta yanayotokana na michikichi kwa wingi sana duniani, lakini mbegu zilitoka kwetu. Sisi wenye ardhi nzuri na ambao tulitoa mbegu, uzalishaji wetu uko chini. Sasa hivi tunatumia zaidi ya bilioni 674 kwa mwaka kuagiza mafuta ya kula, wakati uwezo wa kuzalisha hapa nchini upo, tuna uwezo wa kulima alizeti kwa wingi, tuna uwezo wa kulima michikichi kwa wingi, tuna uwezo wa kulima karanga, tuna uwezo wa kulima mbegu za pamba na nyinginezo, tukazalisha mafuta ya kutosheleza nchi yetu. Kwa nini kila wakati tuagize au tutumie fedha zetu kuagiza nchi za nje wakati sisi tuna uwezo wakuzalisha? Hili ni lazima tulivalie njuga na nitaomba ushirikiano wa Waheshimiwa Wabunge wote tuhakikishe kwa kweli hili tunalisimamia kikamilifu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia pamoja na uzalishaji wa miche ya michikichi Serikali kuitia *TARI* inakamilisha utafiti wa mbegu mpya za alizeti zenyе uwezo wa kutoa mavuno na mafuta mengi, ili kuhakikisha wakulima wanapata mbegu bora kwa gharama nafuu badala ya kuagiza kutoka nchi za nje. Bahati nzuri nimepata maombi mengi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, wananiuliza na wananiomba

mbegu bora, wengine wameomba za michikichi, na wengine wameomba za alizeti.

Mheshimiwa Spika, na mimi niseme tu nitahakikisha wote mnapata hizo mbegu, ili kusudi mwende kulima kwa sababu najua ninyi Waheshimiwa Wabunge ndio wadau wangu wakubwa wa kilimo; na ninyi mkilima ndiyo itakuwa mfano hata kwa wakulima kuja kuiga na kuona namna mnavyolima. Maana nchi hii tumefikia mahali unakuta mtu ana ardhi pale hata kupanda miche miwili ya nyanya pale nyumbani hapandi, halafu tunaagiza ilhali ardhi nzuri na kila kitu tunacho. Hii neeme tuliyopewa na Mungu lazima tuitumie vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, zipo hoja ambazo wajumbe wamechangia. Suala la umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, wamezungumzia sana suala la umwagiliaji; na mimi niungane na ufanuzi mzuri sana alioutoa Naibu Waziri. Nataka niwaambie, katika skimu tulizonazo zote zilizokuwa chini ya umwagiliaji ziko zaidi ya 2,600. Huwezi kupata skimu 10 za mfano zinazofanya kazi, kwa hiyo skimu zote zina matatizo; na sisi tumeangalia ule Muundo wa Tume ya Umwagiliaji tukaona hapa lazima tuifumue. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tumeshaifumua ndiyo maana tumeanza, sasa tunasema wiki hii tunakamilisha muundo mzima na uongozi mpya, na tunawagawia maeneo ya kusimamia. Tunataka kwenye kanda abaki mmoja kwa sababu kwenye kanda hakuna kilimo. Kwenye mkoa wanakuwa wawili, lakini tunataka wale wote, Maafisa Umwagiliaji, ma-engineer wa umwagiliaji waende kwenye halmashauri zetu zinazoshughulika na kilimo wakasimamie skimu kule chini na kila mtu atawekewa malengo ya kuhakikisha kwamba anasimamia. Mimi nina uhakika tukilisimamia vizuri hili litaweza kutatua tatizo letu la miradi mbalimbali ya umwagiliaji ambayo ilikuwa haifanyi vizuri katika nchi yetu, kwa hiyo hili tumeliwekea mkakati wa kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ipo hoja ambayo Waheshimiwa wajumbe pia, wamezungumzia. Wamezungumzia suala la kahawa; na mimi ni mdau wa kahawa, naijua kahawa kwa sababu nimekulia kahawa. Nimefurahi sana mlivyoichangia kahawa, nimeona Mheshimiwa Selasini na Waheshimiwa Wabunge wengi wameichangia sana kahawa.

Mheshimiwa Spika, kahawa lilikuwa ni zao la mfano, lilikuwa linatoa mchango mkubwa sana kwa fedha za kigeni miaka ya nyuma, lakini sasahivi limeshuka uzalishaji, tunazalisha takribani tani elfu 50, sasa hivi tumesema tumezalisha tani elfu 64, lengo tunataka tuzalishe tani elfu 80, hazitoshi. Tumeweka mkakati kwenye uzalishaji, wenzetu wa *TACRI* wakishirikiana na Bodi ya Kahawa tumeamua kuanzisha uzalishaji wa Miche ya Kisasa, ili kuisambaza kwa wakulima mbalimbali na hili tutalisiamamia ili tupate Miche ilio bora ambayo itaongeza uzalishaji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kuna tatizo la bei, wengi wamezungumzia bei, na mimi nimeona kuna tatizo la bei. Mwaka huu nilipoongea na wazalishaji wanasema tunaweza tukapata kahawa safi tani 50,000, *pure coffee*; nimewauliza wanunuzi wanne wakubwa duniani watuambie wanahitaji tani ngapi? Wanahitaji tani 65,000. Kwa hiyo, ina maana mahitaji ni makubwa kuliko tulichozaalisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukasema kama hiyo ndio hali basi tuunde kamati maalum ndani ya Wizara, lakini Wizara inatoa mmoja iwe ni kamati huru, tumechukua Benki Kuu, Wizara ya Fedha na taasisi mbalimbali; tumeunda kamati ili ikutane na wanunuzi wakubwa hawa wajadiliane juu ya bei; wakikubaliana iwe ni kazi ya kuuza tu si tena mara kwenye mnada mara nini na nini. Sisi kwenye mnada tunataka twende tupeleke zile zitakazokuwa zimebaki ambazo zitakua hazijanunuliwa ndio maana Naibu Waziri amesema tunasisitiza *direct selling*, uuzaji wa moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Dunia nzima nchi nyingi zimeenda katika mikataba ya moja kwa moja, Rwanda wamefunga mikataba na Ujerumanî wa miaka kadhaa, na sisi lazima tufike

mahali tusaini mikataba ya mauziano ya muda mrefu, hapo ndipo tutapata ufumbuzi wa changamoto zinazoikabili bei. Si kila mwaka eti tutegemee soko watu wa-*bid* pale, wakilingia kwenye *collusion* bei inakuwa ndogo wakulima hawafaidiki na sisi utaalamu wetu wengine ni mdogo. Kwa hiyo tunafikiri hii timu itafanya kazi vizuri na nina uhakika baada ya wiki mbili watakuwa wamemaliza. Kwa hiyo, katika msimu huu tutatumia njia ya mauzo ya moja kwa moja na zile zitakazobaki ndizo tutazipaleka kwenye minada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ya pili kwenye minada hii, minada ya kahawa, tulichokubaliana tunafanya kwenye kanda. Kanda ya Ziwa utafanyika mnada kule Kagera, Kanda ya Kaskazini watafanyia Moshi, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mbeya, Rukwa, Songwe watafanyia Songwe, na Ruvuma pia kutakuwa na Kanda, tutakuwa na kana nne ambazo mhada itafanyika. Lengo ni kupunguza gharama kwa ananchi za kuhangaika kwenda kupeleka kahawa yao kule Moshi kwa ajili ya kwenda kuuza kwa hiyo; sasa wanunuzi watakwenda kule kwa hiyo, tuna imani itasaidia kupunguza changamoto zinazotokana na zao la kahawa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna pareto, mmezungumza sasahivi zao la pareto ndio nchi pekee inayozalisha. Pamoja na kwamba, tunazalisha kidogo, lakini ndio nchi pekee. Takwimu zimetolewa za bei za pareto, lakini hazikuwa sahihi sana.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema mimi ni kwamba pareto hii ndiyo tunayotaka tuitumie katika uwekezaji wa kuanzisha viwanda vya viuatilifu. Viuatilifu ili vianzishwe vitatumia pareto yetu. Kwa hiyo mimi nina imani hizi jitihada zitasaidia na zitazaa matunda; lakini pia tunahitaji anunuzi wengine. Sasa hivi kuna mnunuzi mmoja, mnunuzi mmoja atashindana na nani? Lazima kuwe na ushindani ndio tunaweza kupata bei nzuri. Kwa hiyo hili tutalifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mkonge. Miaka ya nyuma Tanzania ilikuwa inaongoza kuuza mkonge nchi

za nje, tuliongoza kwa uzalishaji. Sasa hivi tumeshuka tunazalisha kidogo sana. Tumeamua kurudisha heshima ya nchi yetu kuhakikisha tunazalisha mkonge iwezekanavyo. Mashamba ya mkonge yote lazima yafufuliwe na mengine mapya yaanzishwe na changamoto zote tuondokanenazo. Imekuwa ni aibu tunatumia fedha nyingi kuagiza magunia nchi za nje, tunayaleta hapa ilhali tuna uwezo hata wa kutengeneza magunia ya kwetu, lakini pia mahitaji ya mkonge duniani bado ni makubwa. Kwa hiyo tunafikiri nchi yetu lazima irudi kwenyi mstari.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo kuhusu zao la tumbaku. Najua muda hautatosha. Tumbaku ina changamoto nyingi na kuna baadhi ya wanunuizi wako wanne tu wakubwa. Mmoja ametoa tishio kwamba, anakusudia kujiondoa mwakani, hajaingia kwenye mkataba. Najua wananchi wanaolima zao la tumbaku wamepata mfadhaiko kidogo. Hata hivyo nataka niwahakikishie kwamba Serikali yenu inafanya majadiliano na huyu mnunuzi, lakini pia tunatafuta wanunuizi wengine. Sasa hivi tumekwenda China tunafanya majadiliano. Tumewaalika waje kuangalia, lakini pia wao wanasema wana mbegu wanazozitaka. Tunataka watuletee hizo zifanyie majoribio waanje kulima. Pia tunaangalia nchi nyingine zinazohitaji hiyo tumbaku. Kwa hiyo pamoja na mambo mengine mimi nina imani mikakati tuliyoiweka itasaidia sana kutatua hili tatizo.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja imetolewa kuhusiana na Maafisa Ugani. Maafisa Ugani kweli ni changamoto na mahitaji ni makubwa. Maafisa Ugani kwa mujibu wa muundo wetu wa Serikali wako chini ya TAMISEMI, wale ndio wanayisimamia kilimo kule. Sisi kama Wizara ya Kilimo tunatengeneza Sera, tunatengeneza taratibu na miongozo ya kilimo, lakini wanaoenda kusimamia ni wale. Hata hivyo kuna vijiji havina, lakini hata vijiji vingine vina Maafisa Ugani ambako Maafisa Ugani wengine wanakaa bila kufanya kazi. Kwa hiyo sasa hivi kama Serikali tunakaa pamoja na TAMISEMI tunakuja na utaratibu mpya wa kuwasainisha mikataba ya namna ya kusimamia kilimo katika maeneo ambayo wanayisimamia. Kuhusu hoja kuongeza Maafisa Ugani hii

tunakubaliananayo tutaendelea kuifanyia kazi kadiri bajeti itakavyoruhusu tutaweza kuendelea kuajiri hao wakulima.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala moja la msingi. Tumeanzisha usajili wa wakulima. Lengo la usajili wa wakulima ni nini?

Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyosema wakati nawasilisha makadirio ya bajeti ya Wizara, tumeanza zoezi la usajili wa wakulima wote nchini. Lengo la zoezi hili ni kutaka kutambua walipo, wanalima nini? Wana maeneo yenye ukubwa kiasi gani? Wanahitaji pembejeo za namna gani? Wanahitaji zana gani? Wanahitaji msaada gani? Tukiwatambua hawa wakulima ndio tutaweza kuwahudumia; unamhudumiae mtu ambaye hujui? Tunataka kila zao tujue kuna wakulima wangapi? Wanalima eneo kiasi gani? Kwa hiyo, hayo ndio tumeyaanzisha.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa; na kuna mmoja hapa amesema takwimu henzieleweki, nini na nini; naomba niseme, mpaka sasa hivi mazao ya kipaumble ambayo tayari tueshasajili, tumesajili wakulima 1,669,699, hao ndio tunaotegemea kuwasajili. Tuliowasajili ni 1,464,827 ambao ni asilimia 87.3 katika mazao nane ya msingi, yaani kahawa, chai, kosroho, miwa, tumbaku, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwamba mambo yote mengine tutawajibu Waheshimiwa Wabunge, hoja najua ni nyingi, lakini nitumie fursa hii, nawashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kutoa ufanuzi wa baadhi ya maeneo machache kuhusu hoja hii ya Wizara ya Kilimo. Baada ya kusema hayo niwaombe Wabunge kwa heshima kubwa kabisa mkiwa wadau wa chakula, mkiwa wadau wa kilimo, wote kwa pamoja muipitishe bajeti yangu bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Umejitahidi sana kuititia ushauri mbalimbali ambao ultolewa na Waheshimiwa Wabunge na wewe kama mtoa hoja umejaribu kuchambua na kutupatia mwanga wa Wizara yako inaelekea wapi katika kukiangalia kilimo cha Tanzania. Tunakushukuru sana, tunajua muda hautoshi lakini umejitahidi sana kuyapitia maeneo mengi hasa yale yaliyolalamikiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo.

Sasa Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**  
Kamati ya Matumizi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Waheshimiwa Wabunge sasa tunaendelea, Katibu!

#### **KAMATI YA MATUMIZI**

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitabu cha Pili.

**MWENYEKITI:** Kitabu cha Pili.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**  
Wizara ya Kilimo, Fungu 43, ukurasa 252.

#### **KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

##### **Fungu 43 – Wizara ya Kilimo**

Kif. 1001 – *Adminstration and Human  
Resources Management.....Sh. 6,121,823,000*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa kama ilivyo ada kwa sababu ni eneo lenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri kwa hiyo, tunaanza na yale mambo yetu ya kisera na tayari ninayo

orodha hapa ya Wabunge kutoka pande zote. Orodha hii nimeletewa na ma-Chief Whip wahusika, kwa hiyo tutaendelea.

Tunaanza na Mheshimiwa Dua William Nkurua.

**MHE. DUA W. NKURUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika sera yetu ya kuendeleza mazao matano makubwa ya kibiashara yakiwemo pamba, korosho, kahawa, tumbaku, n.k, lengo la Serikali ni kuendeleza haya mazao na ili uendeleze lazima upange mikakati thabiti ambayo mazao haya yataweza kusonga mbele. Sasa katika mkakati huu nikijaribu kuliangalia zao moja la korosho zao hili hivi tunavyoongea wananchi wapo katika maandalizi ya mwisho kabisa ya kuanza uzalishaji wa zao la korosho. Hata hivyo tunaenda huko wakati bado wakulima kadhaa wanadai pesa zaidi ya shillingi billioni 100 wanadai. Sasa tunaenda kwenye uzalishaji lakini wananchi wanadai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri bado nataka maelezo ya kina nijue ni mkakati gani wa ziada kwa sababu tumeshapokea taarifa na matamko mengi sana. Nataka mkakati wa ziada ambao wananchi wangu au wakulima wa korosho watakuwa na matumaini ni lini Serikali itamaliza deni hili la shillingi billioni 100 na zaidi? Lakini pia kuna madeni ya nyuma ambayo wakulima wale walikuwa wanadai miaka ya nyuma. Sasa yale ya nyuma na haya ya mwaka huu nataka kujua ni lini Serikali itaweza kukamilisha? Kama Serikali haitanipa majibu mazuri, Mheshimiwa Waziri hapo, basi mimi nimejijandaa kukamata shillingi. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dua kwa kifupi hasa jambo la uafanuzi sasa, moja kwa moja ni jambo gani?

**MHE. DUA W. NKURUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya korosho, ili tuende kuzalisha vizuri. Muda...

**MWENYEKITI:** Endelea kama unaendelea, bado una dakika moja.

**MHE. DUA W. NKURUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shida yangu nataka tujue ni lini wananchi hawa watapata hizi pesa ili waendane sambamba na uzalishaji kwa sababu muda umeshafika. Kwa hiyo nataka maelezo mazuri yanayojitosheleza. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nakushukuru sana. Ufanuzi kuhusu jambo hilo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, tafadhalii.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana hoja aliyoitoa Mheshimiwa Mbunge Dua. Kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya awali, kwamba kama Serikali hata sisi wenyewe tumejipanga vizuri. Unajua kama tulikotoka Serikali kutokana na kuona masoko hayako vizuri ndiyo maana ikaamua kwamba sasa ichukue jukumu na kuiagiza Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kununua na kuiagiza Benki ya Kilimo kutoa fedha. Mpaka sasahivi tumeshalipa bilioni 624 sasa kamebaki kamkia. Najua wakulima wanateseka na mimi nisingependa kwamba waendelee kuteseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba tunaendelea na majadiliano ndani ya Serikali, lakini tunajadiliana pia na wanunuvi; nina uhakika wiki mbili haziwezi kwisha tutakuwa tumeshafanya kitu kinachoeleweka vizuri kabisa. Namuomba mjumbe asikamate shilingi yangu, ili tuende tukawahudumie tukimaliza hii bajeti, tuende tukakae tukatafute hizo hela na tuiagize Benki ya Kilimo hapo ikiwezekana hata kesho wakope hata ikiwezekana wakope wakamalize hako kamkia kalikobaki kusudi wananchi wetu waendelee kupata malipo, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Asante sana. Mheshimiwa Dua maana yake umeridhika, naendelea.

**MHE. DUA W. NKURUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu atoe maelezo vizuri kidogo. Hajaji-*committ*, Serikali hajatoa maelezo, kidogo tu. Sijaridhika kidogo, aendelee kidogo, ili nielewe sijamuelewa vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dua hilo litakuwa gumu sana kulikubalia kwa sababu, ameji-*committ* amesema kwamba wameshalipa Serikali hadi sasa bilioni 624 ambayo ni hela nydingi. Iliyobakia ni fedha kidogo na amesema katika wiki mbili watajitahidi kwamba wawe wameshalipa na kabla hata ya hizo wiki mbili wanaielekeza Benki ya Kilimo ianze kabisa hata kama ni kukopa mahali waendelee kumalizia huo mkia uliobaki. Ahsante sana, nakushukuru.

Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Mwaka huu mwanzoni Serikali katika kutafuta wanunuvi wa zao la korosho baada ya maamuzi ya mwaka jana kwamba Serikali isimamie basi aliweza kupatikana mnunuzi kutoka nchi jirani ya Kenya, Kampuni inaitwa *Indo Power* na Serikali illingia mkataba. Hata hivyo kutokana na ku-*breach* ile *contract* na sababu mbalimbali ambazo huwa zinasababisha *contract* inakuwa *breached* Serikali iliweza kuvunja mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunajua kwamba, zao la korosho ni moja ya mazao ambayo yanasaidia kuweka *balance of payment*ya nchi yetu ile *unfavourable* kuendelea kupungua; na jinsi tunavyoenda ukiangalia *trend* yake tunaenda *positive*, inaenda inashuka. Sasa hatujapata fedha za kigeni na bado katika *indication* za uchumi tunakuwa kidogo tunaonekana tumeyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kupata maelezo ya Serikali, na yasiponitosheleza nitawenza kukamata shilingi. Nini azma ya hizi korosho ambazo zitaenda katika kutuletea fedha za kigeni zitapatiwa mnunuzi ni lini? Na je, hali hiyo itakuwa *solved* ndani ya muda gani? Nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kupata maelezo ya Serikali na yasiponitosheleza nitawenza kukamata shilingi. Nini azma ya hizi korosho ambazo zitaenda katika kutuletea fedha za kigeni zikapatiwa mnunuzi ni lini na je, hali hiyo itakuwa *solved* ndani ya muda gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, hatima ya korosho zilizopo katika maghala zinanunuliwa lini, ufanuzi.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tulitoa taarifa hapo awali, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbogo kwamba Serikali ipo katika hatua za mwisho za mchakato wa kuza korosho na huu mchakato upo katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni ubanguaji ambao unaendelea wa tani zaidi ya 2,000 na hadi jana tunazo korosho karanga tani 460 ambazo zipo tayari kwa ajili ya kuuzwa, halafu kuna korosho ghafi tani 223,000 hivi, ambazo tunatarajia mpaka katikati ya mwezi Juni zitakuwa zimeuzwa zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *commitment* ambayo tunaitoa na naomba sana Bunge lako Tukufu lisitishwe na kusitisha mkataba wa *Indo Power Solutions* ile ya Kenya kwa sababu hiyo ni kampuni moja tu, lakini tunayo makampuni sita ambayo yameomba kununua korosho, tupo katika hatua za mwisho za kumaliziana nao utaratibu. Kampuni ambayo ni kubwa kati ya hayo sita ni kampuni ambayo ililetwa wachunguzi wake wiki iliyopita, wamekwenda Mtwara, Lindi, Pwani na maeneo mengine yenye korosho, wamefanya uchunguzi wao na wamejiridhisha kuhusu *qualityya* korosho, kwamba korosho hizo bado zipo katika kiwango bora. Kama nilivyosema hadi tarehe 15 nwezi Juni tutakuwa tumeuza korosho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hiyo ndiyo *commitment* Mheshimiwa Mbunge alikua anaitaka. Nashukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Richard.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyasikiliza maelezo ya upande wa Serikali yametolewa na Waziri wa Viwanda na Biashara, tumeona *commitment*

ya korosho ghafi, zinazobanguliwa lakini bado kuna hizo ghafi ambazo ndiyo nyigi sana kwa sababu *Indo Power* mkataba ulikuwa karibuni tani 100,000 zenyé thamani ya karibuni dola 180 milioni. Sasa ningeomba atueleze na aeleze Bunge lako Tukufu, je, haya makampuni sita ni yapi ambayo ina mwelekeo wa kusaini *MoU (memorandum)*?

**MWENYEKITI:** Napata tabu kidogo kuliruhusu hilo swalí, lakini kama Waziri ana majibu, kwa sababu moja tu kwamba wakati mwingine mambo ya mikataba ya makampuni hasa inapokuwa bado haijawa *finalized* na huenda ikawa na ushindani inakuwa siri kidogo, lakini kama Serikali wanaona ni jambo lipo kawaida, mnaweza mkaendelea; Viwanda na Biashara. (*Makofí*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo umegusia, ni kweli kwamba kwanza tani zote zipo kwa sababu ule mkataba wa Kampuni ya *Indo Power* tumeufuta, haupo. Kwa hiyo, tani zote karibu 223,000 zote zipo na makampuni sita haya yamesaini mkataba wa awali ambapo endapo kuna kampuni italipa, hapo ndiyo tutakuwa tumekamilisha mkataba na ndiyo tutaitangaza. Kwa hiyo, kwa sasa hivi kulingana na ushindani wa kibashara ulivyo kama ulivygusia, siyo vizuri kutangaza kwamba kampuni fulani imesaini mkataba wa awali. Ahsante sana. (*Makofí*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Richard. Mheshimiwa Paschal Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba ufanuzi wa Serikali kuhusu mkakati wa Serikali kuhusu yale mazao ya kimkakati ambayo kwa maana ya korosho, tumbaku, kahawa, pamba pamoja na chai.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhusu kutafuta masoko ya haya mazao ya kimkakati kwa sababu ukiangalia mazao hayo ndiyo ambayo yanaingiza fedha nyigi sana za kigeni kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona ukiangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimejaribu kuititia ukurasa ule wa 90, ameelezea kwa ufupi sana pale yaani hata ukurasa mzima haujawkisha katika maelezo yake, hajatueleza vizuri, ameeleza juu juu sana. Sasa naomba suala hili kama halitaweweza kutolewa ufanuzi vizuri, nitashika mshahara wa Waziri ili mwisho wa siku tuweze kujua Serikali inafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba mkakati wa Serikali ni upi kwenye mazao haya ya kimkakati ambayo ni matano ambayo ni muhimu sana kuweza kuliingizia Taifa letu fedha za kigeni.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Haonga anataka kujua mkakati wa Serikali wa haya mazao ya kimkakati. Majibu ni kwamba *marketing* ya haya masoko inabidi iwe *case by case*. Kwa mfano, kama Mheshimiwa Waziri alivyosema kwa upande wa kahawa, tayari tumeshakaa na wanunuzi wakubwa duniani na tumeunda Kamati Maalum kwa ajili ya kukaa nao na kuweka utaratibu mzuri ambao tutauza kahawa kuititia *direct export*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye chai, mkakati wa Serikali kwa misimu iliyopita, chai ya Tanzania ilikuwa inanadiwa Mombasa, lakini mkakati wa Serikali sasa ni kuhakikisha chai inanadiwa hapa hapa nchini ili hata kama ni mambo ya *branding*, chai ya Tanzania inapoenda kwenye nchi mbalimbali duniani, *brand* ya Tanzania tuweze kuitangaza. Kwa hiyo, mazao ya kimkakati lazima twende *case by case* kwa sababu *nature* ya kila zao na uhitaji wa masoko unatofautiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nipende kumhakikisha Mheshimiwa Haonga, Serikali imejipanga vizuri kuhakikisha kila zao la kimkakati tunakuwa na mkakati mzuri

wa kuhakikisha tunapata masoko ya uhakika kwa ajili ya wakulima wetu, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga umeridhika tunaendelea?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba naona Serikali hajajipanga vizuri kwenye jambo hili na kwa nia njema kabisa kwa sababu tumeona karibu mazao yote, kahawa amezungumza Mbunge hapa juzi alipokuwa anachangia Mheshimiwa Heche, kahawa miaka ya nyuma hapo ilikuwa na bei nzuri, lakini mwaka huu imekuwa na bei mbaya kuliko wakati mwingine wowote ule. Korosho ndiyo zao pekee tulikuwa tunategemea na lilikuwa kidogo msimu uliopita tuliweza kuza kwa bei nzuri, Serikali imevuruga hali imekuwa ni mbaya kuliko wakati mwingine wowote ule. Ukienda kwenye mazao mengine kama chai, hali bado ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wabunge waniunge mkono kwenye jambo hili kwa sababu hakika hapa ndipo Watanzania wengi wanategemea kwenye mazao haya. Kwa hiyo, naomba Wabunge waniunge mkono kwenye jambo hili, tuweze kujadili.

**MWENYEKITI:** Sasa wakuunge mkono kitu gani yaani?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Kuhusu mikakati ya Serikali kwa sababu bado haijawekwa vizuri namna gani Serikali itaenda kutafuta masoko, *commitment* ya Serikali kutafuta masoko kwenye mazao haya ya kimkakati...

**MWENYEKITI:** Si ndio hii wametoa sasa?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maelezo hayaridhishi, naomba tujadili.

**MWENYEKITI:** Kwani wewe ulipenda maelezo gani?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo haya hayaridhishi. Naomba Wabunge wote wa pande zote mbili mniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Unajua mambo mengine ni mtihani kidogo maana yake sasa kama huridhiki ultaka uambibiwe nini yaani tabu kidogo kujua...

**MBUNGE FULANI:** Tutafafanua.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Wabunge hapa watajadili, wataeleza, Serikali ipo itatoa majibu. Naomba kwenye hili naomba kidogo usiisemee Serikali, naona kama kidogo unawakingia kifua. Wabunge tujadili ni jambo kubwa sana hili ambalo kwa kweli...

**MWENYEKITI:** Unajua Haonga ili kitu kiwe ni lazima Mwenyekiti aelewé, siyo tu suala la kuhamasisha watu wasimame au nini na lazima hao wanaosimama wawe wanaelewéka wanataka kusema nini. Maana yake hoja yako yaani iko, umetaka maelezo ambayo ni ya jumla ya kisera, umeyapata na wamekwambia ni *case by case* na kadhalika, lakini basi kwa wito wako japo sikukuelewa, nitatoa nafasi hao wajadili basi. Sasa sjui wanajadili yaani, haya tuwasikie; nani wa kwanza kusema anasikika sana.

**MBUNGE FULANI:** Hajaungwa mkono.

**MBUNGE FULANI:** Imeungwa.

**MWENYEKITI:** Haya tunaanza na Mheshimiwa Ruth Mollel, aah ulisimama kuunga mkono. Lucy Magereli hujaongea tangu asubuhi, wengine kaeni nimeshawaona, sio Lucy Magereli pale, ongea basi.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Haonga, majibu ya Mheshimiwa Waziri ni *vague*. Mheshimiwa Waziri awe mweli mbele yake na mbele ya Mungu, tangu mwaka jana hesabu hizo za kutuambia kwamba malipo ya

korosho yamebakia kimkia, ndicho ameendelea kukisema mpaka leo. Kwenye Kamati alituahidi angebandika majina, lakini hayajawahi kubandikwa kokote. Mazao ya mkakati...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Magereli kaa chini...

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** ...unavyozungumzia kwa ujumla, si naendelea na korosho limo...

**MWENYEKITI:** Kaa chini. (*Kicheko*)

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na hoja yangu sijamaliza.

**MWENYEKITI:** Hapana, kaa chini Mheshimiwa Lucy Magereli. (*Kicheko*)

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uendelezaji si ni pamoja na kuza na kulipa?

**MWENYEKITI:** Naomba ukae, yaani upo nje ya uwanja kabisa, hukuwa na sisi humu ndani. Kwa hiyo, hilo unalijadili ni lingine kabisa, lilikuwa la Mheshimiwa Mbogo. Sasa wewe unamuunga mkono Mheshimiwa Mbogo, ndiyo maana nikasema kaa chini tu, maana yake *issue* ya Mheshimiwa Haonga ni nyingine kabisa. Kwa hiyo, sikuonei dada yangu, uko kwenye suala lingine tofauti kabisa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba ndugu yangu Mheshimiwa Haonga, mambo mengine wakati fulani tuwe tunaangalia Bunge hili, kama hoja ipo kwenye mambo ya kisiaza sana tuwe tunaachana nayo. Ameuliza, Waziri amejieleza vizuri sana juu ya mazao haya, ameелеza toka alikuwa ameweka kwenye bajeti, ameingia hapa ameelleza. Waziri mwenyewe, Naibu na Waziri wake wageni, wamejieleza vya kutosha, nongwa ya nini mzee, amrudishie shilingi. Mazao yote yamepangwa kwa kadri ya mpango wao, pamba imepangwa, sisi tunalima

pamba; tumbaku imepangwa na kila kitu kimepangwa, maelezo yote yameleezwa, anatafuta nini huyu mzee? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kinachojadiliwa hapa ni suala la Serikali kuangalia masuala mazima ya mazao ya kimkakati, hayo mengine huko yamepita. Mheshimiwa Haonga hapa anachangia suala linalohusu kahawa pamoja na chai ndiyo yanayopatikana kwenye maeneo yake lakini ni sera kwa ujumla.

Sasa tunataka Waziri, pamoja na haya maneno anayoyaleta kwa sababu maneno kama hayo wameyaongea pia kwenye mazao mengine ndiyo ambayo sasa hivi yanaonesha matatizo na Serikali wamekuwa wakilja hapa ndani na kauli nydingi kwa sababu wameshindwa kupata suluhu ya kuweza kutatua hayo matatizo waliyoyasababisha huko nyuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anachokihitaji Mheshimiwa Haonga ni mkakati wa moja kwa moja, siyo mpaka Rais aje kuingia wakati mambo yameharibika katikati watashindwa kufika nayo mwisho. Sasa tunachotaka Waziri atueleze mkakati ni mipango, wataanzia hapa, watafika mpaka hapa na watakwendwa mpaka kule. Kama Wizara tunajua wana Maafisa Mipango wao kule, watuambie wamejipangaje kwenye chai na kahawa?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana dakika zako mbili zimekwisha. Kwa hiyo, ni mkakati wa kahawa na chai.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Jamani ndicho alichosema yule bwana, mimi nasikia vizuri; unajua ndiyo huwa tunakosana hapo hapo. Amesema Mheshimiwa Mwambe kwamba mazao ya Haonga ambayo ndiyo ye ye ana *interest* nayo zaidi ni

kahawa na chai, kwa hiyo wanafafanua. Hivi Mheshimiwa Heche, aliyeongea si huyo hapo Mwambe hapo nyuma na mimi si ndiyo namsikiliza vizuri?

**MBUNGE FULANI:** Hoja ni ya Haonga.

**MWENYEKITI:** Nasema kahawa na chai, vinginevyo nitakuuliza na karanga, sisi tunalima uwele hapa, utamaliza mazao ya Tanzania yote, haiwezekani. Kahawa, chai, tunaendelea.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kutoa maelezo kidogo kuhusiana na mkakati kwanza kama alivyosema Naibu Waziri kwamba tumejipanga katika mazao ya kimkakati vizuri kabisa. Moja ya mikakati tuliyonayo, nimeeleza wakati nahitimisha kwamba tunaangalia uwezekano sasa hivi wa kungia mikataba katika nchi na nchi ili kusudi tukiingia, kuna nchi zimesaini mikataba hata ya miaka 20, huo ni mkakati wa kwanza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa pili, tunaangalia kila zao namna tunavyoweza kujenga viwanda ili kuongeza thamani, ukiongeza thamani tutapata fedha za kutosha. Mkakati wa tatu, nimesema tumeanzisha Kitengo cha Masoko, cha kwenda kuhakikisha kwamba kinaangalia masoko yote ili kuweza kuhakikisha kwamba hayo masoko sasa tunaunganisha na wakulima wanaozalisha hayo mazao na ndiyo maana tumekuja na suala la usajili wa wakulima ili tujue wanachozalisha, tuwaambie masoko yapo wapi kwa mtandao, kwa hiyo, mikakati ipo mingi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri mdogo wangu Mheshimiwa Haonga anaona mikakati tuliyonayo. Inawezekana kitabu hakitoshelezi, lakini tukikaa mimi na wewe ninaweza nikakwambia mikakati hata 100, iko mingi na tupo tayari kuitekeleza. Naomba tu aiachie shilingi yangu, tuendelee kufanya kazi. Ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, narudi kwako Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hasunga anafahamu na najua ni mkulima, hata mimi ni mkulima. Hili jambo bado Serikali inapozungumza kwamba mikataba ya kuuza moja kwa moja kwa mfano kwenye zao la kahawa, kuuza moja kwa moja (*direct export*) ilikuwepo muda mrefu sana, hawataanza sasa hivi, ilishaanza tayari lakini kahawa ndiyo imekuwa bei mbaya kuliko wakati mwingine wowote ule na hii ilikuwepo muda mrefu. Jambo la kusema kwamba usajili wa wakulima kujua wanachozalisha, hivi ni kweli kwamba Serikali hii ilikuwa hajui wakulima wetu wanazalisha kitu gani hadi sasa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona hata wewe ukipima vizuri unaona kwamba Serikali yaani *commitment* haitoshi kabisa. Kwa hiyo, naomba kwa haya niliyozungumza na kwa sababu tunaipenda nchi yetu kwa nia njema kabisa wala siyo kumkomoa mtu, naomba kura ziweze kuamua; uweze kuhoji najua kwamba inawezekana wakashinda kwa sababu ni wengi, lakini lengo hapa nataka tuingie kwenye *records* uweze kuhoji kuhusu jambo hili. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Hapo sasa Haonga nahoji kitu gani? Hata kama tunahoji, tutakuwa tunahoji nini sasa hapo? Inanipa tabu, kutana na ndugu yako muongee baada ya hapa kuliko *kuli-subject* Bunge kuamua kitu ambacho yaani hata hakieleweki ni kitu gani *in particular* watu watakuwa wanapigia kura. Huenda una mawazo mazuri sana kuhusiana na mikakati namna ya kuiboresha, nashauri Waziri yupo na wewe, wote mnatoka Mbeya huko, pigeni hata kile Kinyiha kidogo mtaelewana tu, mkikosa kuelewana yupo Mbilinyi hapa atawaweka sawasawa; ninyi ndugu moja, lakini umesikika hoja yako na mimi naamini Mheshimiwa Waziri ameisikia vizuri, ni hoja ya msingi.

Tunaendelea na Mheshimiwa Ahmed Katani, halafu Mheshimiwa Jitu Soni jiandae.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi kutoka kwa Waziri japo nimesikia wakati anatoa maelezo juu ya ushuru wa halmashauri na kwa sisi

wakulima wa korosho kwa asilimia 85, mambo mengi tunaendesha kutokana na ushuru wa halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kupata *commitment* ya Serikali pamoja na maelezo ambayo yamesema kwamba hatupati hizo fedha lakini ni jambo ambalo lipo kisheria, Serikali inatuambiaje kwa sababu mfano mdogo mzuri, ushuru wa halmashauri tunazosema ndiyo zinalipa posho za Madiwani, ushuru wa Halmashauri tunazozungumza kwa kwetu Tandahimba liliyyokuja suala la madawati, ndiyo zimetengeneza madawati, lakini hata vinapotokea vimbunga hivi au maafa, ushuru wa halmashauri mara nyingi ndiyo zinatumika. Sasa leo unaposema kwamba halmashauri haziwezi kupata ushuru, kidogo inanipa shida. Sasa nataka kupata maelezo ya Serikali kuhusu suala la ushuru wa halmashauri hizi na kama sikupata majibu yanayoridhisha basi nakusudia kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Hilo majibu yake Mheshimiwa Katani si liko wazi kabisa, serikali ilishasema hakuna; Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika majibu yake ya msingi, Serikali nchi hii ipo moja tu, ni Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, ipo Serikali Kuu na zipo Serikali za Halmashauri.

Kwa hiyo ule mzigo ambao ulikusanywa kupitia Bodi ya Mazao Mchanganyiko ulikusanywa na taasisi ya Serikali, kwa hiyo si jambo rahisi, haiwezekani kwamba Serikali moja au Serikali hiyohoyo ikajilipa yenyewe, yaani utoe mfuko huu kulipa mfuko huu, hapana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshakushauri Mheshimiwa Mjumbe, tunaomba uturudishie shilingi ili tujipange vizuri kuwa mwakani halmashauri zisimamie vizuri zao hili, pamoja na vyama vya ushirika ili na wanunuzi binafsi waje wanunue, wataendelea kupata mapato yao na mfumo utafanya kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani ameridhika, tunaendelea. Ndiyo! Serikali ileile, halmashauri Serikali Kubwa ndio hawahawa. Ahsante sana, nakushukuru sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Jitu Soni, nilishakutaja.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipaye ufanuzi wa ziada; mimi katika mchango wangu niliomba Chuo Kikuu cha Sokoine, chuo pekee cha kilimo ambacho kinatambulika hapa nchini na hata kimataifa, nilishauri na niliomba kwamba chuo hicho sasa kiweze kurudishwa badala ya kuwa chini ya Wizara ya Elimu kirudi chini ya Wizara ya Kilimo ambapo kitakuwa kinasimamiwa vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Wizara ya Elimu inafanya vizuri lakini wao vyuo vyote wanaangalia kama sawa na wanaangalia kwa usawa kama mama na baba na watoto wao nyumbani. Lakini chuo hiki kina mahitaji maalum, kikiwa chini ya Wizara ya Kilimo nina uhakika kwamba watakiangalia vizuri zaidi na yale mahitaji maalum watakuwa wanapata na wataalam wa pale wote wanaotoka bado wanakwenda kusaidia Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo ninaomba *commitment* ya Serikali; je, ni lini sasa mtafikiria na mtafanya mchakato wa kukirudisha kiwe chini ya Wizara ya Kilimo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama majibu hayatakuwa vizuri basi ntaomba na wenzangu wachangie ili Serikali ione umuhimu wa chuo hicho kuwa chini ya Wizara ya Kilimo, kwa hiyo ntaomba kuondoa shilingi kama majibu ya Wizara yatakuwa si ya uhakika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jitu, hujatuambia hata sababu basi angalau tuelewe hoja yako msingi wake ni nini. Kwa sababu kile chuo kina masomo mengi, pamoja na hayo ya kilimo. Kwa mfano watu wa *forestry* wanamaliza pale, watu wa *forestry* hawako kilimo; kuna watu wa *wildlife*

wanamaliza pale, hawako kilimo; kuna watu wa *nutrition*, hawako kilimo etc. (*Makofii*)

Kwa hiyo kule Elimu kilipo ndiyo hao wote wana-fit, na vyuo vingine vinavyofanana na hiki. Sasa sababu za kwako wewe za kukitoa pale kikiwa kilimo, au kiwe cha kilimo peke yake unavyowaza hawa wengine watolewe au inakuwaje?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimependa kirudi Wizara ya Kilimo kwa sababu hata hayo mengine uliyoyataja, kwa mfao *nutrition*, *forestry* inaitwa *agroforestry* bado ni kilimo; ukija kwenye masuala ya mifugo pia huko zamani Wizara ilikuwa ni moja chini ya Wizara ya Kilimo na Mifugo. Yote haya sisi tukzungumzia kilimo, yaani kilimo, mifugo na uvuvi. Kwa hiyo wanaosoma pale *nutrition* pia, *animal nutrition* na hayo mengine yote bado yanalenga hukohuko kwenye kuzalisha wataalam bora ambao watakuwa wanasaidia Wizara ya Kilimo kwenye *production*, kwenye *value chain* nzima...

**MWENYEKITI:** *Veterinary science?*

**MHE. JITU V. SONI:** Naam?

**MWENYEKITI:** *Veterinary science?*

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yote bado yanarudi palepale kwamba kwenye kilimo hiyo *value chain* nzima, mnyororo wa thamani unahitajika kuwa chini ya watu ambao wanaelewa vizuri zaidi na wao watakuwa wanaisimamia kwa ukaribu kwa sababu hata wale wa chuo - mimi nilikuwa Mjumbe wa Bodi pale kwa miaka mitano, na huko nyuma pia tulishapendekeza kwamba iwe hivyo ili ipate kulelewa vizuri zaidi chini ya Wizara hiyo ya Kilimo.

**MWENYEKITI:** Niwaachie Serikali wenye waeleze lakini tunapata taabu kidogo; Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza nichukue nafasi hii kusema kwamba umeliweka vizuri, yaani kile chuo kinatoa elimu mbalimbali; zipo za mifugo, kilimo, misitu mpaka na uvuvi. Na kwa mujibu wa sera masuala ya elimu yote yako chini ya Wizara ya Elimu na mpaka sasa hatujaona tatizo, tunashirikiana vizuri ndani ya Serikali. Kazi ya elimu ni kuwapa elimu wataalam, sisi tunakwenda kuwatumia wataalam wale kwenye Sekta ya Kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikushauri tu Mheshimiwa Mbunge, tuachie hiyo shilingi, mambo ndani ya Serikali yanakwenda vizuri, hivi vyuo ni vizuri vikawa chini ya Wizara ya Elimu kwa ajili ya kutuivishia wataalam walioiva baadaye waje watumike kwenye Sekta ya Kilimo na sekta zingine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jitu.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi ninaomba suala hili lijadiliwe kwa mapana kwa sababu tukizungumza hiyo ya kilimo, na inafundisha vitu vingi, jina lenyewe *Sokoine University of Agriculture*, sasa tutakapoanza kuingiza, sasa hivi wameanza na mitaala mingine mpaka *education*, ambapo tunaondoka huko tulikotakiwa kwenda, inatakiwa iwe *center of excellence* kwenye masuala hayo ya kilimo na mambo mengine yote ambayo yanahusiana kwa ujumla na kilimo, iwe ni *agroforestry*, iwe ni hayo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na bado tunavyo vyuo vingine, kwa mfano kwenye afya chuo kimerudishwa Wizara ya Afya na kuondolewa Wizara ya Elimu ambapo pia wanaweza kufanya kazi kwa ukaribu na kwa pamoja. Kwa hiyo ni jambo ningependa wengine wachangie maoni ili Serikali ione umuhimu wa kuiweka kwa nia njema iwe chini ya Wizara ya Kilimo; na nina uhakika watafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja wenzangu waniunge mkono ili lijadiliwe.

**MWENYEKITI:** Pole sana. Kajipange tena mzee.  
(*Kicheko*)

Jipange tena Mheshimiwa Jitu, najua wewe mpambe wa kilimo lakini sasa jipange tena vizuri zaidi, wakati mwingine.

Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, halafu Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa, Mheshimiwa Cosato Chumi utamalizia.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Wakati nikichangia niliongelea suala la umwagiliaji. Suala la umwagiliaji tulilivalia njuga kweli mpaka tukaiondoa kutoka kwenye Wizara ya Maji kwenda kwenye Wizara ya Kilimo na kwa kweli ukiangalia kitabu hiki cha Waziri, nimeangalia sehemu tatu, kwa kweli kilichoongelewa hakiko *convincing* kuona kwamba hii sekta ya kilimo imeona umwagiliaji ni jambo muhimu kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo kuna mfano mzuri kutoka Wilaya yangu ya Hanang ambapo tulikuwa tumeomba bwawa ambalo linakusanya maji ya Mlima Hanang hajalisemea jambo lolote. Ninaomba kusikia anasemaje, mkakati wenu unakuwa mpya kwa sababu kulikuwa na mikakati hata huko nyuma na Serikali ni ileile, sasa mnaanza upya, je, mahitaji ya umwagiliaji yatangoja mpaka ninyi mkakati wenu uwe tayari, kwa kweli namuomba Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niliona kwamba una uwezo lakini kwa kweli mlichoandika na ulichoongelea bado halitupi sisi imani kwamba tumelifanyia kazi mpaka tukaweka hii sekta au Tume ya Umwagiliaji chini yako na mnatuhidi tu kwamba mnaifanyia mkakati, haitoshi. Mwaka ujao bado tunahitaji umwagiliaji, naomba utoe mfano mzuri kutokana na Bwawa la Gidhababieg ambalo kila Waziri ameliongelea isipokuwa wewe ndani ya Bunge hili wakati wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na usipotoa basi na mimi niseme kuna wengi amba mabwawa yao hayajafanyiwa

kazi watasimama. Lakini ukitupa maelezo yenye *commitment* sina sababu ya kukusumbua, mimi siko hapa kukusumbua wewe, mimi niko hapa kupata Bwawa la Gidahababie, lakini kuongelea mabwawa yote kwa sababu tulifanya kazi, *committee* ya kilimo ilifanya kila linalowezekana...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** ...kuhamisha hii Tume ya Umwagiliaji kwenda kwenye Wizara yako.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Umwagiliaji maji yanapita hivihivi tu, hata ukitoka Morogoro kuja Gairo kuelekea Kongwa pale maji yanayopita Pandambili, Kongwa, Kibaigwa, Mtanana, ni mengi kwelikweli, tunahitaji mabwawa makubwa pale; ufanuzi kuhusu umwagiliaji Tanzania nzima.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli alivyosema kwamba Serikali ndiyo hii hii, tulikuwa na mipango mingi na ndiyo maana tunafanya mabadiliko kila wakati ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la umwagiliaji ni kweli kwamba miradi mingi, kama na ye ye anavyofahamu Serikali tulipeleka hela nyinyi lakini matumizi yake hayakuwa sahihi. Ndiyo maana sasa hivi tumeaulisha huo mpango kuingia kwa kina tuone ni matatizo gani ambayo yalijitokeza na sasa tumekuja na mipango; cha kwanza ni kusimamia ile sheria kwa ajili ya kuanzisha ule Mfuko wa Umwagiliaji wa Kitaifa. Na ndani ya Serikali sasa hivi tunaangalia kuainisha vyanzo vya fedha kwa ajili ya kutunisha mfuo huu ili kwenda kutekeleza miradi hii yote ya umwagiliaji nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mpango kabambe tuliokuja nao kwa kuendeleza sekta ya kilimo kutoka hekta 475,000 mpaka hekta milioni moja ndani ya miaka 15 tunahitaji zaidi ya triliioni 10, na kwa mwaka tunahitaji bilioni 592 kila mwaka ili tutekeleze hilo. Sasa lazima tuwe na vyanzo rasmi ambavyo vinaeleweka, na ndiyo maana tumesema

kimoja wapo lazima tuwashirikishe Sekta Binafsi lakini pia tuzishirikishe taasisi zetu za fedha kama Benki ya Maendeleo ya Kilimo badala ya kusubiri pesa zile za kibajeti pamoja na wadau wengine wa maendeleo. Hiyo ndiyo mipango tuliyokuwa nayo kwenda ku-*address* tatizo kubwa la umwagiliaji ndani ya nchi hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Nagu, haya, endelea.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubali kwamba wana *commitment* ya dhati kwenda kuifanya ile iliyokuepo iwe nzuri, kama ulivyo sema, lakini kwa kweli kwa mimi kukaa chini bila wewe ku-*mention* Gidahababieg haiwezekani, na mimi najua watu wa Bunge hili wanajua matatizo ya ukame wa Hanang na mvua inaponyesha muda mfupi yanayotoka Hanang halafu ninyi mnakataa kusema jambo. Hivi mnakataa mradi ambao umekuwepo na usanifu wake umefanya kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na wewe unisaidie angalau waseme watu wa Hanang wasikie kwamba Bwawa la Gidahababieg liko kwenye *stage* gani, na huu ni mwaka wa kumi toka tulipoanzisha, ninaomba Mawaziri wangu msianze kuleta mambo ya kunyamazia...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, umeeleweka.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** ...mambo ambayo ni muhimu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Jitahidi, gumu kidogo kulitamka, lakini naskia kama vile Gidahababieg; ufanuzi Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa hili la Gidahababieg, ni kweli kwamba halipo kwenye bajeti ya mwaka huu. Bajeti ya mwaka huu tutayaboresha na kujenga mabwawa 16, hili halipo, lakini tumemsikia Mheshimiwa Mbunge, na ndiyo maana nimewambia sasa hivi tunakwenda kutekeleza

mabwawa haya si kwa kutegemea chanzo kimoja cha fedha cha kibajeti. Kimoja cha bajeti, kingine kuititia Benki ya Maendeleo ya Kilimo, lakini kingine kwa wadau au washirika wetu wa maendeleo kama *JICA* na wengine. Kwa hiyo tumekusikia, tumewasikia watu wa Hanang, tuta-*consider* katika bajeti hiyo inayoanza Julai, si ya mwaka huu kwa sababu halimo katika bajeti hii tuliyoweka hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla Serikali haijaingia mkataba wowote huwa inajiridhsia (*due diligence*), kujua hii kampuni ina uwezo kiasi gani, ina sifa kiasi gani, imefanya kazi gani na tuna mfano gani. Sasa Wizara ya Killimo katika sakata la korosho iliingia mkataba na Kampuni ya *Indopower* ya Kenya ambayo baada ya muda...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji Msigwa swali lako haliendi kule kwa Mheshimiwa Mbogo?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana.

**MWENYEKITI:** Liko tofauti?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tofauti kabisa.

**MWENYEKITI:** Tuone tofauti yake.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliingia mkataba na Kampuni ya *Indopower* ya Kenya na ikawaridhisha Watanzania kwamba tatizo na sakata zima la korosho limekwisha. Lakini baada ya muda hii kampuni na mkataba huu, na Waziri hapa

amesema, ukafutwa, lakini tumeingia katika shida kubwa sana kama taifa, watu wameathirika, wamepata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nipate neno na *commitment* ya Serikali watu wote waliohusika kuingiza Serikali na taifa hili katika aibu hii ya kuingia mkataba wa hovyo ambao umelitia aibu taifa letu ni akina nani na wanachukuliwa hatua gani ili Serikali inapofanya mikataba ijue inafanya kazi na wananchi – na sisi tuko hapa kuwawaklisha – ili isirudie kufanya makosa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata majibu ya kuridhisha nitatoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Napata taabu kwa sababu maswalli yanapaswa kuwa ya sera. Napata taabu kama kuna sera ndani ya swalii lako, hebu zungusha kidogo tuone hiyo sera iko upande gani. Maana ukisema ni akina nani ni *event*, ni *issue* siyo sera.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala ya *procurement*.

**MWENYEKITI:** Hebu weka vizuri basi tuone ni sera ipi unaongelea. Nakupa nafasi rudia tena, weka vizuri ili iwe sera sasa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala ya utawala bora watu wanaoingiza taifa kwenye hasara na kwenye aibu lazima wachukuliwe hatua. Na hii itawafanya wale watu tunaowatuma wafanye kazi kwa niaba yetu wawe waangalifu, ndiyo hoja yangu, wawe waangalifu wasije tu kuleta maneno hapa, siku moja wanasema mambo yanawezekana siku ya pili yanakuwa hayawezekani.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo unamuuliza Mheshimiwa Kapteni Mkuchika Utawala Bora maana yake leo Kilimo hapa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, waliohusika kwenye mkataba huu si wanaeleweka? Lakini wamepitia kwenye kilimo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ufanuzi. Leo Mheshimiwa Mchungaji amepata taabu leo uwanja huu; Waziri wa Viwanda na Biashara. (*Makofii*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napata shida kidogo pale anaposema masuala ya *procurement* na nini. Masuala yanayohusu, kama tunavyoendea sasa hivi, biashara ya korosho ambayo Serikali tumeshainunua, tunayo, hatufanyi *procurement* kama ambavyo tunafanya kwenye manunuzi mengine. Tunachofanya sisi ni kupokea ombi la kampuni inayotaka kununua, na akishaleta barua, tukijiridhisha kwamba huyu anaweza akanunua tunaingia mkataba wa awali. Tukishazungumza tukakubaliana mpaka makubaliano ya mwisho ndiyo tunasaini mkataba wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa alichokuwa anazungumza Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, sijamwelewa, ni kuhusu Kampuni ya *Indopower*, halafu akasema tulivyoaini tukatangaza kwamba sasa suala la korosho limekwisha; lingeishaje wakati ambapo yule *Indopower* alikuwa ananunua tani laki moja tu na sisi tulikuwa na tani zaidi ya laki mbili? Sasa hapo ndiyo simuelewi kabisa, anasema eti walitangaza tatizo limekwisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa kwamba tarehe 20, Desemba, 2018, tulipokea barua ya *Indopower* kutaka kununua korosho, tarehe 22, Desemba, sisi tulimuandikia Balozi wetu nchini Kenya atuhakikishie kwamba hiyo kampuni kweli ipo katika orodha ya makampuni ya Kenya na kwamba ina uwezo wa kununua korosho. Tarehe 27 tulipata taarifa ya Balozi wetu nchini Kenya ikithibitisha uhalali wa hiyo kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 04, Januari, 2019, tuliagiza mwombaji alete uthibitisho wa maandishi kutoka

kwa Balozi wake nchini Tanzania, tulipata barua hiyo ya Balozi Dan Kazungu tarehe 27, Januari, alileta uthibitisho wa usajili wa kampuni hiyo na operesheni zote za hiyo kampuni nchini Kenya, Afrika Mashariki na dunia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujiridhisha ndipo mazungumzo yalianza tarehe 10, Januari 2019, tarehe 14, Januari, 2019, mazungumzo yalifanyika chini ya uongozi wa Mwenyekiti wa Timu ya *Negotiation*, Dkt. Mhede, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara na washiriki Bodi ya Mazao Mchanganyiko kutoka Wizara ya Kilimo na Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujiridhisha tarehe 30, Januari, 2019 mkataba ulisainiwa, mkataba ule ulikuwa unamtaka mnunuzi aliye fedha Benki Kuu ya Tanzania ndani ya siku kumi. Baada ya siku tano akaomba *extension*, iwe mwezi mmoja badala ya siku kumi, tulimkubalia. Baada ya miezi miwili kupita tukajiridhisha kwamba huyu sasa nadhani labda makubaliano yake na benki yameshindikana kwa hiyo tukasitisha mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hakuna hasara yoyote, hata senti moja, ambayo nchi hii imepata kwa kusitisha mkataba ule. Sasa mimi namshangaa anaposema tulipata hasara; hakuna hasara hata moja. Na mkataba ule haokusitisha mazungumzo na makampuni mengine ambayo yalikuwa yanaendelea kuleta maombi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Msigwa kwamba, Serikali hii iko makini, ndiyo maana mkataba ule ulisitishwa na ndiyo maana tunaendelea kuzungumza na wanunuzi wengine wanaoendelea kuja. Mpaka leo tumesema makampuni sita yamesaini mkataba wa awali na mpaka tarehe 15 Juni tutakuwa tumeuza korosho, wawe na uhakika kwamba tunafanya kazi kwa umakini mkubwa. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ametumia muda mwingu sana kuzungumzia uhalali yaani *registration* ya kampuni, hata Richmond ilikuwa imesajiliwa Texas na hapa Dar es Salaam kwa hiyo haongei mambo yote mageni, anazungumza kwamba hatujapata hasara kama Taifa, hasara tunayoipata korosho zinapata ule unyaufu, hazinunuliwi, wananchi hawana pesa kule. Serikali walitoa mfumo mzima wa ununuzi wa korosho, wakaingiza kwenye mfumo huo, kwa hiyo ninachotaka kukisema wale wote ambao walihusika katika suala hilo ambao kwa sababu nimezungumzia masuala ya *due diligence*, hapa anazungumzia alipigwa simu na Balozi lakini hapa tuna Mwanasheria Mkuu, tuna Waziri wa Sheria, hawa wote wapo siyo kwa mapambo, wapo hawa kujiridhisha, je, hawa watu tunaoingia nao mkataba ni watu wenye sifa hizo? Kwa hiki tunachokifanya, hiyo kampuni ina uwezo? Sasa baada ya mwezi mmoja wanakuja kugundua kwamba haina uwezo, sasa hivi vyombo vyote tulivyonavyo vina kazi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema naomba nitoe hoja watu tujadili ili Serikali *next time* isitoke tu kwenye vyombo vyahabari...

**SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa, mjadili nini sasa kwa mfano.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Tujadili wale waliotuingiza kwenye mkataba hewa ili *next time* wasituingize kwenye mikataba hewa, kwa sababu korosho bado zinakaa, kwa sababu hawa watu wanakwenda kwenye vyombo vyahabari...

**SPIKA:** Ngoja kidogo Mheshimiwa Msigwa, sisi wafugaji kwa hiyo mifano yetu mingi inaenda kwenye ufugaji, wamekuja watu mmepatana aje anunue ng'ombe wako, halafu hajaja hiyo kesho na ng'ombe wako unaye, sasa kesi ya nini? Ooh, kwa nini wewe ulipatana na yule halafu hujaja au maneno mengine basi mtakuja kuchumbia kwenye boma yenu, mmejiandaa wachumba watakuja, hajaja. Sasa

kesi imanza kwa nini walikuwa waje kuchumbia hawajaja, aliye kubali kwamba hawa sasa waje hawajaja, kwa nini hawajaja? Sasa si hawakuja na sisi tumewakataa hawa wachumba gani hatuwataki, si basi mkataba umevunjika. (*Kicheko*)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**SPIKA:** Iweke vizuri tukuelewe.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi hai endeshwi kama wafugaji wa ng'ombe. Nchi ina endeshwa kwa utaratibu wa kanuni na sharia, tuki endesha hivyo ndiyo maana tunafika hivi tunataka hawa watu ambao tumewapa dhamana, wanapolitangazia Taifa *they shouldn't take us for granted...*

**SPIKA:** Yaani unafikiri kwenye ng'ombe hakuna utaratibu, sheria wala kanuni

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mikataba ya nchi haiko hivyo, mikataba ya nchi haiko hivyo, vinginevyo tutakuwa tunacheza na nchi.

**SPIKA:** Mikataba ya nchi vipi wakati ni *Indo power its private company* na Serikali, siyo Kenya *Government* na Tanzania *Government*, kwa hiyo siyo mikataba ya Serikali mbili, liweke vizuri nakupa nafasi kwa mara ya mwisho vinginevyo itabidi tuvuke sisi inaonekana unatuchelewesha tu. (*Kicheko*)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu nadhani liko *clear kabisa*.

**SPIKA:** Siyo *bilateral, no*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Nakubaliana, utupe nafasi watu tujadili, unipe nafasi watu tujadili, kwa sababu hoja...

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani...

**SPIKA:** Yaani nafasi ninayokupa ueleze ili hata hao watakaojadili waelewe wanajadili kitu gani.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ninayoisema, hawa kwa mfano AG, Waziri wa Sheria na Waziri wa Kilimo, wanafanya kazi kwa niaba ya wananchi kwa hiyo wanapotoka kwenye vyombo vy ya habari na kuwaambia wananchi, wananchi tunawaamini. Sasa wanapotuongoza katika masuala ambayo hayafanikiwi wana-frustrate Taifa. Sasa *they shouldn't take us for granted* kwamba *next time*, wananchi hawajalipwa mpaka sasa hivi tunavyozungumza, kwa sababu ya kutokununuliwa kwa sababu kama haya mambo yangetuwa yametolewa nafasi, mwanzoni tulishauri humu Bungeni namna ya korosho kununuliwa mawazo yetu yalipingwa. Naomba nitoe hoja...

**SPIKA:** Tumsikilize Mwanasheria Mkuu wa Serikali maana yake umemtaja mara kwa mara, tafadhali kama kuna maelezo kidogo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, tumsikilize Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana sana Mheshimiwa Msigwa anapotosha na amepotosha pale alipoanza kulinganisha hiki kilichotokea na Kampuni ya *Richmond*. Kuhusu *Richmond* tulikuwa tunanunua *services* na tunalipa, fedha zinatoka kwetu. Kwenye hii ya *Indo Power* wao ndiyo walikuwa wanakuja kununua korosho kwetu. Tofauti ni kwamba kama ilivyokwishaalezwa katika suala la *Richmond* Sheria ya Manunuzi ilikuwa inatumika na kwamba katika *situation* hiyo, palikuwa pengine na kuvunjwa kwa Sheria ya Manunuzi. Katika suala hili hapakuwa kunahusishwa Sheria ya Manunuzi, kwa hiyo, hiyo ni tofauti ya kwanza na naomba iwe wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia labda Mbunge angejielekeza kwenye Sheria labda ya Maadili ya Viongozi

wa Umma pengine, lakini imeshaelezwa vizuri pia kwamba kilichotokea hapa na sheria iliyokuwa inatuongoza hapa ni Sheria ya kawaida ya Mikataba tena ile inaitwa *Sale of Goods*, kwa hiyo tumeingia mkataba ili wanunue bidhaa zetu. Sasa ule mkataba ume-collapse kwa sababu upande wa pili haujatekeleza yale uliyosema ungetekeleza, lakini cha msingi, hatukupata sisi hasara kwa upande wetu na viongozi hawakutuingiza kwenye hasara yoyote. Kwa hiyo hoja yake haiwezi kusimama na naomba asipotoshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana bahati mbaya Mheshimiwa Msigwa ukiangalia saa yetu tayari ni wakati wa *guillotine*. Nakushukuru sana. Katibu sasa.

Mheshimiwa Cosato bahati mbaya hukupata muda. Katibu endelea

### **Fungu 43 - Wizara ya Kilimo**

Kif. 1001 – <i>Adminstration &amp; Human Resources Management</i> .....	Sh. 6,121,823,000/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh. 1,282,302,000/=
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i> .....	Sh. 1,658,657,000/=
Kif. 1004 – <i>Agriculture Training Institute</i> ....	Sh. 23,796,557,200/=
Kif. 1005 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 419,093,000/=
Kif. 1006 – <i>Procurement Management Unit</i> ...Sh.	481,446,000/=
Kif. 1007 – <i>Government Communication Unit</i> .....	Sh.354,082,000/=
Kif. 1008 – <i>Legal Service Unit</i> .....	Sh. 472,517,000/=
Kif. 1009 – <i>Management Information Systems Unit</i> .....	Sh.370,567,000/=
Kif. 1010 – <i>Environmental Management Unit</i> .....	Sh. 323,887,000/=
Kif. 2001 – <i>Crop Development</i> .....	Sh. 21,714,036,000/=
Kif. 2002 – <i>Agr. Mechanization</i> .....	Sh. 648,634,000/=
Kif. 2003 – <i>Agr. Land Use Planning Management</i> .....	Sh. 877,299,000/=
Kif. 2004 – <i>Plant Breeders' Unit</i> .....	Sh. 149,160,000/=

Kif. 3001 – *Research Development*.....Sh. 0  
Kif. 5001 – *National Food Security*.....Sh. 5,797,686,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 5 - Tume ya Umwagiliaji**

Kif. 1001 – *Adminstration & Human Resources Management*.....Sh. 899,839,000/=  
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 283,088,000/=  
Kif. 1003 – *Policy, Monitoring & Evaluation*....Sh. 264,673,000/=  
Kif. 1004 – *Government Communication Unit*.....Sh. 100,410,000/=  
Kif. 1005 – *Procurement Management Unit*..Sh.174,359,000/=  
Kif. 1006 – *Internal Audit Unit*.....Sh. 96,446,000/=  
Kif. 1007 – *Inform. Comm. Techn Unit*.....Sh. 35,150,000/=  
Kif. 1008 – *Legal Service Unit* .....Sh. 85,822,000/=  
Kif. 1009 – *Environmental & Social Management Unit*.....Sh. 188,613,000/=  
Kif. 2001 – *Design & Research Division*.....Sh. 998,081,000/=  
Kif. 2002 – *Irrigation Infrastructure Dev.*.....Sh. 902,545,000/=  
Kif. 2003 – *Irrigation Research & Techn. Prom.*.....Sh. 23,712,000/=  
Kif. 2004 – *Operations Division*.....Sh. 740,315,000/=  
Kif. 2005 – *Compli. & Quality Assurance Section*.....Sh. 190,575,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 24 - Tume ya Ushirika**

Kif. 1001 – *Adminstration & Human Resources Management*.....Sh. 3,863,991,276/=  
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 150,360,000/=  
Kif. 1003 – *Planning, Monitoring & Evaluation* .....Sh. 96,200,000/=  
Kif. 1004 – *Government Communication Unit* .....Sh. 56,362,000/=

Kif. 1005 – *Legal Service Unit* .....Sh. 26,969,800/=  
Kif. 1006 – *Procurement Management Unit*....Sh. 39,001,300/=  
Kif. 1007 – *Information Comm. Technology*....Sh. 45,500,000/=  
Kif. 1008 – *Internal Audit Unit*.....Sh. 36,452,000/=  
Kif. 1009 – *Research & Training Unit*.....Sh. 65,960,000/=  
Kif. 4001 - *Cooperative Promotion & Coordination  
Section*.....Sh. 76,222,000/=  
Kif. 4002 – *Cooperative Microfinance  
Section*.....Sh. 33,722,000/=  
Kif. 4003 – *Regional Cooperative  
Offices*.....Sh. 1,524,163,224/=  
Kif. 4004 – *Cooperate Marketing &  
Investment Section*.....Sh. 31,954,000/=  
Kif. 4005– *Registration Service Section*.....Sh. 31,044,000/=  
Kif. 4006 – *Inspection & Supervision Services  
Section*.....Sh. 2,249,168,400/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **Fungu 43 - Wizara ya Kilimo**

Kif. 1001 – *Adminstration & Human  
Resources Management*.....Sh. 2,000,000,000/=  
Kif. 1003 – *Policy and Planning Unit*.....Sh. 5,496,262,200/=  
Kif. 1004 – *Agriculture Training Institute*....Sh. 18,348,108,800/=  
Kif. 2001 – *Crop Development*.....Sh. 29,619,819,000/=  
Kif. 2002 – *Agricultural Mechanization*.....Sh. 11,369,750,000/=  
Kif. 2003 – *Agriculture Land Use Planning  
Management*.....Sh. 1,000,000,000/=  
Kif. 2005 – *Irrigation & Tech. Services*.....Sh. 0  
Kif. 3001 – *Research Development*.....Sh. 0  
Kif. 5001 – *National Food Security* .....Sh.75,743,096,140/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 5 - Tume ya Umwagiliaji**

Kif. 1003 – *Planning, Monitoring & Evaluation*.....Sh. 68,500,000/=  
Kif. 1009 – *Environmental & Social Management Unit*.....Sh. 100,000,000/=  
Kif. 2001 – *Design & Research Division*.....Sh. 7,871,500,000/=  
Kif. 2002 – *Irrigation Infrastructure Dev.*.....Sh. 24,176,127,613/=  
Kif. 2003 – *Irrigation Research & Technology Promotion*.....Sh. 0  
Kif. 2004 – *Operations Division*.....Sh. 255,335,000/=  
Kif. 2005 – *Compliance & Quality Assurance Sect.*.....Sh. 30,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilrudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Mheshimiwa mtoa hoja taarifa tafadhali.

### **T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi ya Bunge zima imepitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kuyapitisha kwa pamoja bila mabadiliko. Hivyo basi, naomba Bunge lako Tukufu liyakubali na kuyapitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kama ilivyo ada sasa naomba niwahoji kuhusiana na kukubali kwenu kuitisha Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Nadhani walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba yenu tuipongeze sana Wizara hii, Mheshimiwa Waziri tunakupongeza, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Manaibu, Wakurugenzi na wote mnaofanya kazi katika Wizara hii tunawatakia kila la kheri kwa mwaka unaokuja, utekelezaji wa bajeti hii kwamba uende vizuri, nyinyi ni Wizara kubwa tunatambua majukumu yenu ni makubwa mno, tunawaonea huruma wakati mwingine, mnahangaika sana kwa ajili yetu. Hata hili jambo la korosho tumewalaumu sana hapa Waheshimiwa lakini kwa kweli mmejitahidi. Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wako mmehangaika kweli kweli kwa jambo hili. *(Makofi)*

Kikubwa ni nia, nia ilikuwa njema ya kumpatia mkulima bei ambayo kwa kweli itakayomnufaisha na kawaida ya binadamu unaangalia nia, kama nia ilikuwa ni njema, basi kama umejkwaa mahali si neno sana, ni kujifunza namna ambavyo kesho na kesho kutwa jambo hili litaenda vizuri zaidi. Zao la korosho ni zao ambalo linatupa heshima tunajivunia, sasa hivi linazidi kwenda mikoa mingi zaidi, katika miaka si mingi ijayo huenda Mtwara na Lindi ikawa imezidiwa na mikoa mingine. Hata Dodoma sasa hivi tunapanda korosho, hata mimi napanda korosho, Tabora wanapanda

korosho, Singida wanapanda korosho, hata Mwanza? Mwanza hawawezi Wasukuma hawawezi kulima korosho.

Kwa hiyo ni zao ambalo linazidi kupendwa sana sana na leo tumepata zao lingine jipya, hili Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kaliangalie vizuri na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara hebu angalieni, hili wazo tumepata la lile zao. Kwa kweli bei tulioambiwa leo ni bei nzuri. Kweli iko haja ya kuangalia haya mambo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali aangalie zile sheria sheria zile tulegeze mahali ikiwezekana watu wapate pesa, lile zao watu wanawenza wakaacha hata Ubunge hapa, ukilima heka zao 10 hivi, basi huna shida, kwa maana ya *export* ya Kimataifa lakini. Halitajwi bado mpaka Waziri wa Afya atakapoturuhusu tuweze kulitaja. (*Kicheko*)

Kwa hiyo tunawashukuruni sana Kilimo, msife moyo wakulima ni wengi, *interest* ni nyngi, mazao ni mengi na mambo ni mengi sana. Tunawaomba tu wenzetu wa Uwekezaji na wa Viwanda na Biashara, kwa sababu hata tulime vipi kama *processing industries* hazitakaa vizuri, bado itakuwa ni shida, ndiyo hiyo ili tupate bei nzuri iwe ni pamba lazima tuibadilishe iwe nguo na tuuze nguo, kama ni kahawa lazima tui-*process* kidogo angalau tunapouza kiwe ni kitu cha maana zaidi, kama ni chai tuweze ku-*package* wenyewe badala ya kupeleka Mombasa na kadhalika tuweze kuuza chai duniani, kila kitu, kila *product* ya kilimo tui-*process* kidogo. Hata ngozi, tui-*process* kwa kiasi fulani ili kila wakati tupate fedha nyngi zaidi.

Mtakumbuka michango iliyopita pale nyuma kuhusiana na namna ambavyo wawekezaji hata wa ndani wanawenza kuwekeza kwa urahisi, bado vikwazo ni vingi sana, ule ndio ukweli wenyewe. Kwa hiyo kwa pamoja ule ushauri ambaao tuliuopata, e hawa akina *NEMC*, sijui *OSHA*, sijui *TBS* sijui na wengine kwa kweli iko haja ya kufumua vagingi vagingi vile ili uwekezaji uwe *faster*. Uwekezaji ukiwa *faster* ina maana *processing* itakwenda kwa haraka zaidi na hata malalamiko ya kusema soko, bei na kadhalika yatapungua zaidi. Kwa sababu tutakuwa na soko kwa maana kwamba tutakuwa tunauza bidhaa ambazo angalau zimepita kwenye

chekeche, kwenye chujio, fulani na kwa hiyo ni bora zaidi, zenyenye bei nzuri zaidi.

Kwa hali ilivyo sasa hivi ukitaka kuanzisha kiwanda cha mvinyo lazima uwe na, nilimtembelea ndugu yangu mmoja kuna Kijiji kimoja kinaitwa Nghulabi hapo unapoenda Iringa, ana kiwanda kidogo, ni mkulima mdogo, ananunua zabibu kwa wanakijiji wenzake, ana zile hati kwenye ukuta wake ziko 16. Nikamuuliza hii nini, akaniambia ndiyo vibali ndugu yangu mpaka nifikie hapa nilipofika, nikamwonea huruma. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri, kwa kweli *its just too much*, ndiyo ukweli, yaani mtu ili kuvipata hivyo, ni lazima azunguke kama miaka miwili, mwaka na nusu au mitatu. Sasa na anachofanya ni kuchukua tu zabibu *raw* na kui-*crash* na kuweka kwenye matenki, tayari imeshakuwa unaelekea kwenye *TFDA* tayari na wale wengine wote, hapo *TRA* hajaingia. Hiyo haiwezekani! Matokeo yake wakulima wote wanauza zabibu hivyo hivyo zilivyo, Ukiiza zilivyo ni hasara *at least* twende hatua moja na wengine wanaweza kwenda hatua ya pili na ya tatu. Sasa ili hayo yawezekane, tupunguze kidogo mlolongo wa vibali, kama walivyochangia Wabunge wakati wa bajeti zingine na hasa kwenye bajeti ya Viwanda na Biashara.

Baada ya hapo niwakumbushe tena Waheshimiwa Wabunge kuna futari kule kwa Mheshimiwa Dkt. Kigwangwala lakini pia kuna vijana wanapendeza sana kwenye *gallery* pale wana mashati meupe pale, hawa ni wageni 44 wa Mheshimiwa Godfrey Mgimwa ambao ni wanafunzi 35 na Walimu tisa kutoka Shule ya Sekondari ya Tosamaganga iliyopo Kalenga Mkoa wa Iringa. Karibuni sana vijana wa Tosamaganga, wanaongozwa na Mwalimu Ensy Minzy. Karibuni sana sana, shule hii ni maarufu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge mlisosoma Tosamaganga hebu simameni, wapo bwana, mmewaona wenzenu? Ahsanteni sana na inaelekea ni *A level* kwa mlivyo inaonekana ni *A level*, karibuni sana sana. Hii ni shule

maarufu, kumbe bado mnaendeleza Tosamaganga ile ile ambayo tulikuwa tukiisikia tangu zamani. Jitahidi katika masomo yenu, muweze kufaulu vizuri, tunawatakia kila la kheri karibuni sana Dodoma. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

Baada ya hayo, basi naomba sasa nahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi na kesho tutakuwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,  
Tarehe 21 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*